Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 15 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika(Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 246

**Baa la Njaa Nchini**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitangaza rasmi kuwepo kwa hali ya njaa Tanzania; na kwa kuwa Wwafadhili na wahisani wa ndani na nje ya nchi waliahidi kutusaidia chakula na fedha kwa lengo la kuokoa maisha ya Watanzania ambapo tayari wengine walikwishaanza kula mizizi na majani; na kwa kuwa kwa kiasi kikubwa hali hiyo ya njaa ilisababishwa na ukosefu mkubwa wa mvua; na kwa kuwa mvua zimekuwa zikiendelea kunyesha katika Mikoa mbalimbali kwa kipindi sasa, ambapo wakulima wanaendelea kuzitumia vyema mvua hizo kwa kulima mazao ya chakula na biashara:-

(a) Je, kuna Watanzania wangapi waliopoteza maisha kutokana na njaa hiyo na ni kutoka katika maeneo gani ya nchi yetu?

(b) Je, wafadhili na wahisani wa ndani na wa nje ya nchi wametusaidia tani ngapi za chakula na kiasi gani cha fedha tangu nchi hizo zilipoahidi kutusaidia?

(c) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kutoa tamko rasmi juu ya hali ya chakula ilivyo sasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE.WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, lenye sehemu (a), (b) na (c). Kabla ya kujibu lakini naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilikabiliwa na hali mbaya ya hewa katika kipindi cha mwaka 2002/2003 ambayo ilisababisha ukame na upungufu mkubwa wa chakula katika msimu wa mwaka 2003/2004.

Mapema mwezi Mei, 2003 Serikali kwa kusaidiana na wadau wengine ilifanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao kwa msimu wa mwaka 2002/2003 na kubaini kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula ulikuwa tani milioni 7.55 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula nchini ya tani milioni 8.37. Upungufu wa chakula ulikadiriwa kufikia tani 800,000 katika Wilaya 52 za Mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Singida, Dodoma, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mwanza, Mbeya, Tabora, Iringa, Tanga, Mtwara, Lindi na Pwani. Mwezi wa Julai, 2003 tathmini ya kina ya kubaini kaya ambazo zingeathirika ilifanyika na kuonyesha kuwa watu 1,939,698 wangekabiliwa na upungufu wa chakula.

Baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Hakuna Watanzania waliopoteza maisha kutokana na njaa hiyo.

(b) Wafadhili na wahisani wa nje kupitia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* walitoa kiasi cha tani 29,068 kati ya 45,000 walizoahidi na kugawanywa bure kwa waathirika wapatao milioni 1.2 katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Mtwara, Lindi, Iringa, Mara na Manyara, kama ilivyoonekana katika tathmini ya awali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na misaada ya chakula, wahisani walitoa jumla ya dola za Kimarekani 1,494,000 kupitia Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kununulia tani 915.8 za mbegu mbalimbali zikiwemo mahindi, mpunga, mtama, maharage na kunde. Mbegu hizo zilisambazwa katika maeneo hayo hayo na Mikoa ambayo ilikuwa na upungufu wa chakula.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa iko haja ya kutoa tamko juu ya hali ya chakula nchini wakati wowote panapojitokeza upungufu wa chakula. Itakumbukwa kuwa mwezi Juni, 2004, Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiwasilisha hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake, alitoa tamko la hali ya chakula nchini katika ukurasa wa 19 wa hotuba yake ambapo alisema, namnukuu: "Katika mwaka 2004/2005, hali ya chakula inatarajiwa kuwa nzuri katika baadhi ya Mikoa iliyopata mvua za kuridhisha. Hata hivyo, mvua za masika zimekatika mapema katika baadhi ya maeneo nchini na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao katika maeneo hayo. Kwa hiyo, mavuno katika maeneo hayo yanaweza kuwa pungufu kuliko matarajio. Nachukua fursa hii kuendelea kuwakumbusha wananchi wote kuhifadhi chakula katika kaya zao kama njia ya tahadhari dhidi ya njaa. Kila kaya ijinunulie chakula wakati huu ambapo bei za mazao zimeshuka." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, njaa haipigi hodi, inaweza ikatokea tu na wakati ilipotokea njaa kipindi kilichopita tulikuwa tukitumia Mfuko wa Serikali pamoja na kuomba

misaada nchi za nje. Je, Serikali ina mpango gani wa kujiwekea akiba endapo itatokea njaa ili tuondokane na suala zima la kuombaomba? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi inapaswa kujiwekea chakula kwa tahadhari ya njaa. Lakini tahadhari ya njaa au chakula mtu wa mwanzo kabisa anayepaswa kujiwekea chakula chake ni kiongozi wa kaya. Kila kaya inapaswa kujiwekea chakula cha kujitosheleza na familia yake. Hilo ndilo jukumu la kwanza la kaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweka akiba kwa utaratibu wa kawaida. Tunazo *SGR* ambazo kila mwaka hata wakati yalipotokea matatizo haya tulikuwa na akiba ya chakula kama tahadhari ya Kitaifa ya chakula. Mwaka huu mmemsikia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, akisema anatarajia kununua kiasi kisichopungua tani 100,000. Lakini hata hivyo kwenye *stock* hivi sasa anazo tani ambazo hazipungui tani 30,000. Kwa hiyo, tunayo *stock* ya kutosha kwa tahadhari hiyo. Lakini muhimu kuliko yote kila kaya lazima ijiwekee chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Na. 247

**Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa tangu Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa urejeshwe hapa nchini tarehe 1 Julai, 1992 imedhihirika kwamba Vyama vya Siasa ni miongoni mwa wadau wakuu katika kuimarisha na kudumisha demokrasia hapa nchini:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ipo haja ya kuangalia upya Muundo wa Tume ya Uchaguzi ili baadhi ya wajumbe wake watokane na vyama vya siasa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuangalia upya muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ili baadhi ya wajumbe wa Tume hiyo watokane na vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa ulirejeshwa rasmi hapa nchini tarehe 1 Julai, 1992, baada ya Serikali kukubaliana na pendekezo la msingi lililotolewa na Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania iliyopendekeza, miongoni mwa mambo mengine, kwamba Serikali, ikubali kubadili mfumo wa siasa kutoka mfumo wa chama kimoja na kuwa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huo, Serikali iliwasilisha Bungeni kupitia mabadiliko ya tisa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Muswada wa sheria ili kuruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa kurejeshwa

nchini rasmi ikiwa ni pamoja na kuwa na muundo wa Tume Huru ya Uchaguzi usiohusisha wala kushiriki vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata baada ya mabadiliko hayo ya Katiba kuhusu muundo wa sasa wa Tume ya Uchaguzi, bado wananchi wameendelea kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu haja ya kuangalia upya muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuruhusu baadhi ya wajumbe wa Tume hiyo watokane na vyama vya siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali itangaze azma yake humu Bungeni ya kutaka kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kukaribisha mapendekezo kutoka kwa wananchi, Serikali imekuwa ikipokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali vikiwemo vyama vya siasa, kuhusu muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kuyafanyia kazi mapendekezo hayo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakubaliana na pendekezo ya kuupitia tena muundo wa sasa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuruhusu baadhi ya wajumbe wa Tume hiyo watokane na vyama vya siasa. Muundo huo utafafanuliwa zaidi pindi Serikali itakapowasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne baadaye mwaka huu. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali dogo la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa amekiri sasa suala hilo ni muhimu kulifanya na kwa sababu mbele yetu tuna mambo mengi muhimu ya Taifa hili ikiwemo kuandikisha Daftari la Wapiga kura. Haoni kuwa huu wakati tulionao ni wakati muafaka wa kufanya mabadiliko hayo ili kuondoa malalamiko na manung'uniko mbalimbali?

**SPIKA:** Nafikiri ndivyo alivyojibu, rudia jibu lako Mheshimiwa Waziri nadhani mwenzetu hakusikia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, rudia ile sehemu ya mwisho ya swali.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, tangu itangaze azma yake humu Bungeni ya kutaka kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kukaribisha mapendekezo kutoka kwa wananchi, Serikali imekuwa ikipokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali vikiwemo vyama vya siasa kuhusu muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari na kuyafanyia kazi mapendekezo hayo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inakubaliana na pendekezo ya kuupitia tena muundo wa sasa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuruhusu baadhi ya wajumbe wa Tume hiyo watokane na vyama vya siasa. Muundo huo utafafanuliwa zaidi

pindi Serikali itakapowasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne baadaye mwaka huu.

Na. 248

**_SIDO_ na Maendeleo**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa juhudi za *SIDO* zinaonekana wazi hasa katika kuleta maendeleo endelevu; na kwa kuwa mpaka sasa Mikoa yote ina Makao Makuu ya *SIDO* na kwa kuwa *SIDO* imekuwa ikifanya maonyesho mbalimbali kwenye Miji ya Mikoa na katika Miji ya Wilaya:-

(a) Ili kutimiza dhana ya uboreshaji wa teknolojia rahisi; je, Serikali haioni kwamba ni vyema kuanza maonyesho yake kwenye maeneo ya Vijijini na hasa maonyesho ya zana rahisi za kutendea kazi za kilimo, ufugaji na kadhalika?

(b) Kwa kuwa vitendea kazi katika Ofisi za *SIDO* bado ni haba na hivyo kusababisha *SIDO* kushindwa kuyafikia maeneo ya vijijini; je, Serikali inafikiria nini kuhusu kuiwezesha *SIDO* ili iweze kuyafika maeneo hayo na kufanya kazi zake kwa wigo mkubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na maonyesho ya bidhaa zinazozalishwa na tasnia ndogo katika maeneo ya Mijini na Vijijini na kwa aina zote za bidhaa zikiwemo zana za kutendea kazi za kilimo na ufugaji. *SIDO* imekuwa ikiandaa na kuratibu maonyesho ya kikanda kwa lengo la kujenga uwezo wa wajasiriamali wadogo wa kuandaa maonyesho kama haya katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na hatimaye tutafika Vijijini.

Kwa vile uandaaji wa maonyesho hayo huwa ni gharama ambazo hulipiwa na Serikali; asasi mbalimbali na wajasiriamali washiriki, *SIDO* itaendelea kuwahamasisha wananchi wote kwa ujumla ili waweze kutambua umuhimu wa kutangaza bidhaa zao na hatimaye kuwa tayari kuchangia gharama za kuendesha maonyesho hayo katika ngazi husika. *SIDO* itaendelea kutafuta ufadhili kutoka sehemu mbalimbali ili kuhakikisha kuwa huduma hii ya maonyesho ya bidhaa nchini inaenezwa sehemu mbalimbali na hasa katika Vijiji vyetu nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhaba wa vitendea kazi unaolikabili Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* na tayari hatua zimechukuliwa za kurekebisha hali hiyo. Kwa mwaka 2003/2004 Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kununulia *computer* 30 na magari 12 ambayo tayari yamepelekwa Mikoani na kwa sasa

utaratibu wa kununua magari mengine 5 unaendelea. Lengo ni kuhakikisha kuwa Ofisi za kutolea huduma katika Mikoa yote zinakuwa na nyenzo za usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya tasnia ndogo kuhakikisha kuwa huduma kwa sekta hiyo zinaboreshwa kadri inavyowezekana katika maeneo yote. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa lengo mahsusi la *SIDO* ilikuwa ni kuhakikisha kwamba inakuza teknolojia rahisi ya zana za kutendea kazi ili kuweza kukuza uzalishaji na huduma bora kwa wananchi katika maeneo yote ya Mijini na Vijijini. Mheshimiwa Waziri, naomba aniambie je, anafahamu kwamba bidhaa zinazotengenezwa na *SIDO* na hasa zile mashine nyepesi zinauzwa kwa bei kubwa ukilinganisha na bidhaa zinazotengenezwa na wazalishaji wengine na hivyo kushindwa kununuliwa na wakulima wadogo wadogo na wafanyabiashara wadogo wadogo na hasa katika hayo maeneo ya Vijijini ambako zinahitajika zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, siamini kwamba bidhaa za *SIDO* zina gharama kubwa kuliko bidhaa zinazotoka nje au bidhaa zingine. Naweza nikatoa mifano mbalimbali. Kwa mfano, majiko yale ya *efficient stove* ni rahisi kuliko majiko ya gesi, majembe yanayotengenezwa, *jerry cane* za kununulia maji au za kunyweshea vyote hivyo ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, naomba kumuahidi Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwamba tutafanya maonyesho hapa wakati wa Bajeti yetu wiki ijayo na tunaanza Jumapili, nawakaribisha Wabunge wote kuhudhuria maonyesho hayo na katika maonyesho hayo tutaonyesha bidhaa za *SIDO, CAMARTEC* wanazotengeneza na Mashirika mbalimbali tunaoshirikiana na *SIDO* na kuonyesha kwamba kweli ni rahisi na kumsaidia mwananchi wa kipato cha chini.

**MHE. MWAKA ABRAHMAN RAMADHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza na mimi suala dogo la nyongeza.

Kutokana na utendaji mzuri wa *SIDO,* Waziri haoni sasa umefikia wakati muafaka wa kufungua *branch* zake kwa upande wa Zanzibar? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhani, kwamba Serikali imelisikia ombi hili na litalishughulikia ipasavyo. Ahsante sana.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kuwa Mkoa wa Pwani lipo Shirika la *SIDO* pale Kibaha lakini shughuli zake mara nyingi sana huwa zinafanyia maeneo yale yale ya Wilaya ya Kibaha Mjini au Wilaya zile zilizokuwa karibu na Wilaya.

Je, Wizara sasa hivi itakuwa tayari kuielekeza *SIDO* Mkoa wa Pwani nayo ikaweza kufanya shughuli zake na kuhamasisha juhudi zake katika kuwaboresha wananchi wa maeneo ya Wilaya ya Mafia pamoja na Rufiji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna matatizo ambayo *SIDO* katika Mikoa imeshindwa kufika katika Wilaya zake zote. Tumeliona hilo na ndiyo sababu Serikali imeamua kununua magari kila Mkoa wapate gari moja la *four wheel drive* kuweza kufika katika Wilaya zake.

Mheshimiwa Spika, Mafia hatutanunua boti isipokuwa tutahakikisha *SIDO* tumewaongezea uwezo Mkoa wa Pwani ili waweze kufika kwenye visiwa kama Mafia. *(Makofi)*

Na. 249

**Magari Yanayozidisha Mizigo/Uzito**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA (k.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafanya vizuri kuwa na vituo vya kupimia uzito wa magari yanayobeba mizigo katika barabara zetu kuu kwa lengo la kuzilinda barabara hizo:-

Je, ni adhabu zipi zinazotolewa kwa madreva wa magari yanayozidisha mizigo na hivyo kuzidisha uzito kinyume na uzito unaotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna adhabu yoyote inayotolewa na Serikali kwa dreva kutokana na gari analoendesha kuzidisha uzito katika kituo cha mizani. Sheria inamtaka mwenye gari lililozidisha uzito kulipa gharama za uzidishaji na nyingine zinazohusiana na hilo kama vile kukwepa kupima katika kituo cha mizani, kuharibu mizani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwenye gari ndiye anayeweza kumwadhibu dreva wake kulingana na mkataba wao na ndiye anayejua alimkabidhi mzigo kiasi gani. Sheria hii imezingatia ukweli kuwa mwenye gari ndiye mwenye mkataba na Serikali kuhusiana na umiliki na uendeshaji wa gari na biashara kwa kutumia gari hili.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mafupi ya Waziri, mwajiri au mwenye gari ambaye kwa kawaida huwa hayupo wanampata kwa njia zipi na inachukua muda gani kuweza kumpata na kumwadhibu na kuliachia gari liendelee kama anavyoona yanaendelea?

La pili ni kituo gani katika vituo vyao hasa katika hii barabara ya Mbeya - Tunduma ambacho kinajulikana kukamata magari mengi ambayo yanazidisha mizigo na ni adhabu zipi zimetolewa kwa wenye magari?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, swali lake je, mwenye gari anapatikana kwa njia zipi na kwa muda gani?

Mheshimiwa Spika, mwenye gari anajua kabisa kwamba gari lake linakwenda safari kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya na anajua kuna vituo njiani ni wajibu wake kufuatilia, sio wajibu wa Serikali kumwambia ni wajibu wa mwenye mali kufuatilia. Tukilikamata Kibaha tutalizuia mpaka alipe faini. Baada ya muda wa saa 24 tunatoa taarifa Polisi, hivyo ndivyo sheria inavyosema. Baada ya wiki mbili tunaliuza, hivyo ndivyo sheria inavyosema. Kwa hiyo, yeye ni wajibu wake kufuatilia mwenye gari, sio sisi.

Swali la pili, ni kituo gani kinakamata sana magari? Ni kituo cha mwisho kabisa kabla hujaenda Sumbawanga kituo cha Tunduma. Pale mizigo ni mingi sana na magari yanayotoka Mbeya na yanayotoka huku yanajaza sana. Pale ndiyo kituo kimoja kina kazi kubwa sana sasa hivi.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa kumejitokeza kero kubwa ya wenye mabasi makubwa wanaosafirisha abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha wanapimwa Kibaha, Chalinze na Kabuku wakiwa wamejaza abiria na mizigo na wanapita bila matatizo, lakini wakifika pale Njia panda ya Himo wakiwa wameshashusha abiria na mizigo Same na Mwanga bado wanaonekana kwamba wamezidisha mzigo, je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia upya kile kituo cha Njiapanda pamoja na ku-*check* usanii wa ma-*technician* wanaofanya kazi pale? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, suala la kupima magari yakiwemo mabasi ni suala la sheria. Ni sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ambayo ilipitishwa na Bunge hili na ni wajibu wa Serikali kutekeleza sheria zilizopitishwa na Bunge. Kwa hiyo, magari yanapopimwa yakiwa pamoja na mabasi ni lazima yazingatie sheria hii na kwa kweli sheria hii kwa Tanzania magari mengi yamepewa uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, *gross weight* ya magari ya Tanzania inafika mpaka tani 56 wakati *gross weight* ya magari ya Kenya ni tani 54 na *gross weight* ya magari ya Uganda ni tani 53, ya Uingereza ni tani 48 na ya Denmark ni tani 40. Kwa hiyo, unaweza ukaona utofauti na nchi maskini kama Tanzania lakini bado magari yanabeba uzito mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ukweli magari haya yanapozidisha uzito yanaharibu sana barabara zetu na kilometa moja ya lami kuijenga ni kati ya shilingi 200,000,000 na 300,000,000. Kwa hiyo, tutaendelea kuyashika na kufuata sheria Na. 73 ikiwa ni pamoja na kuyatoza faini ili hawa wanaozidisha waache mtindo wa kuzidisha na kuharibu barabara zetu ambazo zinachangiwa na wananchi wote wakiwemo maskini. *(Makofi)*

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vituo vitatu vya kutoka Dar es Salaam moja kwa moja mpaka Himo vinaachia mabasi hayo yanaondoka bure bila kuonekana kama yana uzito mkubwa zaidi, lakini pale Himo baada ya kushusha kote huko bado yanaonekana yamezidisha uzito, je, kwa nini haionekani kwamba mizani mingine yote inapokea rushwa na kuyaachia mabasi hayo kuondoka na hivyo kuharibu barabara zetu?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nchi nzima ina mizani mingi ikiwa ni pamoja na mizani inayoshtukiza. Magari yanapotoka Dar es Salaam huwa yanapimwa kwenye mzani wa Kibaha, mzani wa Chalinze na mzani wa Himo, lakini pia yanaweza yakapimwa mahali popote kutokana na wale wanaopima mizani watakavyoamua.

Mheshimiwa Spika, gari linaweza likatoka Dar es Salaam likafika Kibaha likawa halijazidisha, likapita. Likifika Chalinze likawa pia halijazidisha, lakini likishafika njiani Mkata likapakia mizigo mingine likifika Himo linaweza likashikwa.

Mheshimiwa Spika, magari haya hayazuiwi kupakia au kupakua wakati yakiwa njiani. Mimi ningeomba nipate ushahidi kutoka kwa Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, kama kuna gari ambalo alipanda kutoka Dar es Salaam likafika njiani likapimwa, likafika Chalinze likapimwa na linapofika Himo likakuta limezidisha, hapo tutaweza kufuatilia na kuchukua hatua. Lakini kuzidisha au kupakia na kutokupakia ni suala la mwenye basi au la mwenye gari. *(Makofi)*

Na. 250

**Magari ya Aina ya *FUSO* Kupima Uzito**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa awali magari ya aina ya *FUSO pick-up* ya mizigo tani tatu na nusu yalikuwa hayalazimiki kupita kwenye vituo vya mizani kwa ajili ya kupima uzito hadi hivi karibuni ambapo magari hayo yametakiwa kupima uzito:-

(a) Je, kumetokea mabadiliko gani ndani ya Sheria ya *The Road Traffic Act, 1973* au Kanuni zake *(The Road Traffic (Maximum Weight of Vehicles) Regulaltions, 2001"),* kuzitaka gari aina hiyo kupimwa uzito:-

(b) Kwa kuwa Sheria ya Barabara *(The Road Traffic Act, 1973)* na Kanuni zake zinatambua *Group of Axles* na kwamba kuwepo kwake kunasaidia kuhimili uzito wa mzigo na kuongeza usalama wa gari na dreva; je, ni kwa nini gari za *FUSO pick-up* zinakatazwa kuongeza *axles* hata kama wanazingatia nafasi ya mita 1.2 hadi 2.5 kisheria?

(c) Je, ni kwa nini Kanuni hizo za sheria katika sehemu "b" ya swali hili zinatofautiana kiutekelezaji kati ya kituo cha mizani Kibaha kinachozuia magari hayo wakati kituo cha mizani Himo kinaruhusu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria ya kudhibiti uzito wa magari hapa nchini inayataka magari yote yenye uwezo wa kubeba tani 3.5 au zaidi kupima uzito katika mizani. Kifungu hiki cha kanuni hakikuongezewa wakati wa marekebisho ya mwaka 2001 bali kilikuwepo tangu awali.

Magari aina ya *Fuso pickup,* kisheria yanatakiwa kubeba kati ya tani 3.5 na hazipaswi kupimwa kwenye mizani, lakini kuanzia tani 3.5 na kuendelea ni lazima zipite kwenye mizani. Kwa hiyo, tangu awali, yaani kabla ya marekebisho ya kanuni za kudhibiti uzito uliofanywa mwaka 2001, sheria iliyataka magari yote yenye kubeba tani 3.5 zikiwemo *Fuso* kupimwa kwenye mizani. Kama baadhi ya magari aina ya *Fuso* yalionekana yakipita kwenye mizani bila kupimwa aidha yalikuwa ni yale yanayobeba chini ya tani 3.5 au yalikuwa yakikiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna badiliko lolote lililofanywa katika Kanuni za Kudhibiti Uzito *(The Road Traffic (Maximum Weight of Vehicles) Regulations of 2001)* kuhusiana na kupimwa kwa magari ya *Fuso* na wala hakuna kipengele kilichowekwa rasmi kwa kuhusiana na upimaji wa magari hayo isipokuwa usimamiaji wa sheria na shughuli za kudhibiti uzito kwa ujumla ndiyo zimeimarishwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli sheria ya kudhibiti uzito inatambua *group of axles* kuwepo kwake kunasaidia kuhimili uzito wa mizigo ambao gari hili limesanifiwa kubeba tangu kiwandani na wala si mzigo wowote ule bila kujali uwezo wa *engine (center of gravity)* na vitu vingine. Kwa hiyo, idadi ya *axles* katika *group* zinazowekwa kitaalam kiwandani huzingatia uwezo wa *engine* ya gari na kuhakikisha uzito unaobebwa na *group* unagawanywa sawa sawa kwenye *axles* zote zilizopo kwenye *group* hiyo.

Mheshimiwa Spika, uongezaji wa *axles* kwenye *Fuso* na magari mengine umekuwa ukifanywa kiholela na wenye magari kwa ajili ya kutaka kubeba mizigo zaidi na siyo kutaka kusaidia gari kuhimili mzigo unaoruhusiwa kubebwa tangu linatengenezwa kiwandani. Licha ya kuongeza *axles* kwa ajili ya kubeba mzigo zaidi, uwekaji holela unafanya mzigo usigawanyike sawa sawa kwenye *axles* za mwanzo *(original)* na zilizoongezwa. Matokeo yake ni baadhi ya *axles* kubeba mzigo zaidi na kuharibu barabara.

Mheshimiwa Spika, kufanya mabadiliko makubwa kama hayo ya kuongeza *axles* katika gari na kuanza kuendesha gari hilo bila kubadilisha *particulars* zikiwemo namba za *axle* za gari husika katika kadi ya gari na kubadilisha leseni ni makosa. Kutofanya hivyo pia ni kuinyima Serikali mapato kwani leseni zinatolewa kuzingatia uwezo wa gari. Tayari mawasiliano yanafanywa kati ya Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu suala hili na mikakati inayotayarishwa ili kudhibiti hali hiyo kwa pamoja.

(c) Mheshimiwa Spika, kanuni za sheria ya Kudhibiti Uzito ni zile zile kwa nchi nzima na hazitofautiani kati ya Mkoa na Mkoa wala kituo cha mizani na kingine.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa, lakini ningependa kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa kiasi cha mzigo uliopo ndani ya gari ukipangwa vizuri na hasa ukisogezwa mbele karibu na *cabin* ya dreva ukipita katika mizani mzigo huo unaonekana kama uko sawa sawa. Lakini kwa kiasi hicho hicho mzigo ukisambazwa katika *cabin* nzima ukipita katika baadhi ya mizani mzigo huo unaonekana kwamba umezidi, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba mashine zetu hazisomi kwa uhakika na kwa ufanisi kabisa kiasi cha mzigo kilichopo ndani ya gari? *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, hasa katika kituo cha Kibaha na hasa katika siku za Ijumaa jioni, Jumamosi jioni na Jumatatu jioni kunakuwa na foleni ndefu kupita kiasi kutoka katika mizani hadi kuelekea katika daraja lililopo sehemu ambapo unaingia katika Mji wa Kibaha, kiasi cha kama nusu kilometa, je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ipo haja ya kufikiria kuongeza idadi ya watendaji wa kazi pamoja na mashine ili gari ziweze kupimwa angalau mbili kwa wakati mmoja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** (a) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi, amesaidia kwa maelezo kusema kwamba mzigo ukisogezwa mbele upimaji unakuwa sawa sawa, lakini ukisawazisha sawa sawa basi mzigo unakuwa umeonekana umezidi. Kwa mantiki hiyo Mheshimiwa Herbert Mntangi, anakubaliana na jibu langu kwamba kuongeza *axles* ni kosa na hilo ndiyo tatizo linalotokea. Wanaongeza ili wabebe zaidi, kwa hiyo, wanausogeza mbele ili uonekane mdogo, lakini wakiutandaza sawa sawa *group of axle* inakataa kwa sababu hilo gari halikutengenezwa hivyo na ndiyo maana kunatokea dosari hiyo. Sasa hivi tumewafundisha watu wetu kugundua *non-original axle, axle* ambazo zimeongezwa.

Kwa mantiki hiyo, inatakiwa kumsimamisha mtu na kumripoti *traffic* kwamba huyu ameongeza axle na *licence* yake *fake,* kwa maana hiyo na hana kibali cha kuendesha kibali iliyoondoshwa *axle* mpaka abadilishe. Kwa misingi hiyo, ndiyo maana hizo dosari zinatokea, lakini gari *original* haina matatizo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Kibaha pana matatizo ya foleni kwa jioni na mimi mwenyewe nimefuatilia na sababu tumepata. Mimi na Waziri tunafuatilia sana Kibaha kwa sababu ni mahali ambapo tunajua pana migogoro mingi sana. Lakini foleni zile zinatokana na wale wenye magari ya mizigo kutoka Dar es Salaam jioni. Wenyewe wanapenda kusafirisha mizigo jioni. Kwanza, wanakwenda kama kundi kwa usalama wao, pili, wanasema matairi hayaharibiki sana na injini haipati moto sana. Sasa huwezi kumzuia mwenye gari kusafiri wakati huo kwa sababu wewe unakataa foleni, sisi tunawaruhusu waendelee.

Mheshimiwa Spika, wakati magari sasa yanakuwa yanazidi mara nyingine huwa tunatumia *traffic* atusaidie kupima magari hayo kwenye upande wa pili, halafu baada ya kupima yanazunguka yanaondoka. Tuna-*solve* kwa njia hiyo. Kwa hiyo, tumejitahidi kufuatilia na tunajitahidi kurahisisha mambo yaende haraka. *(Makofi)*

Na. 251

**Zao la Pamba**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali kwa kipindi cha karibu miaka mitano imekuwa ikifanya mikutano mingi kuhusu zao la pamba ikiwashirikisha wadau mbalimbali: -

(a) Je, wakulima wa pamba wamepata manufaa gani kutokana na mapendekezo ya mikutano hiyo?

(b) Je, kwa nini washirika wa pamba wasipewe fursa ya kuwa wanunuzi kiongozi ili kudhibiti soko holela la pamba ambalo limekuwepo na lengo la kuimarisha Ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia mfumo wa soko huria ambapo shughuli za uzalishaji, ununuzi, usindikaji na uuzaji mazao hufanywa zaidi na sekta binafsi, mikutano ya wadau imekuwa ikifanywa kwa madhumuni ya kujenga maelewano baina yao na inawezesha kutatua baadhi ya matatizo yanayojitoleza kwenye sekta ya zao husika ikiwa ni pamoja na zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, mikutano hiyo pia inatoa fursa ya kubadilishana uzoefu, utoaji wa utaalam na uwekaji wa mikakati ya maendeleo ya zao la pamba ya muda mfupi, kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kufikiwa kwa madhumuni hayo ya jumla na kuzingatiwa kwa mapendekezo ya mikutano hiyo kumewapatia wakulima wa pamba manufaa kadhaa yakiwemo haya yafuatayo: -

(i) Kutokana na utekelezaji wa mikakati mbalimbali iliyowekwa katika mikutano ya wadau, kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa pamba kwa takriban asilimia 22 kwa mwaka ambapo kwa kuanzia msimu wa mwaka 1999/2000 uzalishaji ulikuwa marobota 196,000, msimu uliofuatia wa mwaka 2000/2001 uzalishaji uliongezeka na kufikia marobota 228,591, msimu wa mwaka 2001/2002 uzalishaji uliongezeka kufikia marobota 281,132 na msimu wa mwaka 2002/2003 uzalishaji uliongezeka pia kufikia marobota 354,130.

(ii) Kuboreshwa kwa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima kufuatia kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba. Mfuko huu umeboresha upatikanaji wa viuwadudu kutoka lita 100,000 mwaka 1999/2000 hadi kufikia lita 1,000,000 mwaka 2003/2004.

(iii) Mashindano ya kilimo cha pamba kuanzia ngazi ya Wilaya hadi kando yaliyoanzishwa tangu mwaka 2003 ambapo wakulima wanaofanya vizuri huzawadiwa zana za kilimo na baiskeli yameongeza hamasa zaidi katika kilimo cha pamba nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, sera ya soko huru inayotekelezwa na Serikali toka miaka ya 1990 inatoa fursa kwa wanunuzi wote halali wa pamba ikiwa ni pamoja na vyama vya ushirika. Utekelezaji wa sera hii umesaidia kuongezeka kwa ufanisi katika ununuzi wa pamba kutoka kwa wakulima, hususan katika Kanda ya Magharibi ambapo kwa wastani pamba sasa inanunuliwa katika muda wa miezi mitatu badala ya miezi mitano au zaidi kabla ya kuanza kutekelezwa kwa sera hii.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la ufanisi katika uchambuaji wa pamba kutoka marobota 300,000 kwa kipindi cha miezi sita hapo awali hadi kufikia marobota 750,000 hivi sasa katika kipindi hicho kufuatia sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vipya 22 toka mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya Serikali inatambua kuwepo kwa matatizo kadhaa ya utekelezaji yanayosababishwa na baadhi ya wafanyabiashara binafsi wanaokiuka taratibu na kanuni zilizowekwa. Kwa mfano, kushuka kwa ubora na usafi wa pamba, wakulima kupunjwa kautokana na baadhi ya wanunuzi kutumia mizani isiyofaa na wakulima kulipwa bei zisizolingana na madaraja ya ubora wa pamba yao.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo, Wizara ya Ushirika na Masoko kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba na Umoja wa Wadau wa Pamba *(Tanzania Cotton Association)* inakamilisha kuandaa mfumo utakaowezesha pamba yote nchini kununuliwa katika ngazi ya Vyama vya Ushirika vya Msingi kuanzia msimu wa ununuzi wa 2005/2006.

Mfumo huu utatoa fursa kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi kusimamia shughuli za ununuzi wa pamba katika magulio ya vyama hivyo, kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji na Bodi ya Pamba. Wanunuzi wengine wote wataendelea kununua pamba kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha utendaji na uongozi wa Vyama vya Ushirika vya Msingi ili viweze kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM tumeandika kabisa kwamba nia yetu ni kuimarisha Ushirika hasa kuhusiana na mazao nyeti kama pamba, kahawa na korosho yanayoliingizia Taifa letu fedha za kigeni, naomba Naibu Waziri anithibitishie kwamba, je, wana mpango gani wa kuimarisha Ushirika katika sehemu mbalimbali na hasa katika maeneo ya zao la pamba ili yaweze kusimamia ununuzi wa pamba vizuri zaidi kuliko sasa?

(b) Kwa kuwa katika msimu huu unaoendelea bei ya pamba ilianza kwa shilingi 300 kwa kilo, lakini baada ya muda kidogo tu bei hiyo ikashuka ikawa shilingi 250 kwa kilo, je, ni kitu gani kimetokea mpaka bei hiyo ikateremka ghafla namna hiyo na Serikali

itafanya nini ili kuwafidia wakulima ambao walikwishapima pamba yao kwa bei ya shilingi 300 ili wasipunjwe hizo shilingi 50 kwa kilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** (a) Mheshimiwa Spika, suala la kwanza linalohusu uimarishaji wa Vyama vya Ushirika, nataka tu nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada za Serikali katika suala hili zimefikia kiwango cha juu sana kwa sababu kwanza kimsingi sote tunajua kwamba Sera mpya ya Ushirika iliishaanzishwa ambayo nia na madhumuni yake ni kuimarisha na kuboresha Ushirika nchini ili kuweza kuboresha huduma za ununuzi wa mazao pamoja na huduma nyingine zinazosimamia Vyama vya Ushirika nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia itakumbukwa kwamba, Bunge lako Tukufu lilishapitisha Sheria ya Ushirika hapa Bungeni. Kwa sheria hiyo sasa hivi tunajaribu kufanya maandalizi ya kuandaa programu ya utekelezaji pamoja na kanuni ambazo zote zinalenga katika suala zima la kuhakikisha kwamba Vyama vya Ushirika vinasimamia ununuzi wa mazao kama Ilani ya Uchaguzi ya chama cha Mapinduzi inavyosema.

(b) Mheshimiwa Spika, la pili ambalo Mheshimiwa Dr. William Shija anataka kujua ni juu ya suala la bei ya pamba. Wizara inazo taarifa za kusuasua kwa bei ya pamba katika soko la pamba duniani na hii inatokana na sababu kuu zifuatazo:-

Kwanza, kuongezeka kwa uzalishaji wa pamba duniani kuliko mahitaji ya watumiaji. Hivi sasa pamba imezalishwa kwa wingi zaidi, kwa hiyo, ile *demand and supply forces* ndiyo inafanya mabadiliko hayo ya bei yaweze kutokea. Lakini vile vile, kumetokea ucheleweshaji katika utaratibu wa kutoa dhamana *(guarantee)* kwa wanunuzi wakubwa wa pamba duniani ambao ni China. Wamechelewa kupata *guarantees* na kwa hiyo, wamechelewa kufungua zile *letters of credit* na kutokana na hivyo wanunuzi wamekuwa wachache kulingana na jinsi ilivyokuwa imetazamiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, uhusiano wa shilingi ya Tanzania na dola ya Marekani umebadilika mwezi Juni, 2004. Wakati bei ya mwanzo ilipokuwa inatangazwa shilingi 300 kwa kilo ya pamba, dola yetu ilikuwa shilingi 1,100 kwa dola moja na sasa hivi ni shilingi 1,080 kwa dola, hivyo shilingi yetu imeimarika kidogo. Kwa hiyo, yote hii imeleta athari za bei hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na hali hiyo ya bei kusuasua, wadau wa pamba *(Tanzania Cotton Association)* walikutana Mwanza siku ya Jumanne tarehe 13 Julai, 2004 kuchambua taarifa zote za mwenendo wa bei na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kujihami. Serikali inasubiri mapendekezo hayo yatakapokuwa yameletwa na kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado nina maswali manne na nina dakika 15 tu zimebaki. Kuna jibu la nyongeza, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**WABUNGE FULANI:** Chifu.

**SPIKA:** Chifu gani?

**MBUNGE FULANI:** Chifu ...

**SPIKA:** Amechelewa, lakini Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kama una jibu la nyongeza endelea.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo ya nyongeza kuhusu swali la kupungua kwa bei ya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu kwamba katika majadiliano ya *WTO* suala la pamba ni moja ya jambo ambalo tunabishania sana na ubishi huu unatokana na ukweli kwamba mlimaji mkuu wa zao la pamba duniani ni Marekani ndiyo anayetoa ruzuku kubwa kwa zao la pamba na hivyo ku-*suppress the price of cotton World wide.* Kwa maana hiyo basi, ni lazima bei ya pamba itakuwa inayumba madhali tu Marekani na vile vile Ulaya wanatoa ruzuku kubwa kwa zao la pamba. Kwa hiyo, jibu la kudumu ni ushindi wa nchi maskini katika mjadala wa *WTO* ambao utafanyika mwishoni mwa mwezi Julai, 2004 kule Geneva kama tutakubaliana wapunguze ruzuku kwa zao la pamba. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 252

**Kuzorota kwa Huduma ya Kusafirisha Fedha na Vifurushi**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza: -

Kwa kuwa Kampuni ya Simu na Shirika la Posta ndiyo yaliyoaminika sana na watu wengi kuyatumia Mashirika haya kutuma barua, fedha na vifurushi mbalimbali; na kwa kuwa ilipoanzishwa huduma ya *money fax* wananchi waliendelea kuyatumia kwa wingi kwa huduma hizo na kwa kuwa huduma hizo zimezorota sana kiasi kwamba zikitumwa fedha toka Dar es Salaam kwenda Mikoa kama Mwanza, Singida, Arusha, Tabora, Mtwara na kwingineko huchukua muda wa zaidi ya siku mbili na kwa kuwa kutokana na kuzorota kwa huduma hizo ndiyo maana makampuni ya mabasi kama Scandinavia, Shabiby, *Dar Express* na kadhalika zimeshika hatamu ya kutoa huduma hizo hizo zilizokuwa zinatolewa na mashirika hayo tajwa hapo juu kwa ufanisi mkubwa na kwa muda mfupi zaidi: -

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya uzembe uliojitokeza kwenye mashirika yake hayo na kuwafanya wananchi wakose imani nayo na kuanza kutumia njia nyingine ya kupata huduma hiyo na kuikosesha Serikali mapato yake?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi na za haraka za kukomesha uzembe huo na kuondoa kabisa dosari zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wale waliohusika na kurudisha hadhi zile bora mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Sheria ya Mawasiliano Na. 12 ya mwaka 2003 iliyopitishwa na Bunge, Huduma za Posta hususan usambazaji wa barua na nyaraka za haraka, vifurushi

na utumaji fedha zinaendeshwa kwa misingi ya ushindani tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo Posta ilikuwa inaendesha huduma hizo kwa ukiritimba.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuruhusu makampuni binafsi kushiriki kutoa huduma za Posta umewezesha wananchi kuchagua na kutumia huduma mbadala zinazoweza kukidhi mahitaji yao na kuleta chachu mpya katika sekta ya Posta.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Mamlaka ya Mawasiliano *(Tanzania Communications Regulatory Authority)* imeshatoa leseni kwa makampuni 15 kuendesha biashara ya kusambaza nyaraka na vifurushi. Makampuni hayo yanapaswa kuzingatia sheria za uendeshaji wa biashara hiyo na kanuni zilizoainishwa kwenye leseni walizopewa na Mamlaka ya Mawasiliano pamoja na kulipa kodi ya Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani aina yoyote ya uzembe katika ufanyaji kazi. Kwa hiyo, Uongozi wa Mashirika yote ya Umma ikiwa ni pamoja na Shirika la Posta umeelekezwa kufuatilia na kuchukua hatua dhidi ya malalamiko yanayohusu huduma wanazozitoa. Serikali inaendelea kutathmini muundo, mifumo na matatizo ya uendeshaji wa Shirika la Posta ili kulirekebisha na kuliwezesha kujiendesha kwa ufanisi na kwa kuzingatia misingi ya biashara. Shirika la Posta pamoja na kujiendesha kibiashara limekuwa likilipa kodi za Serikali kama yanavyolipa makampuni binafsi yenye leseni za kuendesha shughuli zinazofanana na zile zinazotolewa na Posta.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza iliyochukuliwa na Serikali kwa lengo la kurekebisha na kuboresha mifumo ya uendeshaji wa Shirika la Posta ili liendeshwe kwa misingi ya kibiashara ni kuingia Mkataba wa Utendaji *(Performance Contract)* baina ya Serikali na uongozi wa Shirika la Posta. Mkataba huo umeainisha vigezo na malengo ya utendaji, gawio na adhabu zitakazotolewa kwa kufikia au kutofikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, tangu kuanzishwa utaratibu wa mikataba ya utendaji mwaka 1997, ukaguzi uliofanywa umeonyesha kuwa Shirika la Posta linafanya vizuri katika kasi ya kutoa huduma, kuwajali wateja na usalama wa mali za wateja. Pamoja na mafanikio hayo ambayo yameliletea sifa Shirika hilo, Shirika hilo halijafanya vizuri katika kuongeza wingi wa biashara na mapato kadhalika faida inayozalishwa haijafikia kiwango kilichowekwa kwenye mkataba wa utendaji. Hii inatokana pia na kuingia kwa teknolojia mpya ya *ICT* ambapo Wananchi wanaona ni njia nyepesi na muafaka. Hatua zinazochukuliwa na Shirika la Posta ni pamoja na kupanua mtandao wa huduma ya *money fax* ambapo hivi sasa huduma hizo hutolewa kwenye ofisi 104 nchini, ikilinganishwa na ofisi 18 hapo mwaka 1994 lilipoanzishwa rasmi. Aidha, Shirika linaendelea kuboresha mtandao wake kwa kutumia teknolojia mpya ya mawasiliano kupitia kompyuta na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mgana Msindai, kwamba kwa mujibu wa sheria Na. 12, Baraza la Watumiaji wa Huduma ya Mawasiliano, ikiwa ni

pamoja na Huduma za Posta limeanzishwa. Mwenyekiti wake ni Mzee mzoefu, Mzee Rajab Yusuf, aliyekuwa *Postamaster* Mkuu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Pamoja na mambo mengine Baraza litasimamia maslahi ya watumiaji wa Huduma za Posta ikiwa ni pamoja na viwango na ubora wake.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja tu la nyongeza na pia nimeridhika sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba kumuuliza.

Je, yale maeneo ambayo hayajawa na uhakika wa magari mazuri ya kufanya hii kazi kama vile Mkoa wa Singida, Tabora na kwingineko Mashirika haya yataendelea kusaidia kufanya hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mgana Msindai, kwamba *priority* inatolewa kwa wenye mabasi wa sehemu ile wanaingia mikataba na Posta kutoa huduma nyingine, lakini napenda nimhakikishie kwamba hali inaporuhusu maeneo mengine yote yatafikiwa.

Na. 253

**Mawasiliano ya Simu**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza: -

Kwa kuwa mawasiliano ya simu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya nchi na kwa kuwa Mji wa Mashewa sasa una umeme na umepanuka sana na kwa kuwa maeneo ya Kizara, Kalalani (Kata ya Mashewa) kuna Kampuni kubwa za uchimbaji wa madini (vito vya thamani), lakini hakuna mawasiliano ya simu na kwa muda mrefu wamekuwa wakiomba huduma hiyo bila mafanikio: -

Je, Serikali ina mikakati gani ya kupeleka simu katika Miji hiyo na hata kuzishawishi Kampuni za *Vodacom* na *Celtel* kufanya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa kupeleka huduma ya simu vijijini, Serikali ina mkakati wa kuanzisha Mfuko maalum ujulikanao kama Mfuko wa Simu Vijijini *(Rural Telecommunications Fund)* ili kufanikisha azma hiyo. Wadau mbalimbali wa simu watahusishwa katika mpango huo. Juhudi za Serikali bado zinaendelea na ni mategemeo yetu kuwa mara Mfuko huo utakapoanza kutumika tatizo la ukosekanaji wa simu vijijini litapungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa simu za mikononi, Kampuni ya *Celtel* inakusudia kufanya tathmini ya soko *(field marketing survey)* katika Mji wa Mashewa mwezi Agosti, 2004. Tathmini hiyo itasaidia kufikia uamuzi wa lini Kampuni ya *Celtel*

itaweza kutoa huduma katika Mji huo muhimu wa kibiashara. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aipe Kampuni ya *Celtel* ushirikiano itakapofanya tathmini hiyo ili kujua ni maeneo yapo hasa yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Vodacom* nayo kwa hivi sasa inafanya tathmini ya soko nchi nzima ili kubaini maeneo ya kuweka mitambo yao ya mawasiliano. Kufuatia matokeo ya uchunguzi wa awali, ujenzi wa mitambo ya mawasiliano utaanza kujengwa katika maeneo yale yatakayoonekana kuvutia zaidi na ambayo yanaweza kuunganishwa kwenye mtandao kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yatawekwa mitambo baadaye kutokana na ubora, kipaumbele *(priority)* na upatikanaji wa njia za simu. Zoezi hili litaendelea nchi nzima hadi sehemu zote zitakapopata huduma za *Vodacom.* Hivyo, mipango ya *Vodacom* kupeleka simu Kata ya Mashewa itajulikana punde tathmini itakapokamilika katika kipindi kifupi kijacho. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo ni ya matumaini, lakini nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa kutoka Mashewa hadi Magoma ni kama kilometa 10 tu na Magoma kuna simu na Mashewa napo kuna umeme ambao ndiyo nyenzo kubwa inayoweza kusaidia kupata siku za *TTCL,* je, Mheshimiwa Waziri haoni kwa sababu pale ni karibu angalau tukapata simu za *TTCL* badala ya kungojea hizo za *Vodacom* pamoja na *Celtel?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutoka Mashewa kwenda Magoma ni kilometa 10 na tutaendelea kuwasiliana na watu wa *TTCL* kama kuna umuhimu wa kufanya utafiti kidogo kuona ni namna gani wanaweza kuwasaidia watu wa Magoma badala ya kusubiri huduma za *Celtel* na *Vodacom.*

Na. 254

**Ujenzi wa Bwawa la Mwisanga**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na wahisani imetumia fedha nyingi sana za kujenga bwawa la Mwisanga kwa lengo la kutatua tatizo la maji katika Vijiji vya Chandama, Mapango, Mlongia, Itolwe, Jangalo, Jinjo, Churuku, Ntinkima, Hamai, Songolo, Madaha, Igunga, Mtakuja, Goima, Jenjeluse na Lusangi Wilayani Kondoa na kwa kuwa bwawa hilo bado halijakamilika: -

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeutelekeza mradi huo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa kukamilisha bwawa hilo ili kuwaondolea Wananchi wa Vijiji husika tatizo la maji?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Ntomoko ulikuwa unapata maji kutoka chemchem zilizopo katika milima ya Ntomoko katika Wilaya ya Kondoa. Baada ya kuona kuwa maji ya chemchem za Ntomoko hayakidhi mahitaji ya Vijiji husika, Serikali ilibuni ujenzi wa bwawa la Mwisanga kama chanzo kingine cha maji kwa ajili ya Vijiji vya Chandama, Mapango, Mlongia, Itolwe, Jangalo, Jinjo, Churuku, Ntinkima, Hamai, Songolo, Madaha, Igunga, Mtakuja, Goima, Jenjeluse na Lusangi. Lengo lilikuwa ni kuwapatia maji safi na salama Wananchi wa Vijiji 16 nilivyovitaja. Ujenzi wa bwawa hilo ulifanyika kwa ufadhili wa Baraza la Kikristo la Tanzania *(CCT)* pamoja na Serikali ya Tanzania. Bwana lilijengwa tangu mwaka 1977 na kukamilika mwaka 1986.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika katika kutekeleza mradi huu ni pamoja na kufunga bomba kuu lenye urefu wa kilometa 4 kutoka kwenye eneo la bwawa hadi kwenye bomba kuu la mtandao wa mabomba ya mradi, kujenga nyumba za watumishi, jengo la maabara, jengo la kuchanganya dawa, tanki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mradi huu haukuweza kukamilika kutokana na fedha kuwa chache. Jumla ya shilingi milioni 400 zinahitajika ili kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mradi wa bwawa ulisimama Serikali iliendelea kuimarisha huduma ya maji katika Vijiji nilivyovitaja kwa kukarabati mabomba katika Vijiji 13 kati ya 16 na maji yaliweza kupatikana kwa mgao wa kila baada ya siku moja. Serikali ilichangia shilingi milioni 30 kutekekeza kazi hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaanzisha chombo chao cha kusimamia mradi huu, Serikali ilitoa shilingi milioni 5 katika Bajeti ya 2001/2002 na shilingi milioni 5 kwa mwaka 2003/2004.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuwaondolea wananchi wa Vijiji husika tatizo la maji, Serikali ina mpango wa kukamilisha kazi zilizobaki hatua kwa hatua kulingana na uwezo wa fedha na kama nilivyomuahidi Mheshimiwa Pascal Degera katika Bunge lililopita katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 20 kwa ajili ya bwawa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wilaya ya Kondoa ni miongoni mwa Wilaya 12 ambazo hivi sasa zinatekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Programu hiyo inatekelezwa kwa utaratibu wa Wilaya yenyewe kuchagua miradi yao kulingana na kipaumbele walichojiwekea. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, aishauri Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa iingize ukamilishaji wa bwawa hili katika kipaumbele chao.

Na. 255

**Matatizo Makubwa ya Maji - Mlalo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza: -

Kwa kuwa ni ukweli usiojificha kwamba Kata ya Shume, Tarafa ya Mlalo ina matatizo makubwa sana ya maji karibu sawa na maeneo kame ya nchi yetu na kwa kuwa tulishaandika maandiko ya mradi wa maji uitwao *Manolu Group* na kuwasilisha Serikalini siku nyingi lakini hatujapata mhisani:-

(a) Je, Serikali imesaidia vipi kuuza mradi huo kwa wahisani mbalimbali nje na ndani?

(b) Kwa kuwa mradi huo bado haujafanikiwa, je, Wizara itawasaidia vipi wananchi wa Kata hiyo hasa Vijiji vya Manolo, Madala, Mavumo, Mkunki, Nywelo na Gologolo?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Shume ina mradi wa Maji wa Manolo uliojengwa mwaka 1968 kwa ajili ya kuhudumia Vijiji vitano vya Gologolo, Nywelo, Mkunki, Gemai na sehemu ya Kijiji cha Manolo kwa kutumia Kijito cha Manolo kama chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la watu na kupungua kwa maji kwenye chanzo kulikosababishwa na uharibifu wa mazingira baada ya kukata miti ovyo kwenye eneo la chanzo hicho, maji hayakutosheleza tena mahitaji na hivyo ikabidi kutafuta vyanzo vingine vya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza tatizo la maji katika Kata hiyo, Serikali iligharamia ujenzi wa visima vifupi vinne katika Vijiji vya Nywelo (visima 2) na Madala (visima 2) katika ya mwaka 1984 na 1987. Hata hivyo, visima 2 vya Kijiji cha Madala na kisima 1 cha Kijiji cha Nwelo havifanyi kazi kutokana na pampu zake zilizoharibika kutofanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba huo wa maji katika Kata hiyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto na kwa kushirikiana na asasi isiyokuwa ya Kiserikali ijulikanayo kama *Tanga Diocese Development Organisation (TADDO)* imetayarisha mradi mpya wa maji ya *Manolu Group* unaojumuisha Vijiji sita kwa ajili ya kuimarisha na kuboresha huduma ya maji katika Vijiji hivyo. Chanzo cha maji kwa ajili ya mradi huu mpya ni Vijito vya Gerwali, Mstari wa Ishirini na Tano, Kwaboya na Sungwi unaokadiriwa kugharimu shilingi milioni 920.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada nilizozitaja hapo juu, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, imeanzisha mpango wa kufufua visima vifupi na pampu za mkono. Kwa mwaka 2003 mpango huo ulitengewa shilingi milioni 9.4, hadi sasa pampu za mkono nane zimenunuliwa na zitafungwa katika Vijiji vya Shume pampu 3, Mwangoe pampu 2 na Mlola pampu 3.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mbunge wa Mlalo kwa kufuatilia kazi hii kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada za ufuatiliaji kwa mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 12 kwa ajili ya mradi huo.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwanza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ni kwamba kama alivyosema ni kweli katika eneo hili watu wameongezeka sana na eneo hili ni chanzo kikubwa cha matatizo yaliyotukumba kwa muda mrefu ya ugonjwa wa tauni. Sehemu ya dawa ya kupambana na viroboto vya tauni ni maji kwa sababu ya matatizo hayo, je, Waziri na Serikali kwa ujumla italichukulia jambo hili kwa umuhimu unaostahili na kuwahimiza na kuleta maombi mazito kwa wahisani ili ikiwezekana mradi huu uweze kufanikiwa haraka, ili tupige ndege wawili kwa jiwe moja? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nakubaliana naye kwamba tatizo la ugonjwa wa Tauni katika maeneo hayo lilikuwepo wakati ule. Lakini tatizo kubwa la Lushoto ni uharibifu wa mazingira na uharibifu wa vyanzo vya maji. Nawaomba sana viongozi wa Lushoto na Mkoa wa Tanga kwa ujumla mshughulikie tatizo hili kwa sababu vyanzo haviongezeki, binadamu wanaongezeka. Hivi sasa kuna watu wamevamia vyanzo vile wanatafuta dhahabu na vyanzo vile vikiharibika ninawahakikishia maji hayatapatikana. Lakini Serikali itaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha mradi huo unapata fedha na ningependa kukuhakikishia kwamba katika mpango wa mwaka 2005/2006 Wilaya ya Lushoto itaingizwa katika Wilaya zitakazofaidika na Benki ya Dunia na mradi huo utahusika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa. Kuna tangazo moja tu la kikao kwa siku ya leo ni Kikao cha Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kikao hicho ni Mheshimiwa Anne Makinda, anaomba wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira wakutane leo saa tano asubuhi hii katika ukumbi namba 231, ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 Wizara ya Nishati na Madini

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Wasemaji wanne wa kwanza leo ni Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Parseko Kone na Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme. Namwita Mheshimiwa Leonard Shango, lakini subiri kidogo

wanaokwenda kunywa chai waondoke. Mheshimiwa Leonard Shango, unaweza kuanza na muda wako wa kusema unahesabiwa kuanzia sasa.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa Bajeti ya mwaka 2004/2005. Awali ya yote mimi ningependa kusema kuwa naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, pamoja na timu yote ya Wizara ambayo imetuletea hotuba nzuri ambayo inatuelekeza tunakwenda wapi na tumetoka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi katika mchango wangu nitataka Waziri anipe maelezo ya kutosheleza katika masuala fulani fulani yanayohusu sekta yake. Wote tunajua kuwa umuhimu wa umeme wa gridi ya Taifa katika maendeleo, siyo suala la mjadala. Lakini linapokuja suala la kusitisha kupeleka umeme vijijini kwa sababu menejimenti ya kigeni, masharti ya kuingia mkataba na Serikali yetu, kuwa ukisitisha umeme kupeleka vijijini basi itakuwa tayari kuchukua shirika lenu kuliendeleza.

Sasa mimi ningeomba kuelezwa hivi inapofanyika hivi pasipokuwa na taasisi mbadala kama *TANESCO* ambayo ilikuwa inaendeleza umeme kabla ya Waheshimiwa hawa wageni kuchukua menejimenti ya *TANESCO* ulikuwa unakwenda kasi sana vijijini, lakini wakasitisha moja kwa moja. Tunajua wote kuwa *TANESCO* inafanya kazi ya kuendeleza sekta mbalimbali kwa kuzalisha nishati ambayo inahitajika kwa matumizi ya binadamu na pia inafanya biashara. Sasa suala la kuwa menejimenti mpya ilipokuja inataka tu ile sehemu ya biashara na siyo sehemu ya kuendeleza nchi maana yake nini? *(Makofi)*

Leo huwezi ukanieleza kuwa unasisitiza maendeleo katika sekta mbalimbali vijijini pasipokuwa na umeme. Nishati gani itatumika kwenye kilimo kwa ajili ya kusukuma maji kupeleka mashambani? Nishati gani itatumika kusukuma maji kutoka mabwawani au visimani kwenda majumbani kwa wananchi kusudi kuboresha huduma za maji kwa watumiaji wa vijiji? Nishati gani ambayo wananchi wa vijijini watatumia kama taa?

Mheshimiwa Spika, athari za kusitisha kupeleka umeme vijijini maana yake ni kuwa kwanza, ni kuchochea vijana na wananchi wengi kukimbia kutoka vijijini kwenda mijini au mahali penye umeme. Athari ya pili, ni kuwalazimisha wananchi au kuhakikisha kuwa wananchi giza linapoingia wasiweze kufanya lolote ila kufanya kazi moja tu, kuongeza idadi ya watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa ikiwa kutakuwa na ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, itakuwa suala la kukua tu na siyo kwa kuendelea kwa sababu idadi ya watu wanaongezeka, idadi ya watu wanazidi kumiminika mijini na mahali penye umeme. Sasa huko vijijini pataachwa na nani wa kufanya hiyo kazi na nguvu kazi inahama inakwenda mijini? Kwa sababu kilichobaki ni wanyamakazi kama punda, ng'ombe na mbwa. Sasa kama wanyamakazi nao wataamua kwenda mijini nani ataendeleza sekta za maendeleo na za kijamii vijijini kwa sababu giza limewashinda? *(Makofi/Kicheko)*

Mimi ninavyoona kwa kweli hiyo, sijaona kwa sababu hata ikiwa tuna taasisi tunazoziunda kama *Rural Energy Agency* na *Rural Electrification Fund* hizo bado zinaundwa. Inakuwaje leo tunasema kuwa tunasitisha na bado hatujaunda zile taasisi?

Mheshimiwa Spika, leo tunaambiwa katika ukurasa wa 10 ibara ya 18 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuwa taasisi hizi bado zinaandaliwa na palifanyika semina kuonyesha kuwa maandalizi yanaendelea.

Mimi ningeshauri kuwa *TANESCO* iendelee kusambaza umeme vijijini wakati taasisi hizi mbili zinaundwa na kukamilishwa kwa sababu hata baada ya kukamilisha kuziunda zitahitaji uzoefu. Kwa hiyo, itakuwa ni lazima wakati mwingine hata zikiundwa taasisi hizi kama *Rural Electrification Fund* itahitaji labda kwenda pamoja na miradi mingine ya *TANESCO* ambayo ni mikubwa, *project joint financing* labda hata kupata *technical assistance* kutoka *TANESCO* kwa sababu *REA/REF* zitakuwa bado changa. Sasa inaachwa inakuwa *(gap)* pengo kabisa, sasa asilimia 80 ya wananchi wa vijijini wameachwa gizani.

Pili, mimi nataka kuongelea suala la umeme Wilaya ya Iramba. Wilaya yangu karibu nusu ya *line* za umeme ambao unakwenda Mwanza, Shinyanga na huko Kanda ya Ziwa zinapitia katika Wilaya ya Iramba. Lakini ukiona umeme ambao sasa wananchi wanautumia ni vijiji vichache sana vimepewa. Kuna vijiji vingine ambavyo vilichangamka sana baada ya kuhamasishwa vikapeleka maombi na vingine vikalipia, lakini kwa sababu zisizoeleweka vijiji hivi havijapewa umeme.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kuondoa utata wa Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Singida arejeshwe kwa wakuu wake kule Dar es Salaam kwa sababu yeye anafikiri kuwa kuwapelekea wananchi umeme vijijini ambako wanastahili kupewa ni kama upendeleo, siyo haki yao. Kwa hiyo, ningeomba huyu meneja aondolewe, hatufai sisi aende kule ambako atawafaa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo vimelipia na vingine vimeomba, ni haki yao vipate umeme viko kama sita hivi, lakini mpaka leo vinazungushwa tu havijapata umeme. Kuna Mji Mdogo wa Kinampanda ambao umeme wa grid uko tayari, lakini *TANESCO* iliahidi kuwapa *transformer* ya kutumia kwa pampu ya kuvuta maji kwa kijiji kile na Chuo cha Walimu na Sekondari ya Tumaini na wanakijiji. Lakini mpaka leo hawajapewa.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, kama itawezekana aingilie kati suala hili kwa sababu vyuo vilivyopo pale ni vya Kitaifa na wananchi wengi wanahitaji maji. Kwa hiyo, *transformer* hiyo inunuliwe na iwekwe. Pia kuna Mji Mdogo wa Ndago, wana bwawa lao ambalo maji hayawezi kufika kwenye Mji Mdogo wa Ndago lakini panahitajika *transformer.* Wananchi wamejaribu kuchanga fedha lakini mpaka leo wanazungushwa na hii ndiyo kazi ya huyu Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Singida ambaye anapenda kuzungusha watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Iramba haina mgodi wa madini, lakini ina mgodi mmoja tu ambao ni Ziwa la Kitangiri. Ziwa hili linazalisha samaki wengi na wako wa aina nyingi sana. Kuna wavuvi kutoka sehemu nyingi za nchi hii. Wengine wanatoka hata

Kenya na Uganda kwa sababu samaki wanaopatikana pale wana soko zuri sana Dar es Salaam, Nairobi, Kisumu na Kampala. Wananchi wa Wilaya ya Iramba walikuwa wameomba wapelekewa umeme kwa sababu samaki wale inabidi wakaushwe kwa mafuta ndiyo wapelekwe kwenye masoko.

Kwa hiyo, naomba umeme upelekwa kwenye Ziwa la Kitangiri, kwa sababu Ziwa la Kitangiri ni kama mgodi wa Wilaya ya Iramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kuhusu madini. Kuna Kampuni ya *Barrick International* kwa miaka mingi sana imekuwa inatafuta dhahabu katika Wilaya nzima ya Iramba na tulisikia wanasema kuwa wameona kuna dhahabu nyingi, lakini kuna usiri mkubwa, hawajaweza kutuambia, baada ya kumaliza utafiti wao wakachukua mawe na udongo kama tani moja au mbili, wakaondoka nao wakasema wanakwenda kufanya utafiti zaidi na hatujasikia lolote mpaka leo.

Kwa hiyo, tungeomba Mheshimiwa Waziri, atueleze huu usiri kama ule udongo kama kulikuwa na dhahabu waturudishie basi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho mwaka 2003 tulifanyiwa semina hapa na Shirika la Maendeleo la Petroli *(TPDC)* tukaambiwa kuwa mafuta (petroli) tunayonunua hapa ni ya hatari sana na tulimwomba Waziri aliyekuwepo kwenye semina ile atoe tamko hapa Bungeni hakufanya hivyo. Nasikia haya mafuta yananunuliwa melini *in high seas,* ni mafuta ambayo hayatakiwi mahali popote duniani lakini yanaletwa na ndiyo maana kimekuwa chanzo cha kuua *TIPPER.* Mafuta haya ni hatari, yana madini ambayo ni hatari kwa afya za binadamu hasa kuvuta moshi unaotokana na magari.

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, atoe tamko hivi kwa nini sisi tununue mafuta ya hatari namna hii wakati mahali pengine yanakataliwa na sisi tujihatarishe kwa sababu ya umaskini wetu au kwa sababu ya kupata rahisi? Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze haya mafuta yanayonunuliwa *from high seas,* kwa nini sisi wenyewe tusiweze kusafisha mafuta au tufufue *TIPPER? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kumalizia kwa kusema kuwa mimi naunga mkono hotuba hii, lakini masuala ambayo yanayoletea vijijini kuwa giza na mijini na mahali pengine pawe na umeme inakuwa ni ubaguzi usioeleweka. Wote tunataka maendeleo na wote hatuna uwezo wa kukaa mijini. Tunataka maendeleo vijijini na vijijini ndiyo vinavyolisha mijini. Sasa kama *TANESCO* itaendelea kuhudumia vijijini ni vema wakati Serikali inaunda ule mfuko au wakala wa umeme vijijini ambao wanatarajia, ningeomba hii kazi iendelee, lisiwe suala la kuwanyima umeme wananchi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii, ili nichangie Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi ngumu wanayoendelea kuifanya na nzuri katika Wizara hii. Aidha, nawapongeza kwa hotuba yao nzuri inayotia matumaini katika kipindi kijacho na kwamba tuna matumaini wanaweza wakafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu ni suala la lazima katika uhai pia wa nchi yetu kiuchumi. Hii ndiyo maana utaona kwamba wachangiaji na wananchi wengi wanajua kabisa kwamba umeme ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo na wengi wetu tunapochangia tunazungumza kwa uchungu sana tukisisitiza kila mtu hitaji hili la umeme ili apate katika eneo lake kwa maana hiyo. Kwa sababu ya uzito huo ndiyo maana utakuta kwamba, Wizara hii utadhani labda inasongwa songwa sana. Lakini hii nataka nieleze kwamba ni kiu ya wananchi kwa kutambua umuhimu wa suala hili la nishati ya umeme ndiyo linalowapelekea kuzungumza kwa uchungu wa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nianze mchango wangu kwa kuzungumzia miradi ya kupeleka umeme vijijini, hasa katika Makao Makuu, kuanzia Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu ningependa kuiomba Serikali kwamba tunao mpango wa kufanya eneo la Iselemagazi kama Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Shinyanga Vijijini mara baada ya mgawanyo wa Wilaya ya Shinyanga. Sasa kwa mipango iliyokuwepo ya *TANESCO,* ulikuwepo mpango wa kupeleka umeme katika *Sangu Ginnery* iliyoko Wilaya ya Kwimba, mradi huu ulifanyiwa kazi kwa kipindi cha mwaka 2002, lakini bahati mbaya watalaam walitoa taarifa kwamba mradi huo hautalipa au siyo *viable* kwa hiyo wakasema labda ni vizuri itazamwe njia nyingine.

Nilitaka kutumia nafasi hii basi kushauri Wizara, ipitishe umeme katika maeneo yafuatayo ili pengine kukidhi haja hiyo ya kuufanya mradi huu uweze kulipa. Napendekeza maeneo yafuatayo yapitishiwe katika mradi huu ili kuweza kufanikisha. Maeneo hayo ni Pandakichiza, Shilabela, Mwang'osha, Mwamakaranga, Iselemagazi yenyewe, Mahigana, Mwabenda, Solwa, Salawe na baadaye sasa *Sangu Ginnery.* Hii nina hakika kwamba kwa kweli itasaidia kuwafanya wananchi wa maeneo haya ambayo ni muhimu na wana kiu kubwa ya kupata umeme huu waweze kunufaika na mpango huu. Haya ni maeneo ambayo nilifikiri kwamba nishauri Wizara iyafanyie kazi kwa maslahi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuzungumzia ni juu ya Nishati mbadala ya umeme. Wachangiaji wengi wamezungumza juu ya suala hili na mimi nakubaliana nao kwamba kwa kweli umeme unakuwa ghali sana kwa kutumia njia hizo za nguvu ya maji au mafuta. Lakini nilifikiri kwamba kwa umeme wa kuendesha mitambo unaweza ukabaki kutumiwa huu, isipokuwa sasa Wizara ikatazama kwamba kwa umeme wa matumizi ya kawaida ni vizuri wakajielekeza katika kutumia nishati mbadala ya kutumia umeme wa jua, kutumia *bio gas* ambazo nina hakika kwamba gharama yake inaweza ikawa nafuu zaidi ukilinganisha na njia zingine hizi za upatikanaji wa umeme. Hii ingeweza ikasaidia kwa kweli kukidhi angalau kiu ya wananchi katika maeneo mbalimbali hasa vijijini kuliko kutegemea tu umeme huu ambao uzalishaji wake unakuwa ni wa ghali na matokeo yake hatuwezi kuwafikishia wananchi wote kwenye maeneo yote kama ambavyo azma yetu ya Taifa letu kuwapa huduma hii.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri ni vizuri tulitazame hili la kutumia nishati hiyo. Lakini ili kupata nishati nyingine kubwa zaidi tulikwishaelezwa hapa na semina ilifanywa na watalaam wetu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, wakati nadhani tunapitisha pia suala zima la sheria ya kutumia nguvu ya *atomic* kwamba nchi yetu ina

madini ya *Uranium* ambayo yanatumika sana katika kuzalisha *neuclear energy* karibu robo tatu ya nchi yetu na kwamba inahitaji kujenga mtambo mmoja tu katika nchi yetu ambao ungeweza ukatosheleza kabisa mahitaji makubwa na madogo ya nguvu ya umeme katika kuondoa tatizo hili na wao walituambia inahitajika kutumia matumizi salama ya kiasi cha 0.03% ambayo ingeweza ikatusaidia kuzalisha umeme ambao ungeweza ukakidhi mahitaji yetu.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwa nini basi labda Wizara pia isijielekeze katika hali hiyo katika kutafuta wawekezaji wa namna hiyo ambao wanaweza wakatusaidia kutumia nishati hiyo licha ya kwamba tuna hilo suala la makaa ya mawe ambalo wengi wamelizungumzia, nayo ni moja ya njia ambayo ingeweza ikatusaidia kuzalisha umeme wa uhakika. Kwa hiyo, mambo haya ambayo tunayapendekeza tulifikiri Wizara, ijitahidi kuyatumia ili kutupatia huduma hii ya umeme ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni suala la uongozi uliopo *TANESCO.* Wazungumzaji wengi wamezungumza juu ya nini kimefanywa na *TANESCO,* ni kweli kwamba katika sera yetu ya uwekezaji moja ya mambo ya msingi ambayo yanafanya tuelekee katika uwekezaji na kuhitaji watu mbalimbali ni suala la upungufu katika uongozi, upungufu katika mitaji, upungufu katika teknolojia. Sasa inawezekana katika *TANESCO* eneo la uongozi ndilo lililoonekana kwamba kuna upungufu na kwa hiyo, tukapelekea kubinafsisha au kuhitaji watu watusaidie katika eneo hilo. Mimi nakubaliana na uamuzi huo, ni sahihi. Lakini yako malalamiko ambayo ni dhahiri yanaelezwa na watumishi kwamba iko tofauti kubwa mno ya malipo ya watumishi kati ya uongozi wa *NetGroup Solution* pamoja na watumishi wengine wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tofauti hii siyo tu kwamba inalalamikiwa, lakini mimi naiona kwamba inajenga chuki katika sekta hii kwa sababu baadhi ya watumishi wanajiona wanyonge katika nchi yao na hasa inapotokea kwamba watu ambao wanafanya shughuli hizi ni wageni basi watumishi wengine wanajihisi kama wao ni watumwa katika nchi yao. Siyo maneno mazuri sana, lakini ni tafsiri kila mtu anaweza akatafsiri anavyoona.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri suala hili la malipo ya watumishi likatazamwa vizuri, kwa nini watu wengine wapewe kiwango kikubwa kuzidi watu wengine na wote wanafanya shughuli ile ile na mahitaji ni yale yale na pengine hata kiwango cha elimu ni kile kile? *(Makofi)*

Sasa kama tulifikiri kwamba labda tunahitaji kuwaboreshea mapato ili watu wafanye uongozi vizuri zaidi, ingetosha kuwafanyia hata wale waliokuwepo wakapewa malipo mazuri zaidi na wakafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kwamba mwelekeo wa uongozi huu sasa umejielekeza katika kukusanya mapato peke yake. Mimi sidhani kama wamefanya mambo mengine mazuri zaidi katika uzalishaji wa umeme wenyewe, kwa sababu kama mahitaji ya umeme ni makubwa, basi nguvu kubwa ingeelekezwa katika uzalishaji wa umeme maana kama makusanyo yanasemekana ni makubwa kama ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri ilivyooeleza kwamba wamefanikiwa kwa kiwango kizuri kukusanya fedha vizuri zaidi, lakini bado hata hivyo haikutosheleza. Maana hivi juzi tulipitisha hapa fedha ya kusaidia *TANESCO* kutoka kwenye mfuko wetu wa Serikali. Kwa hiyo,

nashauri kwamba mtazamo mkubwa uwe katika kuelekea kwenye uzalishaji wa umeme zaidi pengine badala ya kukusanya mapato tu.

Lakini pia kwenye usambazaji, liko tatizo moja linalojitokeza kwamba watu wanahitaji kuunganishwa au kupatiwa umeme lakini matatizo yanayoelezwa ni kwamba shida ni vifaa kama mita. Lakini tukumbuke kwamba mita nyingi sana zimefungwa, ambazo ziko kwa wananchi mbalimbali ambao wameshindwa kuendelea na huduma hii ya umeme. Sasa mimi naona liko tatizo moja kwa *TANESCO* kwamba wao wakishampata mteja wakamfungia mita, akishindwa kulipa, wanaiacha hapo wanaendelea kudai tu. Kwa hiyo, mteja mpya ambaye ana uwezo anahitaji mita, wanasema hatuna mita.

Sasa nilikuwa nashauri kwamba kwa nini msizikusanye mita ambazo watu wameshindwa kuzifanyia kazi halafu mkawafungia wateja wapya na huyu mnayemdai mkaendelea kumdai? Kwa sababu kama *record* zipo, kuna sababu gani ya kutumia mita mpya tu halafu huyu ambaye ana mita ya zamani mnamwachia na halipi inakaa pale miaka miwili au mitatu? Mimi nafikiri huo sio uamuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalotaka kuchangia ni eneo la uwekezaji wa migodi katika uchimbaji wa madini. Wachangiaji wengi wamekwishaeleza tatizo tulilonalo. Mimi nataka kusema maeneo matatu katika eneo hili na la kwanza ni juu ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu waliopendekeza kwamba Mikataba mingine itazamwe upya. Kama kuna haja ya kuifanyia *review* Mikataba hii, nafikiri litakuwa ni suala la hekima tu, hatuwezi kushindwa kusahihisha suala hili kama tunadhani kuna makosa fulani fulani yamefanyika. Inasikitisha kuona maeneo mengine hasa katika Mikataba ya mwanzo kabisa, mgodi ambao uko karibu sana na nilipo ni mgodi wa *Williamson Diamond,* watu wale wanaonekana kama wao walikuja kufanya biashara tu. Inashangaza kuona kwamba watu wanachimba mpaka Uwanja wa Ndege, wanavunja mpaka shule, eti kwa sababu wao wanafanya uchimbaji wa madini na kwa hiyo, mambo mengine haya sio shughuli yao, wao wamekuja hapa kibiashara.

Sasa kama hata huduma za jamii zinakuwa hazitiliwi uzito, siamini kama kwa kweli hii inaleta picha nzuri kwa jamii. Wanafunzi wanasoma katika mazingira yale yale kwa miaka kumi, lakini anakuja mwekezaji pengine anavunja shule ili watu wahame pale waende kuitafuta shule kilometa tano kutoka eneo lile. Huu sio uwekezaji mzuri kwa kweli! Kwa hiyo, mikataba hiyo itazamwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalopenda kuchangia ni suala la mrabaha. Hili ni suala ambalo limeshaelezwa kwa kina na wenzangu na mimi bado naendelea kusema kwamba kwa kweli tunaishauri Serikali ione umuhimu. Maana yake kilio cha mtu mzima lazima kina jambo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wengi, wakieleza juu ya umuhimu wa suala hili, mimi nadhani Serikali yetu ni sikivu, inaelewa na inatafuta utaratibu wa kutatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba ipo Tume imeundwa, hili ndio la tatu nataka kusema katika eneo hili. Tume hii mimi nilikuwa nafikiri inakusanya maoni kweli na bahati nzuri mimi nimeshiriki katika wadau waliokuja kuombwa ushauri.

Ninachotaka kuishauri hiyo Tume kabla haijamaliza kazi yake kwamba, waache mtindo wa kutupa majibu au maelezo ya uzuri wa mfumo uliopo kwa sasa ila wasikilize maoni ya wadau. Nilichojifunza ni kwamba, wao katika kutaka maoni ya wadau, bado tena wanatoa maelezo kwamba, unajua hii iko hivi!

Kwa mfano, ilitoka hoja pale tunaelezwa tunataka kufahamu juu ya mchanga ambao unakwenda nje ya nchi yetu. Wao wanasema, unajua ule mchanga ukishafika kule ukionekana sijui una madini ya hatari zaidi, bado Serikali inaweza ikadaiwa tena kiasi fulani. Sasa mimi sikuelewa kwa kweli kwamba sasa tena ninyi ndio mnaanza kueleza juu ya kwamba sisi tunaweza tukadaiwa pia katika suala hili la mchanga na kwamba kwa hiyo, ukienda kule, ukionekana una matatizo usidai hata kulipwa. Haya ni maelezo yanayokatisha tamaa hata wale wadau wanaotoa maoni wasitoe maoni basi kwa maana ya kuboresha.

Kwa hiyo, nashauri wajitahidi kukusanya maoni ya wadau, wanahitaji mambo gani yarekebishwe ili kuboresha suala hili zima la sekta hii ya madini katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda tena kurudia kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nawapongeza Waziri na watendaji walioko chini yake. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa niaba ya wananchi Wilaya ya Simanjiro na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, natoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kufiwa na mwakilishi wao, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa neno lililopo ukurasa wa saba kwa kuahidi kwa maandishi kwamba watapeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, Orkesumet.

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yangu zaidi, najikita kwenye Ilani Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Uchaguzi Mkuu Oktoba 2000 Ibara ya 25 (4) kinachosema sheria mpya ya madini iliyokidhi haja ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kupata mitaji, zana na soko iliandaliwa na kupitishwa na Bunge mwaka 1999. Halafu ibara ya 26(2) inasema: "Kuihimiza Serikali kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kama ifuatavyo:- Kuandaa mipango ya kuwawezesha kupata zana za kisasa, kuwapatia elimu ya kisasa juu ya madini na uchimbaji wake pamoja na kuwahakikishia masoko na kurekebisha mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitakayokuwa naeleza, nakuomba wewe na Waheshimiwa Wabunge, walinganishe kama yanafanana na yaliyoko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

**MBUNGE FULANI:** CCM oyee!

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, pia hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 45 ambayo ameeleza kwamba: "Wizara imeendelea na juhudi za kuongeza

udhibiti katika machimbo ya *Tanzanite* Wilayani Simanjiro," maelezo yangu yatadhihirisha kama ameendelea kudhibiti hali ya *Tanzanite* pale ama hawakudhibiti.

Mheshimiwa Spika, *Tanzanite* ni madini yanayopatikana Tanzania peke yake duniani kote. Naomba nitakapozungumza Wabunge wanielewe kwa sababu Mheshimiwa Rais aliwahi kusema Mererani ni Tanzania ndogo kwa maana kwamba Watanzania wote unaweza ukawakuta pale Mererani. Kwa hiyo, baya lolote walilofanyiwa Wanamererani huenda ni wa Jimbo lako.

**MBUNGE FULANI:** Eeh, sawa. Wapo! *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, hili suala la kusema Serikali inawasaidia wachimbaji wadogo wadogo kwa suala la *Tanzanite* halipo, wala haiwasaidii. Zana za uchimbaji wanapata kwa kutafuta wenyewe kwa bei ya soko. Sijui kama maeneo mengine wanasaidiwa. Badala yake wanasaidiwa wachimbaji wakubwa kwa kupewa maeneo makubwa na kupewa ruzuku kwa kigezo cha kusema *tax holiday* na hawa ni wajanja kutumia nafasi hiyo. *(Makofi)*

Kwa mfano, waliwahi kupewa watu wanaosema wanachimba *Graphtan.* Kipindi chao cha *tax holiday* kilipokwisha, wakamkabidhi mtu mwingine anaitwa *Sumax,* huyo muda wake ulipokwisha wakamkabidhi mtu anayeitwa *AFGEM.* Kwa maana hiyo, kwa miaka karibu 30 Serikali haijapata kodi kwa sababu ya nafasi hiyo. Sasa kwa nini tunakubali kuwapa wageni tusiwape wachimbaji wetu?

Kama tunawaondolea kodi hao wachimbaji wakubwa, tuwaondolee pia hawa wachimbaji wadogo. Hata hivyo kwa *Tanzanite* hakuna mchimbaji mkubwa na mdogo, kwa sababu kama mchimbaji mkubwa atatumia *carton* kadhaa za fataki kupata *Tanzanite,* hata huyu mdogo atatumia kiwango hicho hicho. Kama atapata kwa mita 200, hata huyu mdogo atapata kwa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha zaidi ni kile kifungu cha pili katika ibara ya 26 ya Ilani ya Uchaguzi ya kujaribu kutatua migogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo. Hawa wachimbaji wakubwa hasa walioko pale Mererani wamekuwa kama miungu watu na hasa kwa kuwanyanyasa Watanzania ambao ni wachimbaji wadogo wadogo. Nitoe mifano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Januari, 2000 waliwang'atisha mbwa ndugu Raymond Masele, Almasi Juma, Lazaro Charles, Ali Bakari, Juma Amiri na Nordin Contry, wengine kutoka Iramba, wengine kutoka Mbozi, wengine kutoka Kagera. Tarehe 10 Novemba, 1999 walimpiga risasi Mohamed Ali Selemani, tarehe 15 Novemba, 1999 walimjeruhi kwa risasi Khalid Ramadhani, Matei Lukas na Kisauti, Tarehe 11 Novemba, 2003 walimpiga risasi Nels Stephano na amefariki dunia.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Novemba, 2003 walimpiga risasi Joseph Paulo, kwa anayemfahamu nyie mnaotoka Simanjiro yule mnayemtania Mwanya. Kama mliwahi kuona picha zilizoonyeshwa, risasi zilivyozagaa mgongoni mwa mtu na wamempiga ndani ya mgodi na sheria hairuhusu mtu kuingia ndani ya mgodi na silaha lakini hawa wanaruhusiwa kwa sababu ni wageni, kwa sababu ni wawekezaji wakubwa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aah, unaona sasa!!

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Spika, mwezi wa Februari, 2004 walimpiga risasi Ramadhani Mohamed na amefariki dunia. Risasi tatu kifuani! Unapiga risasi juu kumtisha mtu, unamvunja mguu; lakini kifuani risasi tatu. Tarehe 30 Juni, 2004 wamemjeruhi Emmanuel Mosses ambaye bado yuko hospitalini Mluzi.

Mheshimiwa Spika, hivi hata kama hawa hawashtakiwi, hata kuwafutia leseni haiwezekani? Tanzania inasifiwa sana kwa ukombozi wa Afrika. Sifa tuliyonayo Tanzania ni kukataa manyanyaso ya Waafrika na hasa Watanzania. Hapa tunakataa nini? Inashangaza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama huo ndio utatuzi wa migogoro kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo, naomba niulize maswali niliyouliza tena juzi, nihakikishiwe leo na Waziri kama hawa wawekezaji wa *AFGEM* wako juu ya sheria, anieleze kama wana haki wao kuchukua sheria mkononi na anieleze watachukua hatua gani.

Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tusipojibiwa hivyo, leo tusikubali. Tusikubali Wanasimanjiro peke yao, hata kama ni Wanasimanjiro peke yao lakini ni Watanzania yaani Tanzania tumefika mahali pa kuthamini hela kuliko maisha ya Watanzania? Nadhani ujumbe umefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui kwa nini tunatumia fedha za walipa kodi wa Tanzania kuunda Tume za gharama kubwa na zinazofanya kazi ambazo hatuzithamini. Waziri wa Nishati na Madini aliwahi kuunda Tume ya *General* Robert Mboma na Mheshimiwa Eliachim Simpasa alikuwepo. Nilimsikia siku moja akiwaomba radhi wananchi wa Jimbo lake la Mbozi Magharibi kwamba hakuwepo kwa sababu alipewa na Taifa kufanya kazi hiyo. Sasa mbona ripoti hiyo haijafanyiwa kazi? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rushwa hiyo!

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Nafikiri haijafanyiwa kazi kwa sababu ya sentensi ya mwisho waliyoandika Tume hiyo. Tume hiyo ilisema, "Tume ina maoni kwamba kwa sababu Tanzania imebahatika kuwa nchi pekee duniani inayozalisha madini ya *Tanzanite,* ingekuwa vyema na busara sana kuwaachia wachimbaji wadogo wadogo wa Tanzania kuchimba madini hayo ambayo hayana ushindani sana kwenye soko la Kimataifa ili wengi wao waweze kuwezeshwa kiuchumi." Hiyo ndiyo Serikali haitaki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunadai taarifa hiyo iletwe Bungeni ili tuijadili na kuiwekea maazimio. La sivyo, naye Mheshimiwa Eliachim Simpassa wananchi watafikiri alikwenda tu kufurahia *Tanzanite. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado Tume ya Mheshimiwa Mang'enya, ilisema katika majumuisho yake: "Sera na sheria zirekebishwe ili kuzuia wawekezaji wageni kujihusisha na shughuli za utafutaji wa uchimbaji wa madini ya vito nchini kama ilivyo kwa nchi ya Srilanka." Nawaomba Wabunge wenzangu tusikubali kupitisha Bajeti hii bila Waziri kuahidi kwamba ataleta marekebisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka. Kwa hapo Mererani, bado nasema Serikali iliahidi Mererani kuwa *EPZ.* Sasa nasikia fununu zinazosema huenda ikahamishwa kupelekwa kwingine. Hiyo hatukubali Wanamererani na Wanasimanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la ugomvi wa madini Losokonoi. Namshukuru Mheshimiwa Daniel Yona na Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hatua waliyoichukua kumnyima huyo kupora ardhi hiyo. Ni mwekezaji anayetoka tu mita 500 kutoka mpaka wa Tanzania anataka kuchukua vyanzo vya maji tisa na ardhi ya mifugo. Wananchi wa Losokonoi, Simanjiro wamenituma niiambie Serikali ardhi hiyo haiendi kwa gharama yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la umeme Makao Makuu ya Wilaya. Serikali iliwahi kutuandikia hivi hivi kwenye hotuba ya Bajeti na hatujaona umeme mpaka leo, tunataka safari hii Serikali itimize lengo hilo. Mnaposema Sweden itasaidia, kuna msemo unasema: "Ukienda kuomba mboga uwe na yako iliyochacha." Sasa muweke angalau yenu hata mkiwakosa Wafadhili msikwame kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kupata maji tusipopata umeme, lakini tukipata umeme nadhani Mheshimiwa Edward Lowassa, utatuahidi kutuletea maji kutoka Nyumba ya Mungu au Mto Pangani kama mlivyofanya maji ya Chalinze. Lakini hatuwezi bila umeme. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapo-*wind up* anihakikishie yafuatayo, kwamba msaada utaletwa wa kusema Watanzania pekee ndio watakubaliwa kuchimba madini ya vito, pili, ahaidi kwamba ataleta taarifa ya *General* Robert Mboma tuijadili hapa Bungeni, tatu, anihakikishie kwamba *EPZ* itakayoanzishwa kwa ajili ya kukata madini itakuwa pale Mererani, nne, anieleze kwamba umeme utakuwa Makao Makuu na eneo la Losokonoi wale wachimbaji waendelee kumiliki mita zao 300 kwa 300, lakini zaidi ya hapo hawatapata hata nchi moja. Kwa nini ugomvi haukutokea wakati wakichimba akina Titus na Ali? Ni kwa sababu ni Watanzania! Sasa mtu akitoka tu mita 400 kutoka mpakani anaitwa mwekezaji hata kama hana sifa hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anihakikishie pia na hilo ameliweka vizuri, aendelee kushikilia uamuzi huo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho wananchi wa Mererani waliwahi kumwomba Mheshimiwa Rais awaongezee Kitalu A na C. Hilo limezimwa. Sasa wananchi wa Mererani, sio mimi, wanafikiri hivi hii Mererani ni kidali cha wakubwa kwamba sisi hatuhusiki? Wadogo hatupewi maeneo hayo! Hata kama walipewa *Block B,* lakini ni eneo lao na ni madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nitaunga mkono hoja hii Waziri atakaponikubalia hayo niliyomweleza. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba nitoe rambirambi kufuatia kifo cha Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nakusudia kuzungumzia kuhusu tatizo la ukosefu wa umeme katika Mikoa ya Kusini, Lindi, Mtwara na Ruvuma. Naiomba Serikali itafute njia ya uhakika ya kuwapatia umeme wananchi wa Mikoa hii ya Kusini. Wizara hii kila mwaka inaleta mpango mpya kupitia bajeti yake ilimradi inayumbisha kwa makusudi kabisa na kutaka umeme uchelewe kwenda Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, kupitia hotuba ya Waziri ukurasa wa 13 naomba ninukuu Wizara ilitamka kwamba: "Aidha, Wizara yangu kwa kuitumia *TANESCO* imefanya uchunguzi wa awali wa gharama za mradi mbadala wa kuzalisha umeme Somanga Funga Wilayani Kilwa kwa kutumia Gesi ya Songosongo na kusafirisha umeme huo hadi Mikoa ya Lindi na Mtwara. Baada ya matokeo mazuri ya uchunguzi huo, Benki ya Dunia imekubali kutoa fedha kwa ajili ya kuufanyia mradi huo upembuzi yakinifu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu katika ukurasa wa 23 naomba ninukuu, Serikali inasema: "Serikali ina matumaini makubwa kwamba Mradi wa Gesi ya *Mnazibay* utafanikiwa. Hata hivyo endapo matokeo ya uhakiki wa Gesi hii ya *Mnazibay* hayataridhisha, Serikali inakusudia kutumia njia nyingine ya kuwa na umeme wa uhakika katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Njia hiyo ni kujenga Kituo kikubwa cha kuzalisha umeme Somanga Funga kwa kutumia Gesi ya Songosongo na njia ya umeme ya *kV132* ya kusafirisha umeme huo kutoka Somanga hadi maeneo husika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kila mwaka tunapewa njia nyingine kwamba umeme utapatikana kwa njia hii, umeme katika Mikoa ya Kusini utakwenda kwa njia hii. Mimi hapa naona uhakika wa Gesi ya *Mnazibay* hakuna kabisa. Kama mwaka 2003 waliamua gesi hiyo itoke Songosongo wajenge kituo kikubwa Somanga Funga, kwa nini mwaka huu wabadilishe wapeleke *Mnazibay* tena?

Mimi ningeomba Serikali sasa hivi itoe tamko rasmi kwamba umeme katika Mikoa ya Kusini utapelekwa kwa kutumia njia gani? Sio kila mwaka wanatupeleka huku, wanatupeleka huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kuna jambo gani hasa Mikoa ya Kusini isipate umeme? Kwa sababu tuna njia nyingi za kupatia umeme. Kuna njia ya kwanza ya kutumia Gridi ya Taifa. Hiyo imezungumzwa, imekufa, tulikuwa na mategemeo makubwa katika Gesi ya Songosongo, lakini bahati nzuri mradi huo wa Songosogo pesa zilibakia tukawa na matumaini makubwa kwamba pesa zilizobakia sasa zingeweza kutumika kujenga Kituo pale Kilwa ili kupeleka umeme Mikoa ya Kusini. Lakini pesa hizo sasa hazijengi Kituo hicho ambacho kiliahidiwa mwaka 2003, zinafanya ukarabati katika njia za umeme ya kupeleka Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna njia ya *Mnazibay* ambayo sasa hivi pia haina matumaini, lakini kama Serikali itafanya kweli, basi ihakikishe kwamba inafanya kweli. Lakini mpaka sasa hivi kuna utaratibu kwamba mpaka wahakiki kwanza gesi

iliyokuwepo. Sasa Gesi ya Songosongo ipo tayari na pesa zimebakia, kwa nini wangoje kuihakiki kwanza Gesi ya *Mnazibay* ndio wawe na utaratibu wa kupeleka umeme katika Mikoa ya Kusini? Kwa nini sasa wasijenge Kituo kwa pesa zilizobakia wakaachana na habari ya *Mnazibay?*

Mheshimiwa Spika, tunayo njia nyingine ya makaa ya mawe, lakini hiyo imezungumzwa na sasa inaonekana haina mategemeo tena. Lakini kuna njia nyingine ya kupata umeme kutoka katika nchi jirani, kama walivyopatiwa wenzetu katika maeneo mengine. Nchi ya Msumbiji ina umeme wa kutosha, lakini hakuna utaratibu unaofanywa na Serikali ili kutupatia umeme kutoka katika nchi hii jirani kama ilivyofanywa katika Mikoa mingine. Mkoa wa Bukoba wanatumia umeme kutoka Uganda, Mkoa wa Rukwa wanatumia umeme kutoka Zambia, sasa kwa nini Mikoa ya Kusini isipatiwe umeme kutoka Msumbiji? Njia hizo zote kila siku inatajwa hii, inaondolewa, inakuja hii inaondolewa. Sasa Wizara ya Nishati na Madini inaonesha kabisa kwamba haiwatendei haki wananchi wa Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iepuke lawama kwa sababu kama wananchi wa Kusini wataendelea kukosa umeme wa uhakika, lawama ya sasa itakuwa nzito kwa sababu umeme wa Gridi umeanzia Mikoa ya Kusini (Kidatu), lakini Serikali imeweza kuchukua umeme wa Gridi kutoka Kidatu ukaenda mpaka Musoma na Arusha ikashindikana kupeleka Mikoa ya Kusini na mpaka sasa hivi hawapeleki!

Lakini tendo la leo la kuchukua gesi ya Songo Songo kutoka Kilwa Mkoa wa Lindi ije Dar es Salaam itengeneze umeme, igawe tena kule kule kulikowekwa umeme mara ya kwanza na wenyewe wa Kusini wasiitumie gesi hiyo, hiyo ni lawama isiyoepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni lawama kubwa ambayo kwa kweli, ni lawama ambayo ni nzito. Sasa naiomba Serikali irekebishe, iondoe hiyo lawama. Sasa inatuyumbisha gesi ya *Mnazibay,* gesi ya Songosongo sasa itafute njia gani? Watatupatia umeme wa uhakika katika Mikoa ya Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba mbinu zilizotumika kupeleka umeme katika Mikoa ya wenzetu, hizo mbinu kwa nini zisitumike kupeleka umeme katika Mikoa ya Kusini? Kutoa umeme Kidatu kupeleka mikoa mingine mbinu zimetumika nzuri na wenzetu wamepata umeme. Gesi ya Songosongo leo inatoka na kutumia umeme kutoka katika nchi zingine wenzetu wamepata umeme. Sasa mbinu hizo zote zilizotumika, ningeomba Serikali sasa ifikie mahali itumie hizo mbinu na itoe njia ya uhakika, watuhakikishie njia ya uhakika kwamba umeme utafika Mikoa ya Kusini kwa kutumia njia hii isiwe mwaka huu wanatupa njia hii, mwaka mwingine wanatupa njia hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka huu hatuna uhakika kabisa kwa sababu kitabu hiki kinasema kwamba tutatumia gesi ya *Mnazibay* kwa kutumia *Artmus Group,* iwapo uhakiki utakamilika kwamba gesi ya *Mnazibay* itakuwa inawezekana kuleta umeme katika Mikoa ya Kusini. Sasa kwa nini uende tena ukafanye uhakiki wakati uhakiki umekwishafanywa katika gesi ya Songosongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi naomba itumike njia moja, naomba pesa zilizobakia katika mradi wa gesi ya Songosongo sasa hizo pesa zilizobakia zipelekwe

Kusini na kijengwe Kituo pale Somanga, kijengwe kituo kikubwa cha kupeleka umeme katika Mikoa ya Kusini. Naiomba sana Serikali iliangalie hilo kwa sababu hiyo ni lawama nzito. Siyo lawama ndogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja lakini nikitamka kwamba Serikali naiomba itoe tamko kwamba ni lini na kwa kutumia njia gani Mikoa ya Kusini itapatiwa umeme wa uhakika. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumzia hoja ya Wizara hii ya Nishati na Madini iliyopo mbele yetu. Kwanza, niwashukuru wale waliowasilisha mada hii ya Wizara ya Nishati na Madini kwa jinsi walivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia mjadala unavyokwenda ni Wizara ambayo inatupiwa lawama kila upande. Mkoa wangu wa Rukwa tunashukuru tulipata umeme kutoka Zambia na unatumika pale Mjini Sumbawanga. Kwa miaka mitatu nimekuwa nikizungumzia kuhusu umeme huu kutoka Zambia kuja Sumbawanga unapitia katika jimbo langu la Kalambo na wananchi katika vijiji unapopita umeme huo wameingia mkataba na *TANESCO* walinde nguzo zile lakini wanauona umeme ukipita tu ukienda Sumbawanga wao wanabaki kizani.

Sasa wananchi wa vijiji vifuatavyo ambavyo vimo ndani ya *line* ile ya umeme kutoka Zambia kutoka Kasesha, Kaluko, Sopa, Matai, Singiwe, Msanzi na Katuka wanaomba umeme uteremshwe Matai, mahali ambapo ni katikati na uweze kusambazwa katika vijiji vyao ili na wao waondokane na giza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme wa Gridi kutoka Kidatu unapopita kwenda Kaskazini huko mbona umeteremshwa sehemu mbalimbali na wananchi wanafaidi umeme huo? Kwa nini katika umeme huu unaotoka Zambia tumeandika barua, nimemwona Mheshimiwa Waziri, tumezungumza kuhusu suala hili, lakini hata barua kunieleza mpango huu utaingizwa lini katika kupeleka umeme vijijini utakuwa lini, hamna lolote.

Mheshimiwa Waziri, nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Kalambo wanaolinda nguzo za umeme huo ambao unakwenda katika Mji wa Sumbawanga, wapewe na wao *priority* ili na wao waweze kupata umeme huo.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wa Wizara za Mawasiliano na Uchukuzi na Ujenzi. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa gati ya Kasanga. Wizara ya Ujenzi wanajenga barabara kwenda Kasanga ili kuweza kuendeleza biashara katika gati ya Kasanga. Gati ile haitaendelea kama hatutapata umeme. Wizara hii ina mpango gani wa kusambaza umeme kutoka Matai ufike Kasanga ili uwende sambamba na Wizara nyingine? Hakuna mpango wowote. Inasikitisha, tusipopata umeme ukafika katika gati ya Kasanga ni kwamba gati hii bado tutaendelea kuizungumzia lakini hatutapata vifaa vitakavyosaidia kupakua na kupakia katika meli zile zinazoegeshwa pale.

Mheshimiwa Spika, kusambaza umeme kutoka Sumbawanga kupeleka Nkansi, Mheshimiwa Ponsiano Nyami amelizungumzia suala hili na tumelizungumzia kwa pamoja. Katika hotuba hii hakuna mpango wowote uliowekwa kwa ajili ya usambazaji

wa umeme huo. Inaonekana ni kwamba yale majibu tunayopewa wakati tunapouliza maswali na tunapoiomba Wizara itusaidie huwa ni geresha tu. Hakuna lolote linalofanyika unapokuja kwenye hotuba hii, vitu havijapangwa, vinatamkwa tu. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa katika kuchangia katika hotuba hii tunaomba uchukue rasmi nimeshaandika, nimeshakuleteeni mawazo yangu ni jinsi gani umeme ule unaweza kusambazwa katika Wilaya ya Sumbawanga. Mkiuteremsha Matai ni rahisi kuupeleka hata katika jimbo la Kwela kupitia Mwanze, Puwi mpaka Laela kwenda mpaka Ulumi na Mwimbi, lakini vitaishia hapa hakuna lolote linalofanyika. Kwa kweli inasikitisha sana. Kama hapa tunakuja kuzungumza lakini hakuna mambo yoyote yanayofanyika. kwa kweli utaendelea kupata malalamiko Mheshimiwa Waziri na jambo hili litakuwa kwa kweli si la kuwatendea haki wananchi wa sehemu zingine za Tanzania, wengine wanapata halafu wengine hawapati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu uhusiano wa Wizara hii ya Nishati na Madini.

Katika kitabu hiki Mheshimiwa Waziri amezungumza jinsi watakavyoshughulikia mazingira katika maeneo ya machimbo. Lakini kushughulikia mazingira katika maeneo ya mabwawa ambayo wanategemea wazalishe umeme wawauzie Watanzania hamna lolote na kama yapo anionyeshe ni mahali gani ambapo wameandika. Mabwawa haya kila mwaka tunapata ukame lakini ninyi wenyewe kama watu wa nishati, hamna mpango wa kuendeleza mabwawa haya yawe na *catchment area* ya mazingira ambayo yataweka maji yaweze kutiririka vizuri katika mabwawa haya, hamna mpango huo.

Sasa mnategemea kufanya nini? Miti iendelee kukatwa, watu watumie mkaa wa miti halafu misitu iendelee kumalizika. Ni lazima muwe na mpango endelevu wa mabwawa yenu. Msipokuwa na mpango endelevu wa misitu kulinda mabwawa yenu haya yasikauke wakati wa kiangazi mtaendelea kupiga kelele kila mwaka kwa sababu mnapata fedha lakini hamtengi chochote kwa ajili ya kuendeleza kuwa na mabwawa ambao ni endelevu hili haliwezi likatusaidia siku zote tutaendelea kuwa katika matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu bei ya umeme. Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu hili suala la bei ya umeme. Ni jambo ambalo linakera sana hasa tukijilinganisha na nchi jirani. Sisi tunapata umeme kutoka Zambia. Tunafahamu umeme Zambia uko bei ya chini sana. Lakini ukishaingia tu ukafika pale Sumbawanga, gharama ya umeme ninakuwa sawasawa na sehemu nyingine yoyote wakati umeme kule tunaupata kwa bei nafuu. Kwa nini inakuwa hivyo?

Tunaomba Wizara hii ifikirie kwa kina ni jinsi gani ya kuweza kupunguza bei ya umeme kwa sababu haiwezekani watu wote, Wabunge waliopo hapa wote wanalalamikia kuhusu bei ya umeme lakini Wizara inasema sisi tunajua bei ya umeme ni juu, wananchi hawana haki ya kulalamika. Tunapaswa kulalamika kwa sababu tunajua bei ya umeme katika nchi jirani uko namna gani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu suala la mradi wa umeme wa Mchuchuma. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukiisoma kwa makini na

ukiiangalia jinsi alivyomaliza ukurasa wa 24 anasema hivi: "Wizara imewataka wawekezaji hao kuthibitisha maelezo hayo ili maandalizi ya mradi huu yaendelee." Hii haionyeshi kwamba Wizara hii inaji-*commit* kwa namna yoyote ile ili kuweza kufanya mradi huu wa mkaa wa mawe pale uweze kufanya kazi. Hamna *commitment* yoyote wala hamwonyeshi nia yoyote ya kufanya kazi hii. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anamalizia ku-*sum up* hotuba yake hii atupe takwimu duniani hapa umeme unaoaminika ni umeme unaotokana na nguvu aina gani? Ni maji, ni makaa ya mawe, ni *nuclear* au ni gesi au ni upepo au ni umeme wa jua? Ni umeme upi ambao unatumika zaidi. Hebu twende katika nchi za Ulaya na Amerika, umeme wao wanaupata kwa njia ipi? Utaona kwamba kihistoria umeme mwingi katika nchi hizi zilizoendelea ulianzia na umeme wa makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo ukaanza kupata *support* ya teknolojia ilivyoendelea ndiyo wakapata umeme kutokana na maji na *nuclear.* Sasa sisi tuna makaa ya mawe yako hapa yamezagaa miaka nenda miaka rudi, lakini tukizungumza watu wanataka kuendesha mitambo kwa mafuta. Watu wanataka kuendesha mitambo kwa gesi. Vyote hivi ni gharama kubwa. Kitu kilicho rahisi ambacho kimekaa pale wala hamtalipa kodi kuchimba mkaa kuanza kuutumia, hakuna kodi yoyote ambayo Serikali italipa. Kwa nini tumekaa miaka yote hii hatutaki kuendeleza umeme wa makaa wa mawe halafu tutoe *statement* kama hii inaonyesha wala siyo *commitment* ya Wizara?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwa uchungu sana kuhusu suala la Mchuchuma, wamezungumza sana. Lakini majibu ni *paragraph* moja tu hii ambayo wala haionyeshi kwamba Serikali iko *committed* na hili na umeme ukipatikana utaingizwa kwenye gridi ya Taifa na utakwenda huko huko tunakojua kwamba ni Kaskazini, utakwenda huko huko. Lakini mnazembea kwa sababu gani? Tunaomba sana Wizara iwe *committed* na ifanye vitu vya uhakika, siyo haya mambo ya kuwadanganya danganya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatulalamikia wanataka maendeleo. Maendeleo kwa sasa, karne hii ni ya Sayansi na Teknolojia, wananchi katika vijiji vyetu, shule zetu, mfano nina shule pale Matai, nina shule Kasote, nina shule Ulumi, nina shule Mwanze. Lakini haziwezi zikaingia katika teknolojia ya kisasa ya kompyuta kwa sababu hatuna umeme. Sasa tunaomba haya na sisi tunataka tuingie katika karne hiyo. Bado tuko nyuma.

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara inakaa kimya, itatoa majibu ya kutudanganya au kuturidhisha tu ili mambo yapite halafu tuendelee hivi hivi. Tumechoka kudanganywa, tunaomba tupewe majibu ya uhakika na mipango iandaliwe, mbona Wizara nyingine zinaandaa mipango inayoonekana inafanyika vizuri?

Tunaomba sasa katika mpango huu wa *rural electrification,* mifuko hii ambayo inaanzishwa kwa ajili ya umeme na sisi tuwekwe humo. Tusisubiri sisi tuje tena tuanze kuomba, tuanze upya na kusema nenda kaandike barua ulete, tumeshazungumza hapa, tumeonyesha nia yetu. Kwa nini haya yasifanyiwe kazi?

Mheshimiwa Spika, barua tunaleta, lakini barua nyingine hazijibiwi, mnataka tu kuendelea kutujibu kisiasa. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hebu tilia maanani. Wekea maanani kuhusu haya malalamiko yetu ili tuweze kupata na sisi maendeleo katika

Mikoa yetu na Wilaya zetu, kama haya yatazungumzwa vizuri hasa kuhusu uchimbaji wa mkaa wa mame na jinsi utakavyotumika. Tunaomba maelezo ya kina mpango uko namna gani na uzalishaji wa umeme utakuwa namna gani na jinsi utakavyosambazwa. Mkiwaachia hawa, wanasema sisi tutajua mahali pa kuuza, watachukua umeme huo watavusha nje ya nchi bila kuteremsha mahali popote wakaenda kuuza huo umeme halafu wananchi Watanzania wanabaki kuangalia mkaa wao unazidi kupungua kwa kuzalisha umeme wa kwenda kuuza nje, watu wanajipatia fedha na sisi tunabaki bila kitu.

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali iwe ni *stake holder* katika hili jambo ili wananchi wa Tanzania waweze kufaidi huu umeme na siyo kumwachia mwekezaji achukue huo umeme autengeneze, aupeleke anakotaka. Ni lazima sisi Watanzania tuwe wa kwanza kufaidi matunda ya kazi hiyo watakayoifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza na kama nitapewa maelezo ya kutosha kuhusu maswali haya niliyouliza, basi na mimi nitaunga mkono hoja Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii na kabla sijaongea ningependa kusema kwamba naunga mkono hoja pamoja na malalamiko yangu kwa sababu na mimi sina umeme, sikupata *royalty.* Lakini pamoja na malalamiko haya yote naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba kwanza ukitaka kuondoa umaskini, kuna vipengele vingi sana ambavyo unatakiwa utimize uondoe umaskini, lakini la kwanza ni kuwa na umeme. Umeme na mafuta ndiyo chanzo cha kuondoa umaskini. Umeme ndiyo unatumika viwandani, kama hakuna umeme hakutakuwa na kiwanda chochote na ndiyo maana katika maeneo mengi viwanda vimefungwa kwa ajili ya watu kushindwa kuzi-*run* hivyo viwanda kwa ajili ya bei kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa tukijadili *NetGroup Solutions* hapa Bungeni tulitarajia mengi. Tulitarajia kwamba hawa wenzetu wakija gharama ya umeme utapungua, tulitarajia tena kwamba umeme utapatikana maeneo mengi na tulitarajia kwamba Watanzania wataweza kupata ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini imekuwa tofauti sana, yale matarajio yetu hayakutimia. Kwanza bei ya umeme imekuwa juu zaidi. Hatukuona ajira iliyopatikana, tulichoona ni watu kufukuzwa kazi. Tulitegemea umeme utasambaa nchi nzima. Ndugu yangu Mheshimiwa Ludovick Mwananzila anayesema kwamba umeme unapelekwa Kaskazini, Kaskazini hakuna umeme. Mimi natoka Kaskazini, mimi niko mwisho kule mpakani, hakuna umeme. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulitarajia hayo. Sasa matarajio yetu hatukupata matarajio tuliokuwa tukitarajia. Tulichopata kwanza ni malalamiko makubwa sana kati ya *NetGroup Solutions* na wananchi. Kuna malalamiko mengi sana kati yetu hapa Bungeni na kwa wananchi. Ningependa Serikali iangalie haya malalamiko yanatoka wapi. Tatizo ni nini? Hatukua na malalamiko mengi kabla ya *NetGroup Solutions* kuingia. Lakini malalamiko hayo nadhani kuna sababu na iangaliwe sana kwa sababu mimi nilikuwa na wasiwasi sana kwa sababu nilikuwa napiga kelele kila siku kudai umeme. Mheshimiwa Rais alikwenda kwenye jimbo langu akasema na kuwaahidi

wananchi akawambia kwamba kabla ya uchaguzi wa mwaka 2000 umeme utakuwa umefika Longido na Namanga.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda alipokuwa Waziri wa Nishati na Madini, niliuliza swali la umeme, alijibu kwamba: "Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, ifikapo mwisho wa mwaka 1999 umeme utakuwa umefika Longido na Namanga," mpaka leo bado huo umeme haujafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na wasiwasi sana kwamba baada ya hii *NetGroup Solutions* kuipokea *TANESCO* ndiyo kabisa sitaupata umeme huo na nadhani imekuwa hivyo. Wapo watu wawili nawashukuru sana katika Wizara hii nikienda kila wakati hunipa majibu ya matumaini. Unajua mgonjwa hata kama hukupata dawa ya kumpa na ukawa na lugha nzuri, atafarijika hata kama atasubiri dawa na atategemea. Kwa kweli namshukuru sana Mkurugenzi wa Umeme Vijijini, Bwana Massawe. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Kamishna wa Madini, hawa watu kwa kweli ni watu ambao ukienda wanakueleza, hata kama haiwezekani wanakueleza kwa utaratibu mpaka uelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba leo tena kuuliza huu umeme ambao kila mwaka nauliza, tunaingia mwaka wa 10 tukipiga kelele hapa kuudai umeme, Mheshimiwa Waziri, hivi ni wewe ndiyo tukufuate kukudai umeme au ndiyo hawa watu wa *NetGroup Solutions* kwa sababu wakati mwingine sielewi, kwa sababu ukipata majibu, majibu ambayo hayana mwisho, subiri leo, subiri kesho, kesho haitafika, kila wakati ni kesho, ni kesho, ni kesho, ni kesho, na mwaka ujao bado utaendelea tu?

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua hayo na jambo lingine ambalo ningependa kuuliza ni utaratibu gani ulitumika Serikali ilipowapa *NetGroup Solutions* waendeshe *TANESCO* wakaamua wakati huo baada ya kuwakabidhi wakaamua kulipa madeni yote ambayo walikataa kulipa miaka mingine yote, ni kwa nini mliona kwamba hawa wanastahili kulipwa sasa madeni yote? Kwa nini hamkulipa kabla? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo mnataka kuwaonyesha kwamba wanafanyakazi? Kwa sababu sisi tunasema kuwa walichofanya ni kudai madeni ya Serikali ambayo hawakutaka kulipa siyo kwamba hawakuwa na fedha. Hawakutaka kujilipa wakati ule. Naomba kujua ni kwa nini hayo madeni hamkutaka kulipa wakati ule mkaja kuona kwamba muwalipe *NetGroup Solutions* nataka kujua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka kujua hivi ni kwa nini imeonekana kwamba Zanzibar wanastahili kufutiwa madeni ya umeme, lakini Taasisi za Serikali hazikustahili kufutiwa madeni? Ni kwa nini? Kwa sababu tunashindwa kuelewa ni kigezo gani mmetumia? Kwa sababu nadhani madeni mliyofuta ya Zanzibar ni ya Taasisi mbalimbali za Serikali kama mlizolipa huku Bara.

Naomba mnieleweshe kwani kulikuwa na umuhimu gani wa kufuta madeni ya Zanzibar? Kwa hiyo, naomba baadaye mnieleze na hilo kwa nini haikuwezekana kuacha madeni hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunalotaka kujua, hapa tunaweka utaratibu wa namna ya kutafuta madini katika vijiji mbalimbali bado naona kuna uvamizi tu. Tuliweka utaratibu ambao tulidhani kwamba ukifuatwa itakuwa hata wananchi wameshirikishwa kutoa maeneo yale. Lakini wanakuja tu wanavamia na kusema kwamba tuko kwenye *PR,* lakini mashimo wanayochimba pale ni makubwa zaidi ya hili jengo. Inabidi kabisa kutoa taarifa wamesema kwamba tuna vibali, tumetoka Wizarani, tumekuja kwa *DC,* ndiyo tunakuja kuchimba. Kuingia tu kwa mtu na kuanza kuchimba na kumwekea mahandaki, huo utaratibu ndiyo tuliukataa hapa Bungeni na tulisema kwamba mtu hawezi kuchimba eneo mpaka kijiji husika wakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kule Mundarara kuna watu sasa wanachimba kule, kwa ajili ya kusema, sisi tumeleta kibali toka Wizarani, wamekuja kwenye Kanda pale Arusha, wamekuja kuingilia tu kutuwekea mahandaki.

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba Mheshimiwa Waziri anieleze utaratibu wa mgodi wa Mundarara kwamba huu mgodi *(Rubby Mine)* ni wa nani sasa? Mgodi wa Mundarara wa *Rubby Mine* nadhani Kamishna anaufahamu kabisa, kwa sababu tulitegemea kwamba na sisi huo mgodi utatusaidia. Mrabaha unaodaiwa na sisi tunahitaji. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia kwamba naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Uzoefu unaonyesha na watu wenye busara wanafahamu kuwa umeme wa kutumia maji sio umeme wa kuaminika tena. Nasema uzoefu unaonyesha na watu wenye busara na mimi nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake ni watu wenye busara kwamba umeme wa maji sasa si umeme wa kuaminika tena. Kwanza maji yanayozalishia umeme kutokana na mvua, mvua ambayo sasa si ya uhakika na hatuna uwezo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, maji kidogo yanayozalisha umeme, hayo hayo wakulima wanayatumia kwa kumwagilia maji mashamba yao. Katika vyanzo vyote vya mabwawa ya umeme, wakulima wanalima kilimo cha umwagiliaji maji na kwa wao kuwaambia kwamba kunahitajika umeme na siyo chakula ni jambo ambalo utategemea miujiza wakukubalie na Serikali imetuambia kwamba kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa hiyo, kilimo hiki huwa kinanyang'anyana maji na miradi ya uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, narudia sentensi yangu ya kwanza umeme wa maji sasa hauwezi kuwa wa kuaminika tena.

Mheshimiwa Spika, duniani kote mchango wa umeme wa maji ni 6% kwa wastani. Kwa hiyo, unaweza kuona jinsi gani sasa tuanze kutumia busara kufanya maamuzi ya uhakika kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile uzoefu umetuonyesha kwamba umeme wa *IPTL* nao sio umeme wa kutegemewa. Kwanza umeme wa *IPTL* ni umeme wa bei kubwa sana.

Kwa miezi kadhaa Waheshimiwa Wabunge wanafahamu tumekuwa tukipata taarifa kwamba mashine za kuzalisha umeme pale Ubungo zinatumia mafuta ya ndege kuendesha mashine za umeme, jambo ambalo hakuna nchi yoyote duniani ambayo inaendesha mashine zake za umeme saa 24 kwa kutumia mafuta ya kuendeshea ndege *(Jet Oil Engine),* hakuna, kama zipo Mheshimiwa Waziri ataniambia. Sisi wenyewe kwanza tumeshindwa kuendesha *ATCL* (Shirika la Ndege) kwa sababu ya gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema mradi wa *IPTL* hivi sasa unafanyiwa marekebisho ili uweze kutumia gesi ya Songosongo. Hili nalo ni gharama kubwa na keshatuambia kurekebisha inatarajia kugharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 11.6. Lakini pamoja na gharama hii, Serikali inatumia pesa nyingi kununua umeme wa *IPTL.* Huu ni ukweli ambao sasa tunauona. Maombi ya Wizara sasa hivi inaomba shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kununua umeme huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maliasili zilizopo duniani gesi ni mali ambayo huwezi kufahamu una kiasi gani ardhini. Huwezi kufahamu gesi ya Songosongo utaitumia mpaka lini? Kiasi cha gesi ya Songosongo ambacho kinafahamika sasa hivi ni *cubic* futi bilioni 297 na hizi zinatakiwa zizalishe megawati 150 na wanatarajia kuongeza 70 nyingine na *Wazo Hill* wanategemea kupata gesi kidogo kutoka Songosongo. Kwa wote hawa gesi hii itatumika kwa miaka 20 tu.

Mheshimiwa Spika, nini nataka kusema? Uzoefu duniani unatuonyesha kwamba umeme wa uhakika ni umeme wa makaa ya mawe. Lazima tuende kwenye A,B,C za jambo hili. Nchi zilizoendelea zimefika mahali zilipo sasa kwa kutumia umeme wa mkaa wa mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu nitoe takwimu kidogo ambazo mwenzangu alimuomba Waziri ampe, mimi Waziri nitakusaidia. Marekani inatumia 55% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, Afrika ya Kusini inatumia 95% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, Urusi inatumia 75% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, India inatumia 70% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, China inatumia 80% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, Australia inatumia 70% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe, Uingereza tunaowaiga wanatumia 60% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe na Denmark inatumia 90% ya umeme wake kutoka makaa ya mawe. Huu ndio ukweli. Ukitaka kubisha haitakusaidia ila utaitumbukiza nchi hii kwenye majanga makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, Tanzania ina makaa ya mawe ya kutosha miaka mingi ijayo. Nataka nimkubushe Mheshimiwa Waziri takwimu zilizopo. Sasa hivi kuna tani milioni 527.8 za makaa ya mawe.

**MBUNGE FULANI:** Hawajui.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Wakati nchi zinazoendelea sasa hivi zinachimba makaa ya mawe kilometa 3,6,7,10 chini, Urusi inachimba makaa ya mawe kilometa 20 chini, sisi makaa ya mawe yako juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzalisha megawati 400 zitatumika tani milioni 1.2 za makaa ya mawe. Fanya hesabu kwa tani milioni 527 ni miaka mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo letu ni *mindset.* Wale watu ni wasomi, Mheshimiwa Waziri msomi, Naibu wake *Doctor,* wote wasomi tatizo ni *mindset. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ambayo nchi hii inatumia bilioni za shilingi kununua umeme ni dhahiri kwamba viongozi na wataalam wetu angalau wangekwenda kuona hiki kitu Mchuchuma kikoje, hawajawahi kufanya hivyo, hii inatisha kidogo. Nasema pamoja na dhana hii ya kuona ni kuamini, ingesaidia kubadilisha *mindset* ya waliopo katika Wizara hii ya kutokuamini umeme wa makaa ya mawe lakini ziko tafiti za kutosha na za miaka mingi zinazoonyesha umuhimu wa kutumia makaa ya mawe na soko la umeme wa makaa ya mawe, vyumba kwa vyumba vimejaa ma-*book* ya utafiti huo. Pengine tatizo siku hizi wasomi tunashindwa kusoma, tunaona uvivu kusoma na ndio maana nitasema hapa mbele kwamba badala ya wataalam wetu kusoma haya wapate ukweli Waziri mwenyewe anasema waliajiri Mshauri Mtaalam wa kusoma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumekwishafika mahali sasa tumekuwa *allergic* na kusoma. Unamtuma mtu mwingine akasomee, mtaalam mshauri na unamlipa kwa kukusomea. Hii ni aibu! Sidhani kama sasa hivi wataalam tumefika mahali tunashindwa kusoma ma-*book* mpaka tutafute mshauri mtaalam wa kutusomea! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimalizie, Waziri katika hotuba yake anatuambia kwamba wawekezaji wa mradi huu wa Mchuchuma wameieleza Wizara kuwa wao wangependa kujenga kituo cha umeme chenye uwezo wa megawati 400. Wako tayari kujitafutia masoko ya umeme na hawatataka *TANESCO* kununua umeme wote. Baada ya Bunge kusikia taarifa hii ya maelezo ya Waziri kuhusu msimamo wa wawekezaji, Bunge lilitegemea kusikia kwamba sasa wawekezaji wale wamepewa *go ahead,* ruksa endeleeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini *what happened?* Kwa nchi ambayo ina matatizo ya umeme kama yetu, kwa nchi ambayo inanunua umeme kwa pesa nyingi sana kama yetu, maelezo ya Waziri pale mwisho yanakatisha tamaa. Anasema Wizara imewataka wawekezaji hawa kuthibitisha hayo maelezo yao. *What, a joke? (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ukisoma yale ma-*book* yenyewe yanathibitisha. Huyu mwekezaji ana pesa zake unamwambia rudi ututhibitishie tena.

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Unapofika mahali hapo unaanza kutia mashaka juu ya *seriousness* ya Wizara hii juu ya mradi wa Mchuchuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wawekezaji hawa wana pesa zao, wakipata hasara shauri yao, wakipata faida shauri yao, lakini sisi tunawaambia rudini, bado! Inatia huruma sana. Nataka mwishoni Mheshimiwa Waziri akiwa ana-*wind up* hapa atuambie, je, yuko

*serious,* Mheshimiwa Waziri yuko *serious* au kuna mtu wanampiga *break,* atuambie kama kuna mtu wanampiga *break* sisi tumuundie Tume hapa? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, mradi wa umeme wa Mchuchuma ndio msingi mkuu wa maendeleo ya *Mtwara Corridor.* Ufunguo wa maendeleo ya Kusini nzima ni mradi huu. Sasa tukitaka kuleta maendeleo ya uwiano hatuwezi kukwepa kuendeleza mradi huu wa Mchuchuma kama msingi wa maendeleo wa *Mtwara Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Lakini kwa usahihi wa rekodi zetu za *Hansard* ingekuwa vizuri Profesa kama baadaye ungempatia Katibu chanzo *(sources)* cha takwimu ulizotusomea hapa, inakamilisha rekodi zetu kwa watafiti wa baadaye.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, salamu zote tumeshazitoa kwa hiyo, naendelea moja kwa moja kwenye mjadala. Mimi naunga mkono hoja kwa sababu wanaomba hela ili waendeshe kazi hii, naunga mkono wapate hela hizo lakini nina mambo mawili, matatu ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli mimi nawashukuru sana kwamba Serikali ilijitahidi sana kuleta umeme Tunduma kutoka Zambia kama vile kwa Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, tunashukuru, nchi zinategemeana. Lakini tunapata tabu sana sisi na kwa sababu hatuna udhibiti wowote, ile ni nchi ya wenzetu, umeme ule unazima kila wanapotaka wao na wala *DC, RC* wetu hana chochote anachoweza kufanya kuvuka kwenye mipaka ya watu wengine. Mbaya zaidi wanaweza kuzima wakati wa sikukuu za *Christmas, Eid,* Pasaka inaweza kupita hata wiki mbili hakuna umeme wanasema tuna matatizo. Mimi ni Mbunge lakini huwezi kwenda kule Zambia kuuliza kwa nini mmezima umeme kwetu? Siku moja nikioza binti yangu ndio walikata kabisa na karibu wiki mbili umeme haukuonekana tena. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Haukutualika.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Nadhani sikuwaalika, sijui. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naomba, nilishaongea na rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwamba umeme uko pale Songwe na nadhani umeme unaokwenda Ileje kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo, kutoka pale ni kama kilometa 7, 8 tu watuunganishie umeme kutoka pale wapeleke Tunduma kama itashindikana basi wachukue kutoka Songwe kilometa 75 wapeleke Tunduma.

Nilishaongea na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, nafikiri ananisikiliza na atafanya, ni mahusiano maana yake hata wao wenyewe mafuta wanapitisha kwetu lakini sasa umeme ni kitu ambacho tunafikiri tuunganishiwe kwa sababu ni karibu sana ili

iweze kutusaidia kuwa na *control* ya umeme wetu sisi wenyewe. Hata Meneja wa pale unakuwa unamwonea tu kwa sababu anasema hata mimi sina uwezo wa kusema chochote.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, umeme huo ufunganishwe na umeme wetu unaotoka Songwe au njia panda ya kwenda Ileje ambayo ni karibu zaidi Watanzania tupate umeme ili kama wale wanazima basi umeme wa kwetu una-*takeover,* hatusemi tukate lakini ukizimika pale unadaka umeme wa kwetu. Nadhani Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, amenisikia maana ndio rafiki yangu.

**MBUNGE FULANI:** Huyo mwingine?

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mwingine ni mla muwa. Wenzetu Wapare wanajua mla muwa maana yake ni shemeji yangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la *IPTL,* ukisoma ukurasa wa 24 hadi 26 wa hotuba ya Waziri ambayo kila mmoja anayo au ukisoma ukurasa wa 10 wa kitabu cha Kamati, *Section 7(1)(3)* au ukisoma ukurasa wa 10 vile vile wa maoni ya Kambi ya Upinzani wote wanaongea lugha moja kwamba hebu tuachane na suala hili, Serikali iamue kununua kile kitu, hatuwezi kuwa tunamtolea mtu binafsi hela nyingi kiasi hiki, Serikali inunue na hilo jambo tuachane nalo kama haiwezekani basi itafutwe njia nyingine yoyote ambayo Serikali sasa haitajiingiza katika tatizo hili. Sababu sasa tukianza kufuatilia tatizo hilo tutavumbua mambo mengi na itakuwa ni aibu ya nchi. Mikataba hii imeshawekwa na watu wengine hawakuwepo lakini leo wapo na Serikali ni ile ile.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi hapa Waziri wa Fedha alisema kwamba mikopo ipo na mikataba ipo, ni kweli na anasema wanaweza kuja kulipa hata wajukuu. Sasa hii ipo imeshawekwa na pengine unaweza kuwa unamwambia mtu ambaye wala hakuwepo lakini ndio Serikali imeshaweka mkataba. Ninachosema ni kwamba inunuliwe, iwe ni yetu au tufanyebiashara ya aina nyingine lakini kwa mtindo huu naona Kamati, Kambi ya Upinzani na upande Waziri, ushauri wake ni mzuri, tununue, tuachane na biashara hii au tutafute njia nyingine lakini mimi siungi mkono kwa taratibu hizo hela bora zote zibakie kwenye *TANESCO* tu hakuna haya ya kupeleka mahali pengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea la mwisho, hili sikutaka kuongea lakini sasa naona mwenzangu mmoja amenitaja sana hapa Mheshimiwa Parseko Kone.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mimi nafikiri kupitia ofisini kwako au nini, maana hawezi kuteuliwa Mbunge bila Spika pengine kuidhinisha na mimi niliteuliwa, nilikuwa kwenye Kamati ya *General* Robert Mboma. Tulikuwa mimi na wanasheria wawili mmoja wa Wizarani na mwingine wa kujitegemea anaitwa Marko wa kule Arusha na Afisa kutoka Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Spika, tulipewa hadidu za rejea, tukazifanyia kazi na ilichukua muda mrefu na mara nyingi ulinipa ruhusa kwenda, tulikuwa tunakuja wakati fulani mara nyingi Mheshimiwa unanipa ruhusa nakwenda na imegharimu hela nyingi. Tumeandika ripoti nadhani ina kurasa 200 na kitu, haijaja, tumeshakabidhi zamani. Lakini kabla hatujakabidhi ripoti hiyo kwa aliyetuleua kukawa na mabadiliko Wizarani. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo akaenda Ofisi ya Makamu wa Rais na Mheshimiwa Daniel Yona, ndio akaingia pale. Ndio tuko katika kukabidhi hata hatukujua tumkabidhi vipi maana tuliteuliwa na Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, siku ile tunakwenda, tunakuta kuna mabadiliko na haya ni ya kawaida wala hakuna anayelaumu, basi ndio ikawa hivyo. Sasa Mheshimiwa Daniel Yona tumemkabidhi, nikaenda kwa Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo nikamwuliza na wewe tukupe nakala anasema aah, Serikali ni Serikali pelekeni kwa huyo aliyepo tu sasa. Ni nini kilitendeka, *nobody knows except God. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekabidhi ripoti hiyo, Kiserikali haijatolewa lakini Mheshimiwa Waziri siku moja alitamka hapa kwamba ripoti tunayo, sijui ataitoa na nafikiri sina kumbukumbu sahihi alisema itatolewa tu lakini nadhani mwaka 2001/2002 tulipotoa hiyo ripoti ni mali ya Serikali, ni mali ya nchi, ni mali ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kwamba pale palikuwa na matatizo makubwa sana. *AFGEM* wana ugomvi na wale vijana wetu. Pale ni kweli vijana wa nchi nzima wapo, mmesikia wa Mbozi ni mmojawapo katika watu waliokufa. Mambo yaliyopo pale, tuliyoyaona, yanatisha. Ni mambo ya kupigana, kuna *forgery* kwa mfano wanapotakiwa kuweka mkataba huwa lazima waweke na Mtanzania mmoja. Lakini walimweka Mtanzania mmoja ambaye anaitwa Nyiti, lakini kwa kweli yeye sio *Director* wala hakuwa *Executive,* alifungua kesi Mahakamani na kesi yake iko hapa kwamba nyie mmenisingizia, mnilipe shilingi bilioni 50, basi wale nao wamekwenda kuweka pingamizi lakini tunashukuru kwamba Mahakama yetu ilikataa pingamizi lao, ipo hapa naweza kuweka mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *shootings, maiming and killings,* mauaji, kupiga risasi wengine wanakufa kama alivyosema Mheshimiwa, kuna *harassment, threatening, dehumanization, bullying and the alienation of the Africans. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme hivi, Mheshimiwa mimi ni Mwalimu *by profession.*

Mheshimiwa Spika, tabia, mimi nilikuwa nafundisha *psychology* tunasema tabia kwanza huanza kujengwa na *repetition of the same thing,* unarudia unavuta siku moja, siku ya pili, siku ya tatu, ya nne unajenga *habit. Habit* ni mazoea, unazoea sasa unaanza kuvuta, kuvuta, kuvuta, sasa *habit* ikijirudiarudia unajenga *character.* Sasa tabia hiyo ikijijenga kuivunja ni kazi ngumu sana. Unaweza ukavunja mazoea lakini tabia utahitaji utumie silaha kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu Waafrika na niliwaeleza siku ile mtu akikatisha kwenye viwanja vya Mheshimiwa Spika, pale...

**MBUNGE FULANI:** Ni sawasawa tu.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Watu wanakuuliza unakwenda wapi bwana? Anasema nataka kwenda kwa Waziri Mkuu. Wanamwambia aah, umepotea njia, njia ipo hapa, wenzetu hicho hawana.

**MBUNGE FULANI:** Ni risasi tu.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Ni risasi tu, wale waliong'atishwa mbwa tuliwaita, wote hawa tuliwaita. Sasa ripoti wanayo watajua la kufanya, lakini nataka kusema ni tabia ambayo tukubali, tusikubali ipo.

Mheshimiwa Spika, *Father* Franken, Mwalimu wangu wa Chuo cha Ualimu Kigurunyembe, aliniambia, mumiani ni mumiani tu, kama amezoea kuchinja, anachinja tu. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, katika hili sielewi watafanya nini, lakini tuna tabia ya kusikia hotuba, tuna tabia na Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, amesema sana lakini hata wewe Mheshimiwa Spika, unasema sisi ni maskini wa mali ndio sentensi ambayo mimi tangu nikae hapa nime-*copy* kutoka kwako lakini ni maskini wa mawazo vile vile. Ndio maana mwandikaji mkubwa sana wa vitabu katika Bunge hili ni wewe, sisi wengine, aaah.

Mimi najiuliza Spika, anakaa saa ngapi kuandika vitabu vyote hivi? Wote Waheshimiwa ni mashahidi, huyu mzee anakaa saa ngapi na kuandika? Mimi sielewi, maana yake mimi mwenyewe nimeshindwa kufanya kitu chochote nilikuwa nasoma *Law, Open University,* imefika mahali miaka miwili tu, huu mwaka mwingine umenishinda kabisa lakini nasema niko *very busy* ni Mwenyekiti tu kwa siku moja moja hapa. Ni uvivu tu, ni tabia ya uvivu, mawazo, nini, mtu hataki kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, amesema siwezi kurudia maneno yake na haitakiwi kurudia kuna uvivu mwingi na tumezoea maneno. Lakini nataka kupendekeza kwamba ile *Tanzanite* inatakiwa isiwe *mechanized* ni kitu cha kuchimba polepole, ni kivutio cha nchi, ni kitu cha kujivunia hakuna haja ya kufanya *mechanization* ya *AFGEM* pale. Imechukua vijana wako pale, hawawezi kufanya ujambazi wako *busy* pale, ni *employment* yao pale, *tourism* iko pale, ni kitu cha aina yake, achana nayo, ondoa yule *AFGEM,* achia na vijana wachimbe, tabia ya kusikia tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi juzi hapa nililalamika jamani tangazo lile la ISHI la watoto kukumbatiana mbele ya wazazi na nini sio mila za Kiafrika. Nimemwandikia Katibu, nimempa Meja Jenerali Mstaafu Herman Lupogo mwenyewe, nimempa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o hapa, wao wanaona inafaa tu.

Kweli na nimeongea nao na juzi nimeongea na Dr. Nguma mwenyewe, nimempigia simu kumwambia matangazo haya ya kikundi cha ISHI hatukatai, mengine ni mazuri lakini mengine hayafai, watu hawa wanaona yanafaa, ni tabia tu. Sisi kwetu Wanyamwanga hatuwezi kuona watoto wanakumbatiana, wanashikana humu na humu na nini na wamelikuza zaidi sasa wakasema akome Simpasa, wote hawa nimewaandikia barua hakuna, ni zuri kwao kwa mila zao na tabia zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wanyamwanga wanasema samaki hawezi kuweka kilio. Wakikaa waanze kulia mle ndani ya maji kilio hakionekani, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu au kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wake, kwa kuileta hotuba hii mbele yetu. Lakini katika mchango wangu napenda kwanza kuanza upande wa Wilaya yangu, halafu baadaye nitakuja kwenye mambo ya jumla.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara hii ya Nishati na Madini mwaka 2003/2004, tarehe 4 Agosti, 2003, mimi binafsi nilitoa Hoja Binafsi ambayo uliniruhusu baada ya kukithiri kwa vitendo ambavyo viliashiria mimi kutoridhika na utekelezaji wa uwekaji wa nyaya za umeme katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, hii ilihusu Vijiji vya Mwena, Ndanda, Chikundi, Chigugu na Chikukwe ambavyo vimetumia muda wa miaka kumi na tano mpaka leo suala la umeme halijakamilika. Tarehe 6 Agosti, Waziri wa Nishati na Madini alinijibu na naomba ninukuu: "Mheshimiwa Spika, nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge wa Masasi kuwa miradi hii itakayogharimu kiasi cha shilingi milioni 84 inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/004." Kipindi hicho kimeisha mwezi wa jana na kazi iliyofanyika mpaka hivi sasa kwa kweli naweza kusema ni ya kusikitisha, ni kidogo mno.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona kwamba hali ya utekelezaji ni mbovu, nimelifikisha suala hili kwa Waziri na kumwomba anieleze *status* ikoje. Lakini nafikiri mpaka wakati huu nazungumza Wizara bado haijanieleza *status* ikoje. Wiki iliyopita niliona afadhali niende Jimboni nikachunguze hasa hasa kulikoni. Nilipofika kule nilikuta kazi imeanza, lakini hakuna kazi yoyote inayoendelea kwa sababu zifuatazo na napenda nimwarifu Mheshimiwa Waziri kwamba nilikuta Kijiji cha Njenga Juu wanahitaji nguzo 23 na hazipo, Ndanda nguzo 40, Mpowora nguzo 17, Mwena nguzo 15, Chikundi nguzo 40, Chigugu nguzo 18, Chikukwe nguzo 16, Namakongwa nguzo 31 na Marambo nguzo 36. Jumla ya nguzo ni 236.

Pia wanahitaji *transformer* kumi za *KVA 100,* tano na za *KVA 50.* Vile vile wanahitaji *conductors* za mita 52,000. Hivi ndiyo vitu ambavyo havipo na ndiyo vitu ambavyo vingekamilisha mradi huu kwa mujibu wa ahadi za Mheshimiwa Waziri Bungeni.

Mheshimiwa Spika, najiuliza kuna maana gani kuwa na *Hansard* hii. Tunasema kiuwazi kwamba Waziri atatekeleza hivi na halafu hatekelezi maana yake nini? Hapa ndani ya Bunge wakati Wabunge wanatoa taarifa zisizo kamili wanachukuliwa hatua na Kamati yako ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kwamba wamesema uwongo ndani ya Bunge. Sasa kama Waziri ameahidi kwamba atatoa shilingi milioni 84 kwa muda wa mwaka mmoja na hivi leo hakuna alichotoa, hii tuchukulie namna gani? Kwa nini Wabunge wanaadhibiwa na mtu aliye katika *Hansard* anatoka *free?* Hii *Hansard* ipo imesema hivyo. Sasa dhana ya uwajibikaji inakuwaje katika Bunge hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nina jambo la msingi kwa Serikali, hivi kama Waziri akiahidi kwenye *Hansard* na hakutekeleza hatua gani zinachukuliwa au sisi Wabunge tufanye nini? Hilo nitapenda niarifiwe katika kikao hiki na Mheshimiwa Waziri pia aniarifu ahadi yake aliyokuwa ameitoa lini ataitekeleza ahadi hiyo na matatizo ni nini, kwa sababu suala la upungufu wa fedha mimi sikubaliani nalo. Kama ni suala la fedha mbona anapeleka shilingi bilioni 3.6 *IPTL* kila mwezi? Mimi kwangu anashindwa shilingi milioni 84, haki hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo aliniahidi kwamba kwa upande wa Nanganga, Nangoo na Ndanda zitatengwa kiasi cha shilingi milioni 600 kwa mwaka huu wa fedha. Mimi naomba kuamini kwamba hiyo ni kweli, atekeleze kama ilivyo katika *Hansard,* lakini kama asipotekeleza, mimi naona ile Kamati yetu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ifanye kazi yake ili tuweze kurudisha heshima ya Bunge hili Tukufu. Tukiendelea namna hii basi Serikali haitakuwa inawajibika hata kidogo na sisi tutakuwa tunalaumiwa na wananchi bila sababu. Hili ni jambo zito na naomba wakati tutakapokuwa katika Kamati ya Matumizi lijibiwe kwa undani kabisa na Waziri mwenyewe au kukiwa na majibu yoyote ya ziada nitashukuru kama yatapatikana. Hilo lilikuwa la kwanza ambalo ni la masikitiko yangu makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili nililotaka kuchangia ni kuhusu mradi wa *Mtwara Development Corridor* kuhusiana na Wizara hii ya Nishati na Madini. Ingawa *Mtwara Development Corridor* ilianzishwa mwaka 1996, inaonekana kwamba mpaka hivi sasa inalega lega katika kutekelezwa. Nashukuru leo katika Bunge hili kuna Wabunge kadhaa wamekwenda kindani zaidi nini nchi hii ifanye na tunaweza kufaidika namna gani ikiwa tutatekeleza mapema mradi wa Mchuchuma.

Mradi wa Mchuchuma ndiyo hasa kiini cha *Mtwara Development Corridor,* lakini kwa kweli inahitaji Wizara ambayo nayo inaelewa maana ya umuhimu wa mkaa wa mawe na pia ina nia kabisa ya kuhakikisha kwamba mkaa wa mawe unaweza kuendelezwa ili tuweze kupata umeme kwa wingi na umeme ulio rahisi zaidi. Sasa katika ukanda huu kuna madini mengi, kuna mengine mazito kama *Titanium, Vanadium, Gypsum* na kadhalika ambayo haya yote hayatumiki. Kama Wizara hii ya Nishati na Madini na jina lake ni zuri sana nishati, maana yake nguvu na madini, ingekuwa imejizatiti vya kutosha, mimi naamini kabisa kuwa ukanda huu wa Kusini sasa hivi ndiyo ungekuwa ukanda wa kiuchumi ambao ungeleta ukombozi kwa Tanzania yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya tukienda kwa wenzetu katika sekta ya madini tunakuta majibu ya labda, labda. Naomba sana Wizara yetu ielewe kwamba ingawa *Mtwara Development Corridor* inahitaji fedha nyingi katika kuiendeleza, lakini kwa kadri tunavyochelewa wenzetu Kusini mwa Afrika wanaanzisha mipango mingine inayopingana na *Mtwara Development Corridor.* Kwa mfano, hivi sasa wenzetu wa Msumbiji wameanzisha *Nakala Development Corridor.* Hii *Nakala Development Corridor* itahusisha nchi za Zambia na Malawi ambayo itakuwa na *conflict* na *Mtwara Development Corridor* na wanafanya hivi kwa sababu kuna udhaifu mkubwa wa utekelezaji kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nawaomba wenzetu hawa katika Wizara hii wazidi kuhamasisha Wizara zingine kama za ujenzi na kadhalika ili miradi hii muhimu iweze

kuanzishwa. Kwa namna nyingine isipoanzishwa mapema basi hizi *Corridors* nyingine baadaye zitakuja kuwa na *conflict* na *Mtwara Development Corridor,* halafu hatutapata biashara yoyote.

Kwa hiyo, naomba sana kwamba hebu kama askari wa miavuli, kama ulikwama kidogo hebu jichomoeni kidogo kwenye nyaya zile ili mkifika chini hapa muweze kuhakikisha kwamba Mchuchuma inaanza sasa, chuma cha Liganga kianze sasa na Songosongo ianze sasa na barabara ya kwenda *Mbambabay* ianze sasa. Hatua hizi ndio zitatuwezesha sisi kuchukua soko lote la Malawi, Zambia na *DRC* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uchumi wetu unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nitangoja majibu mazuri kutoka kwa wenzetu, halafu baada ya hapo nitaamua kuwaunga mkono, lakini kwa hivi sasa naomba sana wajizatiti ili mambo haya waweze kuyaeleza vizuri tutakapofika kwenye Kamati ya Matumizi nami niweze kuridhika halafu tutaona mbele ya safari. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Raynald Mrope, nafikiri majibu mengine unayasubiri kutoka kwa Spika kwa sababu nimesikia ukiuliza hivi mambo yanaweza kufika kwa Kamati ya Mheshimiwa Simpasa?

Utaratibu wa kufanya kazi wa Kamati ya Mheshimiwa Simpasa kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya Mwaka 1988 utaratibu ni sawasawa na wa Kimahakama kwamba lazima kuwe na mlalamikaji, awasilishe malalamiko yake kwa maandishi, halafu ndiyo yaende kwenye Kamati kusikilizwa. Kuwe na mlalamikaji na mlalamikiwa na kuwe na mashahidi. Kwa hiyo, kwamba jambo lipo kwenye *Hansard* tu, Kamati haiwezi kulichukua, lazima kuwe na malalamiko yafikishwe kwa Spika, halafu ndiyo Spika akiridhika kwamba haya yana msingi wa kutosha ndipo anayakabidhi kwenye Kamati ili yaweze kuchambuliwa. Taratibu zile zile za Kimahakama. Kwa hiyo, kama una malalamiko Spika anayasubiri. *(Kicheko)*

Tunaendelea Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo jiandae na Mheshimiwa Aridi Uledi vile vile jiandae. Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga hayupo, haya Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo.

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake na wafanyakazi wote katika Wizara hiyo kwa kutuletea hotuba inayoeleweka ingawa ina mambo ambayo tunaweza kuyahoji. Kama mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nathibitisha kuwa na mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa nishati ni huduma muhimu na nyenzo muhimu kwa uchumi wetu. Changamoto katika suala la nishati ni la upatikanaji wa nishati ya uhakika na ya bei nafuu na inayopatikana kwa wakati wote na kwa wananchi wote. Hivi sasa Watanzania wengi Vijijini wanatumia kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati, lakini sekta ya kisasa inategemea zaidi mazao ya petroli na umeme kama chanzo kikuu cha nishati.

Hivi sasa wanaofaidi umeme wengi wapo Mijini, wakazi wa Vijijini bado wanasubiri na wao wapatiwe umeme. Maendeleo ya haraka yanategemea umeme na ushahidi wa wazi upo. Kwa mfano, kwangu mimi umeme ulipofika Gairo na Kibaigwa hali imebadilika haraka haraka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wananchi wengi Vijijini nao wana hamu hiyo wabadili hali yao ya maisha na hali yao ya uchumi kwa kutegemea nishati ya uhakika. Lakini kwa matukio ya hivi karibuni inaonekana wazi kabisa kutegemea umeme wa nguvu ya maji yaani *Hydro* hatuwezi kutimiza yale masharti niliyoyataja ya nishati ya uhakika inayopatikana kwa wakati wote na kwa wananchi wote. Kwa hiyo, tunaona upo umuhimu wa kuchangamkia nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi kuzungumza kwa ukamilifu zaidi kama walivyozungumzia wenzangu juu ya upatikanaji wa umeme kutokana na makaa ya mawe. Hivyo ipo haja ya kuchangamkia na kufuatilia kwa nguvu zote mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma ili kutupatia umeme.

Mimi nilianza kupata tumaini Waziri alivyoeleza kwamba mwekezaji amepatikana na anaweza kuzalisha umeme wa megawati 400 na huo umeme unaweza kutumiwa na *TANESCO* na vile vile na kuuzwa hata kwa watu wengine. Lakini kilichonishangaza mwekezaji huyo hata hatuambiwi jina lake ni nani ili wote tujue tumaini letu lipo kwa nani! Baadaye tutakuja kuambiwa tu yule mwekezaji ameyeyuka, pengine atayeyuka kutokana na urasimu ambao tunaujua upo Serikalini, atakatishwa tamaa, tutamkosa, tutarudi pale pale na kuambiwa yule mwekezaji ambaye hatukutajiwa jina, bahati mbaya aliona kwamba havutiwi na hali ilivyo amejiondoa. Kwa kweli hiyo itakuwa ni hasara kubwa, kwa hiyo, tumchangamkie huyu mwekezaji na tumfuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme kwa wananchi ni kubwa, hata wale walio na umeme sasa wanaanza tena kurudi kwenye matumizi ya kuni na mkaa. Tusipoangalia vizazi vyetu vitakuja kutusuta kwa kuwa tutakuwa tumeimaliza miti kwa ajili ya kuni na mkaa, kwa sababu tunavyoona hata upandaji wa miti hata haulingani na kasi ya ukataji wa miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulipendekeza au kulisisitiza ni kwamba umeme unapofikishwa Vijijini kama umefikishwa katika kituo kimoja tuhakikishe kabisa Vijiji vilivyo jirani navyo vipatiwe umeme ili vichangie kuongeza idadi ya wateja watakaogharamia ulipaji wa gharama zilizotumika kufikisha umeme katika maeneo hayo. Kwa mfano, tunashukuru Serikali imetupatia umeme Gairo lakini umeishia Gairo hapo hapo. Vipo Vijiji vya jirani ambavyo vinawatazama wenzao wa Gairo kwa jicho la husuda kwa sababu hawana umeme. Vijiji hivyo kwa mfano ni Ibuti, Ngirori, Kibega, Chakwale, Ukwamani, Luwaji, Msingisi, Nipipa na Lubeho navyo vinahitaji kupatiwa umeme na mimi natoa ombi rasmi kwa msingi huo huo kwamba iongeze idadi ya wateja kulipia gharama za kufikisha umeme Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazao ya petroli nayo ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Tumeruhusu biashara ya mafuta kuwa ni biashara huru. Matokeo yake tunayaona sasa, sasa imekuwa sio biashara huru tena bali ni biashara holela. Hivi sasa huwezi kujua hawa wenye makampuni ya mafuta wataota nini usiku na wataamka na bei

gani ya mafuta. Lazima Serikali iingilie kati kusimamia hali hiyo ama uchumi ambao tunajivunia kwamba unaibuka, utasambaratika. Tukubali kwamba tulifanya makosa kuua Shirika letu ya *TIPPER* na kudhoofisha sana Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC).* Naomba majadiliano yanayoendelea, yanayofanyika kati ya Serikali na *Oryx Limited* yawe ni ya kufufua *TIPPER,* turudishe *TIPPER.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo juu ya *TPDC.* Shirika hili linahitaji kuimarishwa sio kudhoofishwa. Shirika hili lina wataalam wa hali ya juu sana katika utaalam wa mafuta, wanahitaji kusaidiwa. Njia moja ya kusaidia *TPDC* ni kuwezesha *TPDC* kukamilisha ujenzi wa jengo lake la *Mafuta House.* Tayari wameshawekeza shilingi bilioni 15. Jengo hili litakapokamilika litakuwa ni kitega uchumi kikubwa sana cha *TPDC* na hivyo kuiwezesha *TPDC* kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Hivi sasa *TPDC* hawapati fedha za kutosha. Kwa mfano mwaka 2003 walitengewa zaidi ya bilioni, lakini ilipofika mwisho wakapata kiasi cha shilingi milioni 230. Sasa kuna uvumi kwamba jengo hili la *TPDC* yaani la *Mafuta House* linataka kupewa Shirika lingine bila hata kuwashirikisha *TPDC* kwa maana nyingine kusema kweli *TPDC* wanataka kunyang'anywa jengo hili. Hii siyo haki, *TPDC* wameshawekeza fedha nyingi na wamekuwa wanajitahidi kuwapata wawekezaji wengine waingie nao ubia tangu mwaka 2000, waruhusiwe na wawezeshwe. Hawa wengine wanaotakiwa kuja basi waje lakini wawe pamoja na *TPDC.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niseme machache juu ya madini. Kwangu mimi Watanzania watafaidika kutokana na madini yetu, kutokana na wachimbaji wadogo wadogo hawa Watanzania wenzetu. Hawa wapewe fursa ya kutumia madini ili wainue hali zao za maisha watokane na umaskini. Hivi sasa wanahangaika tu na ndio maana tunaona kwamba ghafla wanaibuka sehemu fulani, wanaharibu kila kitu kwa kutafuta nao wapate chochote. Wapatiwe zana za kisasa, elimu na waelezwe kabisa utaratibu wa uchimbaji wa madini. Wawekewe mfumo ulio wazi wa soko humu humu nchini.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa soko hilo ndio maana utawaona wanapata fedha wanazitumia ovyo, wanarudi pale pale. Hawa vile vile wahamasishwe waingie kwenye vikundi, vikundi vya kuweka akiba na kukopa vya *SACCOs* ili wawe na uhakika kwamba mapato yale wanayoyapata waweze kuyatumia kwa ufanisi zaidi na kwa faida yao ama sivyo wengine huwa tunaamini fedha inayotokana na madini haina baraka. Maana utaona hawa wanapata fedha nyingi, lakini baada ya muda wanarudi pale pale. Sasa unaanza kujiuliza hii fedha yote imekwenda wapi? Kumbe ni kwa sababu hawajawekewa utaratibu mzuri wa masoko na vile vile hawajaelimishwa vizuri namna ya kujiwekea akiba kutokana na mapato wanayoyapata.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo, kwa kweli mahusiano ni mabaya. Tumeelezwa wazi wazi wajumbe, Wabunge wenzetu wametueleza waziwazi kwamba mahusiano ni mabaya, Serikali iingilie kati kurekebisha hali hiyo ama sivyo Watanzania wanaumia kutokana na mali yao wenyewe. Si haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwanza kuipongeza menejimenti ya *Star TV* kwa uamuzi wake wa busara wa kuonyesha vikao vya Bunge vinavyoendelea moja kwa moja au *live.* Pongezi za pekee nazitoa kwa timu yote ya *Star TV* iliyomo ndani ya Bunge hili kwa kazi nzuri, kazi ambayo haina upendeleo wowote. Habari tunazozipata kutoka kwa wananchi zinakiri kuridhika kwao na matangazo ya *Star TV*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuiomba menejimenti ya *Star TV* kuandaa na kutekeleza mipango ya kuhakikisha *Star TV* inaonekana nchi nzima. Mambo yanayojadiliwa humu Bungeni ni muhimu sana kwa Taifa hili, hivyo wananchi wapewe fursa ya kuyapokea na kuyaona kupitia vyombo vya habari. Hivyo ni wajibu wa vyombo vya habari kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata kile wanachokihitaji yaani habari kwa wingi na kwa ubora. *Star TV* wameonyesha njia, kwa hiyo nawaomba wengine nao wafuate njia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,nitumie nafasi hii vile vile nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi nzuri, lakini vile vile kwa bajeti hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie vile vile nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Lawama hizi za hapa na pale ni kuonyesha kuwa Wizara hii ni nyeti na kwa kweli inahusu nchi nzima. Kwa hiyo, ninachowaomba ni kwamba lawama hizi zisiwakatishe tamaa. Lawama hizi ziwe changamoto ya kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, mimi nashawishika mapema kabisa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga kwangu mkono hoja hii, lakini kuna maeneo machache ambayo napenda kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa usambazaji wa umeme. Umeme ni nyenzo muhimu kwa maisha ya kisasa na hapa sisemi kwa maisha ya anasa, ni maisha ya kisasa. Kuanzia viwanda vya kisasa, mawasiliano ya kisasa, elimu ya kisasa, tiba za kisasa, chakula cha kisasa na hata burudani za kisasa, umeme unahitajika. Kwa hiyo, hakuna sehemu ya Tanzania na wala hakuna Watanzania ambao hawahitaji umeme hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo ni sera ya Chama cha Mapinduzi na kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2000/2005 imetaja wazi wazi juu ya kuitaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba inasambaza umeme kwa Watanzania wote kwa kuanzia Wilayani na Majimboni hadi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Chama cha Mapinduzi kuiagiza Serikali yake ya kusambaza umeme hadi Wilayani, Majimboni na mwishoni Vijijini bado kazi hiyo haijatekelezwa kwa kasi ya kuridhisha. Visingizio tunavyopewa ni ufinyu wa bajeti, lakini vile vile ni gharama kubwa ya kusambaza umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa kwa kushindwa kutekeleza ahadi hii sasa kwa sababu ya gharama kubwa, itatulazimu kuja kutumia gharama kubwa zaidi pengine hata mara tatu hapo baadaye. Kwa hiyo, ningeshauri kasi ya kusambaza umeme iongezwe ifikapo angalau mwaka 2005 Wilaya zote ambazo hazijapata umeme na Makao Makuu ya Majimbo yote ambayo hayajapata umeme yapate umeme, tubakie sasa Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Nanyumbu halina umeme ingawa yapo maeneo machache katika Jimbo hilo wananchi wanauona umeme kwa mbali maeneo ya Nandete wanauona umeme kutoka Lupaso, maeneo ya Namatumbusi wao wanaona mwanga tu wa umeme kutoka Masasi Mjini, lakini vile vile maeneo ya Mtambaswala wanauona umeme kutoka Ngomano ng'ambo huko Msumbiji. Lakini ndani ya Jimbo la Nanyumbu hakuna umeme wowote hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Masasi kuna umeme na umeme wa Masasi unatosha kabisa. Umeme huo umesambazwa kuelekea Newala hadi Tandahimba upande wa Kusini Mashariki, umesambazwa kuelekea Nachingwea hadi Ruangwa upande wa Kaskazini, umesambazwa kuelekea Ndanda upande wa Mashariki, lakini ajabu ni kwamba umeme huo haulekezwi Magharibi iliko Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huku ni kuwanyima haki wananchi wa Jimbo la Nanyumbu, wamekosa nini? Umeme uko Masasi na Nanyumbu yenyewe ni kilometa 50 tu kutoka Masasi lakini hawapelekewi umeme.

Mheshimiwa Spika, safari moja Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali langu hapa Bungeni juu ya kupeleka umeme Nanyumbu aliliambia Bunge hili kuwa gharama ya kupeleka umeme Nanyumbu ilikuwa shilingi za Kitanzania bilioni 2.9, kwa hiyo, Serikali haikuwa na fedha hizo. Mimi nadhani hii ilikuwa siyo haki. Ningeiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ihakikishe umeme huo unakwenda katika Jimbo la Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nanyumbu kuna Asasi mbalimbli, kuna shule kadhaa za sekondari na shule za msingi na hizi zote zingependa kupata elimu ya kisasa, inayotumia kompyuta. Lakini vilevile kuna shamba la mifugo la Nangaramo ambalo licha ya kupewa kompyuta, kompyuta hiyo imewekwa bench kwa kukosa umeme.

Kuna *mission,* Makanisa na Misikiti mingi tu hawa wote wangehitaji umeme kwa njia moja au nyingine. Hali kadhalika kuna Vituo vya Polisi, kuna mbuga hiyo ya Lukwika Lumesule iko gizani. Kwa hiyo, ningeomba suala la kupeleka umeme katika Jimbo la Nanyumbu Mheshimiwa Waziri na Wizara yake walifikirie na kulitilia maanani ili tupate majibu ya kuridhisha. Hapa siombi umeme wa gridi, mimi naomba umeme uliopo Masasi hivi sasa, huo umeme wa gridi basi na uje hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nimalizie kwa kuzungumzia kidogo madini. Jimbo langu lina madini katika maeneo kadhaa, lakini eneo ambalo sasa hivi nitalizungumzia ni lile la chini ya Mto Lumesule karibu na Mto Ruvuma, sehemu hiyo kuna madini ya kutosha na huko nyuma wananchi walianza kuchimba. Lakini kutokana na upanuzi wa Hifadhi ya Lukwika Lumesule, wananchi wale waliondolewa wakaambiwa kwamba inabidi washughulikie kilimo. Sasa matatizo wanayopata sasa

hivi kwenye kilimo ni wanyama waharibifu kutoka kwenye hifadhi hiyo hiyo ya Lukwika Rumesule. Kwa hiyo, kwenye kilimo hawapati chochote kwa sababu mazao yao yote yanashambuliwa na wanyama, lakini vile vile kwenye madini kule wamefukuzwa, kwa hiyo, wananchi hawa sasa wamekuwa maskini na hawana njia yoyote ya kujipatia fedha.

Mimi ningeiomba Serikali kwa sababu Serikali ni moja ikafikiria tena uamuzi wake huo angalau itenge eneo dogo pale ambapo madini yanapatikana ili wananchi waruhusiwe kuchimba. Serikali ina utaratibu wa kuviruhusu vikundi vilivyoko maeneo ya hifadhi kwa ajili ya kazi za uvuvi na kwa ajili ya kazi za kurina asali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba vile vile wananchi hao wakaruhusiwa kujiunga katika vikundi na wakapewa maeneo ambayo watachimba madini. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewaokoa wananchi hawa ambao hivi sasa kwenye kilimo hawapati chochote na ajira zingine hakuna. Kwa hiyo, ajira ya kuaminika ambayo wataipata ni hiyo ya kuchimba madini.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe wananchi hao wanatengewa eneo ambapo wanaweza wakachimba madini. Jana mwenzangu alilalamikia kuwa huko nyuma Mji wa Mtwara ulichangamka kutokana na madini na sehemu mojawapo ambayo madini hayo yalikuwa yanatoka ni hii ya Lumesule Chini. Kwa hiyo, tafadhali Mheshimiwa Waziri, uongee na Waziri mwenzako ili wananchi hao waweze kuyachimba yale madini ili wapate fedha kwa sababu kwenye kilimo imeonekana ni kazi bure na ni vigumu kuzuia wanyama wale wasiharibu mazao. Kwa hiyo, wamenituma niombe waruhusiwe kuunda vikundi na wakachimbe madini hayo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa sina zaidi, baada ya mchango huo mdogo, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii, lakini vile vile niendelee kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niongee machache yanayohusu hii Wizara ambayo ni nyeti sana katika maendeleo ya Taifa hili. Kama mambo ya Wizara hii yangetengemaa *efficiency and productivity level* za nchi hii zingekwenda juu sana na maendeleo yangepatikana. Yapo mambo matatu ambayo nahitaji kuyazungumzia. Moja, ni *Son gas,* pili ni *IPTL,* tatu ni umeme wa Kasulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na mambo madogo mawili. Iko Kamati ambayo imechaguliwa na Wizara hii ambayo sasa hivi ina durufu sera ya madini nchini. Ninachokiomba kwa Kamati hii ifanye kazi kuisaidia nchi na siyo kuifurahisha Serikali. Kwa sababu nchi hii tuna *stake* katika *development* yake na tungependa kama Kamati hizi zifanye kazi nzuri ambazo zitatupeleka mbele na kisha wote tufurahi, maana kama tunataka kwenda peponi Mungu amesema: "Ukiomba utajiri utapata, ukiomba umaskini pia utapata." Kwa nini sisi tuombe umaskini na sisi nchi yetu imejaa utajiri na tunao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza hilo, naomba niseme hivi Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, wakati *IPTL* ilipokuwa inaleta vurugu vurugu katika nchi hii alisema hivi: *"TANESCO decision to issue a notice of default to the Independent Power Tanzania Limited, is a deep satisfaction among those who are concerned with the*

*development of the national economy and of the Tanzanian people, but the same token the default notice represents a resounding defeat for those and local interest who are prepared to mortgage the future of the country for their own rather than national interests." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi naunga mkono maneno yote aliyoyazungumza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba kupitia kwako Mheshimiwa Spika, niwaeleza haya.

Mheshimiwa Spika, leo hii *IPTL* Serikali inailipa *2.6 million dollars* kwenda nje kwa mwezi. *Two point six million dollars* hiyo ni *capacity charge.* Lakini Serikali pia inalipa kitu kinaitwa *Energy Charge* ambayo ni *six point six US dollar cents* na kwa mwaka Serikali inalipa *six point six billion,* kwa hiyo, ukiongeza na zile unapata *close to ten billion* zinalipwa ambazo hatuna maelezo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa *SONGAS* Serikali inalipa *four point two billion capacity charge* na inalipa *four point five cents* kama *energy charge per kilowatt hour* ambayo inakuja kama *another ten billion* ambazo hazina maelezo ya sawa sawa. Kwenye kitabu hiki cha mahesabu na tumehoji hata kwenye Kamati ya Fedha hatukupata maelezo sahihi kutoka kwa Wizara zinazohusika. Hiki kitabu cha *volume two, Estimates of Public Expenditure* ukurasa wa 211 kifungu cha 280700 kinaitwa *Transfers and Subsidy- Non- Profit Organizations* ambapo ndiko fedha hizi zipo. Serikali zile fedha haziende kwenye Wizara hii wala zile fedha hazitumiwi na Wizara hii zinapelekwa *TANESCO,* fedha zile ni *a hundred and twenty six billion shillings* zinakwenda *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, nani ungempa *one hundred and twenty six billions* za bure hata kama ziko gharama zinazofidiwa, lakini akashindwa kufanya kazi nzuri? Hata mimi ungenifanya *Managing Director* pale ningefanya kazi nzuri. *I would indeed perform a better job. (Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waeleze!

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, maana tunajidharau sisi wenyewe kwa kuona kwamba Watanzania waliokuwa pale hawakufanya kazi nzuri, lakini na mimi ungenipa ningefanya kazi iliyokuwa nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, *Commercial Operation* ya *SONGAS* inaanza kesho. Tunaanza kulipa hizi fedha. Wizara ina maelezo ya kutupa kwa haya? Haya yote ni gharama kubwa kwa Taifa na lazima watueleze vizuri tunawawakilisha watu ambao hawana dawa, hawana shule na hawana vitu vingi. Maelezo hatuna, kuna uzembe na *inefficiency* katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya siyo maneno ya mtu, ni maneno yaliyo wazi na sisi tunahitaji mipango ya Serikali ielezwe wazi wazi. Sizungumzi tu jamani, mimi nazungumza nina *data, I have got all the data, I have all the speech, I have IPTL* na ninaweza kufanya *comparison* ya *Privatization Programme* katika Afrika nzima na vinavyoendelea katika *Water and Energy Sector. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote yana *impact* kwa maendeleo ya nchi yetu. Wataalam wa mambo ya *Energy* wanasema hivi *and I am quoting from a source* ya Barren Baum *and Stock Tolhert in their book titled Investing in development,* wanasema hivi: *"If a developing country could hold down energy cost, their need to ensure not only that they are using no more energy than necessary but they are obtaining their energy at the least possible cost."* Huu msamiati wa *least cost* katika nchi hii haupo tungekwenda mbali sana katika nchi hii.

**MBUNGE FULANI:** Kwa nini haupo?

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:**Yapo mengi na nyie Waheshimiwa Wabunge mnayafahamu na yote haya tunahitaji kuyafanyia kazi vizuri. Maana tukiomba tukianzisha utaratibu wa Kamati za Bunge za kupeleleza yanayoendelea kwa kweli ni lazima tuungane tufanye hivyo, vinginevyo haya hatuyawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wataalam wanasema kuna *many dimensions* ambazo zinahusu *relationships* katika *Energy Sector* za *objectives* ambazo zinakuwa *set.* Nyie mnaelewa kwamba *Industrial Strategy* ya nchi yoyote iko *linked to the Energy Sector. It is linked to energy demand and energy cost which have a strong bearing on industrial structure and therefore the efficiency with which those Organization perform.*

Sasa ningeweza kuendelea, nikaendelea nikaendelea, lakini kama unafanya mambo ya uwekezaji bila mpango sahihi na kutumia taaluma sahihi kuna *calamities* nyingi unazozipata, *qualification* yangu ninayotaka kusema hizo *calamities* ndizo hizo zimetupata, maana yapo maendeleo mengi tungeweza kufidia kwa kutumia hayo mabilioni niliyoyasoma hapa kwa *IPTL* na *SONGAS* . *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoka Mkoa wa Kigoma wakizungumzia habari ya umeme katika Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alikwenda Mkoa wa Kigoma.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu niwaambie alitembea kama *rocket,* mimi sikuwepo lakini alivyowatembeza watu nimekuta wanalaumu wanasema huyu Waziri alikuja hapa anatuyumbisha tu, wakaenda Kasulu, twende huku wamekwenda mpaka Uvinza, hakuna *statement* anayowaambia, watu wazima wanamfuata hakuna *statement* aliyowaambia. Hii ni *an industrial age,* yeye amekuwa mwenge, yeye siyo mwenge *you are serving people and these people have interest and their interests must be met, if they are not met,* ondoka unakwenda kuwasumbua kwa nini? Usiende basi, huna *agenda* unakwenda kutembea kwenye Mkoa, *Regional Commissioner* na ma- *DC* kila mmoja anakimbia na yeye *for what?*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, siyasemi hayo bila sababu, ninayasema haya kwa uchungu mkubwa. Hii nchi tukianza kuitaniatania hatufiki popote tunachezea maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa ule una *potential* kubwa ya maendeleo, tupe umeme sisi tutakimbizana na Njombe, tutakimbizana na Kilimanjaro ndivyo tunavyosema. Waha wangapi wako Mkoa wa Shinyanga, Waha wangapi wako Tabora, Waha wangapi wako Mwanza na wanafanya kazi kubwa na nzuri. Wameukimbia Mkoa ule kwa sababu

umeachwa hauna barabara, hauna umeme na hauna chochote. Huku unasema tuko karne ya 21, karne ya teknolojia, *where? All these are words in vain brothers! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia habari ya umeme kutoka Burundi, mkataba uliosainiwa toka mwaka 1993 hivi hatma ya Mkoa huu imefikia wapi mpaka leo? Ni kwa sababu Burundi wana vita na sisi ndiyo tunasuluhisha na majibu mtu mwingine anasimama anasema Burundi hakuna Serikali, hakuna Serikali *can you go there and rule* kama hakuna Serikali? Unawaambia watu wazima kwamba hakuna Serikali. Unasimama mbele ya Wabunge wote hawa. Serikali ipo, *there is government* na umeme haujakatika Burundi ila Tanzania tu.

Mheshimiwa Spika, Kigoma hata magenereta yake ni ya wasiwasi na ni mabovu ya miaka 30 iliyopita ndiyo yapo pale. Lakini tunataka umeme katika Mkoa mzima, vijana wetu wafanye kazi na wao tunapozungumzia karne ya 21 wajue ni kitu gani. Hizi *alternatives* zingine tunataka tu zielezwe leo. Mimi sikuunga hoja mkono kwa sababu ya hayo ninayoyasema. Kwa kweli leo nataka majibu.

**MBUNGE FULANI:** Sawa!

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nataka majibu ya Serikali kuhusu hili kwa nini mmegawanya nchi, sehemu nyingine zinakuwa kwenye madimbwi ya giza na nyingine mnasema ndizo zinazostahili umeme na barabara ninyi ndiyo mnaostahili, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri kupanga ni kuchukua *a complete whole and then you say* sasa tumepanga yale mapungufu tunaweza kujazia. Sasa unasema ujumla ujumla mimi hiyo *Electricity Progamme* ninayo hapa, *I have got a document on Rural Electrification Programme and I hope* itakuwa *implemented* vizuri zaidi. Maana tusiambiwe tu maneno ya kutufurahisha ili kupitisha bajeti hapa, halafu hakuna kinachofanyika tutafika pabaya. Maana tutaanza kugombana na tutakapofika huko kwa kweli hali haitakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, kama unapanga vizuri basi uje na *vision* ya Wizara yako, siyo utusomee maneno ya kutuchanganya hapa ndani. Sema kwamba nchi nzima watakuwa wamepata umeme na zile Wilaya ambazo hazijapata umeme kama Mkoa wa Kigoma, Kasulu, Kibondo na sehemu nyingine ambazo hazijapata umeme nao mpango ndiyo huu. Hiyo yote lazima ije katika mpango mtuonyeshe *a concrete programme* ya kuweka umeme sehemu ambazo hazina.

Mheshimiwa Spika, umeme ni muhimu kwa maendeleo, mtu huna umeme hata macho hufunguki unakuwa kama kipofu, kisha wenzako watakuwa wanafikiri wewe ni taahira.

Mimi nilipokwenda Uingereza nilikuta Waingereza *their capacity to understand things was much higher than mine,* lakini nilivyokuwa naendelea ninaona kama *they are very fast* katika ku-*catch up* mambo na mimi nikasema *I must pool up my sox,* ilibidi nisilale mpaka saa kumi, mimi ndiyo nalala asubuhi, lakini saa moja nimekwishaamka. Saa mbili na nusu au saa tatu niko darasani, nika-*catch up.*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi huwezi uka-*catch up* maana huna *resources, resources* ziko Serikalini, Serikali itufanye tu-*catch up* na wale wengine mnaofanana na sisi mlielewe hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale wote wanaosema kwamba tu tumekosa mpango mzuri kwamba tunakwenda tukifika hapa kitu kipo lakini ngojera hii tunayoambiwa haitufikishi mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme hivi, *understand that energy is an input or output in almost all productive activities and consequently the links between energy and the rest of economy are strong and intimate.*

Mheshimiwa Spika, kama unataka maendeleo hapa ndiyo unayapata, *not only do energy investment compete with those in the other sectors but decisions on them cannot be taken without considering how they inter-relate with policies intended elsewhere in the economy.* Haya ndiyo tunataka wafanye. Wakishafanya hivyo tutaridhika kwa maamuzi mazuri ya Serikali wanayoleta mbele yetu na sisi hatuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, CCM ni Chama kinachojua kujisahihisha wakati wote. Sahihisheni matendo yenu ndani ya Serikali, maana kama ni makosa ya *IPTL* na *SONGAS,* mnayajua, waliyoyatenda wako na mnawajua, tunapohoji mnaona sisi tunakuwa wabaya, ubaya wetu uko wapi? Kwa sababu tunataka kufanya mema katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kila nikisema hivi nataka tufanye *restructuring a*mbayo inakwenda sambamba na *Reform programmes* ambayo tumekuwa tukiifanya, tutaharibu haya tuliyofanya katika miaka hii iliyopita ambayo Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, amekuwa madarakani. Shilingi bilioni 126 unazitumia bila mpango usioelezeka, Waheshimiwa Wabunge, hii ni hatari kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na niwapongeze sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwa mara ya tano nalazimika kuchangia ili nipate maelezo ya ombi na kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Mchinga na Ng'apa kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, linalonikandamiza kama Mbunge na linalowasugua roho Wananchi wa Mchinga na Ng'apa ni tendo la *TANESCO* kupeleka *engineers* wake kijijini Mchinga kuangalia gharama halisi za kupeleka umeme.

Mheshimiwa Spika, tendo la *TANESCO* ni kama kumwonyesha glasi ya maji mtu mwenye kiu na kisha maji hayo kuyarejesha ndani ya chupa. Ni tendo linalosugua roho na kiashiria cha mwisho wa safari yangu ya Ubunge mwaka 2005.

Kijiji cha Mchinga ni Makao Makuu ya Jimbo, Tarafa na Kata. Kijiji hiki kinacho shule ya Sekondari, kituo cha Walimu, kituo cha Polisi, shule mbili za msingi na karibuni kutawekwa kambi kubwa ya ujenzi wa barabara ya Mbwemkuru - Lindi - Mingoyo.

Kijiji cha Mchinga mbali ya kuwa ni kituo muhimu cha usafiri wa Dar es Salaam - Lindi, ipo Mahakama, Zahanati na kinaendesha uvuvi mkubwa ulishao samaki Mji wa Lindi na Dar es Salaam. Aidha, Kijiji cha Ng'apa chenye wakazi elfu sita kina shule za msingi mbili na viwanda vidogo vidogo vya vikundi vya Vijana na Wanawake vinavyojishughulisha na ukamuaji wa mafuta ya nazi. Umeme ungetusaidia sana kuwaondoshea wakulima wa nazi adha ya kutumia mabavu.

Kwa bahati mbaya mchozi wangu upo mbali na hivyo siwezi kulia Bungeni na nafasi yangu ya u-Naibu Waziri nayo inaninyima kutoa shilingi ili kuonyesha uchungu wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hisani yenu nakuombeni mtakapokuwa mnafanya majumuisho, muwatamkie wananchi wa Mchinga na Ng'apa juu ya hatma ya suala hili la kupelekwa umeme ili kuninusuru na tuhuma kuwa jambo hili silifuatilii. Naamini kuwa suala hili halitatiwa katika lile kapu la Waheshimiwa Wabunge, muda ni mdogo kwa hivyo hatutaweza kujibu kila hoja ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mwenyezi Mungu, akuangazieni mwanga ili muone umuhimu wa kulitolea suala hili tamko humu Bungeni. Eee Mwenyezi Mungu niondoshee kadhia hii.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja hii. Pamoja na kuunga mkono hoja, ninayo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Mkoa wa Kigoma kuunganishwa na gridi ya Taifa. Serikali inatakiwa ioneshe ni kiasi gani cha fedha *(committed)* kwa ajili ya kupeleka umeme wa gridi Mkoani Kigoma na siyo kusema tu kwamba, Serikali ya Sweden imeonyesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu. Miaka zaidi ya miwili iliyopita, mpango wa *EPZ* ulianzishwa Mkoani Kigoma lakini kwa ajili ya ukosefu wa umeme, hakuna Mwekezaji yeyote ambaye yuko tayari kuwekeza Mkoani humo.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inakumbushwa juu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliyoitoa mwaka 2000 wakati wa kampeni ya Uchaguzi Mkuu kuwa Mkoa huo utakuwa umepata umeme wa uhakika ifikapo mwaka 2003 na hasa kwamba Mji wa Kasulu utakuwa umepatiwa umeme mwaka huo. Leo hii ni mwaka 2004, vyote bado ni ndoto tu. Hakuna umeme!

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujua kuna mpango gani wa ku-*harness the Malagarasi* ili Mkoa wa Kigoma upate umeme wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta hasa ya dizeli, petroli na mafuta ya taa, zimeendelea kupanda kwa viwango vikubwa sana. Hali hiyo ni mbaya zaidi katika

Mikoa kama Kigoma na Rukwa, ambayo iko pembezoni. Hivi sasa bei ya dizeli Kasulu siyo chini ya Sh.1,000/= na ya petroli siyo chini ya Sh.1,500/= kwa lita. Kutokana na bei hizo kuwa juu, bei ya bidhaa mbalimbali ziko juu sana na gharama ya usafiri imepanda ajabu na hivyo kufanya maisha ya mwananchi wa kawaida kuwa magumu sana. Je, Serikali haiwezi kutoa ruzuku kwa gharama za usafirishaji wa mafuta kwenda Mikoa hiyo ili bei zisipande zaidi? Je, *EWURA* itaanza lini ili kudhibiti bei za mafuta?

Mheshimiwa Spika, kila mwaka kuanzia 2001/2002, Serikali imekuwa ikiahidi kwamba, itatoa mikopo kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo na kuwapa elimu juu ya shughuli hii lakini ukweli ni kwamba, hilo halifanyiki na wachimbaji wanaendelea kufanya shughuli hizi katika mazingira magumu. Je, sasa Serikali inasemaje kuhusu mikopo hii? Je, masharti ya mikopo yatakuwa nafuu kweli?

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe kukamilishwa kwa uanzishwaji wa *REA* na *REF* ili nishati ya umeme iwafikie watu wengi zaidi ambao wanaishi vijijini. Aidha, Serikali iingize nchini na kuuza kwa bei ndogo vifaa vitumiavyo nishati mbadala hasa ile ya jua na upepo. Leo hii *solar panel* ya kuuwasha umeme kwenye nyumba ya kawaida haiuzwi chini ya Sh.350,000/=. Je, mwananchi wa kawaida anaweza kulipia mtambo huu?

Mheshimiwa Spika, kwa nini mradi wa majaribio ya nishati mbadala yafanyike maeneo ya vijijini Mwanza ambako kuna umeme tayari na siyo Mkoani Kigoma ambako hakuna umeme?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja iliyo Mezani. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kazi ngumu ya kipindi kilichopita likiwemo janga la moto lililotokea Ubungo - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kubwa, *technical* na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. Tukianzia na umeme, licha ya bei kubwa ya nishati hii kwa viwanda na matumizi ya kawaida, umeme si *stable.* Nikiwa na maana kuwa nguvu ya umeme siyo *constant* wala *consistent* ni *unstable* kiasi cha kuchangia uharibifu wa vifaa mbalimbali na usumbufu. Tatizo hili lipo hasa Mkoani Kilimanjaro hususan Wilaya ya Moshi Vijijini. Nitaomba Waziri atakapojumuisha Hotuba, atutolee maelezo ya tatizo hili Wilaya ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tukio la moto la Ubungo, ninapenda kuanza kutoa pole kwa Wizara na Serikali kwa ujumla, lakini pia pongezi kwa namna Serikali ilivyohangaika kuhakikisha moto unadhibitiwa. Ningependa kujua wale mashujaa wawili waliofunga *valve* za *tank* kuzuia *leakage* wamepewa zawadi gani kwa ushujaa huo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua jinsi ambavyo Serikali imejizatiti katika kuweka tahadhari za kuzuia na kuwa na vifaa vya kuzima moto unaotokana na mafuta kwa mfano, *special foam* ya kuzima moto na kadhalika. Tunakumbuka Serikali na *TANESCO* walipata tabu sana kupata vifaa hivi kwa haraka kutoka katika soko.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kutaka kununua *IPTL* ni lazima ufanywe haraka. Hotuba ya Mheshimiwa Wami imeashiria kuwa Serikali haina fedha ya kununua *IPTL*. Lakini ni lazima Serikali ipime umuhimu na hasara inayozalisha kutokana na mradi huu *(too expensive)* na *option* ya kutafuta fedha sasa na kuondokana na *long term drain* ya fedha za Taifa hili. Ni vizuri uamuzi ukafanyika wa kutafuta fedha sasa za kununua mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, lakini nitaomba Waziri atoe maelezo katika maeneo niliyoomba maelezo, hususan umeme kukosa nguvu na kuwa *un-stable* Moshi Vijijini. Ninaomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii. Pili, napongeza jitihada za Wizara za kufanya kazi nzuri ya kusambaza umeme hapa nchini, hasa Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya. Vilevile ninapongeza juhudi za kuendeleza sekta ya madini ambayo inakua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa ushauri kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, umeme vijijini, huko vijijini nchini kote upo mwamko na mahitaji makubwa ya umeme. Aidha, wananchi wanazo shughuli nyingi zinazohitaji nguvu ya umeme. Lakini kwa kuwa mahitaji makubwa yanapambana na uhaba mkubwa, matokeo ni *frustrations* kwa umma. Kwa vile umeme wa *Grid* hauwezi kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi, Wizara ikazane kusambaza teknolojia ya umeme wa jua *(Solar Power).* Inashangaza sana kuona mitambo ya *solar* ni aghali mno kwa nini? Umeme ni jua ndilo jibu la haraka la *frustrations* za umma. Fanyeni utafiti wa kitaalamu jinsi ya kusambaza *solar* na kwa bei nafuu. Inatia moyo kuwa mmeanza mradi wa majaribio huko Mwanza. Ongezeni eneo la majaribio lifikie kanda mbalimbali kwani nchi hii ni kubwa kwa ukanda wa kati nawakaribisheni leteni mradi wa majaribio katika Wilaya ya Manyoni, hasa eneo ndani ya Bonde la ufa ili muone matokeo yake. Karibuni.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *IPTL* kwa wakati huu wa ukame unatusaidia sana nchini. Upo umuhimu wa kuendelea nao. Lakini sio kwa mfumo na utaratibu wa sasa. Wizara fanyeni hima ili Serikali iununue mtambo huu. Hatua hiyo itaokoa mambo mengi pamoja na uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Manyoni inazo *deposits* za dhahabu katika maeneo ya Iluma, Mafurungu na miezi michache iliyopita dhahabu imegundulika katika Kijiji cha Londoni. Lakini katika maeneo yote hayo wapo wachimbaji wadogo wadogo tu. Tungependa kupata *opinion* ya wataalam iwapo wamefanya *survey* na kubaini kiwango cha *deposits* hizo. Kama madini hayo yapo kwa wingi, tutashukuru kupata wachimbaji wadogo wapate ujuzi na zana za kisasa ili waongeze uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, narudia kuwapongeza kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza niipongeze Wizara kwa juhudi inazofanya katika kutekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini na hasa katika Wilaya ambazo hazijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ningependa Wizara itambue kwamba, katika vijiji kama Dar es Salaam kuna vijiji ambavyo havijapata umeme hata kidogo. Kwa bahati mbaya, wakati Wizara inapeleka umeme vijijini bila kujali kwamba *TANESCO* itapata faida kwa kuuza umeme huo huko vijijini, kwa Dar es Salaam hali ni tofauti. *TANESCO* wanataka kwanza kuwe na wateja wa kutosha kurudisha gharama za umeme hata kwenye vijiji vya Dar es Salaam. Hii ndiyo maana umeme haujafika vijiji vya Bangulo (Pugu), Ulongoni (Ukonga), Chanika, Nzasa, Mvuti, Msongola na Kitunda. Ni kwa sababu *TANESCO* wanaona hakuna wateja wa kutosha huko.

Mheshimiwa Spika, ningependa kupendekeza Wizara iingize vijiji vya pembezoni mwa Dar es Salaam katika mpango wa umeme vijijini, ili vipate umeme bila kujali faida kwa *TANESCO*. Ni aibu kwa sehemu ya jiji la Dar es Salaam kuendelea kutumia koroboi wakati wakazi wake wamo katika idadi ya watu waishio jiji la Kimataifa la Dar es Salaam.

Aidha, *TANESCO* imelegalega hata katika miradi ya kupeleka umeme Jimboni Ukonga katika maeneo yaliyokuwa tayari yamo kwenye Miradi iliyokwisha kukubalika na *TANESCO*. Mfano ni miradi ya Bonyokwa (Kinyerezi) Ulongoni (Ukonga), Kitunda na Chanika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia ni uamuzi wa Serikali kusitisha kuagiza mafuta ghafi *(Crude Oil)* na kusafisha hapa nchini kwa kutumia kampuni ya *TIPER*. Uamuzi huu umechangia sana katika kupandisha bei ya mafuta nchini, kwani sasa wafanyabiashara wanaagiza mafuta moja kwa moja na kujipangia bei, tena kwa njia haramu ya kukaa na kupanga bei *(Cartel)*.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza kwamba, Serikali iangalie upya kufufua kampuni ya *TIPER* au kuanzisha kampuni nyingine ya kusafisha mafuta nchini ili *Crude Oil* iweze kuagizwa na kusafishwa nchini. Nchi kama Kenya, bei ya mafuta ni *stable* kwa kuwa wana *refinery plant* pale Mombasa na hii inafanya hata wanaoagiza mafuta safi toka nje kulinganisha bei yao na ile inayosafishwa pale nchini Kenya.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa jitihada zao za kuboresha huduma katika Sekta ya Nishati na Madini. Yapo mafanikio dhahiri yanayoonekana, nawatia shime waendelee na juhudi hizo kadri watakavyoweza.

Mheshimiwa Spika, inasemekana Wilaya ya Ileje ina madini ya aina mbalimbali kama vile ulanga, dhahabu, makaa ya mawe na kadhalika. Tuna hakika na madini ya ulanga na makaa ya mawe kwa sababu yanachimbwa. Tafiti kadhaa zimefanyika, lakini hatujui matokeo yake. Je, Wizara ina taarifa zozote za tafiti hizo? Kama zipo, tunaomba tufahamishwe na kushauriwa nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maombi maalum mawili yafuatayo: Kwanza, huduma ya umeme imefika Makao Makuu ya Wilaya (Itumba) na baadhi ya vijiji njiani kutokea Mpemba (Mbozi). Katika mipango ya *TANESCO* au chombo cha kusambaza umeme vijijini, naomba Wizara ione uwezekano wa kufikisha umeme eneo la Tarafa ya Bundali ama kutokea Ikuti (Rungwe Magharibi) na kuingia Luswisi (Ileje) au

kuanzia Makao Makuu ya Wilaya kwenda Bundali. Eneo la Bundali lina utajiri mkubwa na wananchi wako tayari kutumia umeme katika nyumba zao na shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, pili, natumaini Wizara inafahamu na kutambua kwamba, mgodi wa makaa ya mawe Kiwira, sehemu kubwa iko ndani ya Wilaya ya Ileje. Naomba Wizara iendelee kutambua hivyo, menejimenti ya Mgodi wa Kiwira iendelee kutambua hivyo na kwa hiyo, ushuru unaopaswa kulipwa na mgodi kwa Halmashauri ya Ileje, ulipwe kwa kiwango kinachostahili bila kuvutana. Tunaomba taarifa zote muhimu kuhusu maendeleo ya Mgodi ziwe zinawasilishwa kwa uongozi wa Wilaya ya Ileje ili tuweze kwenda pamoja. Tutaendelea kushirikiana na Menejimenti ya Mgodi, tunaomba vijiji vilivyo jirani na Mgodi, kama vile Kijiji cha Kapeta vipatiwe umeme kutoka Mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, nawatakia mafanikio mema. Naunga mkono hoja.

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa utayarishaji wa Bajeti hii na ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo: Kwanza, Utafutaji wa Mafuta. Ningependa kufahamu ni nani anayegharimia huu utafutaji wa mafuta. Je kwa nini utafutaji huu umeanza siku nyingi lakini hadi leo kila mara tunasikia tu ya kwamba, Serikali imeweka mkataba na watafutaji wengine na kwamba mafuta yako kwenye ardhi yetu na itachukua muda gani hadi ukweli ufahamike? Utafutaji huu, Serikali yetu inagharimu kiasi gani? Je tunapata hasara yoyote katika zoezi hili la kutafuta mafuta?

Pili, nishati mbadala, ni kweli kwamba watu wengi wanatumia kuni katika shughuli mbalimbali za majumbani, hii ni kwa sababu umeme ni aghali sana pia hata gharama za kuvuta umeme kwa mtu binafsi ni aghali ambapo Wananchi vijijini itaendelea kuwa ndoto kwao kuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majiko bora, hayo nayo ni gharama kununua kwa wanavijiji wetu. Napenda kutoa changamoto kwa *TEMDO* watengeneze teknolojia ambayo mafiga ya kawaida ndiyo yatumike badala ya jiko bora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme nuru, nishati hii itaendelea kuwa ya kinadharia kwani hadi sasa umeme unaofadhiliwa na wahisani hii ni kutokana na vifaa *(equipment/components)* za kukingia huo umeme nuru ni aghali sana. Kwa hali hiyo, Wanavijiji wetu ambao ndiyo watumia kuni wakubwa, hawataweza kuwa na uwezo wa kuwa na umeme nuru.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji madini wanawake, hali zao ni duni, vitendea kazi hawana, soko la uhakika pia hawana. Serikali ichukue hatua za makusudi za kusaidia kundi hili, kwani kila siku wanazidi kuwa wengi na wana ari ya kufanya biashara hiyo ili kupata kipato.

Mheshimiwa Spika, Serikali isaidie wachimbaji ili watengeneze madini hapa hapa badala ya kuuza yakiwa machafu. Hii inawapunguzia bei na thamani, anayefaidika ni yule anayesafisha na kuuza kwa bei ya juu.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Naomba nianze kwa kuipongeza Wizara, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. Kazi wanayoifanya ni ngumu sana lakini uboreshaji unaendelea kuboreka.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme katika Jimbo langu la Misunguwi unaendelea vizuri, vijiji vilivyopangiwa kupewa umeme vimefikishiwa huduma hiyo japokuwa kuna tatizo la upatikanaji wa *Transformer*. Je, vifaa hivyo vitaletwa lini ili huduma hii ikamilike katika Taasisi za Sekondari ya Misasi, Shule za Msingi za Manawa, Pambani na Misasi, ikiwemo Chama cha Ushirika Misasi ambacho kiko tayari kutumia huduma hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo, umeme kwa ajili ya mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Shinyanga na Kahama utachukuliwa toka Misasi ukipitia Vijiji vya Buhingo, Seeke, Nyamayinza, Isesa hadi Nyang'homango (Ihelele). Naomba Serikali itumie nafasi hiyo kufikisha huduma hiyo katika vijiji tajwa, hii itaokoa uharibifu wa mazingira unaofanywa na wakazi wa maeneo husika kwa kukosa nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Spika pia naishukuru Serikali kuchukua umeme toka Kisesa Mwanza hadi Sumve kupitia Vijiji vya Fullo, Kanyerere A na B, Kolomije, Bugomba hadi Sumve, ni vyema vijiji nilivyovitaja vipewe huduma hiyo kwa nia ya kuokoa mazingira yanayoharibika kwa ukosefu wa nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia gharama ya kutumia umeme ikapunguzwa kwani iko juu mno.

Mheshimiwa Spika, ombi jingine ni katika vijiji ambavyo viko jirani kabisa na umeme ulipoishia mfano Kijiji cha Kijima kilometa nne kutoka Inonelwa, naomba wapewe huduma hiyo. Sekondari ya Busongo ni km. 10 toka Buhingo sehemu ambayo itapita umeme uendao kwenye mradi wa maji wa Shinyanga hadi Kayama. Vijiji vingine ni Nduha, Kasololo, Sumbugu hadi Mbarilla.

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa ufafanuzi juu ya uchimbaji madini katika Jimbo la Misungwi, je, ni maeneo yepi yanafanyiwa upembuzi na ni Kampuni gani zinafanya na je ni wapi wanachimba na ni Kampuni zipi?

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Ng'wamazengo, Buhunda (Ichakaya) Shilalo, Ng'wamanga, Mabuki yana utata, naomba maelezo ili niwafahamishe wananchi kuepusha uvunjikaji wa amani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kukubali bajeti ya Sh.179,933,476,200/= wapewe asilimia mia moja.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaongelea kuhusu kufikisha umeme Wilayani, Mkoa wa Kigoma bado haujapata umeme wa uhakika katika Makao Makuu ya Mkoa. Ieleweke kwamba, mkoa uko mpakani, umeathirika sana na Wakimbizi na tunaambiwa kwamba, Serikali iko kwenye hatua za awali za kufikisha umeme Kigoma. Hizo hatua zitaisha lini? Ujambazi unazidi kwa sababu ya giza.

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Kasulu na Kibondo hazina umeme, kwa nini hazipewi umeme wa *Generator* wakati tukisubiri huo wa *Grid?*

Mheshimiwa Spika, ahadi ni deni, wakati wa Kampeni Mheshimiwa Rais alitoa ahadi kwamba, ifikapo Desemba, 2000, Wilaya za Kasulu na Kibondo zitakuwa na umeme. Je ni kwa nini ahadi hiyo haijatimizwa mpaka sasa? Naogopa, tutawaambia nini Wananchi mwaka 2005 wakati wa Kampeni.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba, Serikali ya Sweden imeonyesha nia ya kutoa fedha, lakini haijatoa ahadi. Je fedha zisipotolewa kuna mpango gani mbadala? Nini kimekwamisha mradi wa umeme wa Mto Malagarasi? Je mpango wa umeme wa Burundi nao vipi?

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa Burundi, Mheshimiwa Nyandwi, ambaye alikuwa Balozi Mdogo wa Burundi nchini Tanzania, alionyesha nia ya kufuatilia suala la umeme wa kutoka Burundi. Sasa hivi Mheshimiwa Nyandwi ni Waziri katika Serikali ya Burundi, je, tunamweleza nini Waziri huyu, aache jitihada zake?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *generator* mpya ambazo Serikali imeahidi tunaomba ziletwe haraka. Tumechoka na kukatikakatika kwa umeme. Vyombo vingi vimeharibiwa na baadhi ya nyumba kuunga.

Mheshimiwa Spika, tabia ya kutuletea *generator* mpya zisizo na baadhi ya vipuri ni tatizo la kawaida Kigoma. Eti vipuri vimefuatwa Ulaya. Je hiyo siyo danganya toto?

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa umeme umekwamisha sana maendeleo ya Mkoa. Tunayo madini mengi lakini uchimbaji bila ya umeme haiwezekani. Hivyo, tunaomba tuambiwe ni lini, kwa tarehe, umeme utafika Kigoma na *generator* zifanye kazi ya uhakika wakati tukisubiri huo wa *Grid?*

Mheshimiwa Spika, nitashukuru kupata majibu ya umeme na nijue ni madini ya aina gani yanayopatikana Mkoani Kigoma? Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa Kagera Nkonda Wilayani Kasulu, ambao hawajui ni madini gani wanachimba na kuuza kwa bei ya kutupa ya Sh.2,000/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuwapongeza kwa dhati Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, pamoja na Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini na pia Viongozi wa Taasisi na Asasi zinazoongozwa na Wizara hii, kwa Hotuba hii nzuri na kwa kazi yao nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nami ningependa kuchangia kwa madhumuni ya kuhimiza maboresho katika maeneo ninayoyagusia hapa chini. Kwanza, Sekta ya Madini, ipo haja ya kuwa makini zaidi katika uwekaji mikataba ili Serikali na

kwananchi kwa ujumla, waweze kufaidika zaidi. Utendaji wa *Williamson Diamond* na *TANSORT* uchunguzwe.

Pili, wachimbaji wadogo wadogo wahamasishwe na kuwezeshwa kwa njia ya ushirika, mitaji na utaratibu bora wa masoko pamoja na kuwapatia usajili bila vikwazo na kuwalinda na vitimbi vya wakubwa. Aidha, mazingira bora ya kuwawezesha kuongeza tija na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, jitihada za makusudi zifanyike ili kupunguza bei ya umeme. Kuwepo na mpango kamambe wa upatikanaji wa umeme mbadala na endelevu pamoja na vianzio vya mkaa wa mawe, gesi, upepo na kadhalika. Uwekezaji katika sekta ya Nishati uhamasishwe ili kuboresha ushindani na hivyo kuwezesha bei ndogo ya nishati ya umeme na pia kuboresha huduma na kukomesha ukatikaji. Ama mkataba na *IPTL* utazamwe upya au Serikali iinunue mitambo ya *IPTL* mapema iwezekanavyo. Pamoja na dhana ya Soko Huria, kuna umuhimu mkubwa wa kudhibiti bei ya nishati, hasa kwa kuzingatia kwamba, bei kubwa ya nishati ina athari kubwa kwa uchumi

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe uanzishaji wa Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* na Mfuko wa Nishati Vijijini *(REA)*. Aidha, kukamilisha mpango kamambe wa upelekaji umeme vijijini ulio wazi mapema iwezekanavyo, ukiambatana na ratiba rasmi ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kumpongeza na kumshukuru Natibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa ziara yake Jimboni Mkinga mwaka 2003. Ziara yake hiyo ilihamasisha sana Wananchi wa Jimbo la Mkinga na kuwapa matumaini mapya hasa wananchi wa Vijiji vya Daluni, Gombero, Kwale, Manza na Mkinga, ambao kwa muda mrefu sana uliopita wanakuwa na shauku kubwa ya kupatiwa umeme. Lakini hivi sasa wameanza kukata tamaa kwani hakuna dalili za utekelezaji tokea wakati huo.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wamekata tamaa hasa kwa kutilia maanani kwamba, sio tu ahadi za namna hii zimekwishatolewa mara nyingi hapo awali, bali hata sehemu nyeti na muhimu kama Kituo cha Afya cha Mkinga bado hakijapatiwa umeme. Pia shule za Sekondari za Zingibari na Lanzohi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusisitiza kwamba, vijiji hivyo vinavyoomba umeme kwa awamu hii si kutokana na mahitaji ya kifasheni au anasa tu. Maeneo hayo yana nafasi kubwa ya uwekezaji katika viwanda vidogo na uvuvi ambao hauwezi kufanyika kwa mafanikio bila umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua kwamba maombi kama haya yapo mengi nchini pote, naiomba Wizara ifanye jitihada ya kukipatia umeme Kituo cha Afya cha Mkinga na angalau vijiji vitatu au viwili kati ya hivyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na kuitakia Wizara utekekezaji wa mafanikio.

**MHE. PAULO N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashauri fedha za mauzo ya Almasi za *TANSORT* zirejeshwe nchini *(Mwadui Mine)* ili kutengeneza

mazingira yaliyoharibiwa kwa machimbo na zisaidie kuleta maendeleo katika vijiji jirani na Mgodi wa Mwadui.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Mgodi wa *Mwadui Mine* na *El Hillal Minerals Limited,* ninaomba Wizara ilishughulikie haraka na kulitolea ufumbuzi, lina athari kubwa kwa viongozi na wakazi wa eneo hilo Wilayani Kishapu.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri na ninaiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umeonyesha kuwa umeme wa kutumia maji sasa si umeme wa kuaminika. Kwanza, maji ya kuzalishia umeme hutokana na mvua ambayo sasa si ya uhakika tena na hatuna uwezo nayo. Pili, maji kidogo ya kuzalishia umeme hayo hayo wakulima wanayatumia kwa umwagiliaji maji wa mashamba. Serikali imetuambia kwamba, kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa hiyo, kilimo hiki kinanyang'anyana maji na miradi ya uzalishaji wa umeme. Mvutano huu lazima utanzuliwe kwa kuondokana na umeme wa maji.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umetuonyesha pia kwamba, umeme wa *IPTL* nao si wa kutegemewa. Kwanza, umeme wa *IPTL* ni ghali sana na kwa miezi kadhaa mashine zake zimekuwa zikitumia mafuta ya kuendesha ndege. Hakuna nchi yoyote Duniani inayoendesha mashine zake za umeme kwa saa 24 kwa kutumia mafuta ya ndege.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Waziri inaonesha kuwa Mradi wa *IPTL* unafanyiwa marekebisho ili uweze kutumia gesi ya Songo Songo. Hata hili nalo ni gharama kubwa. Marekebisho haya yatatumia *US $* 11.6 milioni na tutalipia umeme huu mabilioni ya shilingi kila mwezi. Lakini upo ukweli mwingine wa kisayansi kwamba, katika maliasili zote duniani *(Natural Resources),* gesi ni *resource* ambayo huwezi ukawa na makadirio ya uhakika wa kiasi kilichopo ardhini.

Mheshimiwa Spika, lakini ukweli na uzoefu duniani unaonyesha kuwa umeme wa uhakika ni umeme wa makaa ya mawe. Nchi zilizoendelea zimefikia hapo kwa kutumia umeme wa makaa ya yawe. Sina haja ya kutoa takwimu jinsi gani nchi mbalimbali zinavyotumia umeme wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, Tanzania tunayo makaa ya mawe ya kutosha kwa miaka mingi ijayo. Wakati nchi zilizoendelea zinachimba makaa hayo kilomita mbili hadi kumi chini ya ardhi, lakini Tanzania makaa hayo yapo juu juu tu.

Lipo tatizo la *mind-set* miongoni mwa Viongozi wa Wizara na wataalam wake chini ya Katibu Mkuu, la kutoona umuhimu wa umeme wa Mchuchuma. Lakini ni dhahiri si kwa manufaa ya nchi hii. Zipo tafiti nyingi na za miaka mingi zinazoonyesha umuhimu wa kutumia makaa ya mawe tuliyonayo na soko la umeme huo. Bado ndani ya Wizara kuna kigugumizi juu ya umeme wa makaa ya mawe wa Mchuchuma. Sina haja ya kusema zaidi juu ya jambo hili, juu ya nani anapiga breki mradi wa Mchuchuma. Kielelezo ni ibara ya 30 ya Hotuba ya Waziri.

Waziri katika Hotuba yake amesema kuwa, wawekezaji wa Mradi wa Mchuchuma wameieleza Wizara kuwa wao wangependa kujenga kituo cha umeme chenye uwezo wa Megawati 400, wako tayari kujitafutia Masoko ya Umeme na hawataitaka *TANESCO* kununua au kulipia umeme zaidi ya mahitaji yake.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lilitegemea kusikia kwamba, sasa Serikali imewaambia wawekezaji kuwa wamepewa kibali waanze mara moja. Lakini si hivyo, Waziri anasema, Wizara imewataka wawekezaji hao kuthibitisha maelezo hayo.

Mheshimiwa Spika, unapofika hapo unaanza kutia mashaka juu ya *seriousness* ya Wizara juu ya mradi huu. Wawekezaji hawa pesa ni zao. Kama faida au hasara ni yao. Ni nchi hii ndiyo ina matatizo makubwa ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hatua za Wizara zifanane na haja hii ya umeme.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Maafisa wote wa Wizara hii, kwa kutayarisha bajeti hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ninauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, ninaiomba Serikali iangalie bei ya mafuta, imekuwa kubwa sana jambo ambalo ni usumbufu mkubwa kwa wananchi, bei ya mafuta ikipanda kila kitu kinapanda bei ikiwemo na gharama ya usafiri wa daladala na usafiri wa magari yanayokwenda mikoani. Wananchi wengi wanategemea kutumia usafiri huo, ninaishauri Serikali itafute njia yoyote ya kufidia ili mafuta yasipande mara kwa mara. Ninaomba Wizara hii izungumzie upandaji holela wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei mbaya ya umeme Wizara itafute njia ya kusimamia bei hii ya umeme vinginevyo wananchi walio wengi hawataweza kutumia umeme na baadaye watumiaji wa umeme watakuwa ni wale wenye uwezo tu. Ingekuwa vizuri masuala ya umeme likatazamwa upya ili walio wengi waweze kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji/utafutaji wa mafuta ni vizuri Serikali ikatoa tamko, je, mafuta yapo hapa Tanzania au hayapo? Kwa sababu ni muda mrefu sasa Serikali inatafuta mafuta lakini jibu sahihi Serikali haijatoa.

Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya wananchi wangu wa Korogwe Mashariki, kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wataalamu mbalimbali wa Wizara hii. Mchango wangu nitauelekeza katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu nishati. Umeme wetu mwingi unatokana na maji. Katika kufanikisha zoezi la kufanikiwa umeme wa maji *(Hydro),* ninaishauri Serikali kwa kutumia nguvu zake zote, kutekeleza Mradi wa *Stiggler's Gorge*. Mradi huu ndiyo mkombozi. Hata kama utachukua muda mrefu, ninaiomba Serikali hata kwa

kukopa ianze mradi huu muhimu. Mimi ninaamini mradi huu ndio pekee rahisi na utatuwezesha nchi hii kupata umeme wa kutosha. Ninaamini hata wawekezaji wengi watapenda kuwekeza nchini Tanzania. Hivi ni sababu zipi zinazofanya Serikali isianze mradi huu muhimu? Ninaomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, umeme Wilayani Korogwe, ninasikitishwa sana na ahadi nilizopewa na Wizara hii kwa ajili ya kupatiwa umeme katika vijiji vifuatavyo: Kwagunda, *Gereza East*, Mkwakwani, Kwenzindawa hadi Mnyuzi. Mradi huu niliahidiwa na kupata jibu humu ndani ya Bunge kwamba, ningepatiwa umeme katika vijiji hivyo ambavyo vipo kwenye barabara moja toka Kwagunda hadi Mnyuzi. Ahadi ni kupatiwa umeme katika mwaka 2002/2003, lakini hadi leo hii umeme huu ulianzishwa tu kuwekwa Kijiji cha Kwagunda lakini kuendelea kwenda *Gereza East,* Mkwakwani na Kwenzindawa bado. Kwa bahati mbaya baada ya kupatiwa ahadi hiyo, nilikwenda kuwahamasisha wananchi wajenge nyumba nzuri na kuweka *wiring* lakini sasa kibao kimenigeukia na kuonekana mwongo. Sasa Mheshimiwa Waziri, ninaomba sana mniokoe kwa kumalizia mradi huo muhimu. Ninaomba majibu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili ni kuweka umeme Kijiji cha Kerenge Kibaoni. Kwa bahati nzuri kutoka Kerenge Makaburini hadi Kerenge Kibaoni ni kilometa mbili tu. Ahadi ni kumaliza mradi huo mwaka 2003/2004. Ninaomba sana mradi huu nao utekelezwe na niambiwe utaanza lini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara inisaidie kupeleka umeme katika sehemu Nyeti zifuatazo: *Senkiwa Secondary School,* Korogwe Mjini, *Magoma Secondary School, Hale Secondary School* na *Old Korogwe Secondary School.* Hizi ni Taasisi muhimu ambazo zinahitaji kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika karne ya leo, *Secondary* kutokuwa na umeme siyo sahihi. Kwa bahati nzuri *Grid* ya Taifa ipo karibu sana na Shule hizo hazizidi kilometa moja au mbili. Ninaomba jibu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala la wachimbaji wadogo wadogo wa Kalalani wapatiwe msaada wa vifaa vya kisasa ili kuwaongezea tija. Swala hili ni la muda mrefu, lakini utekelezaji wake umekuwa hadithi. Ninaishauri Serikali isaidie vikundi hivi vya Kalalani ambavyo vipo tayari vimejipanga, wameleta maombi lakini hadi leo hii hakuna dalili zozote za kuvisaidia wapate vifaa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana wachimbaji wa Kalalani watendewe haki kama wanavyofanyiwa wa maeneo ya Mererani. Ninaomba sana na kushauri wachimbaji hawa wadogo wadogo wa Kalalani wapatiwe nyenzo muhimu za kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuinua uchumi kwa Watanzania.

Nitumie pia muda huu kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kukusanya fedha zaidi ya makisio hivyo kabla sijaanza kuchangia, napenda nitamke rasmi kuwa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia nikianzia na huduma ya umeme kama ifuatavyo:-

Naipongeza Serikali kwa hatua kubwa waliyofikia katika kusambaza umeme Mkoani Singida. Hali hii imetia faraja sana kwa wananchi wa mkoa wangu. Naomba huduma hii nzuri iendelee kwani bado kuna maeneo mengi ambayo yana wakazi wengi na uwezo wa kuvuta umeme wanao mfano Makao Makuu ya Tarafa ya Ihanja ambapo kuna Taasisi nyingi, Shule ya Sekondari ya Ufundi, Shule ya Msingi, Kituo cha Afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tayari nguzo zilishasambazwa basi hatua ziendelee, vilevile Iramba ya Mashariki, Nkungi, Iambi, Nduguti, Gumanga, Mkalama, Ibaga na kadhalika, Wananchi wako tayari na wana kiu hasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuishauri Serikali ilitafakari suala la kupanda kwa bei ya umeme kwani Wananchi sasa wanaona Serikali imeshindwa kuwapa huduma. Kwa kuwa huduma hii ilishakuwa chini ya wawekezaji, basi ni kukaa nao kuona jinsi gani wanaweza kupunguza bei ama gharama ya matumizi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ukweli wananchi walikuwa na *speed* kubwa sana kuvuta umeme lakini sasa *speed* hiyo haipo ama imepungua kwa kiasi kikubwa. Hata vitega uchumi vyao vinaanza kufa kwa kushindwa gharama, mfano, viwanda vidogo vidogo zikiwemo mashine za useremala, mashine za kukamua mafuta ya alizeti, mashine za kusaga na kadhalika. Naiomba Serikali iwajali sana Wananchi wenye vipato vya chini ambao ndiyo wengi katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika vilevile naiomba Serikali ikumbuke kupeleka umeme vijijini ambako kuna wakazi wengi, mfano, Kijiji cha Mgongo hadi Nkonkilangi, vilevile Kijiji cha Mgongo kuna machimbo ya Dhahabu. Hivyo, wakipata umeme Serikali itakuwa imewarahisishia kazi ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuieleza Serikali kuwa, Mkoa wa Singida una madini mengi sana hasa ya dhahabu huko Mgongo Tarafa ya Shelui, Misigiri Tarafa ya Kinampanda, Wilaya ya Singida vijijini huko Tarafa ya Ihanja, Minyuge na Mwihintiri, Manyoni Tarafa ya Nkonko.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanatambua sana maliasili zilizozopo vijijini kwao na wanajitahidi sana kuchimba, tatizo kubwa ni vitendea kazi mfano mitambo ya kuchimbia, Mekyuri na vingine vingi. Hasa akina mama sasa hivi wapo mbele sana katika kuchimba madini hasa akina mama wa Mgongo/Senkenke Tarafa ya Shelui.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwasaidie hata kuwakopesha vifaa hivi ili kuwarahisishia kazi hii ya kuchimba madini ya dhahabu. Nawapongeza viongozi wanawake na wake za viongozi ambao wametoa msaada kwa wanawake waliojiunga na kuendesha mradi wa kuchimba dhahabu, mfano, viongozi waliosaidia ni Msaidizi wa

Balozi wa *South Africa,* Katibu Mkuu wa UWT, Mama Halima Khatibu, wake wa viongozi, Mama Anna Mkapa, Mama Esther Sumaye, Mawaziri Wanawake na viongozi wengine wote wakiwemo Wabunge.

Mheshimiwa Spika, akina mama wanajitahidi kuinua hali zao za maisha na familia kwa ujumla bali Serikali haijawasaidia ama kuwawezesha. Kuwasaidia akina mana siyo suala la Halmashauri peke yake au Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ni pamoja na Wizara ambazo mradi huo unahusika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali vilevile iwe makini sana katika kusoma mita kwani mara nyingi inatokea nyumba zenye matumizi makubwa ya umeme hupata bili ndogo na zenye matumizi madogo hupata bili kubwa. Hii inawafanya wateja kutokujenga imani na Serikali yao. Vilevile kuna tabia ya wateja kuchezea mita na kuanza kutoa takwimu ambazo si sahihi. Hivyo, naiomba Serikali ifuatilie nyumba ambazo bili zao zinaleta mashaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitumie nafasi hii kumpongeza Meneja wa *TANESCO* Singida, pamoja na Watendaji wote, kwa juhudi yao kubwa ya kutoa huduma za haraka pale panapotokea hitilafu ya umeme pamoja na kupeleka umeme vijijini. Kwa hakika Singida hali siyo mbaya, naiomba Serikali iwaboreshee vitendea kazi na mafungu ili juhudi hizi ziendelee. Napenda niunge tena mkono hoja.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja hii. Nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Watumishi wote kwa kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, barabara inayojengwa sasa toka Singida kwenda Manyoni imepita katikati ya Mji wa Singida. Ili barabara ipanuliwe ilibidi nguzo za umeme zihamishwe na zisogezwe. *TANESCO* kwa kusogeza nguzo hizo wamelipwa fidia. Tatizo lililojitokeza kuhamishwa kwa nguzo hizo ni kwamba, sasa zimewekwa karibu sana na nyumba za watu. Zingine zipo milangoni mwa nyumba. Nguzo hizo zingine waya zinapita juu ya paa mbele ya nyumba. Ninavyojua upo umbali unaotakiwa kati ya nguzo na nyumba, vipi leo umbali huo umekiukwa?

Mheshimiwa Spika, nashauri wenye nyumba wahamishwe na kufidiwa ili umbali unapohitajika upatikane au *TANESCO* watafute njia nyingine ili wahamishe nguzo hizo pasije pakatokea maafa bure.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa na tayari Wananchi wamelalamika kwangu, Wizara ya Ardhi, maana nguzo zipo kwenye viwanja vyao. Naomba ufumbuzi wenye maelekezo ya haraka wakati unatoa majumuisho. Wananchi wanangojea sana maelekezo ya Serikali.

**MHE. EDWARD N. LOWASSA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wataalam, kwa hotuba nzuri. Lazima tukubali kwamba, umeme ni nyenzo katika dunia ya utandawazi. Nina mambo mawili yafuatayo:-

Kwanza, nampongeza Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Arusha kwa kazi nzuri na ushirikiano anaotupatia.

Pili, umeme wa kutoka Mto wa Mbu kupitia Makuyuni unaanza kujengwa lini?

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Mji wa Tarime, kila mvua ikinyesha ni lazima umeme ukatike Tarime Mjini. Unapokuja unaleta maafa makubwa pamoja na kuharibu vifaa vya watu ambao wanatumia umeme huo kama nishati. Tatizo hilo limeendelea kwa muda mrefu, suluhisho ni nini?

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wanapompa mteja umeme, kama huyo mteja hakulipa, mtu mwingine anayeingia katika hiyo nyumba analazimika kulipa kwa nini?

Je, hatima ya mgogoro kati ya Wananchi na *Afrika Mashariki Gold Mines* ni nini?

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono bajeti hii kama sitapata maelezo kuhusu Wilaya ya Mbinga, yenye zaidi ya wakazi 405,000, Wilaya iliyoanzishwa mara baada ya uhuru, Wilaya inayozalisha zaidi ya asilimia ishirini ya Kahawa Tanzania, Makao Makuu yake kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mbinga una viwanda vikubwa vitatu vya kusindika kahawa na ngano. Mji huo una Taasisi mbalimbali za huduma za uchumi kama vile mabenki, simu, mashule, hospitali vyuo vya ufundi, wafanyabiashara wa jumla na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kila Taasisi inatumia jenereta lake na hivyo, kuhatarisha usalama wa watumiaji. Licha ya kuwa gharama za uzalishaji na huduma ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na mawasiliano mengi kati ya Wananchi wa Mbinga kupitia Wawakilishi wao lakini hakuna anayejali wala kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001, Naibu Waziri alitembelea Mbinga, ili kuhakikisha kama Mbinga upo umeme kama vitabu vya Serikali vinavyoonyesha, Waziri alikiri kuwa Mbinga hakuna umeme. Viongozi wa Mbinga, walimnukuu Naibu Waziri kuwa, aliahidi angalau kupeleka jenereta kama jawabu la muda mfupi. Naomba akanushe kuwa hakutoa ahadi hiyo ili wale aliowaambia wamsikie.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mbinga walimweleza Waziri Mkuu kuhusu tatizo sugu la umeme, walimwashia vibatari, akatoa matumaini.

Mheshimiwa Spika Makamu wa Rais alielezwa kuhusu tatizo hilo, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa, Wizara kazi yake ni kudanganya. Sasa naomba Waziri aniambie, twende kwa nani au Mbinga siyo sehemu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimewahi kumweleza Waziri kuhusu mgogoro kati ya wachimba madini wadogo na wawekezaji wakubwa katika machimbo ya Masuguru. Wilaya ya Mbinga, upo unyanyasaji na vurugu chungu mbovu.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yanaashiria rushwa, kwa sababu Afisa Madini Mkazi alitoa vibali kwa wachimbaji wadogo ambao ndiyo wenye kumiliki mashamba hayo. Lakini Waziri alitoa maeneo hayo kwa Mwekezaji mkubwa, bila hata kukubaliana na Ofisa wake wa Mkoa ambaye anafahamu jiografia ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atamke nani ana haki na kwa nini Wachimbaji wadogo wanyanyaswe kiasi hicho? Kwa nini Serikali imeshindwa kuwawezesha wachimbaji madini wadogo ambao ni raia wa nchi hii?

Mheshimiwa Spika, nashauri eneo hili libakie kwa wamilikaji halali wa maeneo husika na siyo uvamizi wa kibabe kama inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, ilibidi mimi niende kutuliza ghasia katika eneo hilo hasa baada ya Mkuu wa Mkoa kutishia kuwasambaratisha wachimbaji wadogo kwa kupeleka vikosi vya ulinzi na usalama. Niliwasihi wawe watulivu ili Serikali itoe suluhisho. Kwa hiyo, nahitaji majibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nitasita kuunga hoja hii mkono, kwa jinsi Wizara hii inavyoshindwa kuona kuwa kutokana na uzalishaji mkubwa unaofanywa na Wananchi wa Mbinga, wanastahili kuwezeshwa na Serikali yao.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa wengi kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ningependa kutoa malalamiko yangu kuhusu umeme Longido na Namanga. Nakumbuka mwaka 1997, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alitembelea Longido na Namanga, akaahidi kwanza kabla ya uchaguzi wa mwaka 2000 umeme utakuwa umefika Namanga. Naomba ufafanuzi ni lini umeme utafika Namanga?

Mheshimiwa Spika, hii ahadi ya Serikali kwa Wananchi wa jimbo langu mtawaambiaje kwenye kipindi cha Uchaguzi na kwa kuwa ni Rais mwenyewe aliyeahidi, si ingekuwa busara Waziri afike kueleza hali halisi?

Mheshimiwa Spika, kuna tofauti kubwa kati ya *Net Group Solutions* na Wananchi, lakini Serikali wanaona kwamba, *Net Group Solutions* wanafanya kazi nzuri. Je Serikali wataona hiyo tofauti inatokana na nini ili wasuluhishe jambo hili? Hapa Bungeni Wabunge wanailaumu sana *Net Group Solutions.*

Mheshimiwa Spika, tunatazamia kushindana na nchi jirani kwenye Soko Huria, je, kama Viwanda vitashindwa kuzalisha tutaweza kuzalisha?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali wakae na *Net Group Solutions* kuangalia mambo mawili yafuatavyo:-

Kwanza, tofauti kubwa kati ya Wananchi na *Net Group Solutions* ambayo inaonekana hawana imani nao, haiwezekani wateja kuwa na malalamiko kila mwaka. Ni vizuri kubainisha makosa ya pande zote na kuyatatua.

Pili, kuangalia bei ya umeme ipungue ili wananchi waweze kumudu kulipia umeme, ili wenye viwanda waweze kutumia kwa wingi kuzalisha bidhaa kwa gharama nafuu.

Tatu, tofauti kubwa kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo hasa wawekezaji na wenyeji, ambao wana malalamiko kuhusu maeneo ya migodi.

Nne, wachimbaji kuingilia maeneo na kuchimba bila ridhaa ya Wananchi. Kwa mfano, kuna Kampuni ambayo wameingia Kijiji cha Mundarara Jimboni Longido na kuanza kuchimba na kuweka mashimo makubwa hata kama *PR* wanaotoka Ofisi ya Madini inafaa waone wana vijiji ambao ardhi ni yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa malalamiko ni mengi, afadhali uongozi utumwe kila Kijiji kwenye maeneo husika.

Narudia kusema kuwa, naunga mkono hotuba ya Waziri.

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nimelazimika kuchangia Hotuba hii kwa maandishi kwa sababu suala zima la Nishati na Madini linahusu maendeleo ya Taifa na linagusa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wizara, kwa kuleta mbele ya Bunge lako Tukufu, Hotuba yenye ufafanuzi wa mwangaza na matumaini makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti ya Wizara ya mwaka 2004/2005 kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumzia maendeleo kiuchumi, kijamii, kiteknolojia au kiburudani, hatuwezi kutenganisha umuhimu wa umeme kama nishati na nguvu mbadala wa misuli ya binadamu katika kutekeleza nguvu kazi kwenye kufanikisha majukumu na ratiba za maendeleo.

Kwa hiyo, mchango wangu katika suala hili la Nishati na Madini nitaomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi na maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Eneo la kwanza ni lile la kusikitisha na kushangaza kwa Serikali kuamua kusitisha kusambaza umeme vijijini ili kukidhi matakwa na masharti ya Mkataba wa Menejimenti mpya ya *TANESCO (Net Group Solutions)*. Kitendo hiki ni sawa na kutangaza kuwa, Taifa limedhamiria kuvinyonga vijiji kimaendeleo mpaka itakapotayarishwa Taasisi za *REA* na *REF* ambazo ndizo zitashughulikia kuendeleza usambazaji umeme vijijini. Sera hii ya kunyonga vijiji kimaendeleo ni kukidhi matakwa ya Menejimenti mpya ya Wageni *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, leo ni wakati wa utandawazi na Sekta zote kama kilimo, elimu (mashule), viwanda (usindikaji wa mazao), mawasiliano, na kadhalika, yanahitaji

umeme. Serikali inapositisha usambazaji umeme vijijini maana yake asilimia themanini ya Watanzania wananyimwa Nishati ya kujiendeleza kwenye elimu *(computerization),* kilimo (kusindika mazao), mawasiliano (simu, *internet, TV, radio,* magazeti), burudani na kadhalika. Maana yake Serikali inaona heri mijini, maeneo ya barabara kuu, ndio yawe katika mwangaza na vijiji kwa muda usiojulikana vikae gizani.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Mheshimiwa Waziri aelewe kuwa katika Wilaya ya Iramba kwa sasa hatuna migodi ya madini lakini Mgodi wa Iramba sasa ni Ziwa la Kitangiri, ambalo linazalisha samaki wengi sana na kuna wavuvi wengi kutoka mikoa mingi ya Tanzania na hata Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kuteleleza ombi la Wananchi wa Kata za Tulya, Ntwike na Kidaru, kupelekewa umeme kusudi nao wafarijike kuendesha Mgodi wao wa Ziwa la Kitangiri. Ombi la umeme kupelekwa kwenye vijiji hivi ni la siku nyingi lakini wageni walipofika *TANESCO* wakasitisha.

Mheshimiwa Spika, kabla ya Menejimenti ya Wageni kushika hatamu *TANESCO,* vijiji vifuatavyo Wilayani Iramba vilipeleka maombi na vingine vimekwishalipia kupatiwa umeme: Munkonze, Barazani, Mtumbili, Uwanza, Kitusha, Maluga, Kibigiri, Mgongo, Kishalita, Sekenke, Kisiriri na Kinambeu. Wageni walipochukua madaraka wakasitisha na kutia kapuni maombi ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, aingilie kati.

Mheshimiwa Spika, ningeomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, ni nini hatima ya utafutaji *(exploration)* wa Madini ya Dhahabu Wilaya ya Iramba ambao umefanywa na Kampuni ya *Barrick International* takriban kwa miaka mitano. Mwaka 2003 walionekana kufunga kambi yao Kijiji cha Salala, Kiomboi, lakini hawajatoa Ripoti yoyote nini wamepata, yaani wana usiri mkubwa mno. Mwaka wa mwisho wa shughuli zao walileta vifaa vizito *(Heavy Drilling Equipment)* na walichimba na kupata mawe na udongo wa ajabu ajabu. Cha kushangaza karibu mawe yale na udongo, takribani tani moja mpaka tatu, wameondoka nayo lakini kuna usiri wa kushangaza kuhusu mizigo ya mawe na udongo waliondoka nao.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, awaeleze Wananchi wa Iramba, kuhusu hatma ya udongo na mawe yaliyokimbizwa Canada na *Barrick International Corporation*.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie kifedha na kiufundi (vifaa), uwezekano wa kuendeleza miradi midogo midogo ya *biogas* katika Wilaya ya Iramba. Mimi binafsi katika Kijiji cha Munkonze nimeanzisha Mradi wa *biogas*, ambao Wananchi wengi wa Iramba wamekuja kujionea na kujifunza na sasa wanataka kuanzisha katika majumba yao. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha amewahi kutembelea na kuona mradi huu wa *biogas* wa Kijiji cha Munkonze.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALHAJI SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini, naomba kwa ajili ya kumbukumbu za *Hansard* ili hoja yangu iwe katika kumbukumbu za Waheshimiwa Wabunge, nimeona ni vizuri nitoe maelezo ya maombi yangu ya kupatiwa umeme *Berega Anglican Mission Hospital, Mgugu Secondary School,* Berega, Magubike na Maguha katika kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumatatu tarehe 17 Julai, 2000, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya ziara katika Wilaya ya Kilosa. Katika ziara hiyo alifanya kazi nne. Kazi ya kwanza, alifungua daraja la Mto Berega. Kazi ya pili, alitembelea Hospitali ya Berega. Kazi ya tatu, alihudhuria Mkutano wa hadhara katika viwanja vya *Berega Anglican Church.* Kazi ya nne, aliweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mgugu na kufanya mkutano wa hadhara katika viwanja vya shule ya Sekondari ya Mgugu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya mkutano wa hadhara na wananchi katika viwanja vya *Berega Anglican Church,* Viongozi wa Hospitali ya Berega walitoa taarifa kwake ambayo katika taarifa hiyo walimweleza matatizo yao ikiwemo upungufu wa madawa ya binadamu na ukosefu wa umeme. Aidha, walimweleza kuwa Hospitali ya Berega inatoa huduma za tiba kwa Mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma kwa Wilaya za mikoa hiyo zilizokuwa karibu na hospitali hiyo na pia wanatibia watu wa Mkoa wa Morogoro. Walimweleza kuwa wanapata huduma za *Flying Doctors* kutoka Nairobi - Kenya. Walimweleza pia Hospitali ya Berega ndiyo Hospitali kubwa pekee katika mwambao mwa barabara kubwa inayotoka Morogoro kwenda Dodoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikia taarifa hiyo, Mheshimiwa Rais alitamka kuwa, atamweleza Mama Anna Mkapa, apeleke madawa Hospitali ya Berega. Baada ya kuweka Jiwe la Msingi katika Shule ya Sekondari ya Mgugu, alielezwa katika taarifa ya shule hiyo tatizo kubwa la shule hii ni kukosa umeme wa *Grid* ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hesima na unyenyekevu mkubwa, naomba kukueleza kuwa ahadi aliyoitoa kuwa atamwambia Mama Anna Mkapa apeleke madawa katika Hospitali ya Berega, ilitekelezwa. Mama Anna Mkapa alipeleka madawa katika Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kukujulisha kuwa ahadi aliyoitoa ya kupeleka magodoro 200 katika Shule ya Sekondari Mgugu ameitekeleza. Shule hii ya Mgugu ilipata Magodoro 200. Pia ahadi aliyoitoa katika mkutano wa hadhara katika viwanja vya Shule ya Mgugu Sekondari ya kujenga maktaba vilevile imetekelezwa. Maktaba imejengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa hadhara katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Mgugu alitoa ahadi kuwa atakuwa anafanya ziara ya kutembelea eneo hilo la shule bila kutoa taarifa rasmi kila atakapoona inafaa. Naomba kukueleza kuwa ahadi hii aliitekeleza. Alikuja ghafla bila ya kutoa taarifa ya ufanyaji wa ziara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, Mheshimiwa Rais aliahidi ataliwasilisha kwa Wizara inayohusika. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa shukrani zangu kwa niaba ya Wananchi wa Berega kwamba, ahadi yake aliitekeleza. Kwa taarifa nilizonazo, baada ya Ikulu kupeleka suala hili Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ilimwandikia *Regional Manager* wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro awapelekee taarifa inayohusu mradi wa kupeleka umeme kutoka Dumila, Maguha, Magubike na Berega kama upo *viable. Regional Manager* wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro alitekeleza kama alivyoagizwa na Wizara ya Nishati na Madini. Taarifa ya *Regional Manager* wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro, imeeleza mradi wa umeme kutoka Dumila - Maguha, Magubike - Berega ni *viable* lakini ungegharimu kwa wakati ule Sh.600,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, suala hili nimelifuatilia kwa karibu zaidi. Ufuatiliaji wangu umepelekea Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kufanya ziara ili ajiridhishe kama mradi huu kweli ni *viable.* Naomba kumshukuru Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa sababu baada ya yeye mwenyewe kutembelea eneo la *Berega Hospital,* Shule ya Sekondari ya Mgugu, Magubike na Maguha, aliridhika kwamba, taarifa iliyotolewa na *Regional Manager* wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro kwamba, mradi huu ni *viable* ni sahihi. Naomba kukujulisha katika ziara hiyo aliyoifanya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alitoa ahadi ya kutoa madawa. Ahadi hiyo ameitekeleza, amepeleka madawa katika kituo cha Afya cha Tarafa ya Magole pale Magubike.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, wakati alipokuwa anakabidhi madawa katika kituo cha Afya cha Tarafa pale Magubike, alitamka kwenye mkutano wa hadhara kuwa suala la umeme halipo tena katika mabega ya Mbunge wenu ila lipo Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii ya umeme nimeshawahi kutoa ushauri kwa Waziri wa Nishati na Madini kama mradi wote haiwezekani kujengwa mara moja katika awamu moja, Wizara ya Nishati na Madini, ipange utekelezaji wa mradi huo katika awamu tatu. Nilitoa ushauri huo kwa nia ya kutekeleza ahadi iliyotolewa kwa Wananchi katika Mkutano wa hadhara lakini kwa masikitiko makubwa, ushauri wangu haujazingatiwa. Kwa ajili hii, naomba kuleta taarifa hii kwako kukujulisha kuwa ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais karibu miaka minne sasa ya kupeleka umeme Hospitali ya Berega na Shule ya Sekondari ya Mgugu kwa kupitia Vijiji vya Maguha na Magubike kutoka Dumila bado haijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutanguliza shukrani zangu kwako kwa matumaini kwamba, Wizara ya Nishati na Madini itatekeleza ipasavyo kwa sababu mradi huu una uwezo wa kujilipa kama *Regional Manager* wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro, taarifa yake aliyopeleka Wizara ya Nishati na Madini inavyoeleza.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimweleze Waziri wa Nishati na Madini kuwa, lipo tatizo kubwa la upatikanaji wa nguzo za umeme katika Mkoa wa Morogoro na hasa katika Jimbo langu la Kilosa. Mpaka sasa ipo idadi kubwa ya Wananchi wanaotaka kupelekewa umeme lakini wanakwamishwa kwa ukosefu wa nguzo za umeme na sehemu nyingine uhaba wa upatikanaji wa *Transformer.*

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huu, namshauri Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, akubali kupeleka nguzo za umeme na kuwapatia *Transformer.*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Watendaji, Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania katika Karne hii ya 21 ambayo ni karne ya Sayansi na Teknolojia Duniani (ulimwenguni).

Mheshimiwa Spika, kati ya misingi mikuu ambayo inaweza kuipeleka nchi katika maendeleo, ni kuwepo Sera na Mipango mizuri katika Elimu na Viwanda katika uzalishaji na uendeshaji wa uchumi wa nchi husika. Vitu hivi viwili ni muhimu sana kwa maendeleo ya kweli ya nchi na Wananchi wake (raia).

Mheshimiwa Spika, bila ya kuwepo nishati ya umeme wa uhakika katika nchi ambayo inapigania kujenga uchumi na maendeleo, kwa kweli kwa karne hizi za leo huwezi kuendesha shughuli za viwanda katika uzalishaji na kujenga uchumi na maendeleo ya watu wa nchi yako husika.

Mheshimiwa, kwa hiyo, ninaiomba sana sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yake hii ya Nishati na Madini, kuweka mipango madhubuti na ya kweli kabisa kusambaza umeme katika Wilaya zetu zote na vijiji vyetu vyote hapa nchini sambamba na mipango madhubuti iliyowekwa na Serikali katika masuala ya Elimu, Afya, Maji na Barabara.

Mheshimiwa Spika, kuanzia sasa ninaiomba Wizara hii kuona umuhimu wa nishati hii kwa Taifa letu na watu wake wote nchi nzima isiwe kwa baadhi ya miji na Mikoa kama ilivyo sasa. Serikali Kuu kwa kushirikiana na Wafadhili mbali mbali wa Kimataifa, Nchi wahisani na Mashirika ya Fedha na Taasisi nyingine duniani, kuona umuhimu wa kuwapatia wananchi wote huduma hii ya Nishati kwa maendeleo yao na Taifa lao kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Oktoba, 2003, Serikali ilipitisha Sera yake ya Habari na Utangazaji hapa nchini na kuainisha kuwa sekta hii ni moja ya Sekta ya Huduma ya Jamii Nchini.

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa kuwa Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya Raia kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 18 ya Katiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia ni kuwa Wananchi wengi wanaoishi katika miji mikubwa hapa nchini na baadhi ya Mikoa na Wilaya ambazo tayari zimepata umeme wanapata taarifa mbalimbali ya hapa nchini na zinazotoka nje ya nchi yetu kupitia Televisheni na Mitandao mingine mbali mbali, jambo ambalo kwa Wananchi wengi wanaoishi vijijini hawapati kutokana na maeneo mengi ya vijiji vyetu nchini hayana umeme pamoja na kwamba hivi sasa baadhi ya vijiji vingi vina miradi mikubwa ya maendeleo kama vile mashule, zahanati, miradi ya maji na barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye mipango ya kupeleka umeme vijijini kwa haraka iwezekanavyo ili pia umeme huo uwekwe katika haya mashule mazuri yaliyojengwa ili kuwawezesha wanafunzi wetu wa shule za msingi na Sekondari vijijini kutumia na kujifunzia kompyuta na mambo mengine ya kisayansi na teknolojia za kisasa.

Mheshimiwa Spika, pia katika Vituo vya Afya ambavyo vitalazimika kuwa na *Laboratory* , miradi mikubwa ya maji iwekwe *transformer* na kadhalika. Ninaipongeza Serikali ya Norway pamoja na Shirika lake la misaada la *NORAD* kwa kutoa msaada wa fedha shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kuvifanyia matengenezo vituo vitatu vya umeme vilivyopo eneo la Wesha Pemba. Pia Serikali hii ya Norway na Shirika lake hili la *NORAD* hivi sasa linasaidia mradi wa kusambaza umeme katika vijiji 63 vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Serikali yetu ya Muungano, pamoja na Serikali hii ya Norway na Shirika lake hili la *NORAD* kwa misaada hii mikubwa ya kimaendeleo kwa Zanzibar na Wananchi wake kwa ujumla. Kwa kweli hapa nina uhakika na juhudi za Serikali ya Muungano zimetumika pamoja na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ni matumaini yangu kuwa, Norway itaangalia uwezekano wa kukipatia umeme Kisiwa cha Pemba kutoka Tanga.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Viongozi na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri inayoonyesha mwelekeo, mikakati na jitihada za Serikali katika kufanikisha utoaji huduma safi kwa Taifa na Wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nina maombi machache yafuatayo: Kwanza, naomba kwamba Serikali inapopewa fedha za ziada *(Supplement Budget),* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, umeme au Nishati inapatikana wakati wote kwa viwanda na majumbani, basi umeme huo upatikane kweli. Hapa Dodoma *"Area C"* umeme unakatwa karibu kila siku kati ya saa tatu na nusu na saa saba na nusu hadi saa nane mchana kulikoni, isije ikawa ni hujuma ya *TANESCO?*

Pili, kwa kigezo hicho hicho cha hapo juu, *almost every other day if not daily*, umeme unakatwa kuanzia *most times* saa nne hadi saa kumi na nusu jioni, maeneo ya *Jangwani Beach (Whitesands Hotel)* Dar es Salaam kulikoni?

Tatu, Wananchi wananung'unika sana hasa kwa Mkoa wa Dar es Salam kwa kupandisha bei za kuvuta *service line* kwenye nyumba mpya. Bei zilianzia Sh.50,000/= huko nyuma na sasa hivi ni zaidi ya Sh.200,000/=.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, huyu mteja ni wa kudumu, hivyo, kumlimbikizia mzigo wa fedha nyingi hivyo si vizuri. Ni vyema *TANESCO* wakapunguza gharama ya *service line* iwe chini huku *TANESCO* wakijua kwamba, huyu mteja wao mpya ni *for life* hivyo wa-*spread* huo mzigo *over a period of over 20 years. Come down to shillings 50,000/= per service line please.*

Nne, juzi *TANESCO* wamepandisha *tariff* zao kwa home *users.* Najua wamefanya hivi kwa ulafi wa kupata chao mapema, *Net Group Solutions.*

Mheshimiwa Spika, huyu mteja anatumia umeme nyumbani ikiwa ni Sera ya Serikali hii kuleta ustaarabu, maendeleo endelevu ya kutumia nishati hii. Sasa Serikali hiyo hiyo inaanza kumkatisha tamaa huyu mwananchi kwa kuwa mpenda maendeleo, mstaarabu na mtu mwenye kujali mazingira kwa kumpandishia bei ya umeme. Huyu mtu atalazimika kurudi kwenye matumizi ya kutumia mkaa, matokeo yake *desertification* ya nchi yetu. Watakata miti yote na huku *Net Group Solutions* ikatuachia jangwa na wao na *exorbitant profits* wakirudi kwao Afrika ya Kusini. *We will look very stupid at the end of the day. Please please* liangalieni hili tatizo la upandishaji gharama za umeme wa majumbani. Vinginevyo wateja wa umeme watapungua na watakaorudi kwenye kutumia mkaa wataongezeka. Jambo ambalo ni hatari sana kwa mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, naunga mkono hoja. Nitachangia maeneo matatu: Kwanza, eneo la nishati mbadala, umeme nuru *(Solar)* na umeme wa Gridi Kondoa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wanahitaji umeme/nishati mbadala kwa sabu wamechoshwa na kusaka kuni hasa vijijini 80% huishi huko, hasa wanawake wavuja jasho zaidi. Wamechoshwa na adha ya moshi machoni, kwenye nyumba moshi huharibu nyumba, lakini wanawake huumia zaidi wanachakazwa na Moshi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kupata kuni sasa yapo mbali sana. Muda mwingi wa zaidi ya saa nane hutumika kwa ajili ya safari au mwendo mara mbili kusaka kuni. Kiuchumi tunapoteza muda na umaskini hautoki. Hivyo, Serikali kwa kufa na kupona, ieneze kwa Wananchi majiko sanifu na bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, pia Wananchi wetu wanahitaji umeme nuru *(solar)*. Huu ndio umeme wa watu maskini, vijjini upunguzwe bei ili uenee vijijini kwa haraka kwa sababu siyo ghali.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji wawekeze umeme huu kule vijijini ili kusisimua maendeleo ya kisasa kwa sababu mazingira hayataharibiwa, kazi za mitulinga zitapungua sana, Wanawake watapata afueni vijijini.

Mheshimiwa Spika, kazi zenye teknolojia ndogo ndogo zitaibuka, za useremala, upasuaji mbao, uchomaji vyuma, ufundi vyuma, ufundi umeme, kazi za ajira zitaongezeka na kuunganisha vijana. Hatima yake ni kuondosha umaskini. Tutumie mawakala ili kueneza umeme nuru, ambao utakuwa ukombozi kwa wananchi. Kondoa tulipata umeme wa Gridi tangu mwaka 1998/99 mpaka leo ni miaka minane hivi. Umeme huo umetokea Babati. Vijiji vifuatavyo vimepitiwa na nyaya za umeme na wanalinda usalama wa njia: Kijiji cha Puhi, Bereko, Salanka, Masawi, Bukulu, Humai, Kwadimu, Kolo, Choka na Boay (Babati), hivyo ni vya Kondoa, Naibu Waziri anajua hilo kwa nini umeme haushushwi?

Mheshimiwa Spika, Wananchi wamesema kwamba, sasa wataandaa maandamano halali ya kudai haki yao ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ombi maalum kuhusu vijiji hivyo, mahitaji tamko rasmi na maalum, ni lini umeme huo utashushwa kwa walengwa wa vijiji hivyo?

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kukushukuru kwa fursa hii ya kuchangia kwa maandishi, nasubiri ufafanuzi wa Waziri kwenye vipengere vifuatavyo ili niwe katika nafasi ya kuunga mkono au la:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sera ya Nishati ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa nishati kwa kuzingatia uwiano sahihi na endelevu wa mazingira na kwa kuwa wakazi wa vijijini wamegawanyika ifuatavyo kwa matumizi ya nishati: Wanaotumia kuni na mkaa 95%, wanaotumia mafuta (taa na dizeli) 4% na umeme 1%. Jitihada na mipango ya Wizara ni vyema ielekezwe kupunguza idadi ya watumiaji kuni na mkaa badala ya kuzungumzia kujitahidi kuhamasisha matumizi bora ya kuni na mkaa, kama hotuba ya Waziri inavyoeleza katika Kifungu cha 58 ukurasa 34. Si vyema kujitahidi kuhamasisha matumizi ya kuni na mkaa, hata kama ni kwa majiko bora katika karne hii ya 21 na bado uwiano na mazingira ukapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Kigoma, suala la umeme ni nyeti sana ikizingatiwa kuwepo kwa makambi kumi ya Wakimbizi na Makambi matatu yanayopakana na Mkoa huo kwa Kaskazini Wilayani Ngara Mkoa wa Kagera. Pamoja na hayo, yapo makazi ya Wakimbizi katika Wilaya Urambo (Mkoani Tabora) na makazi kama hayo Wilayani Mpanda (Mkoa wa Rukwa), ambao wote wanatuzunguka na wanatumia kuni na mkaa. Mwisho ni kiwanda cha chumvi cha Uvinza kinatumia kuni kwa karne hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hadi sasa Mkoa hauna matumaini ya kuungwa kwenye Gridi ya Taifa na kwa kuwa hata umeme toka Burundi hauna uhakika, naomba Wizara na Serikali ziupatie Mkoa wa Kigoma toka chanzo cha ndani ya Mkoa huo, Maporomoko ya Igamba, kwenye Mto Malagarasi, chanzo ambacho kinaweza kuzalisha umeme katika awamu tatu za kutoa umeme wa Megawati 28 na unaweza kutekelezwa kuanza na awamu ya pili na kuzalisha Megawati nane kwa gharama ya *USD* 13 milioni.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haimudu gharama hii?

Je mawasiliano na Ubalozi wa China tuliojadili na Waziri na kukubaliana Waziri amefuatilia vipi suala hili?

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba yake nzuri. Aidha, napenda kuchukua fursa hii ya pekee kumpongeza Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa juhudi zake za kuweka mbele katika shughuli zake, kutatua matatizo mengi yanayoikabili Wizara hii. Kwa upande wake, nampongeza Katibu Mkuu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, kwa kuongoza timu ya wataalam wa Wizara hii kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusikilizwa hoja za Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, inaelekea baadhi ya Wabunge hawana taarifa kamili ya shughuli za Wizara hii, hususan katika Sekta ya Nishati. Kwa kuwa hivi sasa Shirika la *TANESCO* linafanya mapitio ya Mpango wa Nishati wa Taifa *(Power Master Plan)* na kwa kuwa mpaka hivi sasa *Power Master Plan* imekuwa imegubikwa na usiri mkubwa, ninapendekeza na kushauri kwamba, baada ya kumaliza zoezi linalofanywa la kufanya mapitio ya *Power Master Plan*, rasimu hiyo ijadiliwe kwa uwazi na wadau wote. Aidha, rasimu pamoja na Sera nzima ya Nishati, viletwe katika Bunge na kuwapa Waheshimiwa Wabunge, fursa ya kuijadili na kuielewa kwa undani zaidi kuliko ilivyo sasa. Hii ingeliweza kufanyika katika Kikao cha Bunge cha mwezi Novemba kwa kutenga siku maalum ya semina.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wa Wizara, kwa jitihada kubwa wanayoifanya kuendesha Shirika la Umeme pamoja na matatizo yaliyopo. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa hatua iliyochukua ya kurekebisha matatizo ya umeme Mjini Sumbawanga. Hali ya umeme hivi sasa ni ya kutulia kuliko hapo mwanzoni. Tunatarajia hali hii itaendelea vizuri bila vikwazo vyovyote vile kutokana na kuimarisha tatizo la kukatika mara kwa mara umeme wa kutoka Zambia.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo ningependa Wizara iyashughulikie na kunipatia maelezo ambayo Wananchi wangu wanayasubiri.

Kwanza, Sekta ya Nishati inayotegemea maji kwa zaidi ya asilimia 60 kama hii ya kwetu, ni hatari kama nvua haziwezi kuonyesha kwa kiwango kinachotegemewa. Hali hii tunaweza kuikabili kwa kutumia rasilimali tuliyonayo ya kudumu katika nchi yetu. Rasilimali hiyo ni mkaa wa mawe. Je Serikali mpaka sasa imefanya utafiti wa mkaa wa mawe wa Namwele - Mkoani Rukwa na kuona jinsi ambavyo ungeweza kusaidia kuimarisha uhakika wa upatikanaji wa nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, mkaa wa Namwele (Sumbawanga), umeonekana hauna majivu mengi, hivyo, umeanza kutumika Kiwanda cha Saruji cha Mbeya. Nini maelekezo ya Serikali juu ya mkaa huo na matumizi yake ya baadaye?

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa una madini mengi sana, lakini wawekezaji hawajapewa taarifa kamili. Ni kwa msingi huo, Wizara pia haijautangaza Mkoa ulivyo. Je, kwa nini Serikali isitangaze rasmi aina mbalimbali za madini yaliyomo katika mkoa huu na maeneo husika kwa kuonesha aina ya madini yaliyopo kwa hivi sasa, ili wawekezaji waje pia Mkoa wa Rukwa?

Mheshimiwa Spika, tunaelezwa na wataalamu kuwa Mkoa wa Rukwa, eneo la Ziwa Rukwa na sehemu ya Chala (Nkasi) kuna dalili za kupatikana kwa mafuta. Je nini matokeo ya utafiti huo uliosababisha hata wachimbaji mafuta wafike huko na mitambo mingi katika eneo hilo? Je, ingekuwa vizuri kuwaelezea Wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa nini wawekezaji hao waliondoka baada ya kuwepo kwa muda mrefu? Nini hatima

ya baadaye ya kuendelea kutafuta uwezekano wa mafuta katika eneo hilo ambalo ni sehemu ya Bonde la Ufa lililoko huko Uarabuni?

Mheshimiwa Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri atuelezee ni kwa nini Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini haujaanzishwa na ni vigezo vipi ambavyo vilitakiwa kutekelezwa kabla ya Mfuko huo kuanzishwa? Je Wizara haioni kuwa kutotekelezwa kwa maagizo hayo kunasababisha kuchelewesha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2025?

Je Serikali inapanga ratiba ipi ya utekelezaji?

Mheshimiwa Spika, Mikoa iliyo mbali na Dar es Salaam itaendelea kuathirika na bei kubwa ya mafuta kutokana na gharama za usafirishaji hadi huko mikoani. Lakini gharama hizo hazizingatiwi na umbali huo. Je, kwa nini Serikali ikaanza kufikiria kutoa ruzuku ya usafiri kwa mikoa ya mbali hasa kwa vyombo vinavyotumika kwa ajili ya uzalishaji vikiwemo vya kilimo (matrekta) na viwanda vidogo (mashine za kukoboa) na kadhalika?

Je isingekuwa vizuri Serikali ikaona namna ya kutoa ruzuku kwa ajili ya maeneo ya uzalishaji kwa ujumla? Hatua hii itasaidia kuhamasisha matumizi ya zana bora za kilimo na hatima yake ni kuondoa dhana ya kuogopa kutumia matrekta kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme bado ni kubwa na kwamba ndoto ya kuhifadhi mazingira itashindikana. Kwa msingi huo ni bora ukimaliza hilo, tuwasiliane na kujiunga pamoja.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, umeme ni miundombinu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi, hasa katika sekta ya elimu na viwanda. Katika hotuba ya bajeti inasema, iwapo gesi ya *Mnazi Bay* haitoshelezi kutengeneza umeme, kitajengwa kituo cha kutumia gesi ya Songosongo. Mtu yeyote mwenye akili timamu na kufuatia mwenendo halisi wa maisha, ataelewa wazi kuwa Mkoa wa Lindi tumeonewa. Nasema tumeonewa sana bila sababu yeyote. Kwa nini mtu mwenye njaa amevuna, lakini anaambiwa asile kwanza asubiri shamba lingine livunwe ndiyo apate kula. Kweli hiyo ni haki?

Serikali haioni kuwa ina lengo la kuchelewesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa Wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara? Serikali ya CCM ni sikivu, CCM ina sera ya kujisahihisha, Serikali ya CCM inaona kigugumizi kipi cha kurekebisha Mradi wa *Songosongo gas* sasa badala ya kusubiri hadi Mradi wa *Mnazi Bay* ushindikane? Serikali inajua Wabunge wa Mkoa wa Lindi wana wakati mgumu wa kutetea upelekaji wa gesi ya Songosongo Dar es Salaam wakati Mkoa wa Lindi, kwa miaka 40 ya Uhuru, haina umeme wa uhakika? Naomba Serikali sikivu ya CCM itusikilize.

Mheshimiwa Spika, sitaweza kuunga mkono hoja kikamilifu iwapo sitapewa jibu la kuridhisha.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitumie fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri iliyotia matumaini kwa Wabunge na wananchi wengi wanaouona umeme kama ni nishati na nyenzo muhimu, utakaowawezesha Watanzania kuchupa toka nje ya dimbwi la umaskini. Ibara za 16, 17 na 18 zimeendelea kutupatia matumaini na faraja sisi ambao pamoja na kilio cha muda mrefu wa kuyaombea haya maeneo mbalimbali kama Hungunalwa, Ilula, Mwahijo, Mwamashimba, Sangu Kikubijine na Shilima bila mafanikio.

Hata hivyo, kila mtu anatambua fika kuwa kumfikishia kila mtu umeme kwa nchi maskini kama yetu ni suala la subira. Naendelea kuamini na kutegemea kuwa siku zote si sawa, ipo siku watu hawa ambao kwa kipindi kirefu sasa wamekuwa wakililia kupata umeme, nao bahati itapitia upande wao. Kuonesha kuwa watu wa sehemu kama Itingandwa wanahitaji umeme wamemkaribisha Mwekezaji mmoja ambaye kaweka *Generator* na anawalipisha Sh.4,500/= kwa taa kwa mwezi. Ni aghali lakini watu zaidi ya 100 wameunganishwa japo *at owners risk,* umeme wa *TANESCO* ungelikuwa wa kuaminika na salama.

Hata hivyo, kwa maendeleo naunga mkono hoja.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuboresha nishati na madini hapa nchini. Maendeleo bila miundombinu ya nishati si rahisi kupatikana. Hiyo inathibitika waziwazi hapa nchini, Mikoa yote isiyo na uhakika wa umeme ni duni sana kwa maendeleo kama Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma na Rukwa. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kuboresha miundombinu yote hapa nchini ikiwemo nishati.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka umeme wa gridi Songea, Mbinga na Namtumbo kutoka Makambako mbona Hotuba iko kimya? Mradi huu umefutwa na Wizara? Tungependa sana kusikia ama kufahamu maendeleo ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ifahamike wazi kuwa, Wilaya ya Mbinga ni ya zamani sana lakini haina umeme. Nini hasa makosa ya Wilaya hiyo, kwa sababu iko pembezoni?. Tunaomba *TANESCO* isambaze nyaya mji mzima wa Mbinga, iongeze jenerata moja ili yawe mawili na iendeshe umeme wa Mbinga. Halmashauri ya Mbinga walinunua jenerata lakini wanashindwa kuliendesha hawana uwezo, *TANESCO* iendeshe umeme wa Mbinga kwa kutumia majenereta wakati tukisubiri umeme wa gridi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali na Mwekezaji kwa yote yaliyofanyika hadi sasa kwa mradi wa umeme wa Mchuchuma. Naamini mambo yaliyochelewesha mradi huu kuanza yametatuliwa na Mwekezaji, hivyo, Serikali haitapoteza muda tena wa kumpa Mwekezaji kibali cha kuanza kazi. Tunaamini mradi huu ukikamilika, sehemu kubwa ya maji nchini yatatumika kwa kilimo kwa kuwa huwezi kuzalisha mazao ya kilimo bila maji, lakini unaweza kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vingine kama mkaa wa mawe.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa niaba ya Wananchi wa Mbinga Magharibi, naunga mkono Hotuba ya Waziri mia kwa mia.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na Wataalam wote, kwa hotuba nzuri pamoja na ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya kuchangia kwa maandishi ni juu ya tatizo langu la kupatiwa umeme katika vijiji vya Matui na Engusero, ambavyo vina watu wengi na vyanzo vya uchumi katika Wilaya ya Kiteto. Kijiji cha Matui tayari kimeshafanyiwa utafiti na *TANESCO* ili kiweze kupatiwa umeme, badala yake umeme wake ulipelekwa kijiji cha Isasuma kilichoko Kondoa na kuandikwa kuwa kiko Wilayani Kiteto. Wilaya ya Kiteto imenyanyasika sana kwa Matui kukosa umeme ambako kuna watu zaidi ya kumi elfu.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo ya kina kuhusu umeme wa Matui na Engusero kwani nilifuatilia mara kwa mara kuanzia kwa Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, *TANESCO* Makao Makuu na kuonana na Ndugu Massawe kuhusu suala hili.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, nishati inayozalishwa katika nchi yetu ni ghali sana katika ujumla wake na ni wazi kwa sababu umeme unaozalishwa na *IPTL* na *SONGAS,* ambayo sasa ndiyo itapamba moto, unalipiwa *cost of inefficiency* au gharama ya uzembe kiasi cha shilingi bilioni 5.5 kila mwezi, inayotokana na mikataba mibaya. Fikiria kama watumiaji wa umeme leo hii wangeondolewa gharama hii unafuu ungekuwaje au kama kiwango hiki kingetumika kusambaza umeme nchini hali ingekuwaje? Kufika Mwaka 2005 mwishoni ni wazi ingewezekana kumaliza kwa kiwango kikubwa tatizo la umeme nchini. Si sahihi kwa Serikali kuendelea kulipia deni hilo la ziada badala ya deni lile ambalo ni halisi tu Serikali inunue *IPTL* kulinusuru Taifa, kwa sababu uwekezaji wa namna hii haufai.

Mheshimiwa Spika, tatizo la *development* ya umeme nchini linaletwa na Serikali yenyewe. Serikali inashindwa kuwa na maamuzi yanayozingatia muda na ku-*seize opportunities at the right time.* Ndiyo maana tunaishia kwenye huduma ghali kama *IPTL* na *SONGAS.* Ukurasa wa 23 wa Kitabu cha Bajeti ya Waziri ni uthibitisho wa jambo hili. Inaonekana wazi kuwa, Wizara ina sua sua sana kwenye uzalishaji wa umeme wa Mchuchuma kama ifuatavyo:-

Kwa nini Serikali inataka umeme uzalishwe chini ya *Megawatt* 400, yaani kwa awamu wakati Mzalishaji ni kampuni binafsi na *marketing* ya umeme wa ziada atafanya mwenyewe na hataidai Serikali wala *TANESCO?* Hii ni sawa na hujuma kwa Wananchi. Nashauri umeme huu kwa sababu ni gharama nafuu kuliko umeme wa maji na gesi, usiunganishwe kwenye *Grid*, wacha nchi iwe na *source* angalau moja yenye umeme wa bei nafuu ili kuwa na sehemu maalumu inayovutia wawekezaji kwa kutumia unafuu wa umeme. Kwa hakika sababu zinazochelewesha kuanzishwa kwa umeme wa Mchuchuma zinatokana na Wizara na kwa kweli si sababu zinazoridhisha, kwa nini baada ya bajeti hii, Mradi wa Mchuchuma usianze kujengwa mara moja?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu faida inayotokana na madini tangu madini makubwa ya dhahabu yaanze kuchimbwa ni ndogo na kasi yake haiwezi kutusaidia kuondoa umaskini, ni vizuri tusiharibu mazingira zaidi na rasilimali ya vizazi vijavyo.

Wizara sasa isimamishe migodi mipya mikubwa mpaka rasimu nzuri ya mikataba ya migodi itakapopatikana kwa msingi ufuatao:-

Ni msingi mkuu kwamba nchi lazima iwe na *share* ya nusu kwa nusu kwa chochote kitakachochimbwa aridhini na wageni kwa mfano, kama kwa kila siku *KMCL* inazalisha *carats* 100 za dhahabu basi kwanza mgao lazima uwe nusu kwa nusu yaani *carats* 50 Kampuni na *carats* 50 Taifa. Baada ya hapo ile hamsini ya kampuni ndiyo itozwe kodi na mkataba. Kama wawekezaji hawawezi msingi huo basi vinginevyo nchi hii itatumika kutajirisha makampuni tu. Kiwango cha thamani ya dhahabu kinachobaki nchini ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na hasa kama Serikali itazingatia ushauri huo kwa makini.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu kutoka kwa Waziri kwa hoja zangu ambazo nimekuwa nikizifuatilia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Wizara mwaka 2002, ilikubali kufunga umeme katika vijiji vya Katoke na Irogero. Kwa hiyo, imechimbia nguzo tayari. Pia nimefahamishwa kwamba nyaya zipo. Tatizo ni *transfomer kV 50* za kuweza kupeleka umeme kunakohusika, mwaka 2003 hatukutengewa fedha za *transfomer* hizo, je na mwaka huu pia hakuna fedha?

Mheshimiwa Spika, hii ni kero sasa, kuona nguzo zipo na nyaya zipo, lakini *transfomer* hakuna. Baadhi ya watu wanadhani kwamba, sifuatilii kwa karibu. Ninaomba jibu katika kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Sekondari Izigo unapita juu. Nimeomba Shule hiyo ipate umeme maana ni karibu sana na *transfomer* iko jirani. Jibu nililopewa ni kwamba, patatakiwa *transfomer* ya ziada. Ombi hili analifahamu vizuri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, naomba hiyo *transfomer* ipatikane ili Shule hiyo iwe na umeme. Hii ni shule ya zamani, kwa kweli kuinyima umeme ni kuizuia kupiga hatua ya haraka kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, pili, nimekwishauliza hapa Bungeni maswali mengi kuhusu umeme Kagoma. Aidha, ninafuatilia kwa karibu umeme wa Kagoma. Kagoma ni mji uliojengwa upya kandokando ya barabara kuu. Unawahitaji wadau 60, shule ya Sekondari, Gati inayopendekezwa ya Rwazi iko Kagoma. Kila ninapojibiwa tangu mwaka 2001, najibiwa kuwa umeme huo haulipi. Panatakiwa kwanza pawepo viwanda, mashine mbalimbali na kadhalika. Sasa ninajiuliza ni nani anayeweza kuanza kujenga kiwanda, kufunga mashine, bila kuwepo nguvu za uendeshaji zenye gharama nafuu kama umeme?

Mheshimiwa Spika, naomba Kagoma ipatiwe umeme ambao ukifungwa toka Muleba utagharimu kiasi cha shilingi milioni 93 hivi. Umeme huu utaibua watumiaji wapya maana eneo ni *strategic* linaweza kuvutia wawekezaji na kujenga hoteli kubwa nzuri, maana limetazama ziwani na pana hewa safi..

Mheshimiwa Spika, naomba jibu la kuridhisha, je, Wananchi wa Kagoma watasaidiwa vipi na uanzishwaji wa Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini na lini?

Mheshimiwa Spika, hivi sasa gharama za umeme zimepanda sana. Kufunga *Service line* imekuwa ni gharama kubwa sana. Lakini ukadiriaji huu mpya nao una adha zake kubwa kwa ongezeko la gharama. Je, Serikali inataka kuona watu wenye kipato kidogo hawapati umeme?

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwa wenye mita za LUKU, makundi yaliyopangwa yaangaliwe upya maana kinachofanyika ni makadirio yanayowekwa kwenye kompyuta bila mtumiaji kutumia. Hii inaongeza gharama kwa watumiaji LUKU kwani makadirio yao ni ya kukisia tu na si kweli kwamba yanajirekebisha baada ya miezi sita kama wanavyosema. Hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMZA MENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, tatizo langu ni la muda mrefu. Wilaya nzima ya Morogoro Vijijini sasa haina umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niendelee kuomba umeme kwa Jimbo la Morogoro Kusini. Maombi yangu yamekuwa ni kero, lakini ni ukweli kwamba, Taasisi zilizopo Jimboni zinahitaji umeme ili kutekeleza mambo yao vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wilaya ya Morogoro Vijijini kugawiwa katika Wilaya mbili, Mvomero na Morogoro Vijijini, sasa Makao Makuu ya Morogoro Vijijini yatakuwa Mvuha. Kijiji hiki kipo km. 85 toka Morogoro Mjini. Tafadhali Morogoro Kusini tunaomba umeme.

Naunga mkono hoja.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Wataalamu wake wote.

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia kuhusu suala la upungufu wa maji Mtera.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na tatizo la upungufu wa mvua kwa miaka miwili mfululizo na kusababisha upungufu huu, lakini ninaamini bado uchunguzi rasmi haujafanyika kwa kina.

Mheshimiwa Spika, maji mengi yanayoingia katika Bwawa hili yapo yanayotokea Mbalari, Ruaha, Pawaga, Dodoma. Tatizo kubwa ni watumiaji wa maji walioko kandokando ya sehemu hizo, wengi wanafungulia maji kwenda kuwasaidia kilimo cha mpunga na hawa wanasababisha upotevu mkubwa wa maji yanayoingia katika Bwawa hilo la Mtera.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Wizara husika ifanye uchunguzi wa kina ili ikiwezekana itungwe sheria kuzuia jambo hilo, endapo jambo hili halitafanyika, Serikali itegemee upungufu wa maji katika Bwawa la Mtera.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu wa maji umeathiri sana wavuvi wanaozunguka katika Bwawa hilo wakiwemo wa Migori na Mtera. Pia wanasaidia kupunguza Pato la Taifa linalotokana na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia tena upande huu wa umeme vijijini na hasa katika Makao Makuu ya Wilaya. Wilaya ya Kilolo ni Wilaya mpya na ni Wilaya pekee ambayo inatoa mchango mkubwa sana katika Mabwawa yetu yani Mtera na Kihansi. Kuna vyanzo vingi vya maji katika Wilaya yetu na hii inatokana na utunzaji mzuri wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala siyo jipya hivyo ninaomba maelezo ya kina kuhusu suala hili ili nishawishike kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hii ikitaka kuendelea na kujiendeleza, tusioneane aibu. Mrabaha ni muhimu, ukichangia kidogo upewe kidogo, ukichangia zaidi upewe zaidi. Sasa sioni kwa nini Wizara yako inaona aibu kupeleka umeme Kilolo?

Mheshimiwa Spika, hili ninalisema kwa uchungu sana. Wananchi wa Kilolo watachoka kutunza mazingira na athali yake itaonekana.

Mheshimiwa Spika, nichangie kidogo kuhusu kituo kidogo cha umeme ulioko pale sehemu ya Ilula. Toka sehemu kituo kilipo hadi Makao Makuu ya Mkoa ni zaidi ya kilometer 60 na cha kushangaza ni kuwa, hakuna kituo cha kulipia umeme, mteja inabidi asafiri km. 120 kwenda kulipia umeme, hivyo akipata bili ya Sh.5,000/= kwa mwezi inabidi aongeze Sh.3,000/= za usafiri kwenda kulipia umeme.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupatiwe Kituo cha kulipia pale pale Ilula ili kupunguza kero.

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nitamke wazi kuwa, naunga mkono hoja hii, vile vile naipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni yangu, ningependa kutoa shukrani kwa Wizara hii kwa kuielekeza *TANESCO* kupeleka umeme katika Kijiji cha Magubike na Shule ya Sekondari ya Kalenga. Namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kufika Jimboni kwangu Kalenga kukagua miradi hii miwili ya umeme. Naomba sasa *TANESCO* ikamilishe miradi hii ikiwa ni pamoja na kuweka *transformers* katika maeneo haya mawili.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo nashukuru kuwa *TANESCO* vilevile imeelekezwa na Wizara kusogeza umeme katika Kijiji cha Tagamenda ikiwa ni hatua ya kwanza ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Kilolo. Katika kufanya hivyo, naomba *TANESCO* itekeleze ahadi ya Wizara Bungeni kuwa umeme utafika Kijiji changu kinachofuata cha Nyabula, vilevile vijiji vya njiani kuelekea Kilolo vya Wangama, Kitayawa, Mlanda, Ndiwili, Magulirwa na Ng'enza.

Mheshimiwa Spika, kabla Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, hajatembelea Magubike na Shule ya Sekondari ya Kalenga, niliomba kwake *extension* ya

umeme kutoka Ifunda. Naomba *TANESCO* ifikishe umeme Kijiji cha jirani cha Muwimbi ambacho kiko barabara kuu kuelekea Mbeya. Katika Kijiji hiki kunajengwa Shule ya Sekondari na pia kuna mashamba makubwa. Hapo hapo kuna Kitongoji cha Ulete ambapo kuna Parokia ya Kanisa Katoliki iliyo na vyuo na huduma mbalimbali ambazo zinahitaji umeme katika uendeshaji. Hapo Ulete kunategemewa kujengwa Shule ya Kimataifa. Hivyo, upelekaji wa umeme katika eneo hili una hoja za kibiashara. *It is a paying business.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba umeme usogezwe eneo linalofuata katika Kijiji cha Kibena. Hapo kuna *Camp* ya Utalii ya Kisolanza inayomilikiwa na Mama Nicky Gaur. Katika *Camp* hiyo watalii wapatao 300 wastani kwa mwezi hufika hapo. Tatizo kubwa ni ukosefu wa umeme. Umeme ukifikishwa hapo basi Kisolanza itakuwa ni Kituo kikubwa cha Utalii. Hapo hapo Kisolanza kuna mashamba ya tumbaku. Ukaushaji wa tumbaku unatumia teknolojia mpya toka Zimbabwe kwa kutumia mashine ya *Chongololo,* ambayo hutumia kuni chache sana pamoja na umeme. Kwa sasa wanatumia dizeli kupata umeme ambao ni wa gharama sana. Hivyo, umeme hapo Kisolanza una hoja pia nzito ya kibiashara. Hapo hapo Kijiji cha Kibena kuna Kituo cha simu cha *Vodacom.* Umeme unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe maoni yangu kuhusu umeme wa makaa ya mawe ya Mchuchuma. Kwanza kabisa, maelezo kuwa umeme wa Mchuchuma unaweza kuwa mwingi mno kwa matumizi ya Watanzania ni wazi kuwa ni hoja ambayo haiwezi kukubalika. Maendeleo ya Tanzania vijijini yatapatikana ikiwa tu umeme utafikishwa vijijini. Huko ndiko waliko Watanzania wengi. Mpaka sasa vyanzo vikuu vya umeme ni maji yanayotokea Vijijini.

Kwa hiyo, wanavijiji wanatakiwa walinde vyanzo vya maji na wasitumie sana maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji ili upatikanaji wa umeme usiathirike. Wanaonufaika na umeme ni wachache wa Mijini. Haya ni mawazo ya kibaguzi ya Wataalamu wa nchi za nje ambao tuko nao na sisi tuna *swallow raw.*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu huko mbele tubadilishe Sera kuhusu *sources* kuu za umeme. Kwamba, maji kimsingi yatumike kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, mifugo na kilimo cha umwagiliaji maji. Maji ya ziada yatumike kwa ajili ya umeme. *Sources* kuu za umeme iwe ni makaa ya mawe ya Mchuchuma na gesi ya Songosongo na pia *Mnazi Bay* na kadhalika. Matumizi ya umeme ya *IPTL* yatafikia hatua ya *irrelevancy.*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, katika kasma ya Maendeleo 2004/2005, *Sub-Vote* 3190 *(Electricity IV Project)*. Je, mradi huu uliotengewa Sh. 1.5bn./= unahusu miji ipi?

Mheshimiwa Spika, nakumbuka katika mpango wa awali *(Electricity IV Project)* kwa Wilaya ya Mbulu, utakamilisha kufikisha umeme katika Miji ya Dandi na Dongobesh. Naomba Maofisa wa Wizara na *TANESCO* wathibitishe.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi nzuri kwa majibu Bungeni na

ufuatiliaji wa ahadi za Serikali katika kusimamia kuhakikisha nishati inawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mambo yote waliyotaja katika hotuba yote, napenda nishukuru sana kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sasa Wilaya ya Ukerewe nayo mwaka 2004/2005 itapatiwa umeme. Watu wa Ukerewe wanasubiri kwa hamu utekelezaji wake. Huu ndiyo ukombozi katika kukuza uchumi katika wilaya hiyo. Watafungua viwanda vidogo vidogo vya kusindika matunda na watafanya biashara zao kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifarijika sana na majibu mazuri ya kuhakikisha kuwa mafundi watakapomaliza Sumve, basi watahamia Kijiji cha Malya kuweka umeme. Kwa niaba ya Mheshimiwa Richard Ndassa na Wananchi wote wa Malya, tunaombea zoezi hili liwafikie. Wanasubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kupitia Bunge lako Tukufu kuwa, umeme unaotoka Kisesa, basi upitishwe katika Vijiji vya Kanyelele, Koromije hadi Bugomba Wilayani Misungwi. Kwa kweli huo umeme uko karibu sana na vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kidogo juu yua madini yetu ya *Tanzanite* ya Simanjiro (Mererani). Sioni mahali popote ambapo yamezungumziwa au kuna jina lingine la kitaalam, naomba nielekezwe vizuri katika kiambatanisho 9 na 10 au ndiyo *Gemstones?*

Naomba sana Mheshimiwa Waziri awe karibu sana na machimbo haya, Watanzania wananyanyaswa kwa kupigwa risasi na hawa wawekezaji. Nina jina katika mkataba. Hakuna sehemu yoyote ambayo inasema kuwa Watanania wapigwe risasi kwa ajili ya mali yao inayowazunguka. Kwani hawawezi kuwakamata na wakajadiliana, kuliko kuchukua sheria mkononi? Je, huyu mwekezaji wa vitendo hivi vichafu si atawamaliza Watanzania?

Mheshimiwa Spika, upandaji ovyo wa bei ya mafuta *(petrol na diesel),* nani anatakiwa asimamie? Tangu tupitishe Bajeti ya Serikali tarehe 10 Juni, 2004, kumekuwa na mabadiliko kila siku, leo Sh. 1,000/= au 990/= au kesho vingine kwa lita hata tarehe 1 Julai, 2004 haijafika.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala hili lipewe Tume ya Kusimamia bei za mafuta. Wanyonge watazidi kuumia, maana unapoongeza bei hata nauli ya mabasi inapanda. Wananchi wa hali ya chini hasa vijijini, hawatamudu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia hoja ya Wizara hii. Lakini *Net Group Solutions* hawatufai Watanzania, bei juu sana.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri za usambazaji wa umeme, usimamizi wa madini na kuhakikisha kuwa Tanzania hata siku moja, mafuta hayakauki kabisa katika visima au vituo vya watu binafsi. Hii inatokana na sera nzuri ya uagizaji na usambazaji wa bidhaa hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, ni lini umeme wa *TANESCO* utawafikia wananchi wa Kiroka na Mkuyuni, umbali wa km. 12 tu toka Pangawe?

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme Lubungo, Maseyu, Kidugalo na Mikese Mjini. Maeneo haya ni giza tupu. Niliandika maombi na orodha ya wanaoomba. Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Mwarazi, Kata ya Mkuyuni, wapo wachimbaji wadogo wadogo na wengine wameunda vikundi. Je, mtawasaidiaje ili Mkuyuni na Kibuko wajitoe katika wimbi la umaskini?

Pili, ninaomba sana Naibu Waziri au Waziri, waje watembelee Mwarazi na Ngongh'olo ili mjionee wenyewe maendeleo ya wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri yetu iliunda Tume ya Madiwani wanne na mimi Mbunge wao. Mwezi Oktoba, 2001, tulikwenda Makao Makuu ya *TANESCO* na barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri iliyosainiwa na Afisa Elimu kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri, lengo kujua kama Shule ya Msingi Gwata Ujembe imelipwa fidia, maana ilijengwa 1951. umeme ulipita hapo mwaka 1968. Hivi sasa ni hatari kwa waya wa *High Tension Voltage.* Ili tubomoe, tuliomba tufahamu kama imelipwa na kwa nani na lini? Wananchi wana wasiwasi huenda malipo yalifanywa kwa mtu binafsi au *TANESCO* wamekula. Baya zaidi ni ile tabia mbovu ya *TANESCO* kutojibu barua yangu. Hii ni dharau. Tuelewe vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba jibu kabla kanuni hazijatumika. Waangalie kwenye kumbukumbu zao leo hii au ahadi ya Waziri kufika GwataUjembe kabla ya Agosti. Shukrani.

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Spika, napenda kujiunga na wenzangu kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, kwa hotuba nzuri aliyoitoa mbele ye Bunge lako Tukufu leo asubuhi. Natoa pongezi kwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana anayoifanya Wizarani, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote wa Wizara, wanafanya kazi nzuri na wanastahili pongezi za dhati.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuipongeza *TANESCO* kwa juhudi kubwa na mafanikio yanayoridhisha katika ukusanyaji wa fedha za Shirika, ambazo zilikuwa mikononi mwa wateja. Ongezeko la mapato ya Shirika kwa asilimia 60 siyo kazi ndogo hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imeanza kujenga *line* ya umeme kutoka Mji Mdogo wa Ipinda hadi *Matema Beach*. Mradi huu ukikamilika, utachochea na kuzindua uchumi wa Kata za Ipinda, Makwale, Lusungo na Matema. Kwa niaba ya Wananchi wa Kyela, ningependa kuishukuru sana Serikali kwa kazi hii nzuri ya kusambaza umeme katika vijiji mbalimbali vilivyoko katika Kata nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuitaarifu Serikali kwamba, hivi sasa kazi ya kujenga *line* ya umeme toka Ipinda hadi *Matema Bieach* imesimama. Imesimama kutokana na ubovu wa gari la kubebea nguzo za umeme kutoka Kyela Mjini hadi eneo la mradi. Ninaiomba Serikali itatue tatizo hilo la gari kwa njia yoyote ile ili kazi iendelee na ikamilike katika muda uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba *TANESCO* itoe gari lingine kwa Wilaya ya Kyela. Gari lililopo limezeeka sana. Kama uwezo wa kununua gari jipya haupo, basi tunaomba *TANESCO* iazime gari toka sehemu nyingine mkoani ili kazi iendelee. Ninaomba nipewe taarifa kama ombi langu hili limekubaliwa ama la. Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* yupo hapa, ningeomba anisaidie kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo ninaiomba *TANESCO* isaidie kutatua, ni ukamilishaji wa ujenzi wa *line* ya umeme toka Ntaba, mpakani na Rungwe, hadi Mjini Ipinda (km. 4). Nguzo zimesimamishwa, lakini bado nyaya. Sasa ni mwaka wa tatu tangu ahadi itolewe kukamilisha kazi hii. Tatizo ni nini? Kwa nini ahadi zinatolewa na utekelezaji ni haba?

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninamshukuru Waziri na Naibu Waziri, kwa kufanya ziara katika Wilaya yangu ya Kyela katika vipindi tofauti. Mawaziri wote wawili walitembelea Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira na kujionea wenyewe matatizo makubwa ya *Kiwira Coal Mine Ltd.* Ningependa kuwakumbusha Waheshimiwa Mawaziri juu ya tatizo sugu la malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi waliosimamishwa kazi, la kupewa likizo bila malipo. Je, Serikali bado haijapata fedha za kuwalipa wafanyakazi hawa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE.SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara akiwemo Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Kamishna. Nawapongeza sana kwa kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo machache tu, kushauri na kumwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa Bunge la mwaka 2002, wakati Waziri akijibu swali langu kuhusu Vijiji vya Luchuli, Nyakasungwa, Bukokwa, Nyakarilo, Kalebezo, Nyehunge, Bupandwa hadi kwenye msitu mkubwa wa milima ya mbao Buhundi. Kwa kuwa umeme ni wa kuunganisha kutoka mpaka wa Jimbo la Sengerema na Buchosa na katika jibu lake lile alisema kuwa, Wizara itatenga pesa kwa ajili ya eneo hili, hadi sasa sioni hata dalili. Ninaomba jambo hili litolewe jibu la kueleweka, kwani wakati alipojibu swali hilo, wananchi walifurahia sana kuwa karibu watapatiwa huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili na la mwisho ni kuhusu upandaji wa bei ya mafuta. Hili ni jambo gumu kwa Wananchi. Jambo hili kwa umaskini wa pekee, ningependa kupata majibu yangu hapa Bungeni, wakati Waziri anafanya majumuisho pamoja na kujibu. Nitafurahi kupata majibu haya hata kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TANESCO* kwa kazi nzuri inayofanya ya kukusanya mapato, kupunguza vishoka mitaani, kuendeleza ujenzi wa miradi ya umeme iliyokuwa imesimamama na ile mipya.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee kwa *TANESCO* ni kuhusu ujenzi wa Mradi wa Umeme Sumve na Malya. Naishukuru sana *TANESCO* kwa hatua iliyofikia. Ombi langu kwa *TANESCO* ni kwamba, ile kasi iliyopo hivi sasa, iongezwe ili ndani ya mwaka wa fedha wa Shirika, waweze kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara kama ifuatavyo:

Kwanza, duniani kote, Serikali inafanya kila jitihada kutafuta Nishati mbadala. Sisi bado tumekazana na nishati inayotokana na maji. Wilayani Karatu, kwa mfano, kuna maelezo kuwa kuna Nishati ya Upepo, ambayo gharama yake ni ndogo kuitengeneza na kuiendesha, pamoja na mkaa wa mawe. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa nishati inayotokana na upepo itakuzwa?

Pili, je, Serikali iko tayari kufika Tarafa ya Eyasi, Kijiji cha Mangola, ambapo Mapadri wa Kanisa Katoliki wameanza kutumia umeme unaotokana na upepo, kwa lengo la kujifunza kutoka kwao na hatimaye *TANESCO* iweze kuwekeza kwenye umeme huo kwa lengo la kuwanufaisha Wananchi wa Tarafa nzima ya Eyasi?

Je, ni lini *TANESCO* watafikisha umeme katika Tarafa ya Eyasi na Mbulumbulu chini ya utaratibu wa kawaida?

Kwa vile baadhi ya Wabunge tumepokea *documents* zenye kuonesha kasoro katika Mkataba wa *IPTL*, ambao umetufikishia Serikali kuingia gharama kubwa kila mwezi kwa *IPTL* na kwa kuwa *documents* hizo zinaonesha siyo tu kasoro zinazotokana na manunuzi ya kweli tu, bali hata vyombo vya nje, ikiwemo Benki ya Dunia kuhusika katika kutoa shinikizo na hata Maofisa wao kuchukuliwa hatua na kwa kuwa suala zima la *IPTL* lina wingu zito la rushwa. Je Serikali iko tayari kuunda Tume ya Bunge *(Select/Ad Hoc Committee)*, kufanya uchunguzi wa kina kwa lengo la kupata ukweli kuhusu suala hili ambalo kwa muda mrefu limelalamikiwa?

Serikali inatoa kauli gani kuhusu wingu hilo la rushwa? Ni vyema Serikali ikatoa tamko rasmi, vinginevyo wakati wa vifungu, nitatoa hoja ya kuundwa kwa Tume ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa vile migogoro katika maeneo ya machimbo inazidi kila leo. Isitoshe, wachimbaji wadogo wadogo wananyanyaswa na wawekezaji wakubwa hasa *AFGEM*:-

(i) Je, Serikali inatoa taarifa gani kuhusu idadi ya wachimbaji wadogo wadogo waliopigwa risasi kuanzia 1995 hadi Julai, 2004 na kati yao ni wangapi wamekufa, wangapi wamebaki kilema wa kudumu?

(ii) Wahusika na matukio hayo, yaani waliopiga risasi na au walioamuru risasi zipigwe, ni wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria na wangapi wamefungwa au kupigwa faini?

(iii) Kwa kuwa nimepata taarifa rasmi kuwa *AFGEM* walisaidia Kampeni ya Chama cha Mapinduzi mwaka 1995 kwa kutoa *US $* 6,000 na Mkurugenzi Mkuu wa *AFGEM* binafsi kutoa *US $* 1,500 kwa kampeni hiyo hiyo kwa CCM Mkoa wa Arusha na hatimaye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Daniel Ole Njoolay, kwa jeuri kabisa, akathubutu kusema kuwa iwapo *AFGEM* itafutiwa leseni yake, yuko tayari kujiuzulu Ukuu wa Mkoa.

Je, Serikali itakubali kuwa jeuri hii ya wawekezaji hawa, inatokana na mahusiano yenye sura ya rushwa hasa baada ya kutoa mchango mkubwa kwa Kampeni ya CCM?

Niko tayari kutoa *document* hiyo ya mchango wa *AFGEM* kwa CCM. Serikali iko tayari kufanya uchunguzi wa kina, kwa mchango huo na mingineyo ya aina hiyo ili kuona kuwa matendo hayo ya rushwa yanakomeshwa, wahusika kuchukuliwa hatua na walioathirika kupatiwa haki zao?

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa vitambulisho maalum vimeandaliwa kwa wachimbaji wadogo wadogo. Je, ni vitambulisho vingapi vimeombwa na vingapi vimepangwa kutolewa na hadi sasa vimetolewa vingapi? Kuna taarifa kuwa wale wote ambao hawatapata vitambulisho wataondolewa, tena kwa kutumia *FFU* na gharama ya kuwaondoa imetolewa au itatolewa na *AFGEM*! Je, kuna ukweli gani? Je, Serikali haioni mpango huo unawadhulumu wachimbaji wadogo wadogo na utasababisha vurugu kubwa?

Mheshimiwa Spika, naganguliza shukrani za dhati.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize umuhimu wa sifa kwa Wana-Ruvuma kupata umeme wa *grid* toka Makambako hadi Namtumbo. Suala hili tumelizungumza kwa muda mrefu sana hata kabla ya 2001. *TANESCO* wapo tayari kutuletea umeme wa *grid* toka Makambako hadi Songea na hatimaye kufika Namtumbo (kusindika tumbaku) na Mbinga (kusindika kahawa).

Mheshimiwa Spika, kutoka Makambako hadi Songea kupitia Njombe, ni kilometa 220. Tayari umeme umevutwa toka Makambako (km.50) hadi Njombe. Hivyo, urefu wa *grid* kwenda Songea toka Njombe ni kilometa 170. Kwa kuwa barabara ya Njombe hadi Songea ni ya kupindapinda, lakini barabara ya umeme wa *grid* haiwezi kufika Songea kwa kupindapinda. Hivyo, yawezekana umbali kati ya Njombe hadi Songea ukawa kama km. 100 hivi. Aidha, kutoka Songea hadi Namtumbo ni km. 70 na kwenda Mbinga toka Songea ni km. 70 hivi. Tafadhali sana *extension* ya umeme hadi Njombe (ukigharamiwa na Sweden), tafadhali mradi huu uunganishwe na mradi wa pili hadi Songea - Namtumbo na Songea - Mbinga.

Mheshimiwa Spika, sisi wakazi wa Ruvuma hatuelewi kwa nini tunakosa umeme wa *grid* toka Makambako sasa hivi, maana gharama siyo kubwa sana kama mnavyohofu. Itasaidia sana *rural industrialization* na kupunguza kasi ya vijana kutorokea mijini.

Wabunge wote wa Ruvuma tunaona upo uwezekano wa *grid* sasa hivi kufika, maana tayari umeme unafika Njombe. Tunaomba umeme huo uendelee hadi Ruvuma (Songea - Namtumbo na Songea - Mbinga).

Aidha, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, yupo tayari kusaidia kifedha ili Ruvuma tupate umeme wa *grid* mapema iwezekanavyo. Barua yetu anayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (MIPANGO).

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

**MHE. ISSA MOHAMMED SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, naipongeza hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na nadhani hii ni kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, napongeza pia maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 32 wa Kitabu cha Hotuba, kifungu 55. Maelezo yake yameonesha na kufuta zile kauli za nyuma kwamba, Zanzibar kwa maana ya SMZ, imekataa hatua za utafutaji wa mafuta katika eneo lao.

Mheshimiwa Spika, katika kuichangia hoja hii, nadhani bado naona yapo mapungufu hasa kwenye suala hili la Nishati ya Gesi. Kwa nini Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ina kigugumizi gani cha kutoishirikisha SMZ hadi hivi sasa? Nishati hii ni ya Muungano. Wadau wa Muungano huu ni Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa nini suala hili la Muungano linashughulikiwa na mdau mmoja tu au tuseme mdau huyu ndiye Muungano, akiwa hata peke yake na mdau wa pili wa Muungano si chochote si lolote?

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine una sura ya maombi. Nadhani sasa hali siyo mbaya sana kuhusu ulipaji wa madeni ya umeme unaonunuliwa na Shirika la Umeme la Zanzibar. Hata hivyo, matatizo madogo madogo yanatokea, lakini ustahamilivu unatumika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu wa sasa wa kulitaka Shirika la Umeme la Zanzibar kulipa deni la umeme kwa kipindi cha mwezi mmoja, nina hakika msimamo huo wa *TANESCO* unachangia sana matatizo hayo madogo madogo. Itakuwa ni jambo la busara *TANESCO* wakatoa muda wa miezi mitatu kwa Shirika la Umeme la Zanzibar kulipa umeme walionunua. Kipindi ambacho tayari watakuwa wameshauza na kukusanya mapato ya mauzo yao. Kipindi cha mwezi ule ule, uwe wa kununua na kulipa. Nadhani kibiashara kubwa kama hiyo ni kukomoana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la kumiliki maeneo ambayo Zanzibar imepitisha umeme. Maeneo haya ambayo yapo upande wa Tanzania Bara, bado Zanzibar inakosa hati miliki. Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Shirika lake la *TANESCO,* wanaelewa kwamba, mradi ule wa kuchukua umeme Bara kuja Zanzibar, umefanywa na SMZ. Kwa nia njema sana, SMT ilikubali ardhi ya SMT itumike kuwekeza mradi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hali sasa imebadilika sana. Mambo hayaendi kwa maelewano tu ya kindugu, isipokuwa yanahitaji hati za maandishi. Naomba Zanzibar

ipatiwe hati rasmi ya matumizi ya ardhi yote ambayo SMZ wameitumia kwa kuwekeza mradi huo wa umeme. Hatua hii kama haitachukuliwa, italeta matatizo hapo baadaye, tena makubwa sana.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Igalula ni Jimbo la Vijijini. Katika hoja ya leo, ni kupeleka umeme vijijini. Ni moja ya malengo yenu. Igalula ni Makao Makuu ya Jimbo la Uchaguzi. Pia Kijiji cha Kigwe, ambapo barabara kuu ya Itigi - Tabora inapitia hapo na ambapo kuna Shule ya Sekondari yenye majengo na miundombinu mingi inayohitaji nguvu za umeme ili kuziendesha.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru ikiwa maeneo haya yatafikiwa na huduma hizi ili kurahisisha Igalula ikiwa ni Makao Makuu ya Jimbo, kuna majumba ya Serikali kama vile Ofisi ya Mbunge, Tarafa, Polisi, Mahakama na *Railway Station* ya Kati. Pia hapo kuna maandalizi ya ufunguzi wa Kituo cha Afya na ujenzi wa Shule ya Sekondari. Huduma hizi zote zinahitaji huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kutoka Tabora kupitia Reli ya Kati hadi Igalula, ni umbali wa maili 22 na kutoka Tabora kuelekea Kigoma ni km. 45. Kwa hiyo, umuhimu wa maeneo hayo niliyoyataja, nimeelezea. Kuna majengo ya kudumu na imara, ambayo yataweza kuhimili kuwekewa umeme na wenye uwezo wapo. Tukifanikiwa kupeleka umeme sehemu hizo mbili, itakuwa rahisi pia kuvuta umeme kutoka Igalula kuelekea *Railway Station* ya Goweko ambacho ni kijiji kinachokua kwa kasi ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kusisitiza tu ni kuwa, Jimbo zima halina umeme na Wananchi wanaonekana kunyimwa haki yao ya msingi kijamii. Kwani ni wazalishaji katika uchumi wa Taifa, kwa kuwa na asali nyingi na bora katika Jimbo hili, mpunga mwingi unaozalishwa, unaokwenda sambamba na Mkoa wa Shinyanga na mbao za mninga zinavunwa kwa wingi kutoka Jimbo hili, ufuta na mahindi yanapatikana kwa wingi.

Vilevile njia kuu za Reli ya Kati na barabara ya Itigi, Tabora, Kaliua, Malagarasi hadi Kigoma, zinapita katika Jimbo hili. Kwa hiyo, umeme kuwepo katika Jimbo hili, utaleta changamoto kubwa katika Taifa na Wananchi waishio huko kujikwamua kiuchumi. Pia madini mengi yanaonekana kuwepo katika Jimbo hili. Wawekezaji wamejitokeza kwenda kufanya utafiti katika Kijiji cha Tura, kuna maeneo kunakuwa na dhahabu na wawekezaji wameanza kuchimba ili kuchukua udongo na kufanya utafiti. Pia Kijiji cha Loyo, inasadikiwa madini ya almasi na dhahabu yamegunduliwa na wachimbaji wadogo wadogo wameanza kuvamia na kuanza kuharibu mazingira. Sijui kama Wizara ina habari ya eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa za madini hayo, naomba Wizara ilichukulie na kuona jinsi gani itasaidia ili mazingira yasianze kuharibiwa na hatimaye tujue kama kweli kuna mali zinazodaiwa kuwa zipo na kama zikionekana zipo, basi zilete manufaa kwa Taifa na wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili niweze kuwapongeza Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja kwa 100%, sasa napenda kuchangia machache kuhusu hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha kuwa Wilaya ya Serengeti inapata umeme ifikapo mwaka 2005. Wizara ya Nishati na Madini imefuatilia kwa karibu sana kuhakikisha kazi ya kupeleka umeme katika Wilaya ya Serengeti, inafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuushukuru Uongozi wote wa *TANESCO* kwa kufuatilia kwa karibu sana na kuhakikisha kuwa, Wilaya ya Serengeti inapata umeme. Mimi pamoja na Wananchi wa Serengeti, tunaushukuru sana Uongozi wa *TANESCO* na tumeridhika na juhudi inazofanya *TANESCO* kuleta umeme Wilayani Serengeti.

Mheshimiwa Spika, sisi Wananchi wa Serengeti tuko tayari kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO* kwa karibu sana ili kuhakikisha kuwa umeme unafika Wilayani Serengeti ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais Benjamin William Mpaka, alipotembelea Wilaya ya Serengeti mwezi Oktoba, 2000, aliahidi kuwa Wilaya ya Serengeti itapatiwa umeme ifikapo mwaka 2005. Sasa naiomba *TANESCO* ihakikishe kuwa, umeme unafika Mugumu kabla ya Aprili, 2005. Hii itanisaidia kupeta katika Kura za Maoni. Hivyo, tunaomba *TANESCO* imbane Mkandarasi afanye bidii na umeme ufike Serengeti kabla ya Aprili, 2005.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu mapato yanayotokana na dhahabu na almasi. Tunaomba Wizara ilitupie jicho suala hili na kulipatia ufumbuzi, kwani likiachwa hivi hivi bila kuchukua hatua, nchi yetu itaendelea kupata hasara kubwa, kitu ambacho ni hatari kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, sasa ni miaka miwili, naomba umeme usambazwe katika Jimbo la Kalambo, hata mpango wa aina yoyote hakuna.

Umeme toka Zambia kwenda Sumbawanga, naomba uteremshwe Matai ili usambazwe katika Vijiji vya Matai, Sopa, Kasesya (mpakani), Singiwe, Msauzi na katika vijiji vilivyopo katika *line* ya umeme toka Zambia.

Mheshimiwa Spika, umeme usambazwe kutoka Matai kwenda Kasanga katika gati, ili kuendeleza gati hii iwe ya kisasa. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inajenga gati, Wizara ya Ujenzi inajenga barabara. Ni nishati peke yenu hamna mpango wa gati hii ili iwe ya kisasa. Tafadhali niwekeni katika mpango. Msipuuzie suala hili, kwani uchumi toka *DRC* na Burundi ni mkubwa na manufaa ya gati ya Kasanga ni makubwa kama Wizara hii itatuingiza katika mpango.

Mheshimiwa Spika, umeme ukiteremshwa Matai, utasambazwa kwa urahisi Wilaya ya Sumbawanga kwenda Mwazye, Mpui, Laela, Mwimbi na Ulumi. *TANESCO* imeingia mikataba na vijiji kulinda njia ya umeme, lakini vijiji bado viko gizani. Vinaomba vipewe umeme ili ulinzi wa njia ya umeme uwe na maana zaidi.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba mpango wa kupeleka umeme Nyatwali, Wilayani Bunda ukamilishwe. Nguzo zimewekwa tayari, lakini kazi bado haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu *TANESCO*. *TANESCO* haifanyi kazi vizuri. Kwanza, watu wengi, maeneo yenye msongamano wa nyumba karibu, wanatumia umeme bure bila kulipia. Mfano, kwa Dar es Salaam wanaongoza maeneo kama ya Magomeni, Kinondoni, Mwananyamala, Buguruni, Ilala, Vingunguti na kadhalika. Watu wamejiunganishia umeme.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi wa *line* na mita wanajua na wanakula fedha kila mwezi toka kwa watu ambao nawaita ni wateja wao wa kudumu. *TANESCO* lazima ichukue hatua kudhibiti suala hili. Nayasema haya, nina hakika na ninajua wazi, kwani hata mimi ninapoishi Ilala Dar es Salaam, nayaona waziwazi. Nyumba nyingi sana zimefunga umeme kinyemela.

Mheshimiwa Spika, kuna urasimu mkubwa sana *TANESCO* kwa wateja wanaohitaji kuwekewa umeme majumbani. Rushwa ni ya hali ya juu kuliko inavyojulikana. Mimi binafsi imenitokea Machi, 2003. *TANESCO* iwe makini, ishughulikie.

**MHE. DR. ABDULKADER A.M. SHAREEF:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwa kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia 100 na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuzungumzia mambo mawili. Kwanza, umuhimu wa kuharakisha suala la kuwezesha usafishaji na ukataji wa vito vya thamani, hasa vito vya *Tanzanite* na Almasi ndani ya Tanzania na hivyo kupiga marufuku usafishaji wa vito visivyosafishwa au kukatwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliahidi kwamba, usafirishaji wa *Tanzanite* isiyosafishwa na kukatwa utapigwa marufuku na hivyo kutaanzishwa utaratibu wa kukata madini hayo. Sote tulifurahia ahadi hiyo, kwani siyo tu itarudisha fedha nyingi Tanzania, ambazo hivi sasa zinaishia nje tu, bali pia

itaongeza ajira nchini na vilevile kupanua wigo wa walipa kodi. Aidha, *Tanzanite* ni madini ambayo hayapatikani popote duniani isipokuwa Tanzania. Hivyo, kama madini hayo yatasafishwa na kukatwa hapa hapa Tanzania, siyo tu itazidi kuongeza hadhi na umaarufu wa Tanzania, kwani *Tanzanite* itakuwa *Tanzania Brand,* lakini vile vile itazidisha au kuongeza thamani ya madini hayo duniani na kuifanya itakikane zaidi. Je, ahadi hii imefikia wapi? Kwa nini Wizara ya Nishati na Madini isifuatilie kwa undani zaidi na kwa kasi zaidi upatikanaji wa ama mwekezaji au hata mikopo ya kufanikisha lengo hilo?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, tuwasiliane na nchi kama Botswana, ambayo hivi sasa ina mitambo ya kukata almasi ndani ya nchi, ili kupata ushauri na mwongozo. Aidha, ni vyema kuitisha mikutano maalum ya wawekezaji wa usafishaji na ukataji wa vito vya thamani, ili kuwahamasisha kuja kuwekeza katika sekta hii. Wizara yangu iko tayari kusaidia kufanikisha zoezi hilo.

Pili, kwa miaka kadhaa hivi sasa tumekuwa tunaelemea *West* tu kwa kutafuta au kutoa leseni za utafutaji wa mafuta au gesi. Hata Australia bado ni sehemu ya utamaduni wa *West* au fedha za wawekezaji wa *West.* Hatuna habari wala shauku ya kutafuta wawekezaji kutoka *East!* Wakati umefika wa kutafuta na kuwakaribisha wawekezaji wa *East,* hasa China.

Mheshimiwa Spika, Uchina ina akiba ya dola bilioni 300 zilizotengwa maalum kwa shughuli za kuwekeza katika sekta ya utafutaji nishati kwa njia za ubia. Kwa nini hatuwatafuti? Uchina hivi sasa inatumia dola bilioni 250 kwa mwaka kununua mafuta kutoka nje ili kukidhi matumizi ya mafuta kwa mahitaji yanayozidi kuongezeka nchini. Lengo lao ni kupunguza bili hiyo kwa kuwekeza hasa ndani ya Bara la Afrika katika sekta ya mafuta na gesi. Nashauri tuwatafute na tuwahimize kuja Tanzania. Wana fedha, utaalam na shauku ya kuwekeza kwenye sekta ya nishati ndani ya Afrika na Mashariki ya Kati. Sisi tuna urafiki mkubwa na Uchina. Tutayarishe safari ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Wake na Katibu Mkuu, ama kwenda Uchina au kualika Wawekezaji wa Serikali ya Uchina kuja Tanzania kwa lengo la kuanzisha mazungumzo. Wizara yangu iko tayari kusaidia kufanikisha kwa haraka zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kusema kwamba, wakati umefika wa sisi Watanzania kuchukua hatua za makusudi kuwaalika na kuwashirikisha Wachina katika Sekta ya Nishati. Wana fedha, utaalam na shauku ya kuwekeza kwenye sekta hii na hasa ndani ya Afrika.

**MHE. DR. HUSSEIN ALI MWINYI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukumbushia ombi langu la kupatiwa umeme Kimanzichana katika Wilaya ya Mkuranga. Huu ni mji mkubwa zaidi baada ya Makao Makuu ya Wilaya. Kwa kuwa kuna Mradi wa *Songosongo Gas*, ni vyema eneo hili la Jimbo langu likapewa umeme huu. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri

wanayoifanya baada ya kuondoa ubabaishaji uliokuwa unafanywa na Wakuu wa Vitengo hasa upande wa Shirika la Umeme Tanzania. Kwa sasa kazi ni nzuri, inaendelea kama vile uwekaji wa umeme toka Mtinko kwenda Nkungi. Kwa sasa sina kinyongo kabisa. Nashauri kazi hiyo iendelee na ikamilike kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nikukumbushe ya kwamba, mradi wa umeme unaojengwa sasa ulikuwa uishie Iambi na hatimaye uendelee kwenda Nduguti. Kama tulivyokubaliana na Mheshimiwa Waziri, kwa sasa kutokana na uhaba wa fedha uishie Nkungi kwanza. Naomba huu usiwe mwisho wa kutekeleza mradi huu. Mara fedha zitakapopatikana, kazi ya kufunga umeme toka Nkungi kwenda Iambi hatimaye Nduguti, iendelee.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ndani ya Bunge hili kutoa umeme Kinampanda na kuupeleka Chuo cha Maendeleo Msingi (km. 4). Nitashukuru sana kama Wizara yake itatekeleza mradi huu ambao gharama zake alisema mwenyewe ndani ya Bunge kuwa ni Sh. 83,000,000/=. Nafahamu kabisa ya kwamba, fedha hizi ni ndogo na Wizara yake nina uhakika inaweza ikatekeleza kazi hii 2004/2005. Natanguliza shukrani zangu nyingi kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, naona kwa leo hayo niliyoyaandika yanatosha. Naomba tu ahadi hizo zitekelezwe. Naomba Mheshimiwa Waziri, wakati wa kuhitimisha baheti yake, nipate maelezo juu ya mambo niliyoyaandika hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. MOHAMED H. MISANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Daniel Ndhira Yona, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara. Aidha, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nimekuwa nikieleza tatizo la umeme Ihanja - Singida Kusini, pamoja na kuuliza maswali zaidi ya mara tatu tokea mwaka 2001 hadi sasa. Serikali iliahidi kupeleka umeme Ihanja kabla ya mwisho wa mwaka 2002. Upelekaji wa umeme Ihanja ni mradi mmoja uliozihusisha Manyoni, Puma, Ikungi na kwamba katika maeneo haya, umeme umepelekwa tayari, lakini hadi leo hii Ihanja hakuna umeme.

Nguzo za umeme zimepelekwa Ihanja tokea 1998 na zimelazwa chini tokea wakati huo hadi leo hii. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, nguzo kadhaa zilichukuliwa na kupelekwa Manyoni kwa ahadi kama zingerudishwa. Lakini hadi leo hii nguzo hizo hazijarudishwa. Hivi kitendo cha kuwaachia wananchi nguzo hizo kwa muda wa miaka minane wanaziangalia kwa macho kila kukicha, siyo kuwadhalilisha wananchi wa Ihanja? Je, nguzo hizo ndiyo tuseme Serikali imezisusa kwa wananchi wa Ihanja?

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme Ihanja ni kilometa 11 kutoka Puma, lakini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kupeleka umeme huko wakati miradi ya kilometa nyingi na ambayo ni ya hivi karibuni inatekelezwa. Kwa mfano, Mradi wa

Mtinko hadi Iambi ni kilometa nyingi, lakini sasa unatekelezwa. Je, Wananchi wa Ihanja wana kosa gani?

Mheshimiwa Spika, nilieleza kuwa Shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ihanja imepata Mhisani toka Amerika, ili wasaidie vifaa vya ufundi kwa shule hiyo kama kompyuta na kadhalika. Msaada huo unakwama kwa sababu hakuna umeme. Hivi Ihanja wanajiona vipi? Tafadhali umeme upelekwe Ihanja. Ahsante.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo langu la Kigamboni sasa hivi ni *hotcake* kutokana na ukweli kuwa maeneo yote hivi sasa yanachukuliwa na Wananchi mbalimbali hasa baada ya Wizara ya Ardhi kuanzisha mradi wa viwanja 20,000. Pamoja na hali hiyo, Bahari ya Hindi imekuwa kivutio kikubwa kwa Wananchi na watalii na sasa mahoteli mazuri na ya kisasa yanajengwa kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi na watalii wanaoongeza pato la nchi yetu. Sehemu zinazokuwa kivutio huko ni Mjimwema, Mwongozo, Mbutu, Kimbiji - Yaleyale, Puna, Pembamnazi na maeneo kadhaa yaliyopo kando kando ya Bahari ya Hindi. Tatizo kubwa katika maeneo hayo ni kukosekana kwa umeme kwa muda mrefu. Suala la miundombinu huko, halina tatizo. Kwani umeme huo umeishia Mjimwema tu. Ninayo imani kubwa kabisa kuwa suala la miundombinu halihitajiki, ila kilichobaki ni kupeleka umeme tu.

Mheshimiwa Spika, kupitia Waziri mwenye dhamana, naiomba Serikali ipeleke umeme maeneo niliyoyataja hapo juu, kwani wawekezaji walio wengi wanashindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwa na uhakika wa shughuli zao zitafanyikaje bila umeme. Mahoteli yaliyo mengi yanatumia *generator,* ambayo ni gharama kubwa sana. Hali hiyo inaathiri uchumi wa Taifa letu kupitia watalii walio wengi wanaokuja kutalii kwenye *beach* za Kigamboni.

Kuna wakati Meneja wa Kanda aliniambia tatizo lililokuwepo wakati huo, ilikuwa ni nguzo na nyaya, hiyo ilikuwa mwaka 2002. Je, tatizo la nguzo na nyaya bado lipo, mbona maeneo mengine yanaendelea kupewa umeme na katika hotuba sioni sehemu yoyote aliyotaja kuhusu Kigamboni? Kigamboni ni Jimbo ambalo lipo nyuma sana kimaendeleo. Kipindi hiki ndicho kidogo tunaona mwanga wa mafanikio ya kiuchumi, lakini hatuna cha kujivunia kutokana na kukosa umeme kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yanayotakiwa umeme ni pamoja na Kibada hadi Kisarawe II, Kibada hadi Tuangoma na Charambe hadi Chamazi hadi Mbande. Charambe hadi Mbande ilikuwa mwaka 2003 wapewe umeme, lakini walisema tunasubiri nguzo. Pia sehemu yote ya Kigamboni iliyo na umeme, umeme wake ni wa kubahatisha sana, kwani kila wakati umeme hukatika na wakati mwingine hukaa siku mbili umeme haujarudi mpaka tupige kelele kwa wahusika. Je, tatizo la kukatikakatika umeme litaisha lini na kinachosababisha ni nini?

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali inipe maelezo ni lini umeme utapelekwa sehemu nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yale niliyoyazungumza, naomba Wizara iendelee na nia yake njema ya kuangalia kupeleka umeme Vijijini Manyoni, hasa Mgandu na maeneo mengine kama Kilimatinde na kadhalika. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri, alikwishafika na tumekuwa na mazungumzo naye mazuri, yanayotia moyo na furaha. Hili sikulisema makusudi kuondoa au kupunguza hoja kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo katika Mji wa Itigi, bado hayajawa na umeme kwa sababu vifaa vinaenda kidogo kidogo sana. Naomba vifaa zaidi vipelekwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naendelea kuunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa maandalizi ya hotuba hii. Pia naipongeza Wizara kwa mafanikio yaliyofikiwa ya kusambaza umeme uchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ibara ya 10 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwanza naishukuru Serikali kwa kuupatia umeme Mji wa Ngara - Makao Makuu ya Wilaya na uendelezaji wa kupeleka umeme katika Mji Mdogo wa Kabanga..

Mheshimiwa Spika, umeme wa Ngara unatokana na ahadi ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa aliyoitoa mwaka 1995, wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu. Leo ni miaka karibu tisa, wakati Mhewshimiwa Rais anakaribia kukamilisha muda wa Uongozi wake, kabla umeme haujapatikana Ngara! Tabia ya Wizara ya Nishati na Madini ya kutoheshimu ahadi za Viongozi wa Taifa, siyo nzuri. Sasa Wzara itekeleze na kukamilisha ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, umeme uliahidiwa kufikishwa katika Miji Midogo ya Kabanga na Rulenge, lakini taarifa ya Mheshimiwa Waziri wakati wa uzinduzi wa Kiwanda cha Umeme Ngara tarehe 9 Juni, 2004 kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikataa kupeleka umeme Rulenge. Alisema ungojewe umeme kutoka Kigoma, bila kutaja ni lini umeme huo ungepatikana.

Mheshimiwa Spika, sababu za kusema (kutoa) taarifa hiyo ni woga wa gharama. Wizara ilidanganywa kuwa Rulenge ni kilometa 80 kutoka Ngara Mjini na Wananchi wanadai fidia kwa mali zao hapo njia ya umeme itakapopita. Yote siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, Ngara Mjini hadi Rulenge ni km. 30, lakini pale umeme utakapoanzia ni Murugarama ambapo hadi Rulenge ni km. 28 hivi. Zinahitajika nguzo 24 tu. Wananchi wako tayari kupokea umeme kwa maendeleo yao. Hawadai fidia yoyote na Serikali/Wizara inajua hivyo kutokana na barua nyingi toka Wilayani Ngara, Mkoani Kagera na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, umeme hadi Rulenge, utaipa faida kubwa *TANESCO*. Kuna vituo njiani vyenye uwezo wa kutumia umeme vya Djulurigwa ni *Trading Centre*, Mbuba kuna *Trading Centre,* Parish Katoliki, Zahanati, Shule ya Msingi na wakazi wenye nyumba imara za kisasa, Munjebwe kuna Wananchi wenye nyumba za kisasa, Shule ya Msingi, Zahanati inayopumzisha na kulaza wagonjwa na Rulenge yenyewe yenye umuhimu wa pili kwa Mji Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Rulenge una taasisi na asasi nyingi na baadhi yake ni Hospitali ya pili kwa ukubwa Wilayani, yenye vitanda 156 ya Misheni Katoliki, Makao Makuu ya Jimbo Katoliki Rulenge, lenye Uongozi wa Wilaya za Ngara, Biharamulo na Karagwe, *Trading Centre* kubwa kwenye barabara toka Mwanza, Bukoba, Shinyanga na kadha wa kadha kwenda Burundi na *DRC* na Makao Makuu ya Wilaya. Rulenge inahudumia Tarafa mbili na Kata saba, *Convent* za madhehebu ya dini tatu, Vituo vya kulelea watoto yatima viwili, Kituo cha Polisi cha ukubwa wa pili Wilayani, Mahakama ya Mwanzo kwa Kata tano, Shule za Msingi tatu, Shule za Sekondari mbili, moja hadi Kidato cha VI, *NGOs* imara nne kwa huduma ya Wananchi, Zahanati mbili, moja inayolaza wagonjwa na kuendeshwa na Daktari na ma mengineyo yanayohitaji umeme, mengi sana.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Ngara wanaomba umeme wa *grid* kutokea Bulyankulu (km. 270 hivi) au Geita (km. 280), Muleba (km. 260), na au Karagwe (km. 200 tu) badala ya mawazo ya umeme toka Kigoma kilometa zaidi ya 400! Inaelekea kuwa Mheshimwa Waziri, haifahamu vyema jiografia ya Mikoa ya Magharibi ya nchi na kudhani kuwa hiyo itapunguza gharama. Haya ni mahesabu ya hasara tupu.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Ngara, Mkoa wa Kagera na wakazi wa Rulenge, wanaomba Serikali iwape umeme wakati huu. Maana Mkurugenzi Mtendaji wa *Net Group Solutions* aliyehudhuria uzinduzi tarehe 9 Juni, 2004, alionyesha kukubali hivyo baada kutambua kuwa taarifa zilizopo ni za kupotosha. Ukosefu wa umeme umezuia maendeleo makubwa Wilayani Ngara, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa *nickel.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu na uwekezaji, Viongozi wote wanaotembelea Ngara kutoka Taifa na Mataifa, wanakiri kuwa Ngara ina vivutio vikubwa vya utalii, ila inakosa miundombinu kwa hamasa ya wawekezaji. Umeme ni muundombinu. Ngara ina maporomoko ya Rusumo kwa Mto Kagera. Watu wengi wanafika na wengine watokao nje ya nchi wanapenda kuyaona maporomoko haya yanayoweza kutoa *megawatt* 37 hivi.

Mheshimiwa Spika, ulimwengu unataka kukiona chanzo cha Mto Nile, mto maarufu ulimwenguni. Kandokando ya Mto Kagera, kuna mapori ya akiba ya Serikali ya Kimisi na Burigi, yenye vivutio vya wanyama, ndege, wadudu hata uoto.

Mabonde na nyanda za Wwilaya hii inayolala katika bonde la Bonde la Ufa, bila kusahau kuwa iko juu usawa wa bahari futi 1,800, mapango, chemichemi za maji moto, mabaki ya utawala wa jadi kwa historia ya nchi hii, ng'ombe wakubwa wekundu wenye pembe kubwa sana na ndefu mno na nyeupe, ni maajabu yaliyowavutia Mataifa mengi wakati wa wakimbizi wa Rwanda na Burundi mwaka 1993 na 1994.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa iweke umeme Ngara kwa vile barabara na uwanja wa ndege vipo, ili kukuza utalii na kuondoa umaskini kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono tena hoja hii, nikisikitika Wilaya hii kuendelea kuwa gizani kwa miaka 70 leo.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi zinazofanyika na naipongeza Serikali kwa kuunda Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini. Katika hili, Kamati naitakia kheri. Ila kuhusu Madini, nashauri leseni kubwa zisimame kwanza mpaka tupate matokeo ya Kamati, ni muhimu, kwani wengine wanaendelea na *High Grading.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuleta ombi rasmi, ingawa nimekwisha lileta tena na tena. Sasa naomba Mkurugenzi wa Maendeleo ya Umeme Vijijini na Kamishna wa Nishati - Bwana Mrindoko, alione hili. Hivi sasa Serikali inapeleka umeme Bukombe. Wakati inafanya hivyo, nashauri sana ipitishe umeme huo kupitia Vijiji vya Bukoli, Nyarugusu, Nyakamwaga, *Rwangasa Backreef (East Africa Mine),* Katoro, Nyamtondo hadi kuelekea Bukombe ambako kuna vijiji vitatu vikubwa.

Mheshimiwa Spika, nina imani sehemu kubwa ya Idara hii ni kufanya biashara na kutoa huduma. Umeme uliopitia njia hiyo ni *economical* na faida ni kubwa. Miji niliyoitaja ni ya wachimbaji na ni mikubwa na sasa ni ya kudumu. Wananchi wana uwezo wa kununua umeme. Kuna maduka makubwa na wanahitaji umeme. Miji hiyo karibu yote inazidi Vijiji vya Mlandizi na Chalinze, hivyo wana haki ya kupata umeme.

Pili, umeme huo ukipitia ukanda huo, utasaidia kuinua elimu katika ukanda huo, kwani unapitia katika Shule za Sekondari zaidi ya nane ambazo ni Nyamalimbe Sekondari, Bukoli Sekondari, Nyarugusu Sekondari, Nyakamwaaga Sekondari, Busanda Sekondari, Kasewe Sekondari, Katoro Sekondari na Butundwe Sekondari na kuendelea kuelekea Bukombe. Vijana wetu wanashindwa kusoma masomo kwa mfano ya kompyuta kwa sababu ya kukosa umeme. Geita Wananchi wameamua kujenga Sekondari kila Kata. Sasa nanyi waungeni mkono.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo ni ya wachimbaji wadogo wadogo. Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Ndugu Masawe, walipita huko, wakatoa maneno ya matumaini. Sasa hawa wadau wenu ambao ni wachimbaji wadogo wadogo, mbona hamtaki kuwasaidia ili wazalishe zaidi. Wasaidieni.

Mheshimiwa Spika, hadhi ya Katoro ndiyo kijiji kikubwa kuliko vijiji vyote katika Kanda ya Ziwa. Mji huo unazidi idadi ya watu na majengo ya watu wenye uwezo kuliko miji mingine ya Wilaya nchini. Ni mji wenye ghorofa safi na hata Viongozi ndipo mahali pao pa kupumzika wakati wa kuelekea Kagera au Mwanza. Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, ni shahidi. Tunaomba umeme, uwezo wa kulipa upo. Suala la kusema ni njia ndefu kupitisha umeme kupitia Busanda hadi Bukombe, mawazo hayo si ya kiuchumi au kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Kakola unachimba dhahabu katika Jimbo la Busanda, ingawa umetobozea Kahama. Athari za mgodi ziko zaidi katika Jimbo la

Busanda. Tafadhali kama ni suala la kusaidia sehemu kubwa ya Wananchi, wachimbaji wadogo wadogo na kufanya biashara, pitisheni umeme Busanda, eneo lenye wadau wengi wa kutumia umeme.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ningependa nipate maelezo na ufafanuzi kwa nini *TANESCO* wameshindwa kushirikiana na *Konoike Construction* ili kufikisha umeme Bahi, kama ilivyokubaliwa katika kikao alichokiongoza Naibu Waziri kabla ujenzi wa barabara ya lami kutoka Dodoma hadi Manyoni kuanza? Hii ilikuwa hatua ya kwanza muhimu katika kusambaza umeme katika vijiji vyote kati ya Dodoma na Manyoni.

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme vijijini ni jukumu la msingi la *TANESCO.* Vipi hata anapopatikana mtu wa kuchangia gharama hizo, hatumpi ushirikiano unaostahili? Kwa taarifa nilizonazo, *TANESCO* hawakuonyesha nia ya kushirikiana na Konoike katika azma yao (Konoike) ya kufikisha umeme Bahi ambako walikusudia (Konoike) kuweka kituo chao kikuu *(Base).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala hili lilipata *publicity* kubwa katika vijiji vinavyohusika, ninaomba litolewe maelezo (kauli) wakati wa kujibu hoja mbalimbali za Wabunge, Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Ndugu yangu Waziri, Mheshimiwa Daniel Yona na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kazi nzuri na ngumu wanayofanya katika Wizara yao wakati huu wa utandawazi na uharibifu wa mazingira uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, nasema kazi ngumu kwa sababu ya uchumi wa utandawazi kutokana na huruma wala nafasi ya kumbeba maskini asiyebebeka. Pia changamoto ya kuharibika kwa mazingira na hivyo kuathiri vyanzo vya maji, mvua na kusababisha ukame ambao umekwamisha mitambo ya nguvu za umeme, inayoendeshwa kwa kutegemea mvua na mito yetu. Hongereni sana kwa kuwa na moyo thabiti, ikiwa ni pamoja na Katibu wenu Mkuu katika kukabili hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja ya Nishati na Madini, utalenga katika mambo yafuatayo: Umeme Vijijini, Sheria ya Umeme kwa Wateja, Sera ya Umeme endelevu, Utafutaji wa Madini na Utafutaji wa Mafuta.

Mheshimiwa Spika, nianze na lile la Umeme Vijijini, ambapo hivi sasa Serikali inachukua dhamana ya kupeleka umeme vijijini wakati tunasubiri kuanzishwa kwa *REA* na *REF.* Pamoja na Serikali kukubali dhamana hii na kuandaa mpango kamambe wa kupeleka umeme vijijini, je, mpango huo utajulikana lini hadharani? Kitu gani kilipelekea Shirika la *TANESCO* lisiwe na mpango huo tangu lilipoanzishwa nchini? Ina maana wakati huo *TANESCO* wakihusika na usambazaji umeme vijijini, hawakuwa na *master plan.* Je, walisambaza umeme kwa mpango upi na ukiwa wa wazi au wa siri?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ninaomba kupata majibu linahusu Shirika la Umeme kwa wateja. Kule katika Wilaya yangu ya Same, vyanzo vyetu vya maji ya ardhini, vinategemea mitambo inayoendeshwa na umeme. Katika eneo ambalo kuna visima vyetu vya maji, Halmashauri yetu ya Wilaya ilinunua *transformer* kwa fedha yake ili kutumia umeme unaojitegemea. *TANESCO* ikaingilia *transformer* hiyo kwa kuwafungia watu binafsi *line* za umeme katika nyumba zao, mashine za kusaga na kuchomea. Matokeo yake, hatua hiyo imeitia Halmashauri ya Wilaya ya Same hasara ya Sh. 25.3m/= kwa kuunguza *motor* za *pump* za maji zipatazo nane.

Mheshimiwa Spika, nimemwandikia Naibu Waziri kero hii ya kutaka kwanza, *TANESCO* waachane na *transformer* ya visima hivyo vya maji. Mpaka sasa hakuna majibu. Pili, nimemwomba Mheshimiwa Naibu Waziri awawajibishe *TANESCO* wafidie uharibifu huo wa Sh. 25.3m/=. Mpaka sasa majibu bado. Hiyo ilikuwa tarehe 19 Februari, 2004, wakati namwomba Naibu Waziri atoe majibu. Sasa leo *TANESCO* wako hapa Bungeni, naomba jibu la kuwapelekea Wananchi wa Same.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa tatu unahusu sera ya umeme nchini. Hivi sasa inaelekea Wizara haijaweka msimamo ni vipi italikabili tatizo la umeme nchini. Vyanzo vyetu vya umeme wa kutegemea maji havina uwezo tena kutokana na ukame na uharibifu wa mazingira. Mara tunasikia tatizo hili litakwisha kwa umeme wa Gesi ya Songosongo, mara Gesi ya *Mnazi Bay,* wakati mwingine Mradi wa Umeme wa Mchuchuma au *IPTL.* Tunasikia pia tunaweza kupata umeme wa kuaminika kwa *uranium* ambayo ipo kule Kusini katika Milima ya Njombe na pia milima yetu ya Same.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Wizara itupatie *the most appropriate option or choice* ya tatizo la umeme wa kutosheleza nchi yetu na ikibidi kuuza kwa nchi majirani zetu. Wakati wa kuwa na msimamo huo na uamuzi wa kuwekeza katika msimamo huo ni sasa. Vinginevyo, vizazi vijavyo siyo tu watatulaani, lakini tukiwa hai watatubeza na hata kutufikisha katika sheria. Bunge linahitaji kupata msimamo thabiti badala ya kila mara kusikia hoja mbalimbali ambazo bila shaka hazijachujwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ninalotaka kulisemea ni utafutaji madini na wachimbaji wadogo wadogo. Madini ni rasilimali kubwa ya nchi yetu na ambayo ni muhimu Wananchi wakaifaidi moja kwa moja. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwawezesha Wananchi wetu katika utafutaji wa madini? Je, wale wanaogundua madini hayo, upo utaratibu gani wa Serikali kutambua mchango wao katika Taifa? Wachimbaji wadogo wadogo, tumaini lao liko wapi au tunaachia madini yetu yachimbwe na wawekezaji wa nje peke yao?

Mheshimiwa Spika, sera na sheria za madini za sasa ni zile za kijamaa, ambazo zina mazingira ya kuwapunja watu wetu wakati tumefungua milango yetu kwa utandawazi. Tukiacha watu wetu wasishiriki kwa faida katika rasilimali ya madini yetu sasa, basi tujue tumewapokonya haki yao ya msingi ya uchumi wa madini. Tutalaaniwa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho unahusu utafutaji wa mafuta. Kwa muda mrefu tumeingia katika utafutaji huo kwa Shirika la *TPDC.* Ningeiomba Wizara sasa itujulishe Bunge, kile kinachokwamisha upatikanaji wa mafuta. Je, ni uhaba

wa fedha au utaalam? Iwapo siyo kimojawapo na mafuta hakuna, kwa nini Serikali isiweke mkakati mwingine ambao utakuwa wa manufaa kwa watu wake?

Mheshimiwa Spika, ningeomba pia kufahamu mwelekeo wa sasa wa kuiwezesha nchi yetu kuwa na mafuta yake. Je, kwa nini tumesitisha huduma za *TIPER* na *TPDC,* ambazo ndizo zingeweza kuipatia nchi yetu maslahi makubwa ya mafuta iwapo yangepatikana? Je, kesho tukijaliwa kupata mafuta, hatutajilaumu kwa kuyatelekeza Mashirika yetu ya *TIPER* na *TPDC?* Naomba Wizara iweke mambo haya bayana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, mafanikio wakati huu, wakikabili changamoto hii ya maendeleo ya Nishati na Madini nchini.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya hapa nchini, pamoja na mazingira magumu yanayowakabili. Hivyo, nasema naiunga mkono hoja hii. Hata hivyo, naomba kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme bado ni ya juu sana na ni ghali mno kwa watu wa kawaida, pamoja na vigezo vyote vilivyoonyeshwa na ulinganishi wa nchi za Kenya na Uganda. Nafikiri Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kutuusia kuwa ukitaka kujua kama wewe ni mzima wa afya, usijilinganishe na mgonjwa. Kama ni suala la kodi ya vifaa na zana za umeme kuwa ni kubwa, basi Serikali ijitahidi kudhibiti hali hii. Umeme ni nyenzo ya msingi kwa maendeleo, tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nipendekeze kuwa Serikali kwa kupitia au kwa kushirikiana na nchi nyingine za Afrika, zitafute mbinu/mikakati ya kujadiliana na wawekezaji katika madini. Bado utajiri mkubwa tulionao Afrika wa madini, hautusaidii hata kidogo, bado yanakwenda kuneemesha na kutajirisha nchi za nje ya Afrika. Kama nchi nyingi zinanufaika na maliasili zao kama mafuta na madini, kwa nini Afrika iwe tofauti na ukipeleleza utaona makampuni yote yanayovuna madini ya Afrika yanatoka nje ya Afrika kwa malengo ya uwekezaji na kadhalika? Lakini ukweli unabakia pale pale, tunaishia mrabaha mdogo na kodi zisizo na tija.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati umefika, kwa kupitia *NEPAD* na Bunge la Afrika, kutafuta mbinu/mikakati ya Bara letu la Afrika kunufaika na maliasili zake na hasa madini. *(Collective Strategic Bargaining Powers).* Ahsante

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel N. Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa juhudi zao wanazoonyesha kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa nishati ya umeme katika maendeleo ya nchi yetu, ni suala la dhahiri na linatakiwa kupewa uzito wake ili kuleta ukombozi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya, mimi napenda kuiomba Serikali ione umuhimu wa kuingiza maeneo yafuatayo katika

Jimbo na Wilaya yangu ya Shinyanga Vijijini, wakianzia na Mji Mdogo wa Iselamagazi, ambao unategemewa kuwa Makao Makuu ya Wilaya. Aidha, maeneo mengine ni Pandagichiza, Shilabela, Ng'wangosha, Ng'wamakaranga, Nindo,Monhigana, Ng'wabenda, Solwa, Zunzuli Sekondari, Salawe hadi *Sangu Ginnery.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme upatikanao kupitia maji na mafuta ni aghali sana na hivyo kwa Wananchi vijijini siyo rahisi kueneza, nashauri Serikali ijitahidi kutoa msukumo kwa *biogas, solar power* na mitambo ya upepo kuzalisha umeme unaoweza kutumika kwa matumizi ya vijijini ambako kiwango kikubwa cha umeme hakihitajiki.

Hata hivyo, kwa kutumia sheria tuliyopitisha hapa Bungeni ya *Atomic Act, 2002*, nashauri kwamba, ni wakati muafaka sasa kwa nchi yetu kuanza matumizi ya madini ya *uranium*, ambayo kwa mujibu wa takwimu za wataalam walioko Taasisi ya Teknolojia ya Taifa, tunaweza kuhitaji Matumizi Salama ya kiasi cha 0.03 ya *nuclear energy* kuzalisha umeme ambao utatosha kabisa kwa matumizi yote makubwa na madogo ya nchi yetu yote. Kimsingi huu utakuwa ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo la nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee maoni yangu juu ya Uongozi wa *Net Group Solutions.* Kimsingi kuna malalamiko toka kwa watumishi wengine wa *TANESCO* juu ya namna ambavyo Shirika hili lilivyofanya ubaguzi dhahiri wa malipo yao kati ya *Net Group Solutions* na watumishi wengine. Wenzao wanalipwa kiwango kikubwa mno (wageni), ukilinganisha na wazalendo. Nashauri Serikali ishughulikie tatizo hili kupitia Bodi ya Shirika ili kupunguza chuki miongoni mwa watumishi. Aidha, *Net Group Solutions* wajielekeze katika uzalishaji umeme badala ya mapato tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji wa miradi ya uchimbaji wa madini, napenda kuiomba Serikali itazame upya mambo yafuatayo:-

(i) Mikataba iliyokwishawekwa kati ya Kampuni za Uchimbaji na Serikali, itazamwe upya, yaani ifanyiwe *review,* kwani baadhi inao upungufu kadha wa kadha.

(ii) Suala la mrabaha kwa wilaya husika katika maeneo ya machimbo, siyo la kupuuza, kwani manung'uniko haya yanao msingi kabisa kwa mtangamano wa Taifa letu na kupunguza chuki na hisia za baadhi ya Wananchi kuona Serikali haiwajali.

(iii) Tume iliyowekwa kwa ajili ya kukusanya maoni toka kwa wadau mbalimbali, nashauri wana-Tume wanapokutana na wadau, wasitoe maelezo juu ya uzuri wa mfumo uliopo sasa katika sekta hii, bali wapokee maoni ya wadau juu ya kitu gani kifanyike ili kuboresha sekta.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusisitiza suala la umeme na umuhimu wake katika uchumi, pamoja na kuitakia kila la kheri Wizara hii kwa niaba ya Serikali, ili watekeleze majukumu yaliyo mbele yao kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. PHILLEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Daniel N. Yona, Waziri wa Nishati na Madini,

Mheshimiwa Dr. Ibarhim Msabaha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara hii, kwa kazi yao nzuri wanayofanya katika kufufua uchumi wa Taifa letu na kupiga vita umaskini. Naunga mikono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu na za Wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Rorya, napenda kutoa maombi ya Wananchi wa Jimbo la Rorya kwa Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001, 2002 na 2003, Wananchi wa Rorya walinituma niwafikishie maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri, maombi ambayo nimekuwa nikimfikishia Mheshimiwa Waziri wakati wa hotuba ya bajeti kuanzia mwaka 2001/2002, 2002/2003, 2003/2004 na sasa mwaka huu 2004/2005. Maombi yao ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupatiwa umeme katika sehemu za *Mission* ya Masonga *RC* na *Mission* ya Nyarombo *RC*. Vituo hivyo ni muhimu sana kwa kutoa huduma za matibabu na elimu. *Mission* ya Masonga inayo Shule ya Sekondari ya bweni na kubwa. Pia kuna Seminari na Hospitali. *Mission* ya Nyarombo inayo Hospitali yenye vitanda 40 na huhudumia Wananchi wapatao 20,000, wengi wao ni wavuvi.

(ii) Kijiji/Mji Mdogo wa Riagoro ni Makao Makuu ya Tarafa ya Girango na Kituo cha Afya ambacho kinahudumia Kata saba.

(iii) Kijiji cha Buturi na Shule ya Sekondari ya Buturi, nguzo za umeme zinapita karibu na Shule ya Sekondari.

(iv) Shule ya Sekondari ya Nyandugo na Kijiji cha Utegi, Wananchi wako tayari kuchangia sehemu ya gharama.

(v) Shule ya Sekondari ya Bukama iko mita 20 kutoka kwenye mtandao wa umeme unaokwenda Shirati.

(vi) Umeme wa Chereche.

(vii) Umeme wa Kijiji cha Kibuyi.

(viii) Umeme wa Bandari ya Sote Shirati.

(ix) Umeme wa Kutwaa, mwananchi amekwisha lipia *transformer*.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake wote, kwa kuandaa mradi kamambe wa usambazaji wa umeme vijijini. Naomba sana katika bajeti hii, angalau baadhi ya vituo nilivyovitaja vifikishiwe umeme.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya Mradi wa *Electricity IV - Phase II,* unaopaswa kutekelezwa katika Wilaya ya Babati, zikiwemo

sehemu za Jimbo la Babati Mashariki, Vijiji vya Mwada, Mdori, Minjingu na mashamba makubwa ya Bonde la Kiru na Magugu. Nimepitia hotuba yake, lakini sikuona hata aya moja inayoonyesha kuwa mradi huu bado upo na unaendelea. Nataka kufahamu maeneo hayo yatapatiwa umeme lini chini ya mradi huo?

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri, kazi njema na natanguliza shukrani zangu kwa ushirikiano wake na Naibu wake na Watendaji wa *TANESCO,* hasa sehemu ya Umeme Vijijini.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini katika maeneo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba Wizara ifuatilie suala la ufufuaji wa Mgodi wa Madini ya Bati Kyerwa, ulioko katika Jimbo la Kyerwa. Ni kweli kuwa kuna aina ya madini katika nchi yetu, ambayo hatuyatumiki sana, wala hatuna viwanda vya kuyatumia. Lakini katika suala hili la Madini ya Bati, ni nyeti kwani nchi yetu inahitaji mabati mengi ya kuezekea nyumba za Serikali na zile za Watanzania. Vinginevyo, ningependa nijue Tanzania inapata wapi madini yake ya kutengeneza mabati.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu yuafuatayo kuhusu wawekezaji katika migodi mikubwa ya dhahabu katika Kanda ya Ziwa:-

Hoja ni kwamba, mnamo mwaka 2001, Kampuni ya *Geita Gold Mine,* ilitoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa ingewachukua takriban miaka minane kuchimba dhahabu, kuuza, kulipa mkopo wa Benki pamoja na riba, kwa kuzingatia bei za wakati huo.

Lakini hivi karibuni, hasa tangu mwaka 2003, bei za dhahabu zimepanda katika soko la dunia. Wakati huo huo, uzalishaji umeongezeka katika migodi hiyo na hivyo faida kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo, ninaomba nijibiwe maswali yafuatayo:-

(i) Je, sasa kwa kupanda bei ya dhahabu na makampuni kupata faida, je, faida hiyo wanailipia kodi?

(ii) Je, sasa ni kweli kuwa wataendelea kulipa mkopo na riba ya Benki kwa kipindi hicho cha miaka minane?

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, ninaomba kupata maelezo ya kwa nini Serikali haitaki kuvuta umeme kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe na kusogezea Miji Midogo inayochipua katika Jimbo la Kyerwa kama vile Nkwenda, Mabira, Isingiro na maeneo mengine ya Wilaya ya Karagwe kama Nyaishozi, Rwambaizi na kadhalika? Hii ni kuzingatia kuwa umeme umefika Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe kwa miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, vilevile Waziri azingatie kuwa umeme huo unatoka Uganda na ni wa bei nafuu na hivyo hakuna hasara kwa *TANESCO* Mkoani Kagera. Hivyo, uwezekano wa kupanua usambazaji wa umeme katika maeneo niliyoyataja, hauwezi kuwa na kikwazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijulishe kwamba, je, Serikali inaweza kuruhusu Kampuni nyingine zaidi ya *TANESCO* kusambaza umeme wa bei nafuu bila kuhitaji kupitishia umeme wake *TANESCO?*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijulishe ni kwa nini wawekezaji wa kwanza waliuza ardhi ya Mgodi wa Bulyankulu na Geita na ni kwa nini deni la kuuziana linakatwa katika mrabaha wetu? Ardhi yetu, mgeni anamwuzia mgeni mwenzie!

Mheshimiwa Spika, ardhi yote ya Madini ya Wanamwibara inamilikiwa na wageni (kutoka nje ya nchi) na kwa vile Watanzania wa Mwibara wana uwezo wa kupata vifaa vya kisasa kama ilivyo Nyamongo, je, Serikali iko tayari kuwarudishia ardhi?

**MHE. REJEMIAH J. MULYAMBATTE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote. Nasema hongera, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kwamba, naomba kupewa umeme katika Shule mbili za Sekondari, yaani Kimali na Nghoboko. Shule hizi zimeingia katika miaka mitatu *(Form III)* zote. Shule nyingine ni Nyalanja Sekondari, ambayo imeanza mwaka huu 2004. Naomba nayo ipewe umeme.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ni kuhusu wachimbaji madini wadodo wadogo na wakubwa, wawe na muda wa kupimwa na muda maalum wa kuchunguzwa kama wamepata wanachokitafuta. Siyo kuchukua miaka saba mpaka 10 bado wanatafuta madini tu. Huo ni uongo.

Mheshimiwa Spika, wapo watu wanaotafuta madini kwa muda wa miaka saba hadi kumi Wilayani Meatu na kwingineko. Hata kama wamepata wanachokitafuta, bado hawatasema kuwa wamepata. Watu hawa wanachimba na kuacha mashimo mengi bila ya kuyafukia. Naishauri Serikali ilifanyie kazi suala hili na kuwapa muda mfupi wa utafutaji madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 67 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, takwimu inaonyesha kwamba, jumla ya mauzo ya nje mwaka 2002 yalikuwa ni 38.9% na 2003 ni 55.2% ya jumla ya mauzo ya nje. Mazao mengine yote yapo baina ya 4% na 7.4%.

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kuwa madini yamechukua nafasi kubwa katika uchumi wa nchi. Hivyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri akalieleza Bunge hili, mchango wa madini katika uchumi wa nchi yetu (ikilinganishwa fedha, ajira na mashine kwa mchanganuo wa moja moja).

Mheshimiwa Spika, umeme unaouzwa na *TANESCO* kwa Shirika la Umeme la Zanzibar, inasemekana kuwa wastani wa 40% ya umeme huo unapotea njiani. Lakini katika kumbukumbu za *TANESCO,* umeme huo unatafsiriwa kuwa umeenda Zanzibar. Lakini kumbukumbu za Zanzibar za umeme unaopokelewa, ni pungufu ya huo unaopotea. Hali hiyo huwa ni sehemu ya tatizo au mvutano wa kibiashara kati ya *TANESCO* na Shirika la Umeme Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa vile tatizo hili ni la muda, naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze wamefikia wapi katika ufumbuzi wa tatizo hili. Aidha, naomba nieleweshwe *(technically)* namna tatizo hili la upotevu wa umeme linavyoweza kuepukwa kabisa au angalau kupunguzwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tanzania kujaaliwa kuwa na madini, pia imebahatika kuwa na gasi. Yapo matumaini ya kuwa na mafuta. Lakini kilichojitokeza ni kuwa, Serikali zetu mbili bado hazijafikia au kukubaliana katika usimamizi au utendaji katika miradi hii. Kwa vile miradi hii inaweza kuwa ni sehemu muhimu katika ukombozi wa kiuchumi na kuwaondolea umaskini Watanzania. Nashauri Serikali zetu mbili zikae pamoja kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili haraka iwezekanavyo.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa ushirikiano wao ambao umewezesha kuwasilisha hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa vile inaendelea kuandaa mikakati ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya zote nchini na vijijini. Naomba kasi hii iendelee.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati hii, bado ninaikumbusha Serikali kwa ahadi yake ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe (Ushirombo) kabla ya mwaka 2005. Hata hivyo, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri aliyowasilisha kwenye Bunge hili, inaeleza kuwa bado mazungumzo ya kupata fedha kwa wafadhili, yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, bado kuna mashaka juu ya ahadi hii kama itatekelezwa kama ilivyoahidiwa. Hivyo, naomba Mheshimiwa Wairi wakati wa hitimisho, aeleze mazungumzo haya ya kupata fedha na mfadhili yataisha lini na lini mradi huu utaanza na kwisha?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina madini mengi ambayo yanachangia kwa kiwango kikubwa Pato la Taifa na moja ya madini haya ni dhahabu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wananchi wetu wamekuwa wakijiajiri wenyewe kwa kazi ya kuchimba madini (wachimbaji wadogo wadogo). Lakini kwa hali ilivyo sasa, wachimbaji hawa wadogo wadogo, Serikali haiwasaidii. Kwani mara baada ya

kugundua madini, wachimbaji wakubwa huwavamia kwa kupewa kibali na Serikali bila hata fidia. Hivyo, wachimbaji hawa wanakosa hata utetezi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kudundua madini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ninaiomba Serikali iangalie utaratibu wa kuwatambua wachimbaji wadogo wadogo ili nao wapate haki ya kumiliki maeneo wanayoyagundua. Vinginevyo, wapewe fidia.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba Waziri aeleze kuhusu Mradi wa Kituo cha Uchimbaji na Uchwejuaji Dhahabu kwa Wilaya za Chunya na Bukombe, umefikia wapi, kwani hakuna dalili zozote zinazoonyesha kuanza kwa mradi huu Wilayani Bukombe?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji, kwa ushirikiano wao ambao wamaonyesha nia ya kuupatia umeme Mji wa Ushirombo na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshsimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 32, ukurasa wa 19 wa hotuba ya Waziri, inazungumzia juu ya Mradi wa Gesi ya Songosongo na kwamba gesi hiyo hivi sasa imeshafika Dar es Salaam. Je, ni lini vijiji vya Miji Midogo iliyopangiwa kupata umeme wa gesi hiyo, vitawekewa *transformers* ili viweze kupatiwa umeme? Yaani nataka kujua kwamba itachukua muda gani au miezi mingapi, vijiji hivyo kupelekewa umeme, ambavyo ni Ikwiriri, Kibiti, Bungu, Jaribu Mpakani, Mlanzi, pamoja na Makao Makuu ya Wilaya - Utete?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Net Group Solutions*, kwa vile muda wa mkataba wa kampuni hiyo umeongezwa kwa muda wa miezi mitatu, je, baada ya kipindi hicho kumalizika na lengo linalohitajika halikufikiwa, itatafutwa kampuni nyingine ifanye kazi hizo au itaendelea kampuni hiyo hiyo kufanya kazi ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikiifanya?

Hata hivyo, kampuni hiyo ya *Net Group Solutions* imekuwa ikilalamikiwa na Wananchi hasa kwa upande wa kukatikakatika umeme mara kwa mara. Ingawa ni kweli umeme kutoka *IPTL* unatumika kutokana na uhaba wa maji, lakini pamoja na umeme huo wa *IPTL*, tatizo la kukatikakatika umeme bado linaendelea. Je, *TANESCO* italipa fidia ya vyombo vya wateja vilivyoharibika kutokana na tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, kwa nini mpaka sasa madini yetu hayana udhibiti wowote na mali hiyo inatumika kutajirisha watu wa nje ya nchi? Inasemekana kuna ndege ndogo ndogo zinatua katika viwanja vidogo vidogo vilivyopo machimboni na kuruka kwenda nje ya nchi bila ya ukaguzi wa aina yoyote. Je, hilo linajulikana na Wizara au vipi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa *Stiegler's Gorge Multipurpose Project,* vipi mradi mkubwa wa umeme kama huu ambao ungetoa *megawatt* 2100, kiasi ambacho tungekuwa na uhakika wa umeme sisi wenyewe hapa nchini kwa kutosha kabisa na

tungeweza kuuza nje na kupata fedha nyingi za kigeni. Vipi tunaacha kwa makusudi na kutoushughulikia kuupatia mwekezaji? Pale ilipoonekana kuwa mwekezaji angeweza kupatikana, mpaka sasa bado mwekezaji huyo hajapakubaliwa, kulikoni? Je, Wizara inasema nini kuhusu suala hili la *Stiegler's Gorge?* Kwa vile kwa muda mrefu sasa halijaweza kufikiriwa wala kugusiwa, je, kuna maagizo kutoka mahali fulani, jambo hilo kuachana nalo au ni mawazo tu ya Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini? Naomba jibu wakati wa majumuisho kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkaa wa Mchuchuma, hivi kuna nini mpaka tunashindwa kupata mkaa ule ili kuzalisha umeme? Kwa nini Wizara inakazania umeme wa *IPTL,* kulikoni?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuma cha Liganga, ni lini chuma hiki cha kitachimbuliwa? Haisaidii kutoa jibu la ufinyu wa bajeti, kwani hilo si jibu, bali ni kukwepa kushughulikia jambo muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Hebu tupeni jibu sahihi, lenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji, kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa kwa namna ya kutaka kukidhi matakwa ya kila mdau wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza katika mambo matatu. Kwanza, ni Mgodi wa Dhahabu Tulawaka Biharamulo. Nitakayoyasema yataonekana ni ya ajabu, lakini ni kweli. Baada ya Serikali kusaini Mkataba na Kampuni ya *Pangea Minerals Limited* mnamo Desemba, 2003, Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Chama cha Mapinduzi, iliniweka Kitimoto, Wajumbe walinihoji wakitaka kujua kulikoni.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mwakilishi wa Watu (Mbunge), katika Mkataba huo yaliyomo ni yapi *(contents),* je, utaratibu huo ndio tuliupitisha Bungeni wa kuruhusu pande mbili tu, yaani Serikali na Kampuni peke yao kutiliana saini bila kushirikisha Kiongozi yeyote kutoka katika eneo lenye mgodi? Je, huu ndio uongozi shirikishi? Je, huu ndio uongozi wa pamoja? Je, nini maana ya mahusiano mema?

Mheshimiwa Spika, iwapo mimi Mbunge niliiandikia barua Kampuni ya *Pangea Minerals Limited*, ya kutaka kwenda Mgodini na ujumbe wangu ili tuweze kufahamiana, lakini cha ajabu ni kwamba, mpaka sasa sijapata majibu, huu ndio Utawala Bora? Kwa kuwa sikuwa na majibu ambayo yangejitosheleza, niliomba kikao kinipe muda ili niweze kuyafanyia kazi. Hapa Mheshimiwa Waziri, naomba kwa heshima na taadhima, arejee mazungumzo yetu ofisini kwake namna alivyonijibu/ahadi alizonipa. Namwomba anipe majibu kabla ya mwisho wa Mkutano huu wa 16 wa Bunge kumalizika, ili nirudi Jimboni kwa amani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua iliyokwishafikiwa, nimeshitushwa na mabadiliko ya ghafla ya ratiba ya upelekaji wa umeme Biharamulo bila maelezo sahihi na ya kina, yakieleza sababu za msingi zilizosababisha hali hii kujitokeza, kwani ahadi

iliyopo sasa ni mwezi Desemba, 2003 hadi mwezi Machi, 2004, umeme utakuwa unawaka, kwani *connotation* inayotolewa na Wananchi ni kuwa huu ni umeme wa Uchaguzi, siyo kutimiza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa katika kuruhusu wawekezaji katika Sekta ya Madini, lazima tuwe waangalifu sana ili nchi yetu isije ikapoteza misitu ambayo ni ardhi na nchi, watu wetu wasije wakapoteza uhuru na utu wao, kwa kubakia vibarua tu, pamoja na ajira kuongezeka na kupoteza sauti yetu katika soko la Kitaifa na Kimataifa, kwani wanaousa dhahabu ni wawekezaji, siyo Taifa. Hapendwi mtu, ila faida tu.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Aidha, napenda niwapongeze sana Viongozi wa Wizara hii kwa maandalizi ya hotuba hii nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza sana kwa ujasiri mkubwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hasa wakiongozwa na Simba Mtoto, Alhaj Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar, kwa kuweza kubeba gharama kubwa ya kutengenezwa *generators* kule Pamba na kupeleka umeme kule Kisiwani Pemba.

Mheshimiwa Spika, sote tunaitambua hali ya uchumi wa Zanzibar ilivyo na bado Serikali ya Muungano kwa kulitumia Shirika la *TANESCO,* inaona hakuna umuhimu wa kuwapelekea umeme kule Pemba. Mimi sioni uzito kama kweli sisi ni ndugu, kushindwa kuhudumiana kwa kuisaidia Zanzibar kwa mzigo mkubwa na mzito ilioubeba, ingawa nina hakika wanajua kuwa umeme ni muhimu kule Pemba. Aidha, mimi sioni Pemba imekosa nini hadi kufikia kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba niishukuru Serikali yetu ya Muungano kwa kukubali kukaa na wenzao Zanzibar na hatimaye kukubali kusamehe madeni ya muda mrefu ya Zanzibar. Nasema ahsante sana. Aidha, ninaomba sana Waziri na Naibu wake, waone kuwa kuna umuhimu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar kwa kuangalia uwezekano wa kusamehewa madeni. Ila bado naomba niendeleze maombi yangu ya kuwasaidia watu wa Kisiwani Pemba, kuwapatia umeme wa *TANESCO* kwa utaratibu wa kitaalam, kwa imani kuwa Pemba na Tanga haziko mbali. Kwa nini tushindwe?

Mheshimiwa Spika, mimi sina pingamizi na maombi ya bajeti hii na kwa heshima kubwa narejea tena kuwaomba waandaliwe wataalam wetu wa Serikali zetu kukaa pamoja na waangalie uwezekano wa kupeleka umeme wa *TANESCO* kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, pia kabla ya kusahau, ninaomba nitolewe wasiwasi ambao ninao kwa muda mrefu kuhusiana na *life span* ya *wire* wa umeme unaotoka huku Tanzania kwenda Zanzibar. Nahisi kuwa sasa muda umekuwa mrefu na sijapata habari ya kubadilishwa kwake au hakuna madhara yoyote?

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hotuba hii kwa ukamilifu.

**MHE. ABDULLATIF HUSSEIN ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, pamoja na kuwashukuru Watendaji wa Wizara hiyo, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa mafanikio waliyopata mwaka 2003/2004, pamoja na kuongezeka kwa mapato yake kwa asilimia 36, juu ya kwamba ukame ulituhangaisha sana.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza *Net Group Solutions*, kwa kuongeza mapato ya *TANESCO* kwa asilimia 60 na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa *TANESCO*, pamoja na kudhibiti wizi wa umeme. *It was a wise decision to find such a good management company.*

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukatikakatika umeme lidhibitiwe, kwani linaharibu vifaa vingi, vikiwemo vya Serikali vile vile. *Instant action should be taken to avoid this problem.* Wizara izingatie bei kubwa ya umeme, hasa kwa Wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TANESCO (Net Group Solutions)* kwa kufanya matengenezo bila kuzima umeme. *It is a greatg step forward. Net Group Solutions* iwe na ukakamavu wa kuagizia vifaa ili Wananchi wafungiwe umeme wanapoomba. *Quick service to the public is a must.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Gesi ya Songosongo, kwa kuwa mikataba ya kununuliwa imeshafanywa na makampuni kama *Tanzania Portland Cement, Tanzania Breweries Ltd*. na kadhalika, ningeshauri *Excise Duty should be imposed to generate income for the TPDC.* Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, mshiriki wake *Pan African Energy Ltd. and the Government.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *IPTL* kwamba ni umeme wa gharama, ninaendelea kuipongeza Serikali na Wizara kwa kuendelea na umeme huu na kuepusha kukatikakatika kwa umeme, jambo ambalo lingeturudisha nyuma sana. *Lack of electricity will bring about more loss to the entire economy and well being of our people. Somehow, the government should gradually own the IPTL so as to avoid future dependent on this private ent. of course by the funding of World Bank.*

Mheshimiwa Spika, tuwe na hadhari sana katika kuchimba madini. Tukifanya mchezo, tunaweza kuingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. *Where theres is money, there is fighting. Extra careful should be observed by the Government and Ministry to avoid such calamity.*

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwasiliana kwa karibu na kuelewana ili mafuta ya petroli yatafutwe na yachimbwe. *Time is money.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara na Mashirika ya *TANESCO, TPDC* na *STAMICO,* kwa kazi nzuri wanayojitahidi kuifanya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza sana Shirika la Maendeleo ya Tanzania *(TPDC),* kwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Songosongo hadi kuhakikisha kwamba, gesi imefika Ubungo na *Wazo Hill* na kuanza kutumika viwandani na kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa ushauri na mapendekezo katika maeneo yafuatayo: Kuhusu utafutaji mafuta baharini *(Deep Sea Exploration),* kutokana na tofauti zilizopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, juu ya kuiruhusu Kampuni ya *Shell* kufanya utafiti wa mafuta eneo la ukanda wa Pemba, Wizara iwajibike kikamilifu kuzishauri Serikali hizi kuafiki mpango uliopo kwa manufaa ya umma (Tanzania) na Serikali zielewe kwamba, kucheleweshwa kwa mpango huo ni hasara kwetu kama Taifa moja na inawezekana nafasi hiyo *(opportunity)* ikatoweka kabisa. Lakini pia, Chombo cha Ushauri wa Sheria Serikalini *(AG)*, kisimamie na kushauri uhalali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kushinikiza kucheleweshа kuletwa ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, marekebisho ya Sheria ya Utafutaji Mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa mauzo ya Gesi ya Songosongo, mpango wa awali ulikuwa kuanzishwa kwa Kampuni ya *GASCO* ili ihusike na mauzo ya gesi kutoka Songosongo na kwamba, Kampuni ya *SONGAS* ingejihusisha na uzalishaji na usafirishaji (usambazaji wa gesi hiyo). Je, utaratibu huu umefikia wapi wakati huu, ambapo tayari gesi iko Ubungo? Inaonekana kwamba, *SONGAS* itabeba majukumu yote ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji. Je, *TPDC* itahusika vipi na kuna mantiki gani kuiachia kampuni moja kufanya kazi zote bila udhibiti wowote? Ni dhahiri kwamba, Wizara ya Nishati na Madini isipodhamiria kusimamia mpango au Mikataba ya Gesi ya Songosongo, nafasi ya *TPDC* itakuwa ndogo na hata fedha za mauzo wanazostahili kuzipata, wakazikosa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameendelea kulalamikia miradi ambayo imeanza, lakini haijakamilishwa. Mara nyingi inaonekana kwamba, Wizara ya Nishati na Madini haina taarifa kamili ya aina ya miradi hiyo. Ili kuondoa hali hiyo, nashauri Wizara iitake *TANESCO* kutoa orodha kamili ya miradi yote ambayo imesimama nchi nzima, ili mpango wa kuikamilisha ufanyike ili kupunguza malalamiko ya aina hiyo. Mfano Muheza, upo mradi uliokuwa utoke Muheza hadi Kiwanda, ambapo kipo Chuo cha Ufundi kupitia Vijiji vya Kwasemgaya, umbali wa kilometa saba toka Bombani Tongwe hadi Kiwanda. Tangu mwaka 1999 hadi sasa, mradi umeishia kilometa saba na haukamiliki! Mradi wa kupeleka umeme Kijiji cha Kilulu tangu 2001/2002, haujakamilika licha ya kuwepo katika hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini na Taarifa ya Utekelezaji ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utata uliopo bandarini hivi sasa kati ya zoezi la kufunga *flow meters* na meli zinazotaka kupakua mafuta, pamoja na nia nzuri ya Wiara ya Fedha kutaka kudhibiti mapato, utekelezaji wa kazi hiyo unapoathiri upatikanaji wa mafuta kwa muda, unaonyesha udhaifu wa ushirikiano kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati na Madini. Kwa bahati mbaya, Wizara ya Nishati na Madini ndiyo itawajibika kama huduma za usafiri zikisimama. Ni vyema Serikali ikatambua hilo na kuepusha shari kati ya Serikali na Makampuni ya Mafuta kabla hali haijawa mbaya kama ilivyoelezwa jana tarehe 14 Julai, 2004 na Mheshimiwa Mbunge kutoka Morogoro.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kucheleweshwa kukamilisha taratibu za kutangaza eneo la Sakale (Amani, Muheza) kuwa eneo la wachimbaji wadogo wadogo. Tangu dhahabu kugunduliwa huko Sakale na uchimbaji kuendelea sasa karibu mwaka mmoja, taratibu za kutangaza kupima na kugawa eneo hilo kwa wachimbaji wadogo wadogo, hazijakamilishwa. Tungeomba kujua sababu za ucheleweshaji huu.

Pamoja na ukweli kwamba, sasa dhahabu imepungua sana Sakale na wachimbaji kuhamia maeneo mapya katika Vijiji vya Mlesa na Mbomole. Je, Serikali itatangaza eneo lote ili kuunganisha maeneo haya mapya?

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaomba kujua kama Serikali inafahamu kwamba yupo mwekezaji mkubwa anayefanya utafiti wa madini katika eneo hilo la Sakale na Monga na kama kweli yupo, je, anafanyaje kazi hiyo katika eneo linalokusudiwa kutangazwa kuwa la wachimbaji wadogo wadogo? Hali kama hii inapelekea kukaribisha migogoro ya makusudi kama ilivyo sasa kati ya *AFGEM* na wachimbaji wadogo wadogo Mererani.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Ofisi ya Madini Mkoa wa Tanga imekataa kwamba, inamjua mwekezaji huyo huko Sakale na Monga na kwamba, haijampa leseni ya aina yoyote. Lakini je, wamefanya utafiti kujua kama kweli mwekezaji huyo yupo na anaendelea kuwepo au ameshaondoka baada ya kuzongwa na Wananchi? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. Katika kuchangia hoja hii, nitajielekeza zaidi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, kifungu cha 5(iii), kinatamka kupeleka umeme hadi Makao Makuu ya Wilaya. Katika Mkoa wa Rukwa, ni Wilaya ya Nkansi ndiyo hadi sasa haijapatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa sita wametaja kuwa hadi 2005, Wilaya za Biharamulo, Ngara, Rufiji, Serengeti, Ukerewe na Urambo, zitakuwa zimepatiwa umeme. Je, Wilaya ya Nkansi imewekwa wapi katika utaratibu huu? Ninaomba nipatiwe majibu, kinyume chake, nitatoa shilingi.

Aidha, ninapenda nifahamishwe Serikali inasemaje katika kusambaza umeme katika vijiji na Wilaya zifuatazo za Mkoa wa Rukwa:-

(i) Wilaya ya Sumbawanga Vijijini: Vijiji vya Laela, Mtonisa, Mwimbi, Kasanga, Matai, Sopa, Mwazye na Mpui.

(ii) Wilaya ya Nkansi, hadi sasa haina umeme. Hata hivyo, napenda kufahamu, umeme utakapofika katika Wilaya hiyo, je, umeme utafikishwa katika Vijiji vya Kate, Kirando, Wampembe, Chala na kadhalika.

(iii) Wilaya ya Mpanda: Vijiji vya Karema, Ikola, Inyonga, Ulwila, Stalike na Kapalamsenga.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nipatiwe maelezo mahsusi kuhusiana na maswali yangu niliyoyauliza hapo juu.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono bajeti hii kwa asilimia 50 na kuwapongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam, kwa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango iliyowekwa katika hotuba ya kueneza umeme nchini kote, uwezo utakapopatikana, hakuna *time frame* wala kiwango cha fedha kinachotafutwa. Badala yake wanazungumzia wawekezaji tu ndio tunaowategemea. Je, ni wawekezaji peke yao walioamua umeme wa Gesi ya Songosongo upelekwe mikoa mingine na siyo Mikoa ya Lindi na Mtwara ambako ndiko kuliko chimbuko la gesi hiyo na ambako hakuna umeme wa uhakika? Je, utaratibu huu tumeiga kutoka nchi gani ambaoo sehemu inayozalisha umeme ibaki na giza? Hivyo ndivyo ilivyo Wilaya na Mikoa iliyozalisha umeme wa *grid* ya Taifa Kihansi, Hale, Pangani, Kidatu, Mtera na *IPTL?*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kuwaridhisha Wananchi wa Mikoa ya Kusini, kwa nini Gesi ya Songosongo isitumike kwa mikoa hiyo kama ilivyofanyika katika Mikoa/Wilaya zilizozalisha umeme wa *grid* ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali inajua kwamba, umeme unaozungumziwa wa *Mnazi Bay* ni hadithi za alinacha, hazileti matumaini yoyote, bali ni kuendelea kuwapumbaza Wananchi wa Kusini? Hivi tunavyosema, tunasukuma utalii Mikoa ya Kusini, ina maana gani? Giza litawavutia watalii Kusini?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hali halisi ya umeme nchini na vyanzo vyake, kwani imeelezwa kwamba, umeme unaotumika na kutegemewa ni wa *IPTL.* Vyanzo vingine vina matatizo gani na hatua gani zinachukuliwa na Serikali kurekebisha?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe mipango ya kueneza umeme wa *grid* ya Taifa utakavyosambazwa Wilayani hasa Liwale, kwani hata umeme wa Songosongo au *Mnazi Bay* ungepatikana ungefika vipi Wilaya ya Liwale?

Mheshimiwa Spika, narejea kwa kusema kuwa, ninaunga mkono hoja kwa asilimia hamsini.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na mikakati ya uenezaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha mipango ya kiuchumi katika Wilaya ya Njombe na kutokana na kushusha umeme wa *grid* pale Makambako, naomba *TANESCO* ipeleke umeme *Lupembe Tea Factories,* Mashariki ya Njombe (maili 45 toka Kibena), Vijiji 12 vilivyoko kati ya Kijiji cha Ibumila na Igongolo, eneo hili limeendelea sana

kiuchumi na kuna watu wengi na kwenye vijiji kati ya Njombe Mjini na Kipengere (vijiji 15), kandokando ya barabara. Umeme kwa Viwanda vya Mbao, mwanga na huduma.

Nawapongeza Wizara kwa kushusha umeme wa *grid* Makambako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara ya Madini na Nishati mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa maandishi, nahitaji Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, wanieleze utekelezaji wa masuala yafuatayo yatatekelezwa lini:-

Mheshimiwa Spika, nguzo za umeme kwenye Vibanda vya CCM Shinyanga Mjini, zitawekwa lini ili Wananchi waweze kufanya biashara zao na hatimaye kujiondoa kwenye umaskini? Kwa nini Meneja wa *TANESCO* Mkoani Shinyanga anakidharau Chama Tawala (CCM), kwa kutoa ahadi zisizotekelezwa kila mara, lakini watu binafsi wanapewa nguzo na kufungiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata maelezo lini Wizara hii ya Nishati na Madini itapiga marufuku mtindo wa kutoa bili za umeme za makisio kwa Mkoa wa Shinyanga na Dar es Salaam, ili Serikali isilaumiwe na Wananchi wake?

Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 13, ametaja kero za wateja wa *TANESCO,* lakini kero hizi hakuzitaja.

Naomba aorodheshe kero hizi na azitatue kwa sababu zipo chini ya uwezo wake. Ni kuwatangazia Mameneja kuacha mtindo huo wa dhuluma kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme ni kubwa sana na ndiyo sababu Wananchi wanaotumia umeme tu ni wachache na hivyo kuwasababishia wengi kuathirika na matumizi ya kuni na mkaa, vitu ambavyo vinatoa moshi kwa wenye madhara ya macho na koo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie uwezekano wa kupunguza bei ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya machache ya mchango wangu, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika mazingira ya bajeti ndogo inayopangiwa Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono tena hotuba hii mia kwa mia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kikao cha asubuhi.

Waliokuwa hawajachangia kabisa, waliokwisha changia mara moja tu, waliokwisha changia mara mbili, wote wamepata nafasi, waliokosa ni wale waliokwisha changia mara tatu na mmoja alishachangia mara nne. Kwa hiyo, nafikiri wataelewa kwamba, tumewatendea haki wale wengine. Tutakaporejea jioni watajibu hoja watoa

hoja kwa muda wa saa moja unaoruhusiwa na Kanuni zetu, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*(Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Kabla sijaanza napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kibaha kutoa rambirambi kwa wale wote ambao wamepata matatizo ama ya kufiwa na wazazi, watoto na pia kwa familia ya Marehemu Mwalyego.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana hadi leo Bunge hili limeshuhudia mjadala mkubwa juu ya suala la Nishati na Madini, hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Nishati na Madini mbele ya Bunge lako Tukufu. Awali ya yote napenda niseme kwanza kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini mia kwa mia. *(Makofi)*

Pili, napenda niwahakikishie Ndugu zangu Wabunge kwamba michango yote ambayo imetolewa hapa imekuwa na msisimko mkubwa, changamoto kubwa kwetu sisi na pengine ningenukuu maneno aliyoyasema Mheshimiwa Abdulaziz jana kwamba yeye anatuheshimu sana sisi na hata baada ya michango yake au mchango wake heshima iendelee pale pale na urafiki uendelee pale pale. Napenda nimhakikishie kwamba na sisi ndio tulivyochukulia hivyo kwamba si yeye tu lakini na Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia humu Mheshimiwa Nyimbo, Mheshimiwa Prof. Mwaga, Mheshimiwa Abdulaziz mwenyewe na wengine wote waliochangia. Tumechukua michango yao kama ni changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mambo yaliyochangiwa ni mengi mno haitawezekana kujibu au kuchangia katika hoja hii kila kitu kilichosemwa. Lakini kama ambavyo Mheshimiwa Waziri atasema ni kwamba tumeyachukua yote na tutayafanyia kazi na Waheshimiwa Wabunge tutawaletea majibu kwa maandishi wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kutoa wasi wasi Waheshimiwa Wabunge kwenye suala la ujumla. Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi imejionyesha kama kuna wasi wasi juu ya udhibiti wa Wizara mpaka ikafikia wakati Waziri wangu akaulizwa kama yeye yuko *in-charge* au sio. Mimi napenda niwafahamishe na niwahakikishie kwamba Waziri Yona yuko *in-charge* na mimi namsaidia yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna tatizo la uelewa mdogo pale Wizarani. Sisi hapa Wabunge tunafahamiana, *back ground* zetu tunajuana. *Back ground* ya Waziri Yona mnaijua, yangu mimi pia mnaijua. Baina yetu sisi tuko kwenye kushirikiana na

timu iliyoko kule ya wataalamu wale. Lakini wale wataalamu hawatubabaishi sisi, sisi tuna uwezo wa kuwasimamia ipasavyo.

Kwa hiyo, kama kulikuwa na hisia yoyote kwamba labda Wizara inayumba hapana. Wizara haiyumbi. Wale ni wataalam na katika dunia hii ya sayansi na teknolojia tunawajibika kusikiliza ushauri wao. Tunawajibika kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Serikali. Lakini napenda niwatoe wasi wasi ndugu zangu kwamba hakuna tatizo la kuyumba hapa. Wakati mwingine *size* zetu hizi zina matatizo. Waziri wangu huyu maskini akionekana hivi anaonekana kama labda pengine anayumba. Hapana ni mtu mpole, lakini ni mtu makini sana na ni mtu ambaye mwenye msimamo. Sasa na sisi warefu wakati mwingine mkituona mnaweza ukadhani labda hapana, sisi tuko katika Wizara ile na yeye ndio kiongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo au issues za Wizara ya Nishati na Madini na hasa kwenye upande wa nishati. Ni masuala magumu kwa maana kwamba ni complex, kama nilivyosema mwanzo yanahitaji ufundi wa aina yake na sisi tunashukuru kwamba tuna timu nzuri ya mafundi wakiongozwa na Katibu Mkuu wao. Lakini kama nilivyosema awali si kwamba labda uelewa wetu mdogo hapana. Lakini dunia tunayoishi sasa hivi mambo mengi haya ambayo zamani yalikuwa ni mambo ya sera ya ndani tu, siku hizi ni mambo ambayo yanavuka mipaka. Ni mambo *complex* katika *qualities* zake, katika *qualities* zake, *actors* ni wengi watu wanaoshiriki ni wengi, aina ya uchumi tuliokuwa nao sasa hivi ni uchumi ambao si kama ule wa kizamani ambao unaweza ukatoa amri tu mambo yakaenda kama unavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi sisi tunakubaliana na mawazo ya msingi yaliyotolewa hapa tangu michango ya jana hadi ya leo. Kwamba sote tunakubaliana. Kwa mfano kwenye upande wa nishati juu ya umuhimu wa kuwa na nishati yenye uhakika. Kwenye upande wa umeme na kwenye upande wa mafuta tunakubaliana kwamba ni muhimu lazima tuendeleze vyanzo vyetu vya ndani kikamilifu. Tunakubaliana pia kwa kuwa tunaishi katika dunia ambayo tunategemeana sisi tuko katika eneo lililoko katika ukanda ambao tuna majirani ambao tunashirikiana nao ama katika Afrika Mashariki au katika nchi za Kusini. Sehemu zote hizi tunawajibika kuweza kushirikiana nao kwa mambo mbalimbali. Lakini napenda niwahakikishie kama nilivyosema awali kwamba suala hapa si kwamba labda mambo hayafahamiki, hapana yanafahamika, lakini yachukuliwe kwa kiwango cha hali ya dunia ilivyo hivi sasa na hali ya nchi ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitagusia mambo yafuatayo machache kwanza kwenye suala zima la umuhimu wa nishati Vijijini au nishati kwa ujumla. Kama nilivyosema awali hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi na orodha hii itatajwa na Mheshimiwa Waziri, Wabunge wote ambao wamechangia kwa mdomo na kwa maandishi. Sote tunakubaliana kwamba nishati ndiyo njia kuu ya maendeleo ya nchi yoyote ile. Hata katika historia ya binadamu maendeleo yake yameambatana na ugunduzi wa nishati. Kwa hiyo, sisi tunafahamu na ndiyo maana basi katika sera pamewekwa utaratibu au mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba nishati inafikishwa kwanza katika Makao Makuu ya Wilaya lakini pia si kwa sababu tungojee mpaka Makao Makuu ya Wilaya lakini pia katika maeneo mengine kama ambavyo imekuwa ikifanyika sehemu hadi sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kufikisha nishati kwa haraka zaidi. Kama ambavyo tumesema mara nyingi hapa Bungeni ni kweli kwamba tunahitaji kuongeza kasi ya kuzalisha nishati katika maeneo mbalimbali. Ndiyo maana basi Serikali imeunda au inatarajia kuunda taasisi na mfuko maalum wa Nishati Vijijini. Pamoja na nishati hiyo kuna suala pia la nishati mbadala ambao Wabunge wengi hapa wamechangia. Nishati mbadala tunakubali kwamba ni muhimu. Imetolewa mifano michache ya *solar energy, biogas* na kadhalika. Sasa hivi ipo miradi midogo midogo mbali na majaribio na mengine ya kuendeleza nishati mbadala ambayo iko chini ya Wizara ipo katika mikoa mbalimbali na ile ambayo katika Mkoa wa Mwanza sio iko Mwanza Mjini tu lakini ipo pia katika Wilaya na Vijiji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la nishati mbadala na hasa kwenye matumizi kwa mfano ya *biogas* ambayo tumezungumza mara nyingi kwamba ni muhimu sana. Sisi katika Wizara tungependa wakati wa Bunge hili tupange kikao na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika maeneo yenye mifugo na wale ambao tunaweza tukakaa nao kuhakikisha kwamba sio tu tunapeana taarifa juu ya uendelezaji wa nishati hii lakini kutafuta tuelezane namna gani tunaweza kuiendeleza kwa kasi suala zima la nishati mbadala ikiwemo ya *biogas.*

Kuhusu ndugu zetu wa Mikoa ya Kusini ya Mtwara na Lindi suala la *Mnazibay.* Napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba kama ambavyo tumeeleza hapa mara nyingi katika hali ya kawaida tungetegemea kwamba mradi wa Songosongo ndio ungekwenda mpaka mikoa yote kwa ukamilifu wake.

Tumeeleza matatizo ambayo yametokea kwa sababu miradi hii inafadhiliwa mara nyingi na fedha kutoka kwa wafadhili, lakini tumeeleza pia kwamba imeshapatikana mwekezaji wa kuweza kuhakikisha kwamba mikoa hii ya Mtwara na Lindi inapata umeme wa uhakika.

Sasa jana hapa paliulizwa swali je, uhakika huu ukoje? Napenda nichukue nafasi hii niseme kwamba timu ya wataalamu tayari iko Dar es Salaam ya umeme wa *Mnazibay* na kwamba hawa sasa hivi wanatarajia wiki ijayo baada ya kupata kibali kutoka Maliasili watafikisha vifaa kwenye eneo husika ili kuweza kuanza kuhakiki gesi. Uhakika wa gesi ni muhimu kutokana na ukweli kwamba ugunduzi wa awali ulikuwa mwaka 1982 na ni kwamba lazima ihakikiwe upya.

Lakini kama tulivyosema awali tuna matumaini makubwa kwamba gesi hiyo itakuwepo na itatumika kwa ajili ya kuzalisha umeme na endapo patakuwa na matatizo yoyote basi sisi katika Wizara tunasema kwamba itakuwepo njia mbadala ya kutafuta fedha kwa ajili ya kufikisha umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kupitia gesi ya Songosongo na pengine ningependa kusema hapa kwamba sasa hivi Wizara tayari imeshaamua kutenga fedha kwa ajili ya kufanya *feasibility study* ya kufikisha umeme endapo umeme wa *Mnazibay* utakuwa na matatizo yoyote. *(Makofi)*

Lakini pengine Waheshimiwa Wabunge wangependa kufahamu kwamba suala la *Mnazibay* si la umeme peke yake kutokana na gesi iliyopo pale kule *Mnazibay* inatarajiwa kwamba kuendeleza chanzo kile kutasaidia pia kuanzisha viwanda vingine *Petrol and Chemical Industries* kwa eneo lile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, si suala la gesi peke yake lakini pia itakuwa ni suala la viwanda vingine. Ndiyo maana tunaona kwamba kutokana na historia ya uwekezaji hapo nyuma wafadhili kutokukubali Mradi wa gesi ya Songosongo kwa awamu hii kwenda moja kwa moja Mtwara na Lindi huu mradi ambao umepatikana utakuwa na manufaa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za gesi ya Songosongo. Napenda niliambie Bunge lako Tukufu kwamba fedha zilizobaki kwenye mradi wa Songosongo zipo isipokuwa fedha hizi si fedha zetu ni fedha za wafadhili ambao wao kama tulivyowahi kusema hapa Bungeni watakuwa tayari kuzijadili fedha hizi na matumizi mengine endapo uwekezaji huu wa *Mnazibay* hautafanikiwa.

Lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hizi fedha hazikuchukuliwa kwenda mahali popote fedha bado zipo wanazo wao wenyewe wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme wa Ruvuma kama ambavyo nimewahi kusema. Umeme wa Mkoa wa Ruvuma ni muhimu sana kwamba sasa kumepatikana uwezo wa kujenga *sub station* pale Makambako. Bila *sub station* ya Makambako hatuwezi kuzungumzia umeme wa Ruvuma.

Ni kweli kwamba pamoja na kujengwa *sub station* ile *distribution* ya umeme kwa Njombe na kadhalika. Lakini kituo kile ndicho ambacho kitatuwezesha kuchukua umeme kupeleka Kusini kwa maana ya Mkoa wa Ruvuma. Na kwa sababu Mkoa wa Ruvuma unajumuisha Wilaya muhimu ya Tunduru.

Katika maelezo hapa tumewahi kusema napenda nirejee kwamba Wilaya ya Tunduru ambayo ina umeme sasa hivi wa kutumia *generator* itaunganishwa katika umeme wa *Mnazibay* wakati ambapo mradi ule utakapotekelezwa. Kwa sababu ni karibu zaidi pale kuliko kwa kutokea Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ya ujumla naomba sasa niende kwenye maelezo au mambo mahsusi kama yalivyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa ulikuwa ni mchango wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta, Mheshimiwa Shellukindo. Napenda nichukue nafasi hii kusema kwamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati yake kwa ushauri wao na kwa mwongozo wao kwa Wizara na sisi tunasema kwamba haya yote ambayo yametolewa kama ushauri kwa Wizara tunayachukua na tutayafanyia kazi kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa pia na mchango wa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Cheyo kwenye Wizara hii. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa mchango wake, kwa maoni aliyokuwa ameyatoa napenda nimhakikishie kwamba suala la nishati mbadala nililolisema na sisi tunalitilia maanani sana na nimewahi kusema hapa mara nyingi Bungeni umuhimu wa nishati mbadala kuanzia *biogas* na nishati nyingine mbadala ambayo sisi tunazifahamu. Kwamba suala la deni la SMZ napenda niseme hivi kwamba SMZ ilikuwa na deni la *TANESCO* zaidi ya shilingi 30 bilioni.

Lakini deni hili liko katika sehemu mbili. Sehemu moja ni riba ambayo ni kubwa zaidi kuliko deni lenyewe. Deni lenyewe lilikuwa ni kama shilingi 15 bilioni na riba ni

zaidi ya shilingi 19 bilioni. Sasa kinachojadiliwa hapa namna ya kuwapunguzia mzigo ndugu zetu ni kuondokana na suala la riba ili kama ni deni libaki deni lile deni lenyewe. Sisi wenyewe kama nchi tunasaidiwa na Jumuiya ya Kimataifa katika kupunguziwa au kufutiwa madeni. Sasa sembuse ndugu zetu wa upande wa pili wa Muungano. Mimi nadhani ni ufafanuzi ambao ni muhimu ukatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *IPTL* na kadhalika Mheshimiwa Waziri atakuja kulizungumzia ambalo Mheshimiwa Cheyo amelizungumzia. Suala la Madini kwamba yanaporwa na kadhalika na kwamba hatupati tunachotakiwa tupate.

Mimi ningeomba sana sana Waheshimiwa Wabunge, tuna utaratibu tumejiwekea kwamba likitokea jambo zito kama hili kama ambavyo limetokea katika Bunge la Bajeti la mwaka jana Kiongozi wetu Bungeni Mheshimiwa Waziri Mkuu aliamua kuunda Tume kwa kuitikia wito wa Waheshimiwa Wabunge juu ya uzito wa suala hili. Ile Tume inajumuisha mmoja wetu ambayo yuko ndani humu Mheshimiwa Kabuzi. Tume ile inatarajiwa kumaliza kazi mwezi Agosti.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nina hakika atachukua nafasi kufanya uamuzi namna ya kushughulikia Tume ile lakini kwa vyovyote vile mimi naamini kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge watapata taarifa ya matokeo ya Tume ile. Sasa ningewaomba Waheshimiwa Wabunge tungesubiri kuhusu mapendekezo mahsusi ya Tume ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mchango wa Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Hamad Rashid, Mheshimiwa Waziri atakuja kushughulikia. Labda sasa niende kwenye mchango wa Mheshimiwa Kolimba. Amezungumzia umuhimu wa Chuma cha Liganga na umuhimu wa umeme Ludewa.

Kwa hiyo, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Kolimba kwamba tutajitahidi kadri tuwezavyo tuje huko Ludewa na kwenda Liganga kwenda kuona hali ilivyo. Tumekuwa na timu mbalimbali zinazokwenda na sisi tutakuja. Kuhusu Ludewa na kwamba pana *generator* na kwamba walikuwa wameomba wasaidiwe namna ya kufanya *networking*. Tutawaagiza *TANESCO* wafanye hivyo haraka iwezekanavyo ili wananchi wa Ludewa waweze nao kufaidika na *generator* ile ambayo mmenunua nyinyi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la umeme Vijijini alililolitaja Mheshimiwa Degera kwenye maeneo yake aliyoyataja. Soya nimefika tena wenyewe wanapaita Soya Ulaya Ulaya na Vijiji ambavyo amevitaja. Labda nichukue nafasi hii kumhakikishia kwamba yale maeneo ambayo yako katika mradi wa umeme yaani *Electricity Four Phase Two* ikiwemo Soya yatatekelezwa asipate *pressure* kwamba bado labda hawajakamilisha. Kazi hii inafanyika nimetembelea juzi juzi maeneo mengine ambayo ya mradi huu kazi zimeshaanza na Soya watafika. Ametutajia na Vijiji vingine vya jirani. Tumevipokea tutazama hali jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mabina baada ya kutupongeza suala la fidia ya Geita pia amezungumzia suala la Kamati ya Madini na kama nilivyosema awali tuipe nafasi ile Kamati iweze kufanya kazi yake. Suala la mipaka ya Mgodi wa Geita nimeshawahi kulizungumza hapa. Lakini labda niseme tu kwamba ni vizuri midhali Kampuni hii imeshapata leseni katika maeneo mbalimbali na ambayo yanafahamika kwa

sasa hivi basi ni vizuri tukawashawishi wananchi wetu wakaheshimu mipaka na wakatambua mipaka ya maeneo hayo.

Kuhusu Vijiji ambavyo nimevitaja mbalimbali ya kuvipatia umeme kwa kweli labda la kusema hapa ni kwamba hoja yake inaeleweka na tumevisikia tutaona hali jinsi itakavyokuwa. Mzee wangu Kahumbi kilio chako nakifahamu. Mimi siku zote ndani ya Bunge na nje nimekuwa nikikufahamisha kwamba kwa kweli kilio cha Bukene nakifahamu ingekuwa nina uwezo wa kifedha hata kesho Bukene ingepata umeme. Kwa kweli wananchi wa Bukene wanapaswa kujivunia kwamba wamekuwa na Mbunge mahiri kama wewe hapa Bungeni. Na Mwenyezi Mungu atakukumbuka kwa haya ambayo umekuwa ukiwatetea wananchi wa Bukene. Hata kama ukistaafu kesho. *(Inshallah)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mheshimiwa Mloka Wizara isitoe leseni maeneo kama ya Bwawa la Mindu. Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mloka tunaungana moja kwa moja na kauli aliyoitoa Mheshimiwa Lowassa juzi alipokwenda Morogoro kwamba hawa wavamizi wanaokwenda kwenye maeneo ya vyanzo vya maji wanavunja sheria na wanapaswa kuchukuliwa hatua mara moja. Haikubaliki hata kidogo. Kwa kweli wavamizi wale kwa mujibu wa taarifa zetu hawakupewa leseni. Lakini ikigundulika kwamba baadhi ya maafisa wetu wameshiriki katika kutoa leseni katika maeneo hayo yasiyohusika tutawachukulia hatua hawa maafisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kagonji amezungumzia pia, ndugu yangu Kagonji umuhimu wa Umeme Vijijini na mimi nimepata faraja kubwa sana kutembelea kule kwake na ameniandikia pia anasema maeneo ya nguzo mbili tatu zile ambazo za kufikisha umeme. Napenda kukuahidi Mheshimiwa Kagonji kwamba tutawaagiza *TANESCO* yale maeneo ya nguzo mbili tatu zile yafanyiwe kazi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme wa Kigoma Mheshimiwa Waziri atalizungumzia. Mheshimiwa Lydia Boma alizungumzia suala la umeme wa Nanyamba. Mimi nilidhani wiki iliyopita nilitoa kauli nzito sana kuhusu Nanyamba.

Ningemwomba Mheshimiwa Lydia Boma na Mheshimiwa Mbunge ambaye Kijiji cha Nanyamba kipo basi achukue kauli ile kwamba kwa kweli ndio mtazamo wetu kwamba kwa kweli Nanyamba wana Mbunge mahiri kwa maana ya Mheshimiwa Namkulala. Kwamba wasije wakamsulubu kwa jambo ambalo kwa kweli si lake. Amejitahidi amefikisha ushenga na Waswahili wanasema Mshenga hauwawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mheshimiwa Paul Ntwina kuna maeneo ambayo alikuwa ameyalalamikia kwamba palikuwa na nguzo ambazo zilikuwa zimewekwa tangu mwaka 2000 na mpaka sasa zilikuwa hazijafanyiwa kazi. Nataka nimfahamishe kwamba sasa hivi kazi inafanyika na *Regional Manager* wa Mbeya yupo hapa amekuja na kazi sasa hivi inafanyika.

Mheshimiwa Iwvatta pia amezungumzia maeneo yake yanaeleweka. Kule kwa Mheshimiwa Iwvatta sasa hivi kuna wataalamu kutoka Ujerumani wanafanya *feasibility study* kwa ajili ya kutazama namna gani tunaweza kufikishiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala alilolitaja la umeme wa Songea Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, nimelizungumzia ni muhimu kwamba hatua ya awali imefikiwa. Lakini napenda niongeze kwamba wakati tukingojea hatua hiyo ya kudumu basi kama ilivyokuwa Mtwara, Kigoma pamoja na Ruvuma pia watapelekewa *generators* mpya ili waweze kumudu mahitaji yao ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamekuwa na mchango wa Mheshimiwa Abdulaziz ambao nimeuzungumza kuhusu *Mnazibay* na Songosongo. Mheshimiwa Abdulkarim Shah amelalamika sana ndugu yangu yule kuhusu Mafia. Nitatafuta muda tufike Mafia. Lakini pia tutazungumza na *TANESCO* tuhakikishe kwamba hii roho moja iliyopo pale isije ikakatika kesho ya mashine kwamba tuhakikishe kwamba Mafia wanaendelea kuwa na umeme wa uhakika.

Kuhusu maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Shango kama *Net Group* walisitishwa au *TANESCO* imekatazwa kufanya *Rural Electrification.* Napenda kusema ndugu zangu pamoja na matatizo yote *TANESCO* wanafanya kazi kubwa sana nchini ya kufikisha umeme Vijijini ndio tunawategemea hivi sasa. Tatizo lililotokea hapa katikati au linalotokea wakati hadi wakati ni suala zima la kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kutimiza miradi fulani. Lakini wanafanya kazi kubwa na hawajasitishwa wasifanye kazi hiyo.

Kwamba giza haliongezi idadi ya watu. Tunaelewa umuhimu wa umeme hata mwaka jana wakati nimekwenda kwa Mheshimiwa Magufuli huko Biharamulo na kwake suala hili waliniuliza hivyo hivyo na mimi nikasema ni kweli kwamba pengine tutamsaidia Waziri anayehusika na idadi ya watu kwa maana ya mpango wa uzazi kwa kuhakikisha kwamba panapatikana nishati ili watu wapate na vitu vingine vya kufanya. Kwa sababu pale kwa watani zangu Wasukuma ikifika saa moja wako ndani, kwa hiyo hakuna kazi nyingine matokeo yake wanakuwa ni wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Alhaji Mpeme nimeeleza kuhusu umeme wa Mtwara na Lindi. Mheshimiwa Buzuka amezungumzia Vijiji vyake. Mheshimiwa Parseko Kone Mheshimiwa Waziri atazungumzia na kuhusu Mheshimiwa Mwananzila umeme unaokatika katika. Tumeshawaagiza *TANESCO* wawasiliane na Zambia kwamba suala hili litafutiwe ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yako mengine ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Simpasa na wengineo. Mheshimiwa Waziri atayapatia muda ya kuyapitia. Baada ya kusema yote haya napenda nirejee kwamba Waheshimiwa Wabunge naomba muwe na imani na uongozi wa Wizara chini ya Mheshimiwa Yona.

Sisi kwa kweli tumefarijika sana na *debate* ya humu ndani naamini itatusaidia pia katika utendaji wetu wa kazi. Napenda nimalizie kwa kusema. Watani zangu wale Wasukuma wana usemi wanaosema: *"Uya Akamolaga Maswa Atabulagagwa".* Maana yake ni kwamba aombae amani auwawi ndugu zangu. *(Makofi)*

Kama mwaka jana nilivyosema wakati nazungumza na Mheshimiwa namtaja Mheshimiwa Kahumbi na leo nazidi kumwomba yeye na wengine wote, Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba kwa kweli tatizo ni la uwezo. Tatizo ni la kinchi lakini tuna nia

na ari ya kufanya kazi kuhakikisha kwamba tunatimiza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kama ilivyonadiwa mwaka 2000. Kwa kiasi kikubwa kazi hiyo imefanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba nimkumbushe tena Mheshimiwa Kahumbi Mzee wangu kwamba *"Ulinduguwane, zunyagaishire"*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana mkono na Mheshimiwa Naibu Waziri kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia katika hotuba yetu ya bajeti mwaka huu. Ni wengi, wachache walichangia kwa kuzungumza kama 33, waliochangia kwa maandishi ni 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwataje na kuwashukuru wote ambao wamechangia katika hotuba hii. Kwanza ni Mheshimiwa Naibu Waziri, Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Thomas Nyimbo, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Lydia Boma na Mheshimiwa Paul Ntwina. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Abdulaziz, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Jacob Buzuka, Mheshimiwa Parseco Kone, Mheshimiwa Alhaji Ahmadi Mpeme, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi na Mheshimiwa Lekule Laizer. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Phillip Marmo, Mheshimiwa Alhaji Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa William Kussila, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Jacob Buzuka, Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Hamis Nguli, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga, Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Samuel Chitalilo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Mheshimiwa

Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Gideon Cheyo na Mheshimiwa Dr. Abdulkader Shareef. *(Makofi)*

Vile vile, Mheshimiwa Dr. Peter Slaa, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Robert K. Mashala, Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Margareth Bwana, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Philip Magani na Mheshimiwa Khalid Suru. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa wote ambao wamechangia katika hotuba hii. Kama mnavyoona ni wengi na naahidi kwamba mawazo yao, maombi yao na ushauri wao wote tumeuchukua na tutaushughulikia na tutawajibu mmoja mmoja kama kawaida yetu ili waelewe ni kitu gani tunafanya katika kutekeleza yale ambayo yanawakera.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Naibu Waziri kuhusiana na yote aliyosema kuhusu uendeshaji wa Wizara yetu. Sitaongeza zaidi ya hapa. Lakini nizungumzie Sekta ya Nishati kwa ujumla haya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni asilimia 12 tu ya Watanzania wana umeme wa uhakika hapa Tanzania. Sisi hapa tunawawakilisha Watanzania wote, kwa hiyo, karibu asilimia 90 ya Watanzania hawana umeme wa uhakika, ndiyo maana hata michango hii, kero hizi zinatugusa sisi sote hapa. Siyo ninyi tu Waheshimiwa Wabunge, hata sisi tuliokaa hapa mbele mnaotuita Serikali zinatugusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe Tarafa ninayotoka nimekuwa natafuta umeme kwenye Tarafa hiyo kwa miaka yote tangu nikiwa Waziri wa Nishati hapa, lakini kwa sababu *TANESCO* haina uwezo wa kutosha, imenibidi nivumilie ningoje mpaka hapo tutakapopata fedha za kuweza kufikisha umeme katika Tarafa ninakozaliwa. Kwa hiyo, siyo ninyi tu Waheshimiwa na siyo kwamba kuna upendeleo kama wengine walivyokuwa wakisema labda kuna Mikoa inapendelewa, hakuna upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya umeme inaletwaje hapa nchini na umeme tunauzalishaje, kwa kifupi tu ni kwamba, ni fedha zetu wenyewe za kodi zetu ambazo ni kidogo sana, zinaletwa hapa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndiye anayegawanya na mnaona kila Wizara imepewa kiasi gani. Kwa hiyo, hizo fedha za ndani tunazopewa sisi kwa shughuli za nishati hapa nchini ni kidogo sana. Tunategemea fedha za wafadhili na mikopo.

Fedha za wafadhili tunapewa wakipenda na inachukua muda kweli kuzungumza nao ama sivyo tutafute za mikopo na za mikopo unapewa kwa masharti. Kama

mlivyosikia, fedha zilizobaki kwenye mradi wa Songo Songo bilioni 70, mradi wa Songo Songo tuliupata kwa bei nafuu, lile bomba wanajenga Wahindi. Zilibaki fedha kwenye mkopo ule tukawaambia: "Basi tuzitumie kupeleka umeme Lindi na Mtwara." Wanasema: "Mradi wenu umekamilika ni lazima tuanze upya, kuwe na feasibility study mpya ndipo tutaona kama mnatimiza masharti hayo." Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kwamba, kama hakuna mwekezaji binafsi basi tutafikiria na ni lazima twende tubembelezane nao wakati wote. Ndugu zanguni hatukukaa tu, tunafanya kazi na tunadhalilishwa wakati mwingine! Ni kweli, maana you go there cap in hand unaomba Ubalozi wa Sweden au Ubalozi mwingine. Tunawashukuru wametupatia fedha, lakini inachukua muda mrefu sana na ndiyo maana mnaona kama kwamba tunachelewa. Siyo hivyo, ni kwamba hatuna uwezo wa kutosha, Miradi ya Nishati ni pesa nyingi sana na hatuiwezi sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ile rare aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, *Rural Energy Fund, Rural Energy Agency* tunakamilisha taratibu zake tulete hapa hiyo sheria ipitishwe ili tuweze kutumia vyombo hivyo viwili kwenda kutafuta fedha. Kwanza mtupatie fedha kama mnavyotoa za barabara, *road toll.* Bajeti ijayo mkitaka, muamue kwamba Shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta au Shilingi 5 kwa kila *unit* ya umeme au kwenye gas mtupatie. Mkiamua ninyi Waheshimiwa Wabunge hapa ikiwa sheria, mkimruhusu Waziri wa Fedha zitakusanywa fedha hizo tutazipeleka kwenye *Rural Energy Fund* ili tuweze kufikisha umeme vijijini kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ama sivyo tunategemea mikopo, ndiyo kama hiyo ya Mchuchuma. Niongezee kidogo kwamba, mwekezaji wa Mchuchuma siyo kwamba tumepunguza miguu sisi, tulikuwa tunazungumza naye kila wakati. Anasema: "U-sign hapa kwamba umeme wote utakaozalishwa Mchuchuma utaulipia." Ndivyo ilivyo *IPTL* ndugu zanguni. *IPTL* tulifanya hivyo kwa sababu kulikuwa na shida ya ukame. *IPTL* sasa hivi inatusaidia, lakini ni ghali sana. Mkitaka tunaweza ku-sign mkataba wa Mchuchuma tukawaambia: "Zalisheni 400." Wao ni wawekezaji, ukishawa-*guarantee* kwamba watapata fedha yao kila mwezi *capacity charge* basi watakuwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *IPTL* ilivyo, unatumia umeme, hutumii umeme utalipia kila mwezi, ndiyo maana tukawaambia tufanye basi kwa hatua, wakasema: "Tukifanya kwa hatua labda *megawatts 200,* 200 hauna faida, siyo *economically viable."* Wale ni wawekezaji, pesa za shareholders wao. Tumewaambia: "Haya wekeni." Sasa wanasema watajenga mradi wa megawatt 400 ambao wenyewe watatafuta soko, *TANESCO* itanunua kama mteja mmojawapo pamoja na Migodi ya Madini Kenya na kadhalika. Tumewapa barua tukawaambia: "Nendeni mkatafute soko nje na ndani ya nchi, mkipata njooni tujenge mradi." Ndipo tulipofika hapo.

Tunawangojea waje sasa tu-sign mikataba na kuhakikisha kwamba hatutumbukizi Taifa hili kwenye matatizo mnayozungumza ya *IPTL.* Tumekuwa waangalifu ndugu zanguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba nigusie *IPTL* tu hapo. *IPTL* sasa hivi Serikali yetu na Serikali ya Malaysia na wale wabia wawili wa *IPTL* Mtanzania mmoja VIP Engineering na *MECMA* ya Malaysia, *TANESCO* na Mabenki ambayo yanataka kununua mradi wa *IPTL* tunazungumza pamoja tuone ni namna gani

tutaweza kuboresha mzigo ambao tunaulipia sasa hivi wa *IPTL*. *World Bank* tunazungumza nao vile vile ikiwa watu wanaweza kutupatia fedha zenye interest rate nafuu ili tuweze kuununua mradi huo wa *IPTL*. Tukiununua bei zitashuka, tusipoununua akichukua tu mwekezaji mwingine mzigo umeutoa hapa ukauweka hapa, bado mzigo utakuwa pale. Mazungumzo haya ndugu zanguni yanachukua muda, lakini Serikali nzima tunashughulika katika kutafuta ufafanuzi na utafiti za tatizo la *IPTL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya Mererani. Mererani ni mahali ambapo wachimbaji wadogo ni wengi sana, tunaamini kwamba tanzanite nyingi inachimbwa na wachimbaji wadogo, lakini wapo wakubwa siyo wadogo tu. Kuna Kampuni ya *AFGEM,* kuna Kampuni ya *Tanzanite Africa* ya Bwana Mengi ambaye ni Mtanzania na kuna Kampuni za Watanzania wengine, siyo kubwa sana kama ya Mengi na *AFGEM,* lakini wachimbaji wadogo wadogo ndiyo wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali popote penye uchimbaji wa madini kunakuwa na matatizo. Mfano ukifika Mwadui au mahali popote penye mali panakuwa na wadokozi dokozi, wezi, magomvi kadhalika. Tunayo orodha hapa ya magomvi yanayotokea Mererani kwa wachimbaji wadodo kwa wadogo. Mfano anachimba kufuata ule mkondo wa tanzanite, akifika huko anaingia kwenye kitalu cha mwenzake, lakini wana namna zao za kusuluhisha na mara nyingi Wizara tumeitwa kwenda kusaidia kusuluhisha magomvi kati ya Mswahili na Mswahili, mweusi na mweusi, mweupe na mweusi, mkubwa na mdogo. Tunayo orodha hapa ya matatizo yote ambayo tumeyatatua kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ripoti ya Ndugu Mboma na ripoti zingine na ushauri wenu ninyi Waheshimiwa Wabunge hapa kwa miaka hiyo iliyopita, tumeunda Kamati ya Kusimamia Shughuli za Mererani ina Mwenyekiti wake ambaye ni *DC* na inawahusisha Wajumbe wengi kutoka sehemu ile, wadau wenyewe. Sasa hivi kuna vitambulisho pale Mererani, mtu asiingie hivi hivi tu, maana palikuwa mahali pa holela, ni lazima uwe na kitambulisho.

Pia, kila mwenye mgodi awe na vifaa vya usalama, awe na orodha ya wafanyakazi wake ili wajulikane. Kulikuwa na uhuni, wizi na unyang'anyi wa hali ya juu kabisa. Sasa hivi tumejenga Kituo cha Polisi, tunajenga uzio ile sehemu yote *(controlled area).* Kama nilivyosema, kuna Kamati hiyo ambayo inasimamia migogoro yote ya pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro imetokea kati ya wachimbaji wa aina zote, kama ninavyosema, siyo kwamba ni Wazungu tu wanawaonea weusi. Tunazo kesi hapa ambapo mweusi amemuonea mweusi. Bwana Mengi tayari Kampuni yake imeshalalamikiwa na wachimbaji wadogo kwamba anawaonea, tumekwenda tumesuluhisha. Kwa hiyo, migogoro ya aina hiyo itatokea wakati wote. Tunaendelea kuwafundisha watu wetu, kuwaelimisha, kuwashauri wawe katika makundi ambayo yanaeleweka ili waweze kutatua matatizo yao kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wazungu kwamba wananyanyasa Waafrika, niseme wale Wazungu pale ndiyo ambao ni *organized,* ni Kampuni, wana vifaa na kadhalika. Ni kweli wameingiliwa mara nyingi, hawakwenda majumbani mwa watu huko vijijini wakampiga mtu risasi. Ni mtu ambaye alifikiriwa anaiba au anataka

kuchimba mahali ambapo siyo kwake, wanalinda mali yao. Sisemi wamefanya vizuri wakati wote.

Waheshimiwa Wabunge, nataka kuwahakikishieni kwamba, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ambapo kwa kweli wakati mwingine tunalaumiwa sisi Wizara ya Nishati na Madini, nadhani mengine ni ya usalama. Vyombo vyetu vya Usalama wenzetu wanatusaidia na wanayafanyia kazi. Tumetoa leseni mtu akachimbue madini mahali, leo anaibiwa pale, kwa nini sisi tunaambiwa yule mtu kapigwa risasi au yule mwizi kavunjwa mguu au vipi! Ni Polisi na Vyombo vya Usalama na wanafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo *list* hapa inayoonyesha baadhi ya matukio na nitaisoma kwa ufupi tu. Mwaka 2003 Bwana *Chris Delpot; M-South Africa* ni mtuhumiwa, muathirika alikuwa Emmanuel Martin kajeruhiwa. Hapa Mzungu kamjeruhi Mswahili. Ilikuwa attempted murder na kesi hiyo iko mahakamani, huyo bwana ametolewa kwa dhamana. Hiyo ni kesi ya kwanza hiyo, hatua chache tu tarehe 14/11/2003 *Collin Martin; M-South Africa* alimuua Bwana Neil Stephan, nadhani huyu ni Mswahili. *A murder,* alimuua na kesi hiyo iko mahakamani na huyo Mzungu yuko rumande. *Nobody is above the law,* wanatiwa rumande, wanapelekwa mahakamani na hakuna ambaye anaachiwa, Polisi wetu wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 30/06 Joseph Kimble; *M-South Africa* alimjeruhi Bwana Emmanuel Urassa, kesi iko mahakamani, mtuhumiwa yuko rumande. Tarehe 04/01/2004 huyu hajapatikana, lakini alimuumiza Bwana Edward Edson, shauri bado liko Polisi. Halafu kesi nyingine ni ya Said Ali Kilango, yeye alimuua Said Mohamed, hao ni Mswahili kwa Mswahihi, kesi iko Mahakamani na mtuhumiwa yuko rumande. Mfano wa mwisho ni nyakati mbalimbali wachimbaji wa *AFGEM* wanaingiliana na kusumbuana, lakini Polisi wakati wote wapo na wale *AFGEM* wana walinzi wao, wale wachimbaji wadogo kila mtu anatumia ulinzi wake, mwingine mkuki, mwingine rungu, mwingine magongo kutegemeana na uwezo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninataka kusema kwamba tuna Polisi ambao ni Wizara ya Mambo ya Ndani, Vyombo vyetu ya Usalama na sisi Wizara tunahakikisha kuwa migogoro hii inapungua na ndiyo maana ile Kamati ya Dr. Kipokola kazi yake mojawapo ni hiyo ya kuangalia ni namna gani tunaweza kupunguza migongano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kone, tunajaribu sana kupunguza matatizo yaliyopo huku, nadhani tuone Kamati ya Ndugu Kipokola itatuambia nini zaidi ya hayo ambayo tumeyafanya mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie lingine la jumla kuhusu hali ya mafuta hapa nchini. Labda mmesoma magazeti yakisema kwamba kutakuwa na *shortage* ya mafuta na nini. Sababu yake ni kwamba, tumeona ili kulinda mapato ya Serikali, Sekta ya Mafuta ndiyo Sekta ambayo inatoa mchango mkubwa sana katika Pato la Taifa. Kuna Makampuni ya Mafuta hapa nchini yanalipa Shilingi bilioni 5, bilioni 6 au bilioni 7 kwa mwezi, Kampuni moja. Kwa mwaka *you are talking out 60 or 70, billion shillings,* lakini bado kuna wizi mkubwa au upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Kwa hiyo, tumeona tuweke *flow meters* kule mafuta yanapoingilia, mafuta yote yapitie kwenye mita ili tujue ni kiasi gani mtu ameleta asitubabaishe tena baada ya hapo na hiyo tunataka kuanzia na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ilitolewa kwa waagizaji wa mafuta wote kwamba, tafadhali tarehe fulani tunafunga *flow meter.* Tumewapa muda wa kutosha, ile *KOJ,* pale mafuta yanapoletwa, itafungwa ili tufunge hiyo mita, yaani meli hazitaweza kupakua mafuta yao. Kwa hiyo, walikuwa na muda wa kutosha. Sasa kazi hiyo hatuwezi kuchelewa kwa sababu tunazidi kupoteza mapato na mkandarasi yuko tayari, kwa hiyo tumemwambia aanze kazi baada ya kuhakiki *stocks* za mafuta hapa nchini. Tumewaambia wenyewe wenye mafuta kila mmoja atuambie ana kiasi gani cha mafuta ya *diesel, petrol* na kadhalika. Tunazo *figures* zao kutoka kwao wenyewe, tena wengine hawakutupatia, tunaamini hiyo itakuwa ni ziada, lakini *stock* iliyopo inatosha kwa siku kama 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kazi ya kufunga hiyo flow meter itachukua wiki moja tu tunavyoambiwa na mkandarasi. Kwa hiyo, kama kutatokea tatizo hasa bei zikipanda kwa kweli hawa wafanyabiashara tutawachukulia hatua kali sana kwa sababu itakuwa ni kuhujumu uchumi wetu. Hakuna sababu ya bei za mafuta kupanda kwa sababu hiyo, hawana sababu maana *stocks* zipo. Tunawashauri Wananchi wawe waangalifu katika kutumia mafuta, lakini wasi-*panic* na wakaanza kulundika mafuta au kuhodhi mafuta majumbani mwao. Niliona nielezee hilo, mtayaona kwenye magazeti tumetoa taarifa kwa kirefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa na mimi nijaribu kugusia hoja chache ambazo zilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Hatutazimaliza zote kama nilivyosema, lakini naomba nianze na hoja ya Mheshimiwa Shellukindo.

Hoja za Mheshimiwa Shellukindo na Mheshimiwa Naibu Waziri amezizungumzia na tumesikia ushauri uliotupatia, ni Mwenyekiti wa Kamati yetu. Kwa hiyo, nadhani tumesikiliza mawazo yenu na ushauri wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Isaac Cheyo aliuliza na alisema Serikali ya Tanzania ni nchi pekee ulimwenguni ambayo madini yanachimbwa na Makampuni ya nje bila kuwa na share za aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hilo siyo kweli, kwa sababu Serikali nyingi hazina *shares* kwa mfano Nigeria, Afrika Kusini na Mali hawana *shares* kwenye Makampuni. Hata hivyo, ni kati ya masuala yanayofanyiwa kazi na hiyo Kamati ya Kipokola. Tumemwambia aangalie kwamba; je, *shareholding* au umiliki wa hii migodi uweje? Serikali tulikuwa na *share*, hata Mwadui tuna share 25. Tulikuwa na *shares* Nzega, tulikuwa na shares Kahama, lakini kwa sababu za kifedha kabisa za kiutaalam tulishindwa kuendelea kushikilia *shares* zetu kwa sababu wakati ukifika wa kupanua mgodi unaambiwa: “Changia Dola zako milioni 30.” Hatuna! Sasa yeye anaendelea na kazi ni lazima aifanye. Kwa hiyo, wanaku-*dilute* wanaita, maana ataweka za kwake wewe sasa unapunguzwa weeee mpaka unakwisha. Mwisho wake tukaona kwamba kwa kweli tungojee sisi tupate kodi zetu, tupate mrahaba wetu, tupate maslahi yale yote ambayo yamo katika mikataba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TANSORT,* Mheshimiwa Isaac Cheyo, alizungumzia kwamba *TANSORT* iwe na Mchambuzi Mkuu wa Almasi yote itokayo Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi mtaona kwenye hotuba yetu kwamba *TANSORT* tuliiundia Kamati ya Serikali mwaka 2000/2001 na tumepeleka wakaguzi. *Accountant General* ameenda kule na Mkaguzi wetu katika Wizara yangu ameenda kule kuangalia. *TANSORT* tumeirudisha sasa Serikalini kama tulivyosema kwenye hotuba yetu, itakuwa ni Chombo cha Serikali na bajeti yake itatengenezwa kama ilivyotengenezwa mwaka huu na Serikali na fedha zote zitakazopatikana kwa kazi ya kuchambua almasi zitaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Waziri wa Fedha ili zisaidie kujenga Taifa letu. Kwa hiyo, chombo hicho kimebadilishwa kabisa sasa kiko chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Njelu Kasaka aliuliza kuhusu mradi wa *Gaga Mining Company.* Tulipata mfadhili katika mradi huu akatupatia fedha tukajenga mashine kule Matunda. Ni mashine ambayo kwa kweli tulitegemea itatumika kufundisha wachimbaji wadogo wadogo na watakodisha pale wanakwenda wanafanya kazi, tukipata fedha tunaongeza miradi ya namna hiyo. Bado nia yetu ni hiyo hiyo. Walipofika kulikuwa na tatizo, hata mimi kuna wakati nilipofika nilikuta tatizo lipo, lakini limerekeshishwa sasa hivi na mradi naambiwa unafanya kazi

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba Sekta binafsi isafirishe miamba na mmiliki pia anunue akipata faida, eneo la kuhudumiwa ni kubwa zaidi ya kilometa 20. Pia, kuhusu namna ya kufikisha miamba kwenye mitambo, hilo tunaliangalia na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Njelu Kasaka aliuliza vile vile vyombo vingapi vinaweza kukodishwa na ada zake. Tumetoa hapa, lakini kwa sababu ni tarakimu nyingi naomba nimpatie Mheshimiwa au pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao watataka nitawapatia maelezo hayo kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mheshimiwa Njelu Kasaka aliuliza ni kwa nini Serikali iliuza hisa zake za asilimia 5 katika Mgodi wa Kahama? Kama nilivyoeleza, tulishindwa kuendelea kwa sababu hatukuwa na uwezo wa kuchangia katika kupanua ule mgodi. Tuliuza hisa zetu asilimia 5 tukapata Dola milioni 5 na tukapatana kwenye ule mkataba kwamba kila mwaka watatupatia 100 million dollars kwa kufundishia Watanzania mambo ya madini na kuboresha Institutions zetu ambazo zinahusiana, hizo fedha tunazipata kila mwaka. Tunapata fedha hizo kutoka kwenye mgodi ule, mwaka zikichelewa zinaenda mwaka wa pili tunazikusanya pamoja, lakini hazipotei.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nafika kwenye hoja za Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ambaye aliuliza kuhusu jedwali namba 8 kwamba ni nchi gani inafaidika zaidi katika kugawanyishwa. Jedwali namba 8 kwenye hotuba yangu linaonyesha *comparison,* ulinganisho wa *incentives* au *package* au vivutio kila nchi inavyotoa. Ni nchi nyingi tu pale za Afrika, za Latin America na Asia, vitutio vinavyotolewa ili kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji ni wale wale, Latin America, Asia na hapa. *They are the same people, you have to attract them.* Ukimshindwa hapa, akiona hapa hapafai anaenda Latin America au anaenda kwingine.

Kwa hiyo, vivutio vyetu tulifanya bidii sana vifananefanane ambavyo ni mrahaba, kodi*, customs duties,* sijui *exemptions* ya muda gani. Mkitazama lile jedwali namba 8 mtaona tumelinganisha pale na naomba mkiisoma mtazame *in totality,* usitazame mrahaba tu. Utakuta mrahaba wetu ni 5, lakini wengine wana 0 na wengine wana 3.

Kwa hiyo, utazame *package* nzima na utaona kwamba inafanana fanana na nchi nyingine. Ndiyo maana tumeweza kuwavutia wawekezaji kuja Tanzania na sasa hivi wanawekeza katika sehemu mbalimbali za madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu suala la Kigoma. Tuna fedha tumeahidiwa na Serikali ya Sweden, tumepata fedha za kufanyia upembuzi yakinifu *(feasibility study).* Narudia tena, miradi mikubwa ni lazima ifanyiwe *feasibility study. Feasibility study* moja *you are talking of half a million to a million dollars.* Ni lazima uifanye hiyo, hakuna atakayekupa fedha yake awe ni *World Bank* ni Mswidi au ni nani bila hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ninavyosema tumepata fedha kutoka Serikali ya Sweden kufanya *feasibility study* ya kutoa umeme wa gridi ufike Kigoma. Tukishafanya *feasibility study* sasa inakuwa rahisi kupatiwa fedha hata za mkopo za *World Bank.* Ndiyo maana hata kutoka Makambako kwenda Songea ni *feasibility study* vile vile, bila hiyo *World Bank* hawawezi kuja na bila hiyo hata Sweden ambao wako tayari kutupa umeme wa vijijini Mkoani Songea katika zile Wilaya za Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Sweden wamesema: “Bila kuunganisha umeme wa gridi kutoka Makambako mpaka Songea Mjini hatuwezi kuwapa fedha za kusambaza umeme huko vijijini.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunafanya hatua kwa hatua na Kigoma nawaahidi kwamba hiyo *feasibility study* itaanza, ikimalizika sasa tutatafuta fedha za kuweza kujenga mradi huo. Lakini kwa wakati huu tunapeleka jenereta, *TANESCO* wako hapa wameagiza jenereta zingine mbili ili ziende kule zikaongeze nguvu pawe na umeme kidogo wa kuaminika kama tulivyofanya Mtwara na tutakavyofanya Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda uliobaki naomba nijaribu kugusia mambo machache ambayo yalizungumziwa na baadhi ya Waheshimiwa. Mheshimiwa Mrope tumeanza kazi. Sasa kama utanishtaki kwa Mheshimiwa Simpasa nadhani unanionea.

Kwa kweli azma ilikuwepo, lakini tukaingiwa na ukame siyo wewe tu ambaye miradi iliahirishwa, hata kufunga umeme *TANESCO* wameshindwa kufunga umeme sehemu ambazo walikuwa wameahidi, lakini katika Vijiji vyako tumeanza na leo nimezungumza na Mameneja wetu kule wanasema kazi inaendelea. Tafadhali tuamini na tukubalie kwamba tuendelee hivyo hivyo kwa uwezo uliopo tukufikishie umeme kwenye Vijiji vyako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mbunge wa Morogoro Kaskazini, alizungumzia kuhusu mafuta. Nadhani nimejibu kwamba mafuta yapo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu *TIPPER,* tulifikia wakati ambapo ilikuwa inatuingiza gharama ya Dola milioni 15 mpaka 20 kila mwaka kuiendesha. *TIPPER* ni mali yetu sisi na wale Waitalia. Lilikuwa ni *technology* la zamani, limechoka na lilikuwa linaingiza hasara. Mkisema mnataja Kenya, hata la Kenya ni hivyo hivyo. Nimo

kwenye nishati, nazungumza na wenzangu wa Kenya, Kenya nao lile wanafanya kulikongoja tu, lakini ni hasara kubwa sana, linawapa hasara kubwa sana.

Kwa hiyo, tukaona tusipoteze pesa milioni 20 kila mwaka kuliweka pale, tununue mafuta ambayo yapo, lakini tunatafuta mwekezaji. Kama kuna mheshimiwa Mbunge anafahamu mwekezaji yeyote ambaye anataka kuja kufungua refinery hapa tutamkaribisha. Tutazungumza naye na *TIPPER* bado iko pale na kuna *spare parts* ambazo zinaweza kutumika. Hatumkatazi mtu yeyote, ila kwa kweli kulirudisha jinsi lilivyo hatuwezi na kuliweka la kwetu wenyewe jipya ni fedha nyingi sana hatutaweza kulimudu.

Ndugu zangu wa Kusini, nadhani wamehakikishiwa. Narudia tu kwamba tuna kila nia na azma na mikakati ipo na *feasibility study* ya pili ndiyo hiyo sasa ya Somanga - Funga ya kupeleka umeme kule. Tutakuwa sasa na mkanda wa suruali na hizi za hivi. Mkanda ni ya Tumas ile ya *Mnazi Bay* na hizi za hivi ni huo wa Somanga - Funga. Kwa hiyo, yote miwili ndugu zanguni hatutaweza kushindwa, mmoja kama hautakamilika mwingine utakamilika na tutahakikisha kwamba umeme unawafikia na ninyi watu wa Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimegusia yale ambayo ni ya jumla na tukitoka hapa tutawaletea majibu wale wote ambao hawajapata maelezo ya kutosha. Muda haukunitosha kumtaja kila mmoja, lakini naomba mtupatie bajeti yetu ili tuweze kufanya kazi na mtupatie fedha za bajeti ijayo. Naomba hivyo mtupatie fedha nyingi kwenye allocation ili tuweze kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye madini tungoje ripoti ya Mheshimiwa Kipokola, inagusa mambo yote na itatusaidia kuendelea mbele na kuiboresha vizuri Sekta yetu ya Madini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kifungu 1001 - *Administration and General*..Tshs. 2,002,163,700/=

**MBUNGE FULANI:** Aya ya! ya! ya!

**MWENYEKITI:** Haya sasa Waheshimiwa Wabunge msubiri hapo hapo tuwaandike majina wote. Tugawane kazi mwingine aandike huku mwingine huku. Mheshimiwa Gwassa Sebabili unaweza kukaa, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura kaa, Mheshimiwa Ruth Msafiri unaweza kukaa.

**MBUNGE FULANI:** Huku?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huku wanaandika wengine msiwe na wasiwasi kila kitu kinakwenda vizuri. Mheshimiwa Beatus Magayane kaa, Mheshimiwa Eliachim Simpasa kaa, Mheshimiwa, Edson Halinga, Mheshimiwa Mporogomyi, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Lydia Boma mnaweza kukaa. Huku tayari wote? *Okay.* Haya tunaanza huku. Naomba niwakumbushe ni dakika tano na utake ufafanuzi.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kulingana na haya yafuatayo; kifungu 1001. Mwaka jana wakati kama huu Mheshimiwa Waziri, katika hotuba yake kifungu cha 7 aliweza kuonyesha kwamba ametenga shilingi bilioni 4 kwa ajili ya umeme wa Ngara.

Lakini katika kitabu cha maendeleo cha nne akaonyesha shilingi milioni 300. Mategemeo ya wananchi wa Ngara ilikuwa ni kwamba umeme huu ambao ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ungeweza kwenda mpaka Lulenge. Wakati huo tarehe 9/6 Makamu wa Rais, alikuja kuzindua mradi ule, malalamiko ya wananchi wa Ngara ilikuwa ni kwamba umeme huo uende mpaka Lulenge.

Wizara ya Nishati na Madini ilishapata taarifa ambayo ni ya uongo sijui kutoka wapi kwamba wananchi wa Ngara walikuwa wamekataa kuruhusu umeme upite katika mashamba yao wakitaka fidia kitu ambacho haki hakipo na sasa hivi nasema nao wananchi wa Ngara wanasikia, si kweli. Kwanza njia yenyewe haina mazao yoyote kwenda Lulenge. Wakasema kwamba ilikuwa ni karibu kilometa 90 kutoka mahali ambapo umeme huo ungeanzia kama tawi Kijiji cha Mrugalama kwenda mpaka Lulenge. Nasema ni kilomita 24 tu. Sasa ninaomba nipate majibu kwa nini umeme hauwezi kwenda Lulenge? Sehemu ya kilometa 24 zinahitajika nguzo 22 peke yake. Vinginevyo ninaahidi kwamba nitashika shilingi moja kutoka kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ili kila mmoja apate nafasi tufanye *brief to the point* ili ipate kujibiwa, kila mmoja wetu apate nafasi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Gwassa Sebabili kwa jinsi anavyofuatilia shughuli za umeme katika jimbo lake. Ni kweli nimefika kule mimi wakati Mheshimiwa Makamu wa Rais, alipokuwa kule juzi juzi wakati wa kufungua mtambo wa umeme pale Ngara. Suala la kupeleka umeme Lulenge lililetwa, tuliambiwa kwenye risala na mimi ahadi yangu ni ile ile kwamba tunajaribu kila tuwezelo tupate fedha ili tufikishe umeme Lulenge. Mheshimiwa Gwassa Sebabili na wananchi wa Lulenge naomba mvute subira tukipata fedha hizo tutafikisha umeme katika sehemu hiyo ambayo haijapata umeme. Lakini tumefika Ngara kuonyesha kwamba kwa kweli tuna nia na tunasogea pole pole tufike huko ambapo bado hawajapata umeme. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri naomba afute taarifa yake aliyoitoa kwa Makamu wa Rais kwamba umeme wa kwenda Ngara ungetokea Kigoma. Naomba afute hiyo kwa sababu kwa

wakati huu ma-*engineer* na mafundi wote wako kule. Ikiwa watakuwa wameondoka kule kwa kusimika nguzo 22 tu kwa kilometa 24 nafasi inayohitaji transformer mbili peke yake itakuwa ni vigumu watu hawa kuwarudisha. Shilingi bilioni 4 zingeweza kutosheleza. Aniambie hizo shilingi bilioni 4 zimekwenda wapi wakati ambapo kila kitu kingeweza kikafanyika kama kilivyokuwa kimepangwa? Kwa sababu zilikuwa zimepangwa *kilovolt 33* zikapunguzwa zikafika ki-*lovolt 11.* Nafikiri kuna hujuma hapa naomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri aone kwamba wananchi wa Ngara hawakubaliana na mawazo anayotoa hapa mpaka aahidi kwamba umeme kwa kweli utakwenda kule kabla ya walioko kwenye *site* hawajaondoka kurudi Dar es Salaam. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sikumbuki kusema hayo anayosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba umeme utatoka Kigoma kama yapo kwenye hotuba basi kwa kweli ni *typing error,* au ni kama ni magazeti mimi sikusema maneno hayo. Lakini narudia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nia yetu ni kufikisha umeme Lulenge ambako haujafika na sasa hivi tunakamilisha pale Makao Makuu ya Wilaya Ngara atupe muda ili tupate fedha tuufikishe umeme sehemu ambazo hazijafikishwa katika Wilaya/jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nitakuwa nachukua wawili huku, wawili huku.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mshahara wa Waziri. Kifungu 1001 mwaka 2002, Naibu Waziri alikwenda Mbinga alitoa ahadi kwa viongozi kwamba kwa kuwa *TANESCO* ilifanya *wiring* angeleta jenereta ili iweze kukidhi mahitaji ya umeme kwa muda mfupi wakati tunasubiri kupata ufumbuzi wa muda. Nilipomwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, alikataa kwamba hakusema. Sasa ningependa aseme hapa kwamba hakusema ili wamsikie wale aliowaambia. *(Makofi/Kicheko)*

La pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitembelea Mbinga wananchi walimweleza matatizo ya umeme katika Wilaya ile. Hali kadhalika Makamu wa Rais alitembelea Mbinga wananchi walimweleza, wakamuwashia na vibatari. Kama mimi ni mwongo Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi hapa. Watu walianza kupata matumaini. Sasa mimi nimeambiwa na nimetumwa na wananchi, ikiwa kama viongozi ndiyo tunaowaeleza matatizo kuhusu umeme wa Mbinga sasa watuambie hapa tumwambie nani? Vinginevyo nitatoa shilingi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimthibitishie ndugu yangu Mheshimiwa Ngwatura, kwamba sikutoa kauli nilipokuwa Mbinga, kwamba *TANESCO* ingepeleka jenereta. Tulichofanya pale ni kutembelea mradi wao ambao ulikuwa na matatizo na kuwaombea kiwanja *TANESCO* ambao pia walionyeshwa sehemu ya kujenga ofisi hapo itakapofika wakati wa kujenga ofisi. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Ngwatura, awafahamishe rasmi wananchi wa Mbinga kwamba sikutoa ahadi hiyo. La pili, kuhusu ahadi ambazo au malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa kwa viongozi wakuu ni kweli kwamba Serikali inafahamu tatizo la umeme au ukosefu wa umeme Mbinga. Lakini Mbinga ni sehemu ya Mkoa wa Ruvuma na ndiyo maana tumesema hapa kwamba hatua ya kujenga *substation* Makambako ndiyo chanzo muhimu na chanzo sahihi cha kupeleka umeme Mkoa wa Ruvuna hapo fedha zitakapopatikana.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kwamba amekanusha na viongozi aliowaambiwa wamesikia. Sasa kama itathibitika kwamba alisema, basi atakwenda kwenye Kamati ya Mheshimiwa Simpasa. *(Makofi/Kicheko)*

La pili, bado sijaridhika kuhusu kauli kwamba Mbinga, wasubiri muda wote huu wakati sisi tunapata matatizo makubwa sana ya kusindika kahawa na kadhalika. Kama tunaendelea hivyo maana yake tunaua uchumi wa taifa. Mimi nisingependa niambiwe hapa kwamba Serikali haina fedha, kwa sababu fedha tunailipa *IPTL,* kwa nini tusifute hiyo *IPTL* ili hizi hela zikajenga? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumsaidia Mheshimiwa Mbunge Ngwatura, kuwa akisema hawezi hailewi kwa nini angoje na tutoe fedha tunazolipa *IPTL,* ili tuzipeleke Wilayani kwake na sehemu nyingine, fedha tunayolipa *IPTL,* ni ili tupate huu umeme unaowaka hapa sasa hivi. Ni fedha ambayo tusipolipa tutaingiza taifa letu kwenye mgao. Tukishaingia kwenye mgao hata hiyo, kahawa ambayo sasa hivi inazalishwa sehemu zake na sehemu zingine haitafika sokoni na uchumi wa taifa utaanguka moja kwa moja ndiyo sababu tulikuja hapa kutafuta *supplementary budget* mwezi wa nne na tunashukuru Bunge hili lilipitisha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge aelewe hivyo na atupe muda tupate fedha.

Fedha tutazipata kama nilivyosema lakini hata kama tungekuwa nazo za pale jimbo kwake peke yake kama hatuna *grid* utakuwa ni umeme wa jenereta na hiyo tutafanya mara *TANESCO* watakapoweza kupata fedha. Tunajaribu kupeleka jenereta kidogo kidogo kila tunapopata fedha. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti*, sub vote 1001 item 261100. Other goods and other services not classified above.* Kama nimemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri, amesema *TANSORT* kwa sasa imebadilika na katika kifungu hiki *TANSORT* imetengewe shilingi milioni 561 kwa ajili ya *other charges* na hiyo ndiyo inayodhihirisha kwamba kweli sasa hivi iko chini ya Serikali na Serikali wataisimamia na kwamba amesema *revenue* yote itakayopatikana kutokana na uchambuzi wa almasi itakuwa kwa *exchequer.* Lakini nikisoma *Auditor Generals Report* inazungumzia juu ya 2.5 billion ambayo kwa muda mrefu sana haziweza kurudishwa Serikalini. Kwa hiyo, nategemea kwamba katika hali kama hii aweze kuliambia Bunge lako tukufu ni lini wataamlisha ile fedha iweze kurudi kwa ajili ya matumizi ya nchi. Hilo moja.

La pili, tuli-*suggest* kwamba hivi sasa wachimbaji wa almasi wameongezeka zaidi ya Mwadui, kuna Nyarumasi katika taarifa yake amesema Nyarumasi yenyewe itaanza kuchimba na kuna wana wachimbaji wengine na kwa hiyo, almasi yote itakuwa *directed* katika chombo kama hiki. Kwa nini basi kusiwe na *Government Executive Agency* ambayo itachukua zote za almasi na ikaweza kuzichambua ni lini kuna *time frame* ambayo pia unaweza ukaa-*point general manager* wa *TANSORT* na ikawa *agency?* Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Cheyo, kwa maswali yake mawili.

Kuhusu fedha za *TANSORT* ambazo anasema kama dola milioni 2.3 hivi, fedha hizo ni kweli ziko kwenye akaunti na sasa hivi *Accountant General* wa Serikali anafungua akaunti maalum ya kupokea fedha hizi ili zisikae kule ambako zilikuwa zinakaa kwenye mikono ya *Debeers*. Fedha hizo zikishafunguliwa akaunti yake, basi *is part of the Government revenues* popote pale zitakapokuwa na zitamilikiwa na *Accountant General* wa Serikali yetu.

Kuhusu ku-*sort* almasi kwamba kwa nini tusiwe na *Executive Agency,* almasi zinazochambuliwa na *TANSORT* ni zile za Mwadui tu, ndiyo mkataba ulivyo. Mkataba wetu sisi na *Debeers*. Hawa wengine wanaochimba almasi zao, wana namna yao ya kuzichambua na kuziuza kwa sababu ni soko huria. Lakini wazo lake la kuwa na *Executive Agency* ni wazo zuri tutalitazama kama lina *merit* ya kuweza kutekelezwa siku za usoni. Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko kwenye mshahara wa Waziri kifungu 250100. Kwa bahati mbaya Waziri hakupata muda wa kujibu hoja zangu zote nilizozisema kwa hiyo, naomba kwanza kwa mujibu wa kanuni kifungu cha 50 kuna makosa katika hotuba yake na ni vizuri akasahihisha. Kosa la kwanza ni takwimu alizozitoa ukurasa wa 40 ambao utaishia kwenye mapato ya Serikali sasa ni vizuri akasahihisha. Amesema kwamba katika mwaka 2003 mgodi wa *Williamson Diamond* ulizalisha karati 207,400/= kwa mujibu wa taarifa yake mwenyewe iliyopitia mpaka Benki Kuu ya Tanzania kwa kamishna wa kodi na kadhalika inaonyesha kwamba ni karati 211,286.90 ambayo hiyo inakuwa dola 24,529,213.93.

Halafu katika hotuba hiyo hiyo amesema kwamba mwaka uliopita 2002 walizalisha karati 177,250. Lakini siyo si sahihi. Sahihi ni karati 316,202.20 ambayo ni sawa sawa na dola 35,777,750.24. Sasa makosa haya yanakosesha mapato Serikali. Kwa hiyo, Wizara inaonekana haina takwimu sahihi za kusimamia mapato ya Serikali na hili ni tatizo la msingi ambalo Waziri umesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hilo ndiyo maana katika jedweli la 10 alilolisema Waziri katika hotuba yake nikamtaka achambue yale mapato ya almasi, nikielewa kabisa kwamba takwimu zake zina matatizo. Takwimu ambazo nazisema nilizipata kwenye Serikalini kwake yeye mwenyewe Wizarani kwake ambazo zimeidhinishwa na vyombo vyote vinavyohusika. Sasa ukichukua hesabu hizo kwa miaka ile mitano ya Waziri aliyoonyesha katika jedwali 10 tumepata dola 126,529,001.61 kutokana na hesabu ya jedwali yake. Hiyo inatoka *Williamson diamond* peke yake. Ukichukua *up front* ambayo wanaichukua milioni 12,652,902.26 na s*orting fees* ya milioni 5,029,964.15 na *rent* ambayo inapata Serikali milioni 6,326,450.13 jumla inakuja ni dola 124,009,314.54. deni ambalo Williamson wanadaiwa ni milioni 22,000,000/= jumla ni milioni 46,009,314.54.

Sasa ukichukua mapata ya miaka mitano na ukichukua gharama zote ya Williamson si kweli kwamba Serikali haiwezi kupata gawio lake la asilimia 25, wala siyo kwamba Serikali ina sababu za msingi kutokana na mkataba kwamba wasamehewe kodi katika mwaka 1995 mpaka 2000 kwa sababu hiyo naomba Mheshimiwa Waziri ajibu yale masuala yangu niliyomuuliza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa yake hiyo, kwa kweli anasema takwimu zake zimetoka Wizarani kwangu basi mmoja wetu labda ameandika vibaya. Aidha mimi nimeandika vibaya kwenye hotuba yangu au wewe umezi-*copy* vibaya. Lakini naomba unipe muda twende tukazi-*check* kwa sababu ni mapato ya Serikali hatuwezi kuyaachia yakapotea hivi hivi. Kama wewe umetoa takwimu sahihi basi tutachukua za kwako. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Naomba Mheshimiwa Waziri aahidi jambo moja tu katika Bunge hili, kwamba atahakikisha *Williamson* wanalipa kodi, pale ambapo Bunge hili litaridhika kwamba kuna haja ya kulipa kodi hilo la kwanza?

La pili, kwamba Waziri ataunda Kamati ya Bunge itakayoripoti katika Bunge hili kwenda kufuatilia mapato halisi yanayotokana na almasi Mwadui? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, kwamba pale ambapo itabainika kwamba Williamson hawakulipa kodi zake halali watalipa kodi zake halali, watalipishwe. Lakini tukubaliane na jambo moja tufanye kazi kitaalum, tuna *Board Members* pale, tuna *auditors* pale na wanakagua haya mahesabu ya *Williamson.* Lakini kama kuna makosa yametokea nakubali kabisa kwamba tutayafuatilia ili tupate mapato ya Serikali. Kamati ya Dr. Kipokola inaangalia na hilo na tuna mtalaam ambaye ni *independent* kabisa anaangalia shughuli za *Williamson Diamond* mines ikiwa ni pamoja na mkataba tulionao na yeye maisha ya mgodi ule kwa hiyo, wote hawa wanafanya kazi hiyo, tuwape muda ili tuweze kupata ushauri mzuri. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. mimi niko kwenye *sub vote 1001* kifungu kidogo 250100. Kama nilivyotoa mchango wangu kwa maandishi kwa Mheshimiwa Waziri, nimeeleza masikitiko yangu ya kukosa *transformer* mbili katika Jimbo la Muleba Kaskazini kwa mfululizo mwaka wa tatu sasa. Katika vijiji vilivyopewa *priority* katika jimbo langu kupata umeme ni pamoja na Katoke, pamoja na Ilogelo, ilikuwa pamoja na Bunywambele, Bunywambele wakapata umeme kutokana na kwamba pale kulifungwa mitambo ya *mobitel* kwa hiyo, kile kijiji kikapata umeme. Sasa vijiji vingine ziko nguzo, ziko nyaya lakini umeme hauwezi kuwepo kwa sababu hakuna *transformer* ni jambo ambalo linanisikitisha sana. Kwa hiyo, nimeona kwamba ni vema kitu ambacho nilifikiria kwamba gharama zake ni kidogo na Serikali, haiwezi kukubali kuachia nguzo zikasimama muda wote ule na nyaya zipo pale, lakini kinachoshindikana ni kupatikana *transformer* mbili tu.

Suala la pili ambalo nilipenda katika hilo hilo la *transformer* kuliuza leo kwamba ni kwa nini halifikiriwi ni *transformer* ya kupeleka umeme katika Shule ya Sekondari ya Izigo ambayo iko karibu kiasi cha kilometa 1.7 kwa hiyo, inahitaji kupata *transformer* moja ili iweze kupata umeme.

Suala lingine la tatu ambalo nimekuwa nalo kwa muda mrefu sana ni umeme wa mji, ni kama sehemu ya Mji unaitwa Kagoma, Mji ule unao watumiaji ambao wako tayari wapatao 60 ni eneo la kijiji lakini wako tayari, kuna shule ya sekondari pale, kuna *gate* inaanzishwa mpya. Lakini nilipofuatilia nikaambiwa kwamba umeme pale unaweza kugharimu kama kiasi cha shilingi milioni 92 na *point* kufikia pengine 92.5 milioni.

Lakini tatizo ni kwamba haulipi. Sasa nikauliza ili ulipe unatakiwa kufanyika nini kwamba kufungwe pale mashine, kufungwe pale na mitambo mingine.

Sasa mimi nikawa najiuliza ni nani anaweza kupeleka mitambo kufunga mahali ambapo hata ahadi ya kufunga umeme pale haipo? Kama si suala tu la kutaka kuonyesha kwamba haiwezekani. Sasa ninachopenda ni kutoa majibu kwamba inawezekana au haiwezekani? Lakini majibu ya kisiasa katika masuala ambayo yanakuwa yanagharimu haja za wananchi kwa kweli yanakuwa ni magumu kuyafuatilia. Ninaomba majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri ameshawahi kuwasiliana nami kuhusu masuala ya *transformer* na hata wakati huu ambao tumekuwa tunajiandaa na bajeti kwa kweli nilikuwa nashughulikia masuala yake. Sasa kuhusu hizi *transformer* mbili napenda nifahamishe kwamba zitashughulikiwa haraka iwezekanavyo, hizi *transformer. (Makofi)*

Kuhusu Sekondari ya Izigo kwa kweli ni muhimu sana shule zilizo karibu na njia za umeme zipate umeme. Hilo kila mtu anafahamu. Lakini nadhani tatizo limekuwa ni kwamba wakati mwingine uwezo wa kufikisha umekuwa siyo mkubwa sana. Lakini napenda nimwahidi kwamba kwa kuwa amesema *within* kilometa 1.7 basi tutalitazama hilo na watu wa *TANESCO* tuone namna gani linaweza kufanyiwa kazi haraka. *(Makofi)*

Hili la Kagoma kwa kweli namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwa sababu siwezi nikalitolea kauli sasa hivi mpaka hapo tutakapoweza kulitazama vizuri zaidi. Lakini haya mazuri ya mwanzo nadhani tunaweza tukayashughulikia. *(Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 1001 mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mshahara siwataumaliza kabisa?

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Kati ya Wilaya 18 ambazo ziliwekwa katika ilani ya uchaguzi kwamba zitapatiwa umeme katika kipindi hicho mpaka 2005 ni pamoja na Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo. Wilaya ya Kasula imetambuliwa rasmi kama Wilaya mwaka 1919, Wilaya ya Kibondo imetambuliwa rasmi mwaka 1934 zimetambuliwa kama Wilaya.

Lakini katika ukurasa wa 6 hizi Wilaya hazizungumziwi hata *plan* iliyoko ya kuweka umeme katika Wilaya hizi. Kuna tatizo gani hivi sasa Wizara ijielekeze kupeleka umeme vijijini wakati Wilaya hizi kongwe hazijawahi kupata umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakati Wizara inanijibu kuhusu upelekaji umeme Kigoma, Serikali ilisema kwamba kazi imeshaanza Kaulia ya kupunguza nguvu za umeme kutoka kilovolt 132 kuwa kilovolt 33. Lakini leo Mheshimiwa Waziri, anaanza kutoa hadithi nyingine kwamba sasa ndiyo zinatafuta fedha za kufanya upembuzi yakinifu. Lakini pia waliahidi kwamba ifikapo mwaka 2005 Mkoa wa Kigoma utakuwa umepata umeme wa uhakika wa grid. Leo inakuaje Serikali inaanza kujikanyaga upya na kubadilisha maamuzi yake ambayo imekwishafanya? Naomba maelezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Beatus Magayane kwa maswali yake kuhusu umeme Kasulu na Mkoa wa Kigoma. Tukitoa ahadi za muda mrefu sana tunalaumiwa kwamba hatutimizi ahadi zetu.

Kwa kweli ahadi tunazozitoa hapa ni pale tu ambapo tuna uhakika wa kupata fedha za kutekeleza mradi au za kufanyia upembuzi yakinifu au *feasibility study* au ya kujenga ule mradi wenyewe. Kwa hiyo, Kasulu na Kibondo hatujapata uhakika. Kazi tunafanya, tunatafuta fedha za kupeleka umeme sehemu hizo, lakini hatujapata uhakika ndio maana hatutaki kutaja katika hotuba zetu kwa wakati huu, sio kwamba tumepasahau, hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme wa Kigoma kwamba tulisema umefika Kaliua, hapana ni *feasibility study.* Tumesema *feasibility study* ya kupeleka umeme Kaliua na Urambo, hiyo iko tayari na kazi huyo ya *feasibility study* inafanyika. Tulifikiria *feasibility study* hiyo hiyo itakwenda mpaka Kigoma lakini wataalam wametuambia afadhali tumalize kazi ya umeme wa Kaliua na Urambo na hii ya kupeleka umeme Kigoma tutumie fedha ambazo tumeahidiwa na Sweden kuufanyia *feasibility study* yake ili uwe mradi ambao unasimama wenyewe. Hapo ndipo tulipofika.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuja kutembelea Mkoa wa Kigoma, yeye mwenyewe kwa kauli yake na mimi nilikuwa kwenye msafara wake, akiwa katika Ofisi ya Chama Mkoani alitamka wazi kwamba ifikapo mwaka 2005 Mkoa wa Kigoma utakuwa umeshapata umeme wa uhakika wa *Grid.* Leo inakuwaje tuanze mradi upya wakati yeye alipokuja alikuwa na *agenda* ya kutuambia kwamba kuna umeme? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilisema hivyo, narudia kauli yangu kwamba fedha hizi tunapewa na wafadhili. *At the end of the day* Mfadhili ndiye anayekwambia fedha hii hapa anaachia *cheque,* kazi inafanyika. Mfadhili huyo huyo ndiye amesema *feasibility study* tuliyokuwa tumetaka ipeleke umeme Kaliua na Urambo haiwezi kwenda, hawataki kufadhili mpaka Kigoma. kwa hiyo ni lazima tuanze tena upya. Sasa mimi ningefanya nini? Nilikuwa na matumaini kwamba itachukua zote mbili. Kwa hiyo, naomba nieleweke hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya kujitetea aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, naomba aahidi kwamba sasa baada ya kuwa amepata uhakika wa hizo pesa; ni lini umeme wa uhakika utafika Mkoani Kigoma? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kigoma wakubali maelezo kwamba upembuzi yakinifu, fedha zimepatikana ambazo zitatuambia mradi huo upitishiwe wapi, uwe wa aina gani na utagharimu kiasi gani. Ikipatikana hiyo, ndio sasa tunatafuta fedha kutoka kwenye *World Bank* za kukopa au kwa watu wa Sweden au Serikali nyingine yoyote ile ambayo itatupatia msaada. Kwa kweli hizo ndio hatua ambazo tunazifuatilia wakati wa kutekeleza miradi ya umeme ambayo inafadhiliwa na mikopo au na wafadhili.

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kutumia kifungu cha 1001, Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nipate mambo mawili. Kwanza Mheshimiwa Waziri atufahamishe sisi Wabunge wa Kigoma tulioshiriki kwenye ziara yake, nini tuwaambie watu wa Kigoma ambao waliahidiwa umeme mbele ya kadamnasi kwa kutumia njia ya Urambo na Kaliua? Kwa nini kama yeye alijua wafadhili ni watu fickle namna hiyo aliweza kwenda kutoa kauli nzito kwa watu ambao tayari wanatapatapa na suala la maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mkoa wa Kigoma ulikuwa uunganishwe na umeme wa uhakika kutoka Burundi tangu mwaka 1993 na mimi mwenyewe kwa mazungumzo niliyokuwanayo na Waziri wa Nishati wa Burundi na Rais Buyoya wakati ule walinithibitishia kwamba wao walikubali kutoa nusu ya gharama ambayo ni Dola milioni 20 kupitia *ADB*.

Sasa kama Waziri anaona kuna tatizo la kupata pesa za wafadhili/wahisani ambazo wala hajatuambia ni pesa ngapi watatoa; ni kitu gani kinachomzuia sasa kwenda kurudia Mkataba ambao tulikwishatiliana sisi na Serikali ya Burundi ili sisi tupate umeme kwa sababu *feasibility study* ilikwishafanywa kule na ndio maana tulikubaliana hivyo? Atuambie kwa nini kunakuwa na kigugumizi kwa watu wa Kigoma kupewa umeme kutoka Burundi au Kongo na hapo hapo umeme unatoka Zambia, Uganda na kila mahali kuwapa Watanzania wenzetu kama sisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niambiwe kwa nini Waziri harudii Burundi? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Kabourou maswali yake mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kabourou anasema akifika Kigoma awaambije wananchi wa kule. Naomba awaambie kwamba, Serikali inaendelea na juhudi zake za kupata fedha ili kupeleka umeme Kigoma na *infact* tunaongeza juhudi hizo ndio maana kwa sasa wakati tukingoja umeme wa uhakika tumesema tutapeleka *generators* ziende zikasaidiane na zile zilizoko pale kama tulivyofanya Mtwara ili umeme uwake pale Kigoma Mjini kwa wakati wote. Hiyo ni hatua ya awali tu. Lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kama kweli anayosema, sija-*check* na watu wangu na ninamwamini Mheshimiwa Mbunge, nitakwenda ku-*check* na watu wangu wa *TANESCO* kwa sababu Wizarani kwangu sikuliona hilo na niko tayari kwenda hata Burundi nikazungumze na mwenzangu kule tuone uwezekano huo wa kuweza kupata umeme huo kutoka kule. *(Makofi)*

**MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameahidi sasa kuangalia njia ambayo ndiyo rahisi na ya uhakika na ambayo ikitumika ndiyo itakayoweza kuwahudumia wananchi wa Kigoma kwa wingi wao Wilaya zote tatu kwa mpigo, sasa mimi nimwulize tu, anaahidi nini kuhusu generator ambazo hata mwaka jana zilisemekana zingekuwepo Kigoma na zingezalisha umeme kama ambavyo inafanya Mtwara sasa inatoa *Megawatt 1.8* na tuliambiwa zimenunuliwa pamoja huko India na hata aina ya hizo *generator*, na sisi watu

wa Kigoma Mjini ndio tunaolala bila umeme kwa siku tano? Tunapewa mgao wa siku moja kila wiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tupewe *generator* yetu au tuondoe Shilingi hapa, yaishe. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namwomba ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Walid Kabourou, asiondoe Shilingi. La pili ni kwamba kweli matatizo ya umeme Kigoma yanafahamika na mwaka jana tatizo ambalo lilikuwepo na ndio sababu ya msingi kwamba haikupatikana *generator* mpya katika kila sehemu ambayo tulikuwa tunataka kupeleka majenereta mapya, ni kutokana na hali ya ukame na hali ya kifedha ya *TANESCO* na ndio maana hata hivyo kulikuwa na kazi ya ukarabati ilifanywa ya zile *transformers.* Lakini hivi sasa kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, tunatarajia sasa *generator* kama ile iliyopelekwa Mtwara itapatikana moja kwa Kigoma na moja kwa Songea. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* 1001 kifungu 250100 Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati nachangia hoja, kuna maswali nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, lakini amenijibu hapa sikumwelewa sawasawa. Kwenye hotuba ya Waziri ndiyo iliyonichanganya zaidi. Waziri anasema hivi, naomba ninukuu; "Serikali ina matumaini makubwa kuwa Mradi wa *Mnazibay* utafanikiwa. (Hana matumaini) Hata hivyo, endapo matokeo ya uhakika wa gesi hiyo ya *Mnazibay* hayataridhisha, Serikali inakusudia kutumia njia nyingine ya kuwa na umeme wa uhakika katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Njia hiyo ni kujenga Kituo kikubwa cha kuzalisha umeme Somanga Funga kwa kutumia Gesi ya Songosongo kwa njia ya umeme ya *KV132* ya kusafirishia umeme huo kutoka Somanga hadi maeneo husika."

Swali langu ni kwamba, kwa nini Serikali iendelee kubahatisha *Mnazibay* wakati ina uhakika kwa Songosongo gesi yake ipo katika kupeleka umeme Mtwara? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Pili, hapo Serikali itakapokuwa tayari kuamua sasa kwamba Mnazibay haifai, inafaa Songosongo, watapata fedha kutoka wapi? Kwa sababu ziko pesa zimebakia Shilingi bilioni 70 na Waziri amekiri pale mbele; walishindwa kujenga hoja ili hela hizo ziende Kusini? Leo wakishindwa kule *Mnazibay,* watapata fedha hizo kutoka wapi kama walishindwa kujenga hoja pale mwanzo hizo hela ziende Kusini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba zile fedha zilizobakia Shilingi bilioni 70 zimeelekezwa katika mradi gani? Sikuelezwa! Lakini la mwisho nilisema, *Mnazibay* itakuwa ni Gridi ndogo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara. Je, wananchi wa Lindi na Mtwara wanaweza kumudu kulipa gharama za umeme ule peke yao? Sikupata majibu. Naomba maelezo. Hapa leo naona hela hazitoki. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi kwa maswali aliyouliza Mheshimiwa Abdulaziz kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya kusema kwamba tuna matumaini kwamba mradi huu wa *Mnazibay* utafanikiwa ni lugha ya kistaarabu na ya kawaida unaposhughulikia miradi. Siku zote Mheshimiwa Abdulaziz anafahamu kwamba unapopanga lazima uweke akiba kwamba huenda pakawa na jambo litakalojitokeza lisilokuwa la kawaida. Hii ndio maana yake. Suala la kusema kwamba baada ya hapo tutafanya Mradi wa Songosongo inakuwaje, mradi wa Songosongo tumeutaja hapa kama tulivyosema awali kama ni *fallback position.* Unapokuwa unashughulikia masuala mazito kama haya, lazima uwe na *fallback position. Fallback position* hii ya Songosongo kwa sasa hivi *as long as Mnazibay project* ipo na mwekezaji *is not an option* kwa wale ambao ni wafadhili waliotoa fedha hizi kwa ajili ya kuendeleza gesi hiyo, *it becomes an option* pale ambapo *Mnazibay* yenyewe inakuwa ime-*fail* na sio suala la kushindwa kujenga hoja. Hoja imejengwa na tulieleza hapa lakini hatimaye fedha za Wafadhili zinategemea na matashi, hoja peke yake sio inayokupatia fedha. Lakini pia na matashi ya yule mtu ambaye anatoa fedha hizo. Suala kwamba fedha hizi ziko wapi, tulisema kwamba fedha hizi haziko mfukoni mwa Serikali. Ni sawasawa na wewe umepeleka rasimu ya kuomba fedha inasema mradi utakuwa na Sh.70/= lakini baada ya kazi kubwa kufanyika ikaonekana kwamba gharama ya mradi imepungua Sh.60/= yule mwenye Benki au mwenye kukupa fedha atakupa zile Sh.60/= za ule mradi na ndicho kilichotokea sasa hivi kwamba fedha hizi bado wanazo wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bei za umeme, kwa mujibu wa tathmini ya awali ya mradi huu tunatarajia kwamba gharama hizi hazitapishana sana na gharama nyingine za umeme hapa nchini. Lakini hata hivyo, hawa wakishafikia hatua ya kuhakikisha kwamba sasa wamehakiki ile gesi, upo utaratibu wa kukaa na *TANESCO* kukaa na Asasi mbalimbali ya Serikali pamoja na Kampuni hii kuzungumzia suala zima la gharama ya umeme ule kwa hatua ile ambayo itakuwa imefikiwa. Kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Abdulaziz kwamba pasingekuwa na mradi na Serikali isingeshawishi mradi kwenda kule ambao utakuwa kabisa kwa asili yake *by its very nature* hauwezi kabisa ukalipika. Kutokana na *feasibility study* na *proposal* ambazo zimeletwa na hawa wafadhili ndio maana tukaridhika kwamba pengine mradi huu utakapofanikiwa unaweza ukawa wa manufaa kwa watu wa Kusini na napenda nisisitize kwamba Mradi huu utakuwa na manufaa kwa watu wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na Wilaya ya Tunduru endapo utakamilika.

**MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Songas au *Songosongo Gas* ndio iligundulika mapema kabla ya *Mnazibay.* Kwa nini *fallback* isiwe *Mnazibay* iwe Songosongo ambayo ndiyo ilianza zamani? Hilo la kwanza. Lakini la pili ninachosema, kwamba suala la kujenga hoja kwamba kama wafadhili hawatakubali kwa mawazo ya Waziri kwamba itategemea utashi wa wahisani, kama hao wafadhili hawatakubali, je tuamini kwamba sisi umeme basi hatupati tena umeme kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri? Naomba nipate majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abdulaziz, kama ifuatavyo:-

Suala kuhusu kwa nini fallback isiwe *Mnazibay,* wakati mradi wa *Mnazibay* unafikiriwa kuanzishwa, nilishawahi kutoa taarifa hapa Bungeni kwamba palikuwa na fedha ambazo zilitolewa na Benki ya Dunia ambazo hazikutosha, zilitakiwa wakati ule apatikane mwekezaji ili kuweza kuhakikisha kwamba mradi ule unaendelea na tulieleza

kwamba mwekezaji hakupatikana ndio maana ule mradi haukuendelea. Kwa sababu mradi haukufanyika wakati ule, usingeweza kuwa *fallback position.*

La pili, napenda nimhakikishie kwamba Serikali inafahamu umuhimu wa umeme wa uhakika kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi na Mikoa ya Ruvuma na Kigoma na kwamba kwa vyovyote vile itatafutwa njia wakati huo ya kuweza kuhakikisha kwamba wanapata umeme wa uhakika. Sisi tuna matumaini makubwa kwamba mradi huo wa *Mnazibay* utafanikiwa na kama ambavyo nimetoa taarifa hapa mwanzo wakati najibu, nimesema sasa hivi timu yenyewe ya wawekezaji tayari iko Dar es Salaam na wanangojea kibali kutoka Maliasili kwenda kupeleka vifaa na kuanza kazi.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile kile cha 1001 na 250110, lakini sikusudii kukamata mshahara wala Bajeti yenyewe na sababu zinajulikana nilisema Asubuhi; lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu suala la Tunduma alisema Mheshimiwa Waziri atafafanua kuhusu umeme kutoka pale njia panda kwenda Tunduma badala ya kutumia umeme wa Zambia ambao unatusumbua sana. Sasa maadam Waziri nadhani hakupata nafasi ya kutosha, ningependa nisikie kauli yake anasemaje kuhusu usumbufu huu ambao tunao pale Tunduma. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumjibu Mheshimiwa Simpasa swali lake kuhusu usumbufu wa umeme katika sehemu hizo za Tunduma. Nataka kumuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeagiza *TANESCO* mara moja wakafuatilie waone ni kitu gani kinaleta matatizo hayo na ninaahidi kwamba tutakapopata ripoti hiyo basi tutaishughulikia mapema ili kero hiyo iweze kuondoka kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tuelewane tu na Mheshimiwa Waziri, niko pamoja naye. Nataka ieleweke tu kwamba tunapata umeme unatoka Zambia, lakini unatusumbua sana kwa sababu hatuwezi kuudhibiti ule umeme, wanazima wanavyotaka na sisi hatuwezi kufanya lolote. Ila sasa kuna umeme ambao unakwenda kama kilometa saba au nane kwa Mheshimiwa Cheyo ambao ni wa Tanzania sasa na ni kilometa saba au nane kutoka pale kwenda Tunduma kwa hiyo tukaomba Mheshimiwa Waziri aweze kuunganisha kutoka pale kupeleka Tunduma umeme wa nchi yetu ili kama wale wakizima, basi tuwe na *alternative* kuwasha umeme wetu. Kama hiyo inashindikana, kutoka pale basi waweze ku-*connect* kutoka Songwe watupelekee pale ambapo ni kilometa 75 ili tupate umeme wa uhakika kuliko usumbufu huu. Likieleweka hili na nikajibiwa vizuri kama alivyosema Mwenyekiti, sina tatizo na mambo mengine.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nia ya Mheshimiwa Mbunge Simpasa inaeleweka, ni *reliability of supply* na ni nia njema na sisi tuna-*share vision* yake. Tutalifanyia kazi hilo suala ambalo amelisema. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze, mwaka 2000 nilipewa ahadi ya kupewa umeme wa kwenda Iyula, Igamba na Hasamba na nguzo zikalundikwa kwenye njia hiyo ya kwenda Iyula. Zimekaa mpaka mwaka 2002. Nikauliza swali hapa Bungeni, nikaambiwa sasa wewe ukirudi

huko umeme utakuta umefika. Niliporudi nikakuta nguzo zile zimeungua na mpaka sasa hakuna kinachozungumzwa humu. *(Kicheko)*

Sasa nina mawili. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje juu ya suala hili ambalo hata watu walimsikia akisema umeme umefika kule tulikopangia?

Pili, Mheshimiwa Waziri akubali kukiri kwamba alinijibu uongo Bungeni na kwamba atarekebisha mambo haya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusikia maafa yaliyotokea huko katika Jimbo la Mheshimiwa Halinga. Kwa kweli nia yetu sio kuacha nguzo chini mpaka ziungue moto na hilo ni tukio ambalo linatusikitisha sana na tunaomba radhi kwa wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Lakini ahadi ambayo naweza kutoa ni kwamba tutawatuma wataalam wetu wa *TANESCO* waende wakaone ni kitu gani kinatakiwa kufanywa, ni nguzo ngapi nyingine kama ni mpya au zile zile zinaweza kutumika na kujaribu kutafuta namna ya kupeleka umeme kule ambako ulitakiwa kupelekwa kabla nguzo hizo hazijaungua. Ninamhakikishia Mheshimiwa Halinga kwamba tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M.MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye mshahara wa Waziri Yona. Katika mchango wangu nilijaribu kumwelewesha Waziri kwamba umeme wa makaa ya mawe ndio umeme wa uhakika na wa bei poa, uzoefu na utafiti wa kisayansi unaonyesha hivyo. Nataka maelezo kama Waziri ameelewa na anaamini hivyo. Hilo la kwanza. *(Kicheko/Makofi)*

La pili, kama ameelewa somo hili na anaamini, atachukua hatua gani za dhahiri kuhakikisha kwamba umeme au mradi wa mchuchuma unaanza mara moja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu na ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa maswali ya Mheshimiwa Profesa Mwaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba Profesa Mwaga anafahamu kwamba sisi tunao uwezo mkubwa wa kuelewa yale ambayo ameyasema na kama ambavyo nimechangia ni kwamba tulielewa na nilisema kwamba kwa kweli hakuna tatizo la *mindset* kama ambavyo alisema. Tunamheshimu sana kwa fikra zake, lakini napenda niseme kwamba sisi hatuna tatizo na umuhimu wa umeme wa makaa ya mawe. Nilisema tunakubaliana juu ya umuhimu wa umeme wa makaa ya mawe. Nilisema pia kwamba tunakubaliana juu ya umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na chanzo cha umeme cha uhakika kama hicho ili hata tunapoingia katika ushirikiano na nchi nyingine, basi tunaingia kama sio *from a position of strength at least from a position of equity.* Hayo niliyasema. *(Makofi)*

Kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba asiwe na wasiwasi na sisi juu ya suala hili na nilisema wakati ule pia kwamba Wizara ya Nishati na Madini ni moja ya Wizara chache au ni moja ya Wizara ambazo zina wataalam wa hali ya juu kabisa na wana uelewa wa hali ya juu. Kwa hiyo, hilo napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge.

La pili kuhusu mradi wa mchuchuma, kama nilivyosema wakati nachangia, baada ya maelezo ambayo tumeyatoa na hatua ambayo imefikiwa na nia yetu ilikuwa ni kuhakikisha kwamba *we put a strong bargain* na wawekezaji. Baada ya kufikia hatua kwamba yale mambo ambayo yangeweza yakatuletea matatizo hayatakuwepo, sisi tumesema kabisa kwamba sasa tumewataka wathibitishe kwa maana ya kwamba mkizungumza maneno kwenye meza ni vizuri na ndio utaratibu kwamba yawekwe katika maandishi ili shughuli hii iweze kuendelea kwa hatua inayofuata. Sasa napenda nichukue nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Profesa Mwaga kwamba kwa kweli, kwanza hakuna tofauti baina ya msimamo wake na msimamo wetu sisi.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu hicho hicho 1001 mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa sita wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kipengele kinachohusu umeme Makao Makuu ya Wilaya. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2000 kifungu cha (5)(3) kimeeleza kwamba ifikapo mwaka 2005 Makao Makuu ya Wilaya zote umeme utakuwa umeshafika na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza Wizara ambazo zitapatiwa umeme na ameeleza pia kwamba kuanzia kipindi hiki mpaka mwaka 2005 kuna Wilaya ambazo zimetajwa hapa zitakuwa zimepatiwa umeme.

Swali langu ambalo nilikuwa nahitaji ufafanuzi; Wilaya ya Nkansi ni Wilaya ambayo ni ya muda mrefu sana na kuna Wilaya nyingine hapa ambazo zimekuja nyuma baada ya Wilaya ya Nkansi kuwa imeshaanzishwa na Wilaya ya Nkansi haina umeme hata kidogo. Nilikuwa napenda nifahamu Mheshimiwa Waziri anasemaje, ile Wilaya ya Nkansi imerukwa kwa makosa katika kuchapwa au vipi? Nilikuwa naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana linalotaka ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba Wilaya ya Nkansi kama alivyosema haijapata umeme na katika ratiba ya Wilaya zilizobaki kupata umeme, Wilaya hii ya Nkansi hapo awali ilikuwa imetajwa kwamba ingeweza kupata umeme kati ya mwaka 2003/2004. Lakini wakati tunapotaja takwimu hizi kwamba Wilaya hii inatarajiwa kupata umeme mwaka huu, ni taarifa za matarajio kama ambavyo tumesema awali kwamba wahisani wangeweza kutusaidia na sisi kuchangia kuhakikisha umeme unafika katika Wilaya fulani kwa mwaka huo.

Lakini imewahi kujitokeza kama ambavyo imejitokeza kwa Wilaya ya Nkansi kwamba fedha zinachelewa kupatikana lakini Wilaya nyingine zinakuwa zimepata fedha. Pia inategemea na wahisani wakati mwingine huwa wana sababu zao wenyewe wangependa kupeleka umeme katika Wilaya fulani kwanza kabla ya Wilaya nyingine.

Kwa utaratibu huo huo kwa mfano Wilaya ya Ukerewe ambayo ndio inapata umeme hivi karibuni, ilikuwa hapo awali imepangiwa ipate umeme mwaka 2001 hadi 2002, lakini haikuwezekana, lakini sasa ndio taratibu hizo zinakamilika. Inatokana na

sababu nyingi ikiwemo taratibu za kupata fedha. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ipo pale pale na kilio cha watu wa Nkansi kinafahamika na Mheshimiwa Mbunge wa Nkansi na Mheshimiwa Mbunge Margareth Bwana tunawashukuru kwa kufuatilia kwa karibu suala hili la umeme wa Nkansi.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Mheshimiwa Waziri ni kauli ya Serikali na Mheshimiwa Waziri alikwishaahidi kwamba ifikapo mwaka 2005 mwezi Desemba umeme utakuwa umeshafika Nkansi na sisitulipofika Nkansi tuliwaeleza wananchi, wakaipokea taarifa ile kwa furaha na makofi wakatupigia.

Kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri ananipa uhakika gani ili nikawaeleze wananchi wa Wilaya ya Nkansi uhakika ambao hautakuwa kama huu utabiri wa Hali ya Hewa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi tena kwa Mheshimiwa Margareth Bwana kama ifuatavyo. Ili mradi tunategemea mchango mkubwa wa fedha kutoka nje katika usambazaji wa umeme. Ni dhahiri kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri wakati anachangia kwamba hatuwezi kuwa na uhakika wa mia kwa mia kwamba Wilaya fulani itapata umeme wakati tunatoa takwimu hizi za matarajio na kwa kiasi kikubwa kwa kweli tumefanikiwa. Sasa Taarifa za aina hii kama ni za Hali ya Hewa basi ndiyo hali yenyewe ilivyo.

Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu wa kupeleka umeme Nkansi unaohitaji zaidi ya shilingi bilioni 3.7 unafanyiwa kazi na pale fedha zitakapopatikana basi umeme huu utafikishwa Wilaya Nkansi. Napenda nimthibitishie kwamba orodha mzima ya kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya inatokana na ahadi ya chama chetu Chama Cha Mapinduzi, mwaka 2002 kwamba tungeweza tukafanya kazi kwa kadri na Ilani inasema katika kifungu cha 51(iii) kwamba kutoa kipaumbele, kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Hiyo ndiyo ahadi ambayo Chama Cha Mapinduzi ilifanya kwa wananchi na Serikali imekuwa ikitekeleza ahadi hii kwa kadri ya upatikanaji wa fedha unavyoruhusu.

Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge na ninajua yeye ana uzoefu mkubwa wa Sera za Chama chetu alifahamu hili na tutajitahidi pamoja naye kuhakikisha kwamba hii inatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Kwa hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba ile Desemba 2005 kwa maelezo yake haya maana yake imefutwa kauli ile ili mimi nikawaeleze kule. Tulishaeleza kule.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *schedule* iliyopo kwa umeme wa Nkansi kwa sasa hivi *again schedule* ya matarajio ni 2004 hadi 2005. Sasa nadhani hili ulilolisema ni wazi hata kama fedha zitapatikana kesho keshokutwa umeme utafika. Lakini kama fedha zitakuwa hazijapatikana ni dhahiri kwamba utekelezaji wake utakuwa bado haujafikiwa kwa kiwango hicho. Nadhani ningependa niishie hapo kwa sasa na Mheshimiwa Mbunge ni mzoefu sana nadhani anafahamu ni kauli ataweza kwenda kuwafikishia wananchi wa Nkansi.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi wa mambo muhimu yafuatayo. Mheshimiwa Waziri alipoulizwa akaambiwa *statement* aliyoitoa kule Kigoma mimi sikuwepo, lakini ni kwamba nilikuta watu wana-*celebrate* juu ya ahadi yake ya kupata umeme mwaka 2005. Sasa Mheshimiwa Waziri jibu alilotupa hapa anasema yeye hakusema. Sasa namwuliza je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda Kigoma? Maana CCM tumezoea kujisahihisha. Akakanushe jambo hili mwenyewe mbele ya Uongozi wa Mkoa. *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa maelezo yake ya umeme wa Gridi kama alivyoyatoa kuhusu Urambo na Kaliua yanahusiana sana na baadhi ya *conditions* alizozitoa kuhusu jibu alilolitoa kwa swali aliloulizwa tarehe 12 Julai, 2004 wakati akijibu swali la Mheshimiwa Mabina, Mheshimiwa Waziri alisema, Kigezo mojawapo cha kupeleka umeme mahali fulani ni kuwepo na barabara ya uhakika na umbali wa chanzo hizo cha umeme. Sababu ambazo zinaucha nje Mkoa wa Kigoma. Sasa anasema anayo mipango. Waziri kwa hotuba zake mbili zinazopingana anaeleza nini wananchi wa Kigoma, kama hoja zake ndiyo hizo hata mpango wake anaoueleza katika hotuba hii sio sahihi na wala siyo kweli. *(Makofi)*

Tatu, katika nyongeza ya majibu yaliyotolewa kwa swali hili la Mheshimiwa Mabina, Mheshimiwa Waziri anasema, *TANESCO* na Serikali wanapenda kupeleka umeme mahali ambapo tutapata watu wengi wenye uwezo wa kulipa huduma na kuleta faida. Je, Mkoa wa Kigoma amekwisha ulaani kwamba hauna wateja watakaolipia huduma hizo na kuleta faida katika nchi hii? Je, anategemea angepeta wateja kabla ya umeme kuwapo katika Mkoa wa Kigoma. Anategemea viwanda kuwepo katika Mkoa wa Kigoma bila kuwa na umeme, kama hakuna umeme suala la kuku na yai kipi kianze? Naomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mporogomyi maswali yake matatu nadhani kama ifuatavyo. Kuhusu kauli yangu nilipokuwa Kigoma na kwamba labda niko tayari kurudi Kigoma tukafanye mkutano, tusome *minutes* ili nikanushe niliyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi nilipofika Kigoma, nilipozungumza kama *minutes* zingekuwepo tungebishana na Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa sababu *minutes* hazipo na yeye hakuwepo nilipokuwepo kwenye ziara yangu basi naomba akifika awaambie wananchi wa Kigoma kwamba Serikali bado nia yake ya kuleta umeme Kigoma ni ile ile na Serikali sasa imepata fedha za kufanya upembuzi yakinifu ya kupeleka umeme wa uhakika Mkoa wa Kigoma na hayo ninayasema mimi ambaye nilifika kule nikasema hayo naambiwa nimesema mimi siamini nilisema umeme utafika hapa mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa tuna wataalam wengi sana *TANESCO* na pale Wizarani, kwa kweli Waziri yoyote wa Nishati hawezi kwenda mahali akasema umeme utakwenda umbali wa kutoka Tabora kwa mfano mpaka Kigoma tarehe aseme Desemba 2005. Hiyo haiwezekani. Mimi nilikuwa nawaambia, Serikali inashughulikia kutafuta fedha na kazi inaweza ikaanza kabla ya 2005. Sasa ukiwa na njaa ukisikia harufu unasema chakula kimeiva. Kumbe ni cha jirani kwa sababu nyumba ziko karibu karibu. *(Kicheko)*

Kwa kweli ukweli ni kwamba nilikuwa nasema kazi itaanza ya kupeleka umeme kule pamoja na upembuzi yakinifu na bado unasema upembuzi yakinifu naamini kabisa utaanza kabla ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba nilijibu swali nikasema *TANESCO* inapeleka umeme mahali penye barabara. Nadhani Mheshimiwa Mbunge, *would you be respect* amechukua jibu hilo *out of context.* Nadhani tulikuwa tunazungumzia kama nakumbuka vizuri kwa nini Serikali haipeleki umeme kwa wachimbaji wadogo wadogo, nadhani walioko sehemu mbalimbali ambao wanafanya kazi za huduma. Nikasema wachimbaji hao mara nyingi wanakwenda wanachimba kama Muheza kule wiki mbili, wakishachoka wanakwenda sehemu nyingine huwezi kuwapelekea umeme, kwa sehemu kama hizo. Lazima wawe mahali ambapo kuna ka-*settlement* Kijiji, Mji kama Kigoma vile kama Kasulu, kama Kibondo hizo sehemu ambazo Serikali ikipeleka umeme pale unajua una wateja na utapata watumiaji wa umeme huo.

Kwa hiyo, kama nilieleweka kwamba mahali pasipo na barabara hapapelekwi umeme sikuwa na maana hiyo. Nilikuwa na maana kwamba Kigoma, Kasulu, Kibondo sehemu hizo ambazo bado hazijapata umeme bado zitapelekewa umeme maana kuna *potential* kubwa ya kutumia umeme huo na kuendesha viwanda kama anavyosema na kilimo na kusukuma uchumi wa sehemu hizo. Kwa hiyo, nawahakikishia wananchi wa Kigoma na wananchi wa wilaya zake zote kwamba umeme tutaupeleka mara tutakapopata fedha za kufanya kazi hiyo.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la umeme kwa Mkoa wa Kigoma lingekuwa la ku-*convince* mtu yoyote anayesimama hapa wa Mkoa ule kama mpango wa Serikali ungeonyesha kuna kitu ambacho wanakifanya. Mimi ni Mchumi, ninaelewa maana ya *feasibility study* unaweza kuandika *feasibility study* leo ukachukua hata miaka 10 au zaidi kupata pesa. Tunachokitaka Serikali yenyewe ina mpango gani wa kuonyesha kwamba wana nia ya kupeleka umeme Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri amekubali kwamba kwa kweli kwa majibu yake haya hana mpango wa kupeleka umeme Kigoma. Akubali hivyo, kisha tujue tunakwenda vipi. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mporogomyi kwa mawazo yake. Kwa kweli yeye ni Mchumi, anaelewa mambo ya *feasibility study* ni kweli kabisa *feasibility study* inaweza ikaonyesha kwamba mradi unafaa ama haufai. Lakini kwa huduma hizi kama vile huduma za elimu.

Sasa hivi tungeulizwa Serikali ina mpango gani wa kupeleka sekondari kila Kata. Hata Waziri wa Elimu na Utamaduni hawezi kusema tarehe 10 Januari, 2005 kutakuwa na sekondari Kijiji fulani na Kata fulani na Kata fulani. Ni matumaini. Ni mategemeo. Mnaona wenyewe katika Bajeti zetu na Serikali *must be positive must be forward looking, must be encouraging* sisi tuna nia ya kupeleka umeme kila mahali. Na tunajaribu. Kule ambako haujafika nduguzanguni hakikisha ya kwamba tumepasahau, mmeona Mtwara huko tunavyojaribu kupambana na Wawekezaji, kubembelezana na wafadhili na Kigoma nako ni hivyo hivyo tutafikisha umeme mara tutakapopata fedha hizo na tunazungumza na Serikali ya Sweden.

Mimi namkaribisha Mheshimiwa Mbunge Mporogomyi kwa sababu yeye ni mwelewa wa mambo haya aende Ubalozi wa Sweden akazungumze nao. Waheshimiwa Wabunge wengi wanaenda kwenye mabalozi hapa na kuzungumza nao akahakikishe kwamba je kuna matumaini ya kupatiwa fedha hizo za kufanyia hiyo *feasibility study* ili tuweze kupeleka umeme kule.

Tukishamaliza *feasibility study* maana tuambiane ukweli. Tukiwaahidi wananchi kitu ambacho hatutaweza kukikamilisha tunajitia kwenye matatizo yenyewe. *Feasibility Study* ikimalizika na ndivyo ilivyofanyika katika miradi yote mikubwa mikubwa. Miradi yote mikubwa hata ya barabara, Mheshimiwa Magufuli atawaambia hapa kwamba fedha za kwanza zinatumika mabilioni ya kufanyia *feasibility study* hujui mpango ukoje, ndiyo upate fedha zingine za kutekelezea.

Tukimaliza *feasibility study* wa kupeleka umeme Kigoma tutatafuta sasa mfadhili. Ukiwa nayo ile ambayo ni *positive* unaenda sasa kupiga hodi kwa wakopeshaji kwa wafadhili ili wakupe fedha za kutosha kupeleka pale. Kama huwezi kupata fedha za namna hiyo, basi unarudi kwenye bajeti yako umwombe Waziri wako wa Fedha atafute fedha za aina ili upeleke mradi kule.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mporogomyi naomba tuelewane kwamba kweli na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kigoma kwamba kweli nia tunayo na tunafanya kila njia ya kupata fedha hizo ili tupeleke umeme Mkoa wa Kigoma mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho, mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwanza kabla sijatoa maelezo yangu kwa dakika moja. Nashukuru kwamba haya niliyozungumza na maelezo nitakayoyatoa wako mashahidi kutoka Mererani ambao ni ndugu ya hawa watu ambao wamejeruhiwa ama kuuawa. Hebu wasimame, wako pale. *(Makofi)*

*(Hapa wahusika Ndugu wa Marehemu na waliojeruhiwa walisimama katika sehemu waliokuwa wamekaa Bungeni)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Waziri amejibu suala la mauaji ama watu kupigwa risasi Mererani, lakini hapa nitasoma baada ya wakati muafaka. *FAX* niliyoletewa na *AREMA* Taasisi halali ya kuwatetea wachimbaji wadogo wadogo. Ameeleza kesi kama tatu nne hivi. Lakini wao wanasema mauaji ni watu 7. Kutumia risasi na kujeruhi ni matukio 27. Baadaye nitasoma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo yafuatayo. Kwamba atatuletea taarifa ya Tume ya Mboma ili tujadili kwa sababu itakuwa na haya mauaji ya Marerani hajajibu hilo. *(Makofi)*

Nimemwomba aahidi kuleta Muswada utakaosema kwamba watakaoruhusiwa kutafuta na kuchimba madini ya vito ni Watanzania tu. Hajaeleza hilo. Nilimwomba anieleze na kukubali kwamba Mererani litaanzishwa eneo la *EPZ* ya kukata madini ya Tanzanite hajaeleza hilo. Nilimwambia anieleze suala la umeme makao makuu Prekesimeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuomba kwanza atoe maelezo hayo ndiyo niweze kuridhika ama kutoridhika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwamba Mheshimiwa Kone tunaanza kukubaliana kubaliana katika yale tunayoyasema na nitamjibu haya ambayo yamebakia nadhani baada ya hapo ataridhika. Tume ya Mbona kama nilivyosema hapo awali Tume ya Generali Mbona ni Tume ya Waziri wa Nishati na Madini. Mimi nilipoingia nilipewa ripoti hiyo na tipoti hiyo tumeifanyia kazi ndiyo iliyotufikisha hapa tulipo katika kutekeleza yale yote yale ambayo tuliona kama Serikali yanafaa kutekelezwa pale Wizarani. *Controlled area* kwa mfano, kusuluhisha, kuanzisha Kamati hii ya Kusimamia, yale yote ambayo nimesema tumeyafanya zaidi pale Mererani kuleta amani yamefanywa kutokana na Tume ya Mboma na Kamati nadhani inahusiana na Sekta yangu Wabunge wengi wameshaona ile ripoti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge watataka kuona hiyo ripoti ambayo ni ya siku mwaka 2002 na kama nilivyosema tumetekeleza mengi, haya yote tunayofanya kuhusu *Tanzanite,* kuhusu mipaka, kuhusu usalama wa pale mahali, kuhusu soko, yote hayo yametokana na Tume ya Generali Mboma. Kwa kweli tunaweza kumwonyesha Mheshimiwa Mbunge kama atahitaji ripoti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba tutoe tamko kwamba wawekezaji wa madini ya vito yawe ni ya Watanzania tu. Tukumbuke Waheshimiwa Wabunge kwamba tunatekeleza Serikali inatekeleza Sera za Chama kilichopo na Sera ya chama chetu ni kwamba wawekezaji kutoka nje watakuja na watawekeza kwa taratibu na sheria zetu ambazo zipo. Sasa kama kuna haja ya kubadilisha na huyu ni mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi anaielewa kabisa kama ana haja ya kubadilisha hilo basi afuate taratibu zile ambazo zitatumika katika Chama chetu. Lakini kwa kweli mimi kama mtekelezaji tu peke yangu siwezi kutamka hapa kwamba wawekezaji sasa hawapo hapa au wapo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EPZ.* Naomba tuelewane Waheshimiwa Wabunge kuhusu *EPZ. EPZ* ni *Economic Processing Zone*. Katika nchi yenye fedha, nchi yenye uwezo, hizi zinajengwa na Serikali yenyewe. Waziri wa Fedha, na Waziri wa Viwanda na Biashara wanachagua eneo mahali wanasema hapa tujenge *EPZ.* Wanaweka *infrastructure* yote, miundombinu yote, maji, umeme, simu, mabanda kila kitu kinakuwa pale. Wawekezaji sasa wanakuja, anakodisha tu, anachukua kibanda, anachukua sehemu anafanya biashara yake. Lakini kwa mahali ambapo hakuna uwezo wa kutosha hii hapa *EPZ* ambayo Mheshimiwa Ngasongwa wanasumbuana nayo hapa Ubungo, majengo tuliyakuta, kuyabadilisha kufanya pale ilipofika ni kazi kubwa sana. Tumeshindwa sisi Wizara yangu na *TANESCO* hata kupeleka umeme maana sehemu nyingine unaambiwa umeme unatakiwa shilingi bilioni 4 labda ili *upate* umeme wa kuufikisha kwenye *EPZ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sisi Mheshimiwa Mbunge with all due respect ukisema ijengwe pale na Serikali maana yake you asking for the moon na unaomba kitu ambacho ni kigumu sana, *what will happen* sisi tunasema eneo hilo hapo, anayetaka kuja kuwekeza kujenga *EPZ* yake aje awekeze pale na hilo halikukatazwa. Kuna mawazo kwamba Mheshimiwa Shellukindo, Kamati yake imeshauri kwamba ili *EPZ* ijengwe *Kilimanjaro Airport* kwa mambo ya *Tanzanite* kwa sababu pale ni rahisi, wageni wanakuja wananunua vitu vyao pale wanaondoka. Tusijengee sehemu ya mbali.

Lakini mimi hilo mimi haliko kwangu liko kwa Mheshimiwa Ngasongwa na kwa uwezo ambao utapatikana wakati wa kutekeleza hilo, siyo wa Serikali lakini ni wa wawekezaji. Mererani haijakataliwa kuwa *EPZ* kama kuna mwekezaji ambaye yuko tayari kujenga *EPZ* pale na kufanya kazi hiyo ya madini pale Marerani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme Loiksimeti. Nitoe ahadi vile vile kwamba tunategemea wafadhili watusaidie kupeleka umeme pale. Sasa ni *SIDA* ya Sweden zikipatikana *feasibility study* narudia *feasibility study* tena lazima ipatikane ndiyo Mfadhili akupe fedha zake. Lakini kuna matumaini kwamba *SIDA* watatusaidia katika shughuli hiyo. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza tukayajadili baadaye lakini nieleze hili la mauaji. Bahati nzuri leo nimepokea *FAX* kama nilivyosema kutoka *AREMA*. Wamesema hivi, wananchi wa Mererani wamekuwa wakinyanyaswa, hutendewa kila maovu na kuuawa. Wamelilia vyombo vya dola hawapati msaada. Wanawalilia ninyi Wabunge wachaguliwa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mkubali kuwasilisha kero hii Serikalini kupitia kwenu ninyi Wabunge, wamesema. Miongoni mwa vitendo viovu tulivyothibitisha hapa kufanyiwa wachimbaji hao ni pamoja na kuwafyatulia risasi. Kuwaumisha mbwa, kuwafungia ndani ya konteina na kuwasulubisha kwa kuwavua nguo na kuwachapa bakora. Maandishi yako hapa. Kinachotushangana ni kwamba pamoja na vitendo hivyo vilivyostahili kuvumiliwa na Serikali yetu haionyeshi kuchukua hatua madhubuti dhidi ya watuhumiwa hawa.

Waheshimiwa Wabunge kitendo hicho cha kusitikisha kinatafsiriwa na wengi kuwa Serikali imeondoa huruma kuwatoa kafara wananchi wake kwa Makaburu bila kujali kuwa wananchi hao ndiyo waliweka madarakani Serikali hii kwa kutumia kura zao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kutokana na muda tulionao na wewe una mambo mengi.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Nimeacha hilo ulilolisema

**MWENYEKITI:** Kaa chini kwanza, kaa chini. Mimi najua una mengi ya kueleza. Lakini nadhani Waziri ameelewa. Kwa sababu tunazo dakika 10 tu kwa haya tunayoyazungumza kumi tu. Na watu ninao kumi. Kwa hiyo, kila mmoja apate nafasi.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuzungumzia hili vizuri naomba kutoa hoja mbili. Moja, muda uongezwe. Pili, naomba kwa kutumia kifungu 104(ii) baadaye nitoe maombi ya kuunda Tume Teule ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hebu toa hoja moja kwanza unayotaka iamuliwe. Hoja kwanza halafu tuendelee.

## HOJA YA KUONGEZA MUDA WA KUKAA BUNGE

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uongezwe muda wa kukaa Bunge lako Tukufu.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hapa Wabunge zaidi ya kumi walisimama ikiwa ni ishara ya kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Parseko Kone)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni kaeni nimewaona. Waheshimiwa Wabunge natafuta ile Kanuni nadhani ya 21(iv) pole pole, mimi ndiyo naongoza kikao hapa. *(Kicheko)*

Sasa kifungu hicho Kanuni ya 21(iv) inasema hivi, isipokuwa kama Bunge litakuwa limeahirishwa mapema zaidi, Bunge litaendelea kukaa mpaka saa 2.45 usiku wakati ambapo Spika, atasimamisha shughuli na kuahirisha Bunge bila hoja kutolewa hadi kesho yake au siku nyingine itakayotajwa. Lakini iwapo hoja ya kuongeza muda wa kikao hicho itatolewa na kukubaliwa, Spika, ataahirisha Bunge wakati muda utakaoongezwa utakapomalizika. Sasa niishie hapo. Sasa Mheshimiwa Kone alivyotoa hoja ile alitaka muda uongezwe, hakutaja muda. Lakini Kanuni inasema isizidi dakika 30. Kwa hiyo, hoja imetolewa na imeungwa mkono kwamba muda uongezwe. *(Makofi)*

Muda huo utaongezwa baada ya muda wa kawaida kwisha. Kwa hiyo, sasa nitawahoji ili muda uongezwe wa shughuli za Bunge uongezwe kwa nusu saa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Bunge hili linaamua kuongeza muda kwa nusu saa ambayo itatufanya tumalize shughuli saa 2.15.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliongeza muda wa kukaa mpaka saa 2.15 badala ya kumaliza kazi zake saa 1.45 usiku ili kuendelea kupitia vifungu vya Wizara ya Nishati na Madini)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 21. Naomba maelekezo yako, umetuhoji tukiwa kwenye Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge naomba tuelewane taratibu tu. Tuende taratibu tutakwenda vizuri sana. Umesema kuhusu utaratibu. Nimekuuliza Kanuni. Sasa nilikuwa nangojea kusikia Kanuni Namba ngapi.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Hiyo hiyo ya 21

**MWENYEKITI:** Kanuni ya?

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** 21 kifungu cha nne.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 21, hebu eleza.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo inazungumza tukiwa kwenye Bunge. Sasa hivi tuko kwenye Kamati na umetuhoji kwenye Kamati. Ilitakiwa turudi kwenye Bunge ndiyo utuhoji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawasawa, kuna Kamati ya Matumizi kifungu cha taratibu tukiwa kwenye Kamati. Hivyo kila kitu kimeandikwa humu ndani. Kwa hiyo, kila mtu atapata haki yake na Kanuni zitaendelea vizuri. Sasa kuna Kanuni ya 81. Kwa kawaida tunaitafuta hiyo Kanuni ambayo inaruhusu wakati wa Kamati ya Matumizi, sawasawa. Kama nilivyosema, Kanuni ya 81 kwenye Kanuni ndogo ya (vi), endapo Spika, ataona kuwa muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili Bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kwisha, basi atafunga mjadala ili aweze kumpatia mtoa hoja nafasi ya kujibu ndani ya muda uliosalia.

Hiyo ni katika mjadala. Hali kadhalika wakati Bunge liko katika Kamati ya Matumizi, isipokuwa, naomba msikilize sana na vizuri. Isipokuwa kama itatolewa hoja ya kuongeza muda wa Kikao cha Kamati hiyo. Kwa mujibu wa Kanuni ya 21(4) ya Kanuni hizi, zikibaki dakika 10, isipokuwa kama imetolewa hoja kwa mujibu wa Kanuni ile ya 21. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Tuendelee!

**MWENYEKITI:** Tuendelee, sawasawa. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kanuni Na.104(2) inasema Mbunge kwa kusimama mahali pake na kuzungumza anaweza kutoa hoja lakini ni baada ya hoja inayozungumzwa kukamilika.

Kwa hiyo, Mwenyekiti nitatoa hoja yangu baada ya hii kukamilika katika kipindi kilichoongezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawasawa. Umeitafsiri vizuri sana kanuni, tunaendelea!

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Kifungu hicho hicho cha 1001, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri analilia umeme wa Tarafa yake, mimi nalilia umeme wa Mkoa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa saba amesema Serikali ya Sweden ina nia ya kutoa fedha za upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupeleka umeme Mkoa wa Kigoma. Lakini katika maelezo yake amesema kwamba Serikali ya Sweden imetoa ahadi ya kufanya upembuzi yakinifu, je, tuelewe lipi ina nia au imetoa ahadi na kama imetoa ahadi ni ya fedha kiasi gani na lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anaelezea alisema wakati tukisubiri Mkoa wa Kigoma utapata *generator.* Lakini ieleweke kwamba sasa hivi Mkoa wa Kigoma, Makao Makuu ya Mkoa zipo *generator 9* ni 4 tu zinazofanya kazi na hizo 4 zinazofanya kazi ni kwa zamu. Je, akitoa *generator* moja itaweza kufanya kazi ya *generator 9* au anaahidi kutoa *generator 5* zisaidiane na zile 4 ambazo zinafanya kazi au atazitengeneza zile 5 zilizobakia pamoja na ile mpya tutakayopewa ili kusudi tuweze kupata umeme wa uhakika kama alivyosema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ikumbukwe kwamba kutokana na kukatikakatika kwa umeme kumeleta madhara kwa wananchi wa Kigoma sio madhara tu ya vifaa vya vyao vya umeme lakini hata na vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea kifo Dr. Msofe huko Kigoma kutokana na yeye kukatiwa umeme wakati anajaribu kutafuta *generator* kwa koroboi *generator* likalipuka Dr. Msovu amefariki, mfanyakazi wake amefariki, mjukuu wake ameumia na mke wake baadaye amefariki kwa *pressure.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini umeme wa uhakika tutaupata vipi?

**MBUNGE FULANI:** Waziri!

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Waziri, umeme wa uhakika tutaupata vipi kwa *generator* mpya zaidi ya 1 ziwe 5 kufidia zile 4 au kama ni 1 ni ya *megawatt* ngapi ya kuweza kutosheleza Mkoa wa Kigoma? Naomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ndaboine kwa maswali yake. Nasikitika sana kwamba kumetokea vifo kutokana na umeme huko Kigoma. Kwa kweli tunasikitika sana lakini tunawapa pole.

Tunachosema ni hivi *generator 2* nyingine zitakuja Kigoma na ziko njiani kutoka huko zilikonunuliwa kwenda kuongeza nguvu katika *generator* ambazo tayari zipo na zile kazi ya kuzikarabati na kuhakikisha kwamba zinakuwa *in working order* itaendelea wakati wote. Hiyo ni ahadi ambayo tunatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo au athari zozote zile za vyombo vya wanaotumia umeme, kama tulivyoeleza, uchunguzi utafanywa na wataalam wa *TANESCO* na wanaohusika ili ijulikane kama tatizo lilikuwa ni la *TANESCO* au ni la mwenye nyumba au ni la yule ambaye alifikwa na tatizo hilo. Tunaomba washirikiane na Meneja wetu kule kama tunahusika basi *TANESCO* itasaidia kama taratibu zinavyotaka, ahsante.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kujibu swali langu lakini swali la kwanza hakulijibu. Niliuliza hivi katika kitabu

amesema Serikali ya Sweden ina nia lakini katika maelezo amesema imetoa ahadi na nikauliza kama wametoa ahadi ni ya shilingi ngapi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katika hili hili alipouliza Mheshimiwa Mporogomyi alimwambia anaweza kwenda hata Ubalozini aka-*check* lakini maadam umeuliza ni kiasi gani basi tumpe nafasi Waziri ajibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina kiasi cha kwamba ni shilingi ngapi kwa hapa nilipo lakini kwamba ni ahadi au tunatarajia yaani kuna uhakika au vipi hilo naweza kusema fedha hizo Serikali ya Sweden imekubali kutupatia ili tufanye hiyo *feasibility study.* Tuliachie hapo, tupate fedha na nitakapopata hiyo *figure* yenyewe nitampatia Mheshimiwa baada ya *session.*

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara za Mkoa wa Kigoma, Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Frederick Sumaye, Makamu wa Rais, Waziri Kazi, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto wote wamefika. Juzi kwenye ujio wa Makamu wa Rais akiwemo na Waziri wa Mazingira na yeye alikuwa ni mgeni wa Mkoa ule sisi ndio wenyeji, maandamano ya Mkoa wa mzima wa Kigoma walikuwa ni watoto wadogo wanakimbia wanasema tunataka umeme, fikiria Mkoa mzima watoto wanasema tunataka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kauli ya Serikali ilikwishasema, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini anayoyatoa humu kutoka Kaliua kwenda Urambo mpaka Kigoma, *Hansard* pale zipo. Sasa inapokuwa Kauli ya Serikali inajipanda hatuwezi kuwa na imani namna hii, Kauli ya Serikali haiwezi kubadilika kamwe itatetea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo alipotoa jibu la kumjibu Dr. Amani Kabourou kwamba kunafanyika upembuzi yakinifu sijui utoke Burundi, Kongo utoke wapi ukipeleka Hansard za namna hii Kigoma hawawezi kuelewa tena yaani umefuta. Wakishasema ‘ndansi’ yaani ni kiapo cha mtu wa Kigoma yeye amekataa kabisa yaani ina maana sisi Wabunge wa Kigoma hatuwezi kueleweka katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya majibu ya kujikanyagakanyaga, ngoja nieleze, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini miaka iliyopita mwaka 1993, Mheshimiwa Kikwete, Waziri wa Burundi alikuja, Mkalimani alikuwa Mheshimiwa Ntagazwa, ndiye alikuwa anakalimani kujua kule umeme wanauitaje, umeme kwa Kirundi unaitwaje, wanaita *‘muyagankuma’*, sasa maana yake nini hiyo? Alikuja tulikaa hapa *Dodoma Hotel* na maelezo yakawa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti. wale kule Burundi wana umeme mwingi tu wala Serikali haikusema izingatie yale maelezo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile taarifa ukimfuata Waziri Kikwete tena bahati nzuri ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ina maana aende kabisa ule umeme uje, kesho uwe umefika. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wote wamefika, Waziri Mkuu amefika, wengine wamefika leo unapotujengea *VETA* yenye thamani ya shilingi bilioni 5 Mkoani Kigoma uendeshaji wake unatumia umeme kutoka wapi? Yaani ujenge jengo la shilingi bilioni 5 lakini umeme ambao kwa Mkoa wa Kigoma huwezi kufikisha shilingi bilioni 5, haliwezekani! Nalifikiri wangeanza kutuletea umeme wa shilingi bilioni 5, naamini shilingi bilioni 5 zinaweza kusambaza umeme Mkoa mzima wa Kigoma. Hebu tuwape akina Mporogomyi wana uchumi wajaribu kufanya mahesabu haya kama shilingi bilioni 5 haziwezi kupeleka umeme Kigoma. Sasa mnatujengea *VETA* kwa shilingi bilioni 5 lakini hakuna umeme hata wa shilingi bilioni 1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo haya yako namna gani, mnatuyumbisha tu. Hivi watakuwa wanakuja viongozi sisi tunawaasha vibatari tu, akija Waziri Mkuu tuwashe vibatari, Makamu wa Rais vibatari, Rais vibatari, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, vibatari, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira yeye ni nyumbani kwao ataota giza hilo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tumruhusu ajibu.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Sasa naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Ahaa!

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Umeme unakuja lini, hapo sasa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Halimenshi Mayonga na kwa kweli jibu letu ni lile lile. Lakini nimepata hapa taarifa kwa ufupi tu, niliahidi wakati nikimjibu Mheshimiwa Kabourou kwamba niko tayari mimi na wataalam wangu kwenda Burundi kufuatilia huu umeme ambao tunaambiwa mazungumzo yalishafanyika, hiyo ni moja, nitafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hiyo, nina taarifa hapa ya wataalam kwamba umeme wa Burundi katika mazungumzo yaliyofanywa kati ya watu wetu hapa na watu wa Burundi hautoshi kuja huku kwetu isipokuwa twende kule tukawekeza ili kuuongeza nguvu kuja huku. Hiyo ndio taarifa ya kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naahidi kwamba niachieni mimi nitalifuatilia, nipeni muda nikalifuatilie ili nipate uhakika wa umeme kutoka Burundi. Kama hatukupata huo basi itabidi kwa kweli tutafute njia zetu za huku huku na naomba Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma na wananchi kule watuamini kwamba tunafanya kila tunaloweza kuwapelekea umeme mapema iwezekanavyo.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu na linaleta kero hasa yaani inakereketa hili kuthibitisha hayo majibu je, atakubaliana kwamba hiyo *delegation* ya kwenda Burundi ili sisi tukawe Wakalimani wake je, uko tayari hata kufuatana na wajumbe wawili ambao tunaweza kuelezea akiwemo na Waziri wa Mazingira kwa sababu anajua *'muyagankuma',* je, yuko

tayari ili tumalize tatizo hili ili umeme Mkoani Kigoma uwake kwa sababu ni kero kubwa kwetu, hilo atakubali, hapo sasa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwenda na ujumbe ambao utakuwa na wawakilishi kutoka Kigoma. *(Makofi)*

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Kifungu 1001, namwomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi wa masuala yangu mawili ambayo nimechangia kwenye mchango wangu wa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu mtindo wa Maafisa wake, Mameneja wa Mikoa kutoa makisio ya bili za umeme, mtindo huu utasitishwa lini kwa sababu ni kero kwa wananchi wote wa Tanzania kupewa bili ambao hazina ukweli. Hili nilichangia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini sasa hivi nataka Waziri anayehusika alijibu suala hili na Watanzania wasikie. *(Makofi)*

Pili linahusu suala zima la Mkoa wa Shinyanga kutopewa umeme katika vibanda vya Chama cha Mapinduzi ambapo wafanyabiashara ndogondogo wanateseka kwa sababu mpaka sasa hivi umeme hawajafungiwa. Sababu wanazozitoa wataalam wake kwa kweli hazipendezi kwa sababu zinaonekana zinaweka uficho wa kitu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikwenda kuulizia hilo wakasema Makao Makuu ya *TANESCO* wanafanya Bajeti. Nikarudia tena mara ya pili wakasema bajeti ni Sh.800,000 kwa hiyo wanatazamia watalishughulikia hilo mapema. Nikaja kwa Naibu Waziri hapa kaka yangu Dr. Msabaha, nikamueleza hilo. Akapeleka fax kuwauliza kwa kweli majibu yao tangu mwezi wa Februari, 2004 bado hawajatekeleza kitu chochote.

Sasa kwa nini wataalam wake wanapenda kudanganya viongozi wao, Wabunge wadanganywe, Naibu Waziri wamdanganye. Sasa nataka nimsikie Waziri anasema nini katika hili na umeme tutaupata lini ili watu waweze kufanya biashara zao pale na waweze kujikwamua kwenye umaskini.

Kama hawakufanya hivyo basi wanampiga vita Waziri anayeshughulika na kuondoa umaskini kitu ambacho kinashangaza kupigana vita wenyewe kwa wenyewe yeye anaondoa umaskini wao wanarundika umaskini, naomba maelezo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa maelezo ya dada yangu Mheshimiwa Esha Stima kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda nikubaliane naye kwamba makisio ya bili za umeme ni kero na moja ya kazi ambazo *TANESCO* inapaswa kufanya na imekuwa ikifanya kwa kiwango kikubwa ni kuhakikisha kwamba wanaondokana na tatizo la makisio ya bili. Kwa sababu kazi hii inaendelea, naamini kabisa watafikia hatua ambapo suala la makisio halitakuwepo tena. Nachukua nafasi hii na kwa kuwa viongozi wa *TANESCO* wapo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi kuwaagiza tena wahakikishe kwamba suala hili la makisio ya bili waondokane nalo, hilo la kwanza.

Pili kuhusu Mkoa wa Shinyanga na vibanda vya Chama cha Mapinduzi, napenda niseme ni kweli kwamba Mheshimiwa Esha Stima alinifuata kwenye suala hili na mimi nimekuwa nikifuatilia sio kwamba wananidharau hapana, kwa kuwa nilikuwa nafahamu kwamba viongozi wa *TANESCO* wangekuja hapa wakati wa bajeti tungechukua nafasi hii kulimaliza.

Kwa hiyo, namwomba dada yangu avute subira baada ya *session* hii ya Bunge tutakuta na viongozi hao tutalimaliza suala hili.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa kutumia kifungu hiki cha 1001 niweze kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwanza naomba Mheshimiwa Waziri kama anaona suala hili kama mimi ninavyoliona kwamba kuna hizi raslimali za Taifa hazigawiwi kwa usawa. Kwa sababu sasa hivi wakati baadhi ya Mikoa au baadhi ya Wabunge wanalalamikia kupata umeme Makao Makuu ya Mikoa au Wilaya, Mikoa mingine wanazungumzia umeme kwenda vijijini.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii Mikoa hasa ya pembezoni Kagera, Mtwara, Lindi, Rukwa, Kigoma anazidi kuididimiza na kuangalia ndio hiyo Mikoa maskini? Je, haikubaliani na mimi kwamba kwa kweli sasa Serikali inapaswa kukaa chini kuangalia upya Mikoa hii hasa kwa upande wa umeme? *(Makofi)*

Pili, katika hotuba yake ukurasa wa 6, ameeleza kwamba ifikapo mwaka 2005, Wilaya alizozitaja ikiwemo Biharamulo na Ngara zitakuwa zimepatiwa umeme. Suala la umeme wa Wilaya hizi imekwishakuwa ni kero tena ni kichekesho sana ingawa wanacheka kikerokero hivi. Kwa sababu tulikuwa tunatarajia umeme ungepatikana miaka mitatu iliyopita lakini kwa sababu zile nilizoeleza katika hoja yangu ya kwanza fedha inayotengwa ni kidogo ambayo haiwezi kukamilisha kazi katika muda mfupi unavyowezekana.

Lakini ninachotaka kujua kwa vile amesema ifikapo mwaka 2005 na hii ni lugha ya ujanjaujanja ambayo haieleweki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kengele imelia, nadhani ameelewa yote ambayo...

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Hapana, naomba nimalizie basi kidogo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hapana, naomba ukae, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Batenga na wasiwasi wake kwamba labda fedha zinatoka kidogo kidogo na kama tutaendeleza labda miradi ya umeme vijijini basi Wilayani na Mikoani utachelewa. Kuna ukweli katika hilo kwa sababu fedha zetu mfuko ni huo huo kwa sasa kila mwaka tukishapanga bajeti basi kama tumesema tupeleke kwenye miradi fulani basi ni miradi

hiyo mingine yote inabidi ingoje mpaka tukipata fedha tena ndio maana inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapoanzisha huu Mfuko wa *Rural Energy Fund* itakuwa na vianzio vyake vya fedha vinaweza kutokana na misaada kutoka kwa wafadhili, kodi zetu wenyewe au mikopo tunatumbukiza pale na fedha hizo sasa zitakuwa zinatumika kwenye kupeleka umeme vijijini. Tukifika hatua hiyo basi fedha nyingine zote tunazopata nyingi nyingi hizi zitakuwa za miradi mikubwa kupeleka Wilaya na Mikoani. Kwa hiyo tunakoelekea ni kwamba tutaweza kufanya mengi kwa wakati mmoja ili mradi tuwe na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule alikosema Ngara sasa hivi kama ninavyosema mitambo inafungwa na tunategemea umeme utawaka hivi karibuni. Tukisema mwaka 2005 tunajaribu kujihami Waheshimiwa Wabunge...*(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoa tarehe, tunaambiwa tarehe fulani ulisema umeme utawaka. Kwa hiyo, tunajipa muda mrefu yakitokea mapema basi wote tutafurahi yakichelewa kidogo kwa sababu shughuli hizi ni kubwa na za kitaalam basi tunakuwa hatukupotea sana ndio maana tunaweka tarehe ndefu ya mbele ili kuwapa watu matumaini lakini kuwa realistic vile vile. *(Kicheko)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kuuliza swali dogo kwa sababu katika mahesabu yake sikuona fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya miradi hii ya Biharamulo na Ngara aweze kunieleza kwamba basi bila shaka huo mradi umekamilika kama kweli ifikapo 2005 umeme utakuwa umewaka kwa sababu sikuona mahali popote alipotaja kiasi cha fedha zilizotengwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kuna mahali umetaja pesa? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini zipo mahali, nitampa Mheshimiwa Mbunge tukishamaliza kikao hiki nitazipata kutoka kwa wataalam wangu, kifungu gani na kiasi gani wataweza kupata.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana zipo au umepata jibu kutoka kwa wataalam, naona karatasi hapo?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nazungumzia *Vote 58,* Fungu 1001, mshahara wa Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Sisi Tunangoja *Development* huku. *(Kicheko)*

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbinga ni Wilaya za zamani sana ni Wilaya ya mwaka 1965. Wilaya hii imeahidiwa

umeme kwa muda mrefu sana kila muda unapofika wanapeleka mbele hadi leo hii Wilaya haina umeme. Hii ni Wilaya ambayo kwa muda mrefu inachangia sana mapato ya fedha za kigeni kwa nchi hii kutokana na zao la kahawa lakini haijafaidika chochote kwa upande wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haja yangu ni maombi kwanza naiomba Serikali ishirikiane na *TANESCO* ikamilishe Usambazaji wa nyaya za umeme Mji wa Mbinga.

Pili, naomba sana Serikali ikishirikiana na *TANESCO* wanunue *generator* ikashirikiane na *generator* iliyonunuliwa na Halmashauri ili *TANESCO* iendeshe umeme Mji wa Mbinga wananchi wapate umeme wakati wakisubiria mradi wa muda mrefu wa *National Grid* toka Makambaku, Songea, Mbinga, Namtumbo. Mheshimiwa Waziri anasemaje, tunaomba utusaidie ili wananchi wa Mbinga wawe na imani na Serikali yao, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, ombi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi kwa maelezo ya Mheshimiwa ya Dr. Thadeus Luoga kama ifuatavyo.

**MWENYEKITI:** Najua umechoka lakini sauti ongeza kidogo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ahaa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Luoga kuwa tunafahamu shida ya watu Mbinga. Kuhusu maombi yake mawili aliyoyasema moja la kuzungumza na *TANESCO* kutizama uwezekano wa kusaidiwa kusambaza nyaya za umeme kwa sehemu zilizobaki na lingine la *generator,* napenda niseme kwamba naomba atupe muda tuyafanyie kazi haya badala ya kumpa ahadi kwamba kesho au kesho kutwa itawezekana.

Lakini nataka nimfahamishe kwamba kwa kweli tutayachukulia kwa uzito unaostahili na tutayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado nawakumbusha itakapofika saa 8.05 tutaingia kwenye *guillotine,* tutapitisha vifungu vyote.

**MBUNGE FULANI:** *My God!*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu nimekuwa nikieleza tatizo la umeme wa Ihanja...

**MWENYEKITI:** Hawasikii sogeza hiyo mic.

**MHE. MOHAMMED H. MISSANGA:** Kwa muda mrefu nimekuwa nikieleza tatizo la umeme Ihanja toka nimeingia kwenye Bunge hili. Serikali iliahidi kwamba

mwishoni mwa mwaka 2000 itakuwa imepeleka umeme Ihanja. Nimerudia kuhoji Serikali kupitia maswali zaidi ya mara tatu na ahadi imekuwa ni kama hivyo lakini mpaka sasa hakuna. Kinachosikitisha ni kwamba nguzo za umeme zimepelekwa toka mwaka 1998 zikatandazwa chini na wananchi wale kila siku wakipita wanazisalimia tu habari za asubuhi, habari za jioni, sasa wamechoka. Lakini zaidi ya hapo baadhi ya nguzo zikachukuliwa zikapelekwa Manyoni kwenda kumalizia mradi wa Manyoni kwa ahadi kwamba zitarudishwa mpaka leo hazijarudishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe mradi huu wa Ihanja ilikuwa ni mradi pamoja na Ntinko kwenye Nkungi kule kwingine kote kumetekelezwa imebaki Ihanja ambayo ni kilomita 11. Kule Ntiko - Nkungi ni kilometa 35 lakini Puma - Ihanja ni kilomita 11 mpaka leo hakuna maelezo yoyote.

Nimezungumza sana na Mheshimiwa Naibu Waziri ofisi kwake na maeneo mbalimbali na yeye mwenyewe yupo ananisikia akinipa matumaini kwamba *inshallah* mambo yatakwenda sawasawa. Sasa wananchi wa Ihanja wamefika mahali wanaona kwamba Serikali yao ya CCM inawaongopea na mimi sidhani kama Serikali ya CCM inaweza kuwa na sifa ya kusema uongo. Je, Mheshimiwa Waziri ataniambia nini na kuuondoa huu udhalilishaji uliopo kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi isionekane kama ni ya uongo na itatekeleza lini ahadi yakupeleka umeme Ihanja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pale pana shule ya Sekondari inayoendeshwa na KKKT. Askofu amepata uhisani kutoka Marekani wa kusaidia vifaa vya ufundi, ile ni *Technical Secondary School* lakini kwa sharti kwamba pawepo na umeme. Kila siku Askofu nawasiliana naye, anatoa masikitiko yake kwamba atakosa ufadhili kwa Wamarekani kwa sababu ya kukosa umeme na ile ni *Technical Secondary School.* Je, Serikali haioni kwamba imewakosesha msaada watu wa Ihanja kwa ajili ya shule ile ili kuinua viwango vya elimu vya shule ya Ihanja na Singida kwa ujumla. Naomba maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa maelezo ya Mheshimiwa Alhaji Missanga kama ifuatavyo: Kwanza napenda nithibitishe kwamba suala hili amekuwa akilifuatilia kwa muda mrefu, lakini napenda nimhakikishie kwamba Serikali haina nia wala haijawaongopea wananchi wa Ihanja na kwa kweli haina nia ya kuwakosesha miradi muhimu ya maendeleo kama shule. Nadhani kazi ya Serikali ya sasa hivi ni kusambaza elimu ya Sekondari nchi nzima na kunaushahidi tosha kwamba ndio mwelekeo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi tu nilikutana na Mheshimiwa Missanga, akanipa kazi hii, nikamfahamisha kwamba nimeipeleka kwenye Makao Makuu ya *TANESCO.* Kwa bahati mbaya nilikuwa sijapata muda wa kuonana na viongozi wa *TANESCO* ambao wamekuja hapa hivi karibuni kwa ajili ya Bajeti hii.

Sasa mimi nadhani hili ndugu yangu, Sheikh wangu Missanga namwomba aliache, mimi na yeye na viongozi waliopo hapa wa *TANESCO* tukimaliza hapa tukakutane ili tujue namna ya kuli-*handle.* *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kunihakikishia kuwa

*TANESCO* haijasitisha kupeleka umeme Vijijini. Mimi nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri anieleze kwa nini Vijiji vya Barazani, Mtumbili, Mngonze ambao waliomba umeme na wakalipia lakini mpaka leo hawajapewa ule umeme. Sasa labda suala lilikuwa kwa kuwa *TANESCO* haijasitisha, labda Meneja wa Mkoa wa Singida ndiye aliyesitisha. Sasa ningeomba tu anihakikishie kuwa Vijiji vya Mngonze, Barazani na Mtumbili ambavyo wananchi walilipia kwa siku nyingi watapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna shule ya Kinampanda na Mji Mdogo wa Kinampanda na Mji Mdogo wa Ndago, wameomba *transformer* ya kutumia ku-*pump* maji kupeleka kwenye shule hizi mbili na kwenye Miji hii Midogo. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie kuwa wananchi watapewa au watanunuliwa na *TANESCO* hizi *transformer* ili wapate maji ambayo wanahitaji kwa shule hizi mbili na Miji hii Midogo? Nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa maelezo ya Mheshimiwa Shango kama ifuatavyo: Kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Shango, nimefika mpaka kwenye eneo lake, mpaka kwenye nyumba yake na yeye ni mfano bora sana wa watumiaji wa nishati mbadala ya *biogas.*

Kuhusu haya aliyoyasema sasa, kwa sababu ni taarifa ninazozipata sasa hivi kwa vitu ambavyo ni *very specific* na kwa sababu uongozi wa *TANESCO* upo hapa pamoja na *Regional Manager* wa Singida yupo, naomba atupe muda mimi na yeye tushirikiane tuone hali ikoje. Lakini napenda niseme moja kwamba, kwa kweli *TANESCO* Singida kwa kadri ninavyofahamu wanafanya kazi kubwa, wanajitahidi vya kutosha na huyu *Regional Manager* anayetajwa hapa pia anafanya kazi kubwa kwa kweli.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefikia ule wakati wa *guillotine,* hakuna tena michango.

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* … … … … … … … … 230,218,800/=
Kifungu 1003 - *Policy Planning* … … … … … … … … … … 2,374,348,900/=
Kifungu 2001 - *Minerals* … … … … … … … … … … … …2,262,402,800/=
Kifungu 2002 - *Madini Institute* … … … … … … … … … … 607,721,400/=
Kifungu 2003 - *Research and Laboratory Services* ... ... ... …3,576,048,100/=
Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum* …... … … … … … 127,085,144,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Kifungu 1001 - *Administration and General* …... … … … 273,000,000/=

Kifungu 1003 - *Policy Planning* ... ... … … … … … … … 45,000,000/=
Kifungu 2001 - *Minerals* ... ... … … … … … … … … 5,900,002,300/=
Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum* .... … … … … 40,679,932,400/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi limepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yaliyofanywa. Hivyo basi naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wakati ule kwenye Kamati Mheshimiwa Kone alisema alikuwa na hoja na akatoa *note* kwamba wakati huu atapenda kuitoa. Sasa nampa nafasi hii Mheshimiwa Kone.

**KAMATI TEULE YA KUCHUNGUZA MIGOGORO NA MATATIZO KATI YA *AFGEM* NA WACHIMBAJI WADOGO WA MERERANI**

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Kanuni ya Bunge Namba 104(2), naomba kuomba Bunge lako Tukufu, kwa unyenyekevu na kwa heshima kabisa wakubali kuteua Kamati Teule ya Bunge, ili kuchunguza migogoro na matatizo kati ya *AFGEM* na wachimbaji wadogo wa Mererani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Umesema ni kanuni namba ngapi?

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Namba 104.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni Namba 104, Kifungu kidogo cha pili au cha kwanza?

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Kifungu Kidogo cha pili.

**NAIBU SPIKA:** Unatumia cha pili?

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Ndiyo Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa acha nikisome, kifungu hicho kinasema hivi: "Kamati Teule yaweza pia kuundwa endapo baada ya Bunge kujadili hoja fulani, litaamua kupeleka jambo fulani lililotokana na hoja hiyo kwenye Kamati Teule ambapo utaratibu wake utakuwa kama ifuatavyo":

Waheshimiwa Wabunge, naomba hapa tusikilizane vizuri: "Mara tu baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa Mbunge yeyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii aweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule.

Baada ya hapo Mbunge huyo atatoa taarifa ya hoja yake kwa maandishi kwa Katibu na hoja hiyo itashughulikiwa wakati unaofaa kwa kuzingatia mpangilio wa shughuli uliowekwa na kanuni ya 23(4)". Kwa hiyo, mimi naichukulia hiyo kama ni taarifa rasmi, kwa hiyo nafasi yako sasa kupeleka rasmi kwa Katibu kumjulisha jambo hili. *(Makofi)*

*(Hapa Hoja ya kuunda Kamati Teule ya Bunge iliafikiwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wakati nipo kwenye Kamati pale na Mheshimiwa Kone alitoa hoja ya kuongeza muda, nilipokea vi-*note* vingi vikisema mbona muda unakwisha hatapata nafasi ya kusema. Ningependa kufafanua hili kwamba unapoomba muda uongezwe na Bunge zima likakubali, ule muda ulioongezwa siyo wako peke yako, ni wa Bunge zima ambalo limekubali muda uongezwe. Kwa hiyo nashukuru kwamba yote tumeyamaliza kabla ya wakati haujaisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la pili, leo wote mnajua kulikuwa na mjadala mkali. Mimi kwa kweli kwa dhati kabisa, nawashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa na kwa kweli leo nimejifunza sana. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Baada ya hapo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.13 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 16 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*